Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 25 Julai, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama ) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**:-

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**:-

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA - MSEMAJI WA MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:-**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Juu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 293

**Mgogoro wa Mipaka Kati ya Wilaya ya Kiteto na Kondoa**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa mpaka kati ya Wilaya ya Kondoa na Kiteto iliyosababisha wananchi 72 wa Kondoa katika Vijiji vya Itolwa na Mlongia kukosa makazi kwa kuvunjiwa nyumba zao na wale wa Wilaya ya Kiteto?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa mwaka 1999 lilitokea tukio la vurugu lililosababisha uvunjifu wa amani kati ya wananchi wa vijiji vya Itolwa na Mlongia Wilaya ya Kondoa na Kijiji cha Katikati Wilaya ya

Kiteto. Moja ya matokeo ya vurugu hizo ni kuchomwa kwa nyumba 72 za wananchi wa vijiji hivyo vya Kondoa . Kiini cha Mgogoro huo ni kugombania matumizi ya rasilimali hususan ardhi na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa ili kutatua mgogoro huu ili kuhakikisha hali ya utulivu na amani inakuwepo. Juhudi hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya mikutano ya ujirani mwema baina ya pande zenye mgogoro ili kurejesha hali ya utulivu amani na maelewano.

(ii) Tarehe 22 Desemba, 1999 aliyekuwa Naibu Waziri, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, alifika na Tume iliyokuwa imeundwa kushughulikia mgogoro huo na kutembelea eneo hilo na kutoa maagizo ya kutatua mgogoro huo. Moja ya maagizo aliyotoa ni kurudisha alama za mipaka zilizokuwa zimeng'olewa baada ya kuwekwa na wataalam wa upimaji kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wakishirikiana na wataalam wa ngazi ya Mkoa na Wilaya husika.

Agizo hili lilitekelezwa tarehe 31 Agosti, 2001 na wapima ardhi kutoka ofisi za Halmashauri za Wilaya ya Kondoa na Kiteto kwa kurudisha alama zote zilizokuwa zimeng'olewa wakitumia tangazo la Serikali Namba 65/1961 ambalo lilitumika kuweka alama hizo hapo awali.

(iii) Mwaka 2001 Wakuu wa Mkoa wa Arusha na Dodoma pamoja na Wakuu wa Wilaya za Kiteto na Kondoa walikutana na kuagiza Wakurugenzi wa Halmashauri zote mbili wakutane na kubainisha vijiji/vitongoji vitakavyohamia na watumishi watakaohamia Wilaya ya Kondoa kutoka Wilaya ya Kiteto baada ya mpaka kubainisha rasmi. Kazi hii ilikamilishwa tarehe 20 Oktoba, 2001 ikiwa ni kutekeleza azimio la Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi zote kufanywa na Serikali, mgogoro huu umeendelea kujitokeza ambapo baadhi ya wananchi wa (kijiji cha Olboroti) walitaka kuendelea kuwa upande wa Wilaya ya Kiteto kiutawala. Kutokana na hali hii kuendelea Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI imepanga kuwakutanisha viongozi na wawakilishi wa wananchi wa Wilaya zote zenye migogoro zikiwemo Kondoa na Kiteto ili waweze kujadiliana na kukubaliana namna bora zaidi ya kuwatoa wananchi wetu kwenye migogoro ya aina hii. Naomba kutoa rai kuwa wananchi wa pande zote mbili za Kiteto na Kondoa kuheshimu maelekezo ya Serikali kuhusu mgogoro huu na kurejesha hali ya utulivu katika maeneo hayo.

**MHE. FELISTER A. BURA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nyingine na nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Pamoja na majibu yake nina maswali mawili madogo tu ya nyongeza. Kwa kuwa mgogoro huu wa mpaka kati ya Wilaya ya Kondoa na Wilaya ua Kiteto umedumu kwa zaidi ya miaka kumi. Je, Serikali haioni kwamba ni muda mwafaka wa kuweka alama zinazotambulika kwa pande zote mbili ili mgogoro huu ufikie kikomo? Swali la pili, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba mgogoro bado upo na bado unaendelea. Je, Naibu Waziri yupo tayari kufuatana nami kwenda kuwakutanisha viongozi wa pande zote mbili ili kusuluhisha mgogoro huu?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu pamoja na kufuatana na Mheshimiwa Felister Bura. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili la pili naliafiki moja kwa moja niko tayari kufuatana naye kwenda mpaka kwenye ule mpaka tukaangalie wote kwa pamoja itakuwa faraja kwangu, hilo la kwanza. Lakini la pili, kuna Wabunge wengi wana maswali yanahusiana na mambo ya mipaka. Labda niliweke vizuri. Mimi nilipokuwa Mkuu wa Wilaya ya Arusha nimehusika katika mgogoro huo na tulikwenda sisi kwa ajili ya kutetea jambo hili na kulifanyia kazi kama tulivyoeleza hapa.

Kwa hiyo, wala si jambo ambalo mimi nalisikia hapa leo kwa mara ya kwanza nalifahamu *as District Commissioner* nalifahamu kwamba lilitokea hili jambo.

Tatizo lililoko hapa na ambalo tumeelekeza hapa tarehe 14 mwezi huu tumewaita wataalam wetu wote wamekutana pale Kondoa. Wamekaa wamezungumza na wameona kwamba kweli maazimio yaliyofanyika pale sasa yanatakiwa yafanyiwe kazi kwa mara ya mwisho na nichukue nafasi hii

kumpongeza sana Mheshimiwa Bura kwa sababu anatusaidia katika jambo hili. Ni jambo ambalo kwa kweli tulishaelewana lilishakwisha lakini bado tunaona kwamba linajitokeza.

Tumeagiza tarehe 15/8/2011 wataalam wote wanaohusika wakutane Babati, sasa kama tutaunganisha na hiyo ziara tunayozungumza hapa twende tukakutane kule na tumetoa maelekezo watakwenda na chopo kinaitwa *Global Positioning System (GPS)* ikipigwa hapa na ikisema mpaka ni huu hapa mawe yanawekwa pale.

Yakishawekwa mawe pale kuonyesha hapa ndiyo kwenye mpaka tunawaomba wananchi wa pande zote mbili waheshimu maelekezo ya Serikali. *Otherwise* itakuwa ni ngumu kila wakati tutakuwa tunakwenda wanang'oa na kama tunavyozungumzia hapa watu wamechomewa nyumba hapa na hili jambo hatuwezi kulichukua kama ni jambo dogo na la kawaida tu.

Ni jambo ambali pande zote mbili tunatakiwa tuheshimiane tusaidiane, tushirikiane ili watu wetu wasiendelee kugombana. Tanzania hii ni moja, ukiambiwa leo unakwenda Kondoa, au unakwenda Mtwara, unakwenda wapi, nchi hii imeturuhusu kwenda mahali popote na kwa maana hiyo mimi nitoe rai jambo la kwamba unakuwa upande huu au upande ule halina tatizo lolote. Mtu akitaka kushika ardhi Kondoa atashika, hakuna mtu atamzuia. Wabunge tulioko hapa tumekamata viwanja hapa kutoka maeneo mbalimbali hakuna mtu aliyewazuia. Watu wa hapa Dodoma hawakuzuia kufanya hivyo. Tujenge umoja wa kitaifa tushirikiane katika jambo hili, sisi wote kwa pamoja, viongozi wetu watusaidie kuwaelekeza wananchi ili tuondokane na tatizo hili. *(Makofi)*

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi nipate kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Tatizo la Itolwa Mlongia na Mrijo halina tofauti sana na lile ambalo sasa limeanza kujitokeza katika kijiji cha Handa mpaka na Singida. Tarehe sita mwezi huu, wananchi 13 walichomewa mahindi na nyumba zao na askari wanaodaiwa kwamba ni wa Wanyamapori. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu tabia hii ambayo imeanza kujitokeza pia? Wananchi hao wanatoka katika Jimbo la Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara. Naomba kauli ya Serikali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo linazungumzwa hapa linahusu Sheria na taratibu za nchi. Mimi natakiwa kauli ya Serikali kwamba inasema nini. Kauli ya Serikali tuheshimu taratibu na Sheria za nchi. Kama tumekubaliana kwamba utaratibu ni huu tuuheshimu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali naomba kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Habari hii mimi naisikia kwa mara ya kwanza. Lakini kwa ujumla zimekuwepo taarifa za matendo ya namna hiyo kwenye maeneo mengi yakifanyika ambazo tunapofuatilia tunakuta ni kweli lakini wakati mwingine sio kweli. Nitumie fursa hii kutoa ufafanuzi kwamba askari wa Wanyamapori na hata watumishi wa sekta ya misitu hawaruhusiwi kufanya kitu hicho kwa maana ya kuvuruga mazao ya wananchi. Utaratibu unaotakiwa kufanyika ni kuwakamata watu wale na kuwafungulia mashtaka kwa mujibu wa Sheria inayohusika. Kwa maana hiyo suala hili tutafuatilia kuona kama kitendo hicho kilifanyika ili tuweze kuchukua hatua zinazostahili. *(Makofi)*

Na. 294

**Tatizo la Maji Mbozi Magharibi**

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA (K.n.y. MHE. DAVID E. SILINDE)** aliuliza:-

Serikali ya awamu ya nne imeahidi kutatua kero ya maji maeneo mbalimbali ya nchi:-

(a)Je, ni lini Serikali itatatua tatizo la maji Mbozi Magharibi hasa katika maeneo ya Tarafa za Tunduma, Kamsamba, Ndalambo na Msangano?

(b) Je, Serikali ina mipango gani mahususi ya kufufua vyanzo vya maji vya muda na kudumu kama hatua za kutatua kero hiyo ya maji?

(c)Je, Serikali inachukua hatua gani kwa watendaji waliohujumu shilingi milioni 5000 zilizotengwa katika Bajeti iliyopita kwa ajili ya uchimbaji wa visima?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ilitenga shilingi milioni 255.8 kwa ajili ya miradi ya maji kama ifuatavyo:-

Kujenga mindombinu ya maji katika Tarafa za Tunduma, Kamsamba, Ndarambo na Msongano, kuchimba visima virefu 21, kuweka mitambo ya kusukuma maji katika vijiji vya Chilulumo na Kamsamba, kukarabati mitambo miwili ya kusukuma maji katika vijiji vya Ndalambo na Chiwanda pamoja na ununuzi wa mitambo ya kusuma maji. Mipango yote hii imetekelezwa kupitia mpango wa miradi ya maji yenye matokeo ya haraka (*quickwins*).

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali wa kufufua miradi ya maji umewekwa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi imetenga kiasi cha shilingi milioni 95 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji katika mradi wa Kamsamba na Mkulwe. Vijiji vya Itambula, Chilulumo, Iyendwe na Namtambalala vinatazamiwa kujengewa miradi ya maji kupitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji *(RWSSP)* ambapo katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 zimetengwa shilingi bilioni 1.12 kwa uhisani wa Benki ya Dunia.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya mwaka 2009/2010, Mamlaka ya Maji Tunduma ilipatiwa fedha shilingi milioni 50 kupitia Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mbeya kwa ajili ya kununua mabomba ya maji, kununua dira ndogo na kubwa za maji, kusafisha kisima cha maji na kukarabati pampu pamoja na mota yake. Ardhi, ni kweli kwamba Mheshimiwa Waziri wa Maji mwaka 2010 aliahidi kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya miradi ya maji lakini fedha hizo hazikutolewa na Halmashauri inaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha hizi.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa pesa nyingi zimetengwa na hakuna kazi iliyofanyika na kwa kuwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) mojawapo ya ahadi ilikuwa ni kuwapatia maji na haijafanikiwa. Haoni kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kutekeleza hilo?

Swali la pili, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi ambao wana shida ya maji hususan katika Kata ya Nembanyamigogo, Serikali ina mpango gani wa kupeleka maji?

**MWENYEKITI:** Swali limehama, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mimi sikubaliani kabisa na kauli yake kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kutekeleza wajibu wake na *i have to be concrete on that*.

Mwaka 2007/2008 tulipeleka katika Halmashauri ya Mbozi milioni 127, mwaka 2008/2009 tulipeleka shilingi milioni 218 na mwaka 2009/2010 tumepeleka milioni 50, mwaka huo huo Halmashauri ya Mbozi imetenga shilingi milioni 36 kwa ajili ya kuendeleza maji kule.

Sasa hapo Serikali ya CCM ndiyo imeshindwa? Mimi nimhakikishie Mheshimiwa Mbassa, kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imesimama imara kabisa.

Hizi takwimu sikutaka kuzitoa lakini zimenipa tabu baada ya kuambiwa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa. Serikali ya Chama cha Mapinduzi *is on top of business* inafanya kazi tena kwa uhakika mkubwa kabisa na ndiyo maana nataka nimhakikishie wakati atakapokuja Waziri wa Maji hapa mtasikia atasema ni nini kitakachofanyika hata katika Halmashauri ya Biaharamulo.

Kazi kubwa imefanyika tunaomba mtupe ushirikiano, Mheshimiwa Mbassa wala usiwe na wasiwasi utaona vitu vitakavyofanyika chini ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ni ukweli usiopingika kwamba Mji wa Tunduma ambao sasa umepata hadhi ya kuwa Mji kamili lakini pia na Mji wa Vwawa ambao ndiyo Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi, miji hii inakuwa kwa *speed* kubwa, Tunduma leo ina watu zaidi ya 50,000 lakini wanaotembea pale mchana kwa ajili ya shughuli za biashara ni zaidi ya 100,000 na Mji wa Vwawa wenye wakazi 40,000/- na kwa mchana unakuwa na wakazi zaidi ya 80,000 kwa ajili ya shughuli za biashara lakini miji yote hii ina matatizo makubwa sana ya maji.

Waziri ana wahakikishia nini wananchi wa miji hiyo miwili kwamba maji ambalo ni tatizo kubwa litatatuliwa katika kipindi kifupi kinachowezekana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii miji miwili anayozungumza Mheshimiwa Mbunge, Vwawa na Tunduma ni miji midogo ambayo inakua na ndiyo maana Halmashauri imeomba kwamba tuangalie uwezekano wa kupandisha hadhi yake iwe ni Mamlaka za Mji Mdogo. Kwa hiyo Mheshimiwa Zambi mwenyewe anakumbuka kwamba nimefanya ziara katika haya maeneo, ni kweli anachosema na hiki anachozungumza ni kweli kabisa. Kwa hiyo, tutashirikiana na yeye, tutakwenda kukutana na wenzetu wa Wizara ya Maji, hawapo, Mheshimiwa Mwenyewe anaumwa na mwenzake pia amesafiri, ili tuone jinsi ambavyo tutasaidia Vwawa na Tunduma. Lakini, nataka nimhakikishie kwamba kwa utaratibu huu kwamba Mamlaka inakua kwa haraka, tutasaidiana naye, kusaidiana katika jambo hili kuhakikisha kwamba wanapata maji. *(Makofi)*

Na. 295

**Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na za Mwanzo nchini**

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA** aliuliza:-

Serikali inaonekana kuweka mkazo mkubwa juu ya ujenzi wa Mahakama za ngazi ya juu, yaani Mahakama Kuu, Mahakama za Kanda na za Mkoa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama za Wilaya na za Mwanzo kwani zilizoko hazikidhi mahitaji na ziko katika hali mbaya?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Mahakimu wa kutosha wa Mahakama za Mwanzo na kuboresha mishahara ya Mahakimu wote ili iendane na watumishi wengine?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n. y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosweeter Faustine Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango endelevu kujenga Mahakama za Mwanzo na za Wilaya ambazo hazikidhi mahitaji na ziko katika hali mbaya nchi nzima. Lakini, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Serikali kwa sasa inajenga Mahakama hizo kufuatana na upatikanaji. Aidha, hivi karibuni Bunge lako Tukufu limepitisha Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama ambayo pamoja na mambo mengine imeanzisha Mfuko wa Mahakama ambao utaiwezesha Mahakama kujipangia mipango yao ikiwemo ujenzi wa Mahakama za Mwanzo na za Wilaya.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka huu wa fedha ina mpango wa kuajiri Mahakimu wa kutosha wa Mahakama za Mwanzo. Aidha, ni lengo la Serikali kuongeza mishahara ya Mahakimu wote

ilingane na mishahara ya watumishi wengine. Hata hivyo, tunashukuru Serikali mwaka huu wa fedha uliopita iliongeza mishahara ya Mahakimu na Majaji.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini, ninaomba kuuliza maswali mawili tu madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Nkasi haina Mahakama ya Wilaya na hii humfanya Hakimu kutoka Sumbawanga awe anakwenda kusikiliza kesi Wilaya ya Nkasi kila inapobidi. Anaporudi Sumbawanga, inabidi tena aondoke na mahabusu kwenda kuhifadhiwa huko kwa sababu hakuna jengo la kuwahifadhia. Kwa kuwa Mkoa mzima wa Rukwa una upungufu wa Mahakama za Mwanzo kwa asilimia 89; na upungufu wa Mahakimu wa Makama za Mwanzo kwa asilimia 81. *(Makofi)*

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya, Wilaya ya Nkasi yenye Mahakimu kulingana na ikama. Lakini pia, ni lini Serikali itajenga Mahakama za Mwanzo kwa kila Kata na angalau Mahakimu wawili wawili kama ilivyo azma ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Kwa kuwa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, nafikiri umeishauliza mawili tayari! Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alichokisema Mheshimiwa Mbunge, Wilaya ya Nkasi kwa sasa haina Hakimu wa Wilaya.

Lakini, juhudi za Serikali zipo, dhamira ya Serikali ipo na niseme tu kwamba kama utaridhia Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mawasilisho ya Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, iko mipango mingi ambayo itaelezewa. Lakini kwa sasa ningependa kumhakikishia tu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba kwa mwaka huu ambao tumeuanza sasa hivi na ambao taarifa zake nyingi zitajitokeza katika hotuba ya Bajeti ya Wizara, Serikali inakusudia kuwaajiri Mahakimu wa Mahakama za Wilaya wasiopungua 200, na pia Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wasiopungua 150. Tunaamini katika hili pia, Wilaya ya Nkasi itazingatiwa kupata watumishi na miundombinu ya makazi ya Mahakimu inayohitajika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo wa Lituhi aliondolewa kwenda kusoma na Hakimu huyu alikuwa anashughulikia Mahakama zote kando kando ya Ziwa Nyasa. Sasa hakuna Hakimu katika hiyo Mahakama na kwa hiyo, kando kando ya Ziwa hakuna Hakimu hata mmoja. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Hakimu pale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naomba ulijibu, ingawa Mheshimiwa Komba amedandia swali la Mheshimiwa Kombo! Kwa hiyo, baada ya majibu hayo itabidi nimpe sasa Mheshimiwa Kombo aulize nafasi yake. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rosweeter, ni kweli tatizo hilo la Mheshimiwa Komba analolisema linafahamika Serikalini. Lakini, kama nilivyosema kati ya hawa Mahakimu wasiopungua 200 wanaotarajiwa kuajiriwa katika mwaka huu wa fedha, pia eneo hili ambalo Mheshimiwa Komba amelizungumzia litakuwa limezingatiwa. Ahsante sana.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshmiwa Komba, ameninyang'anya nafasi yangu. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Mahakama ndiyo chombo cha kutoa haki kwa wananchi wetu tulionao nchi nzima hii; na bahati mbaya sana Mahakama muhimu sana ni hizi Mahakama za Mwanzo. Kwa nini miaka 50 hii tunayoingia, Serikali pia haichukui mfumo ule ambao iliamua wa kujenga shule za Kata ili kuondokana na tatizo hili na wananchi wapate haki yao? Ahsante sana.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ni mzuri sana; na ninaamini kwamba ni jambo zuri la kuzingatia huko tuendako na hasa kwa kadri ambavyo Wizara inaendelea kupewa kasma kubwa zaidi tuone jinsi gani tunavyoweza kutekeleza jambo hilo.

Na. 296

**Serikali Kuajiri Wanasheria**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Hivi sasa nchi yetu ina wasomi wengi wa taaluma ya sheria wa kutosha wenye Diploma na Shahada hata Shahada ya Uzamili, lakini wasomi hao wapo mitaani hawana kazi wakati Mahakama zetu hazina watumishi wa kutosha na hivyo kudumaza zoezi zima la utoaji haki kwa wananchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi kuajiri wanasheria wa kutosha?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na wanasheria wa kutosha katika kila Wizara, Mikoa na Wilaya kwa minajili ya kuimarisha utawala wa sheria na utoaji haki kwa wakati kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji halisi ya Mahakimu Wakazi ni 450 ili hali Mahakimu waliopo kazini ni 336. Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo waliopo kazini ni 758, wakati mahitaji halisi ya Mahakimu hao ni 1452. Kwa upande wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mahitaji halisi ya Mawakili wa Serikali ni 1246, ilihali Mawakili waliopo hivi sasa ni 362.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua uzito na changamoto hii ya upungufu wa Mahakimu na Mawakili wa Serikali, Serikali imejiwekea mkakati wa kuajiri watalaam hao kwa kadri hali ya kifedha inavyoruhusu. Mathalani, juhudi za kuendelea kuajiri Mahakimu zinaendelea hususan wa Mahakama za Mwanzo ambako ndiko kwenye upungufu mkubwa wa Mahakimu. Kuanzia mwaka 2007 hadi mwaka 2010 jumla ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 198 waliajiriwa.

Aidha, katika kipindi hicho hicho jumla ya Mahakimu Wakazi 127 waliajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kutekeleza Mkakati huo wa Serikali imejiwekea mpango wa ajira wa muda mfupi, wa kati na mrefu wa kila mwaka. Kuanzia mwaka 2007 hadi mwaka 2010, jumla ya Mawakili 344 waliajiriwa. Aidha, Mahakama imeanza kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wenye shahada ya kwanza ya sheria ili kukidhi mahitaji katika Mahakama hizo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa katika nchi hii bado tuna tatizo kubwa sana la Mawakili wa Kujitegemea ambao huwa ni msaaada mkuwa sana katika kutatua matatizo ya kesi Mahakamani. Na kwa kuwa wanafunzi wetu ili waweze kuhitimu lazima wapiti *Law School*, lakini Serikali imekuwa haiwalipii fedha kwa ajili ya elimu hii ya vitendo. Je, Serikali ni lini itaanza kuwalipia fedha hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya hata Mkoa, na Serikali inasema imeanza kuajiri Wanasheria wenye Digrii ya Kwanza. Lakini mpaka sasa hivi ni kwamba Wanasheria wengi wenye Digrii ya Kwanza wapo bado mitaani wamezagaa wakati Serikali ina upungufu wa Mahakimu.

Je, ni kwa nini isiwaajiri Wanasheria hawa badala ya kuendelea kuadhirika mitaani?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua mahitaji katika nchi yetu ni mengi na ni makubwa. Lakini uwezo wetu wa kifedha kama nchi bado haujafikia mahala ambapo tunaweza kutekeleza yote yale tunayoyakusudia kwa wakati mmoja. Hili la kuwalipia wanafunzi wanaokuwa wamemaliza Digrii zao za Kwanza wanapokuwa mafunzoni, ni jambo zuri.

Lakini, niseme tu kwamba utekelezaji wake utaendelea kutegemea upatikanaji wa rasilimali fedha kwa kadri ambavyo mahitaji yetu yanahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira kwa Mawakili wapya ambao wanakuwa wamemaliza mafunzo yao ya uanasheria, jambo hili limekuwa likiendelea, na kama nilivyosema wakati najibu swali la Mheshimiwa Rosweeter kwamba kwa mfano mwaka huu, Mahakimu wengi wataajiriwa kwa mwaka huu wa fedha. Lakini muda wote Serikali imekuwa ikifanya hivyo kama nilivyotoa ufafanuzi kwenye jibu la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine, Serikali inatambua pia kwamba katika fani hii ya sheria ambayo mimi na Mheshimiwa Blandes wote ni Mawakili na Mawakili wa Mahakama Kuu na Mahakama zilizo chini ya hapo, ni kweli kwamba Serikali imeendelea kushirikiana na sekta binafsi na ndiyo maana kuna kile chama chetu cha Wanasheria wanaitwa Watanganyika, na upande wa Zanzibar kuna chama kama hicho ambacho kwa kushirikiana na juhudi za Serikali kwa sababu Serikali inafahamu haiwezi kuajiri wote wasomi wanaosomea fani ya sheria kwa wakati mmoja katika ajira za Umma.

Basi sekta binafsi kupitia ofisi za Mawakili zimeendelea kusaidia kutoa ajira kama ambavyo wote tumeshuhudia wakati *Tanganyika Law Society* imeendelea kufanya kazi. Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Mawakili wako wengi na kwa kuwa Tanzania kuna migogoro mingi sana ya ardhi na wananchi wanashindwa kupata huduma za kisheria. Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu kuwapeleka Mawakili katika Vijiji ili kusaidia migogoro ya ardhi na umilikishaji wa ardhi katika maeneo ya Vijiji?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kupitia ajira ya Umma na hasa Mahakama zetu kuhakikisha kwamba wananchi wanapata ushauri, huduma ya kisheria kwa kadri inavyowezekana.

Kama nilivyosema, kwa kutumia Chama cha Wanasheria, *Tanganyika Law Society*, pia chama hicho kimekuwa na utaratibu wake, zaidi ya kupitia Mawakili wenyewe kwa maana ya kutoa huduma kwa wale ambao wanaweza kumudu gharama zinazohitajika kutoa huduma hiyo kwa sababu huduma ya kisheria siyo ya bure, ni biashara kama kwingineko, lakini pia *Tanganyika Law Society* ina utaratibu wake wa kutoa huduma za bure kwa wananchi ambao kulingana na mazingira yalivyo. Lakini pia uwezo wa kuhimili gharama hizo ni mdogo, *Tanganyika Law Society* imekuwa ikitoa huduma hizo bure, na utaratibu upo mzuri.

Kwa hiyo, naendelea kumshauri Mheshimiwa Mbunge na Taifa kwa ujumla kwamba tutumie sana *Tanganyika Law Society* kwa sababu ina utaratibu huo wa kutoa huduma bure mahala ambapo panahitajika kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizopo.

Na. 297

**Mpango wa Kujenga Kiwanda cha Saruji Shinyanga**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Kulikuwa na mpango wa kujenga Kiwanda cha Saruji Mkoani Shinyanga:-

Je, utekelezaji wa mpango huo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni binafsi ya *Tancem Cement Limited* ilionyesha nia ya kujenga kiwanda cha saruji Mkoani Shinyanga. Kampuni hiyo ilikwishabainisha eneo la kujenga kiwanda lililoko Neregani na kulipa fidia kwa wananchi waliokuwa wanaishi maeneo ya karibu. Kabla ya ujenzi kuanza kampuni hiyo ilifanya upembuzi yakinifu wa kubainisha kiasi cha mashapo ya madini ya chokaa *(limestone)* ambayo yanahitajika kwa wastani wa asilimia kama 90 hivi katika uzalishaji wa saruji.

Utafiti huo ulibainisha kuwa kiasi madini hayo kilichopo katika eneo la malighafi lililoko Igusule kinatosheleza kwa uzalishaji wa *clinker* kwa muda wa kama miaka 7. Makubaliano yalifikiwa kuwa mahitaji ya ziada ya *clinker* kwa ajili ya mradi huu yangefikiwa kwa kuagiza bidhaa hiyo kutoka ndani na nje ya nchi kulingana na mahitaji kwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya utekelezaji kuanza wa mradi huo, mdororo wa uchumi uliikumba Dunia na hivyo waendelezaji wa mradi huo wakashindwa kupata mitaji waliyokuwa wanahitaji katika kuendeleza mradi huo kutoka Benki. Kufuatia changamoto hiyo, mbia mmoja kati ya watatu alijitoa katika uendelezaji wa mradi huo na wawekezaji waliobaki walishindwa kuendeleza mradi huo. Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga inafuatilia wawekezaji husika ili kujua hatima ya mradi.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Jibu nimelipokea, lakini undani wa jibu hili ni kwamba hawa wawekezaji wameshindwa. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa haraka kutafuta mwekezaji mwingine ili kiwanda hiki kijengwe kwa manufaa ya Kanda ya Ziwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; Yule mwekezaji aliyeshindwa, jibu nililolipata kipindi kilichopita maana ninauliza kwa mara ya pili juu ya kiwanda hiki. Je, itakuja jitokeza tena kwamba hakuna malighafi ya kutosha kama nilivyojibiwa kipindi kilichopita?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ulikuwa na wawekezaji watatu. Kati ya hawa, mmoja baada ya kuona kwamba hali ile imebadilika, alijitoa kabisa akarudi zake India. Wawili ni wawekezaji kutoka Kenya. Mmoja kati ya hawa inaonekana katika mawasiliano yaliyofanywa anaitwa Bwana Shah, ndiye *majority share holder*, imeonekana kwamba naye ameona kwamba uwekezaji katika mradi huu bila wenzake hauendelei. Kwa hiyo, ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Hewa kwamba katika kipindi hiki nadhani ni vizuri zaidi tukakubali kwamba wawekezaji hawa wameshindwa.

Lakini kama alivyoomba kujua, mimi nadhani ni jambo ambalo linawezekana, eneo hili likatangazwa kupitia taratibu mbalimbali ili likaonekana kwamba madini yaliyokuwepo pale, na kama nilivyosema chokaa *(limestone)* iliyoko pale kwa kiwango walichokuwa wanataka kuzalisha wao, kinatosha kwa kuzalisha kwa miaka kama sita au saba hivi.

Kwa hiyo, siyo kama madini hayapo, na kwa kawaida kwenye viwanda vya *cement* kama madini ya chokaa yamekwisha katika maeneo yale, watu wanaendeleza kwa kuleta *clinker* ambayo ni *raw*, inaletwa pale, wanachanganya na *gypsum* na biashara inaendelea.

Kwa hiyo, kama kwenye majibu ya msingi nilivyosema, *clinker* inaweza ikaletwa hata kama madini yamekwisha. Hiyo nadhani siyo sababu. Lakini soko la Shinyanga limeonekana ni zuri kwa kiwango hiki. Kwa hiyo, Mheshimiwa naomba nipokee suala hili na nitawapa wenyewe suala hilo.

Na. 298

**Wastani wa Muda wa Ndugu wa Marehemu Kupewa Maiti Muhimbili**

**MHE. ALI KHAMIS SEIF** aliuliza:-

Mgonjwa anapofika katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili na bahati mbaya akafariki dunia.

(a) Ni wastani wa muda gani ambao Ndugu wa Marehemu wanaweza wakapewa maiti yao?

(b)Je, ni taratibu gani ambazo ndugu hao wanapaswa kukamilisha ili kukabidhiwa maiti yao?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa marehemu kukabidhiwa kwa Ndugu huanzia muda wa saa 2 baada ya kifo hadi siku kumi na nne (14) kutegemeana na sababu na mazingira ya kifo.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaofariki kutokana na magonjwa ya kawaida na sababu ya kifo inafahamika, Ndugu wanatakiwa kwenda wodi alikofia Marehemu ili kuchukua kibali cha mazishi (*burial permit*) ambacho huwasilishwa chumba cha maiti kwa ajili ya kukabidhiwa mwili wa Marehemu.

Iwapo mgonjwa amefariki muda mfupi baada ya kufika Muhimbili, Daktari aliyekuwa anamhudumia hujaza fomu maalum ya kuomba mwili wa marehemu ufanyiwe uchunguzi wa kitaalam ili kubaini chanzo au sababu ya kifo *clinical post-mortem*. Ndugu wa Marehemu wakifika kwanza hupelekwa chumba cha maiti kwa ajili ya utambuzi wa mwili wa marehemu. Zoezi hili hufanyika mbele ya Daktari aliyekuwa anamhudumia mgonjwa kabla ya kufariki. Baada ya utambuzi Daktari aliyefanya uchunguzi wa kifo cha marehemu hutoa kibali cha maziko na hatimaye Ndugu hukabidhiwa mwili wa Marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo kifo kimetokana na ajali, Ndugu wanapaswa kuwasiliana na kituo cha Polisi ambacho ajali iliripotiwa. Polisi atajaza fomu *PF.99* ya kuomba uchunguzi wa kitalaam '*Medico legal post-mortem'*. Katika chumba cha maiti Ndugu hufanya utambuzi wa mwili wa Marehemu chini ya usimamizi wa Askari Polisi na Daktari aliyefanya uchunguzi.

Baada ya utambuzi Daktari aliyefanya uchunguzi hutoa kibali cha maziko na Ndugu wanaruhusiwa kuchukua mwili wa Marehemu kwa maziko.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:**Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa tarehe 23 Februari, 2011, Ndugu wa Marehemu walikwenda wodi ya Kibasila saa 12 kumwangalia Mgonjwa wao na akaelezwa kuwa amefariki bado yupo wodini, ilichukua masaa matano kumpata Marehemu huyu wakati alikuwa anaumwa ugonjwa wa kawaida.

(a) Je, Wizara inaridhika na utendaji huu wa kazi?

(b) Kwa kuwa, urasimu huu ulitokea sana pale katika wodi ya Kibasila kupeleka maiti katika chumba cha kuhifadhia maiti. Je, Serikali ipo tayari kuanzisha utaratibu wa kukabidhi maiti katika wodi badala ya kupeleka katika chumba cha kuhifadhia maiti?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mgonjwa amefariki, manesi hawaruhusiwi kuchukua kwanza maiti kupeleka *mortuary* mpaka Daktari wa wodi au Daktari wa zamu afike kuja kuthibitisha kwamba kweli mgonjwa amefariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uthibitisho ndiyo mwili wa Marehemu unapelekwa *mortuary* kwa ajili ya kwenda kuweka rekodi. Kwa sababu inatokea wakati mwingine inatokea Ndugu wa Marehemu wanachukua mwili wa Marehemu wanaondoka kabla haijarekodiwa kule *mortuary* na unakuta kwamba waliochukua maiti siyo Ndugu yao au mwili wa Marehemu usiowahusu.

Kwa hiyo, utaratibu ni kwamba mtu anayefariki ni lazima athibitishwe amefariki, maiti inapelekwa *mortuary* anakuja Ndugu anajitambulisha kwamba yeye kweli ni Ndugu wa karibu anaandikiwa *burial permit*, anakwenda *mortuary* kusaini kitabu cha kuchukua maiti kwa ajili ya kwenda kuzika, ndiyo sababu unakuta kwamba kama Daktari anakuwa na shughuli nyingi, wakati mwingine Daktari anakuwa na *admission* nyingi. Kwa hiyo, anakuwa hapati nafasi ya kuja kuthibitisha mapema ndiyo sababu mwili wa marehemu unaweza ukachukua muda mrefu pale wodini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhakikisha kwamba tunatoa maiti kutoka wodini, naomba nimwambie Mbunge kwamba hilo haliwezekani. Ni lazima mwili wa marehemu uende *mortuary* ukarekodiwe na mtu anayechukua kule *mortuary* ni nani akarekodi, ili kama kunakuwa na *disputes*, kunakuwepo na kugombania maiti basi ijulikane ni fulani kachukua na alisema yeye ni Ndugu wake wa karibu kwa kuthibitisha wodini pamoja na kule *mortuary*.

Na. 299

**Kusogeza Huduma za Afya Vijijini**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Shabaha ya Serikali katika sekta ya Afya ya Msingi MMAM ni kusogeza huduma za afya karibu na watu vijijini kwa kujenga zahanati kila Kata lakini tatizo kubwa ni upungufu mkubwa wa watalaam wa afya kama Madaktari na Wauguzi, vifaa na Watumishi wengine:-

(a) Katika kutekeleza azma hiyo nzuri ya kujenga zahanati hizo na vituo vya afya. Je, si vema Serikali ikaongeza Bajeti kwa Wizara husika ili kuwezesha utekelezaji wa mpango huo pamoja na kuboresha mishahara ya watalaam wa sekta hiyo?

(b)Katika kuleta ufanisi mzuri. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ujenzi huo uende sanjari na upatikanaji wa watalaam wa kutosha na upatikanaji wa vifaa vyote muhimu kwa kila zahanati na kituo cha afya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanzishwa kwa MMAM mwaka 2007/2008, Serikali imekuwa ikiongeza Bajeti kila mwaka kwa Wizara na sekta ya afya kwa jumla. Lengo la Serikali ni kufikia kiwango cha asilimia 15 ya Bajeti ya Serikali kutengwa kwa ajili ya sekta ya afya kama ilivyoafikiwa katika Azimio la Abuja.

Hadi kufikia mwaka 2010/2011 tumefikia kiwango cha asilimia 12. Ingawaje mwaka wa fedha 2011/12 kiwango cha Bajeti kimepungua kutokana na ufinyu wa Fedha. Hali ya mapato ya Serikali ikiwa nzuri mwelekeo utakuwa mzuri. Aidha, mishahara ya Watumishi wa Afya imeendelea kuboreshwa mwaka hadi mwaka. Hali ambayo imewavutia watalaam wengi wa afya kujiunga na Utumishi wa Umma.

(b)Katika utekelezaji wa MMAM, Wizara imeweka mikakati ya kuboresha upatikanaji wa dawa, watalaam, vifaa tiba na masuala mengine yote yanayoambatana na upanuzi wa huduma yamezingatiwa kama ambavyo anashauri Mbunge. Katika kuhakikisha upatikanaji wa watalaam wa kutosha ili kukidhi mahitaji ya MMAM, Wizara inafanya upanuzi na ujenzi wa Vyuo vya Afya kwa ajili ya kuongeza idadi ya wadahiliwa katika vyuo vya afya ambapo idadi ya wanaoingia vyuoni imekuwa ikiongezeka kutoka 3,831 mwaka 2007 hadi 5,021 mwaka 2010.

Lengo ni kufikia wadahiliwa 10,000 kwa mwaka. Hii itawezesha kupata watumishi 80,659 ifikapo mwaka 2017 kulingana na mahitaji ya MMAM. Tokea kuanzishwa kwa mpango huu, jumla ya wanafunzi 16,468 wamedahiliwa. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza namshukuru na kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Kwa kuwa, Serikali imejitahidi sana kama ambavyo Naibu Waziri ameainisha kwenye majibu yake kusomesha Watalaam wa sekta ya afya tena kwa gharama kubwa. Lakini utakuta vituo vingi vya afya na zahanati za Serikali nyingi katika nchi hii zina uhaba mkubwa sana wa watumishi wa sekta ya afya na sababu kubwa, ikiwa kwamba wengi wanaomaliza masomo yao, aidha wanajiunga na sekta binafsi ili kusaka mshahara mkubwa.

(a)Je, Serikali itakubaliana nami kwamba ili kumaliza changamoto hii sasa iweze kuleta sheria ya kuhakikisha kwamba wahudumu wote wa sekta ya afya bila kujali ni Serikali ama ni *private* wawe na marupurupu au mishahara inayolingana ili kumaliza changamoto hii?

(b) Kwa kuwa, Mkoa wa Manyara Wilaya zake zote katika zahanati na vituo vya afya vya Serikali vina uhaba mkubwa sana wa wahudumu wa sekta ya afya, na kwa udahili na masomo ambayo ameyaainisha Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kuipa kipaumbele Mkoa wetu wa Manyara ili vituo vyetu viweze kuwa na wahudumu kunusuru maisha ya Wananchi wetu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba baada ya wadahiliwa hawa kumaliza mafunzo yao, wana uhuru wa kuomba kazi mahali popote kwa sababu kwenye *private sector* na kwenye sekta ya umma wote tunamlenga mtu mmoja ambaye ni Mtanzania, kama anaona kule anakokwenda anakwenda kupata mshahara mzuri wanakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishieni kwamba kwa sasa hivi ninavyozungumza wahitimu wengi wameomba kuingia Serikalini kwa sababu kwanza kuna *Job Security* pamoja na kulipiwa pensheni, siyo sawa na kwenye *private sector*.

Kwa hiyo, wengi wanaomba kuondoka kwenye *private* sekta wanarudi kwetu kwa sababu mishahara yetu ni mizuri, mazingira ya kufanyakazi ni mazuri lakini zaidi ni motisha ya kuweza kuendelea kusoma kwa sababu kwenye kila Kanda kwenye Kanda nne za Tanzania za kiafya kuna masomo ya *continuing education.* Kwa wahitimu wa sekta zote za afya kuweza kuendelea kupata mafunzo na wanaweza kusaidiwa kulipiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba kuna upungufu mkubwa sana wa Wahudumu wa afya katika mkoa wa Manyara. Naomba nikupongeze kwa *concern* hiyo. Lakini mapungufu haya yote yapo katika Mikoa yote ya Tanzania ndiyo sababu tumekubaliana kwamba tupitie upya ile mtaala wa kufundisha ili tuweze ku-*produce* watalaam wengi kwa muda mfupi ili kila Mkoa uweze kupata watalaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *commitment* yetu kama Wizara ni kutoa mafunzo na kuhakikisha tunawapeleka kwenye Halmashauri. Lakini hatuwezi kuwafundisha kwa mwaka mmoja ila kwa kipindi cha miaka mitano tutakuwa tumezalisha zaidi ya wahudumu 80,000 na vituo vingi vitapata wahudumu.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mhehsimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa, mpango huu wa MMAMutekelezaji wake ni wa miaka kumi na sasa umeshafikia nusu ya utekelezaji wake na kwa kuwa Kata nyingi katika Wilaya nyingi nchini hazina zahanati bado, mfano Jimbo la Babati Mjini, kati ya Kata nane ni Kata mbili tu zina zahanati.

Je, Waziri haoni kwamba mpango huu unaelekea kushindwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango huu ni wa miaka kumi sawa, miaka mitano imefikia hapo. Kuna maeneo ambayo hatujajenga zahanati, lakini zahanati zinajengwa kwa ushirikiano wa wananchi pamoja na Serikali.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Gekul ukiwa kama kiongozi wa wananchi, naomba ukawahimize kule Babati ili waanze ujenzi na Serikali itakuja kumalizia na Serikali hii italeta dawa pamoja na watalaam. *(Makofi)*

Na. 300

**Hatua za Kisheria kwa Mauaji ya Vikongwe**

**MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR)** aliuliza:-

Mauaji ya Vikongwe (Wazee) yanayoendelea hapa nchini licha ya Serikali kuchukua hatua mbalimbali za kisheria dhidi ya watu wanaofanya mauaji hayo ambayo huhusishwa na imani za kishirikiana:-

Je, ni wahalifu wangapi wamechukuliwa hatua za kisheria kutokana na mauaji hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faid Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo lenye kuhuzunisha Taifa letu. mwaka 2005 hadi 2010 matukio ya mauaji ya vikongwe yaliyoripotiwa nchi nzima ni 2,575. Watuhumiwa 2,183 walikamatwa na kuhojiwa kuhusiana na mauaji hayo. Kati yao 1,599 walifikishwa Mahakamani, baadhi ya kesi zao zimekwisha na nyingine zipo katika hatua mbalimbali za kutajwa na kusikilizwa.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Ni heri kuzuia kuliko kutibu, ni nini mkakati wa Serikali kuhusu kuelimisha jamii kuhusiana na jambo hili, kwa kuwa zaidi ya vikongwe 2000 wameripotiwa kuuawa eti kwa sababu wengine wana macho mekundu? Naomba Waziri anijibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi hili ni suala ambalo kwa kweli linasikitisha na ni suala ambalo linaiwekea doa Taifa letu. Mkakati tuliokuwa nao ni kwamba hakuna mkakati uliokuwa mkubwa kama ziara aliyoifanya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda mwaka 2008 alipotembelea Kanda ya ziwa na akahimiza kwamba Kamati mbalimbali za ulinzi na usalama kuanzia katika Wilaya mpaka katika Mikoa. Lakini pia ushirikishwaji wa wananchi wote kwa ujumla na kuweza kuwafundisha na taasisi za dini mbalimbali kuwaelimisha wananchi na kuwaambia kwamba mauaji ya namna hii ambayo yanatokana na imani za kishirikina, ni imani potofu, imani ambazo zimepitwa na wakati ni mambo ambayo ni lazima tuwe tunakumbushana na ni mambo ambayo hayafai na hayaendani na wakati tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mikakati ya Serikali ipo na wananchi wote wanahusika katika kuhakikisha kwamba imani za namna hii zinakomeshwa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii. Namshukuru sana Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani kwa maelezo yake mazuri sana, hata hivyo napenda kutoa maelezo ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tutakubaliana kwamba hakuna njia muafaka zaidi ya kuwaelimisha wananchi ili waweze kuwa na mawazo ya kubadilika ili kupiga vita suala hili la mauaji ya vikongwe. Lakini nadhani kama kuna njia iliyo sahihi zaidi ni kuwapatia vijana wetu elimu iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema kuwapatia wananchi elimu bora hasa vijana, ni kwa sababu kijana ambaye ameelimika kiasi cha kutosha atakuwa anaelewa sana mahusiano yaliyopo kati ya binadamu na mazingira yanayomzunguka. Kijana ambaye ameelimika kiasi cha kutosha atakuwa anaelewa binadamu anapofikia umri wa miaka 45 viungo vyake vya mwili vingi vinapoteza uwezo wake wa asili. Macho yanaweza kubadilika rangi, meno yanapoteza uwezo wake, masikio yanapoteza uwezo wake wa kusikia na viongo vingine vya mwili kadha wa kadha vinapoteza uwezo wake wa asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi ndiyo maana nasema suala la msingi hapa tuendelee kuwapatia elimu vijana ili waweze kuelewa kwamba mabadiliko haya yanayotokea, ni mabadiliko tu ya msingi na haiwezekani kabisa kijana mwenye umri wa miaka kumi na nane au msichana mwenye umri wa miaka kumi nane macho yake yaweze kulingana na mtu ambaye ana miaka sabini au themanini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasisitiza tuendelee kuwapatia vijana elimu ya kutosha. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo mazito ya nyongeza ambayo ni elimu kubwa sana kwa Watanzania wote. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Amos Gabriel Makala, Mbunge wa Mvomero, kwa swali linalofuata.

Na. 301

**Uharibifu wa Mazao na Vifo vya Watu – DOMA**

**MHE. AMOS G. MAKALLA** aliuliza:-

Katika Kata ya Doma iliyoko mpakani mwa Mbuga za Mikumi, Tembo huharibu mazao na kusababisha vifo vya wananchi lakini fidia kwa waathirika huwa ndogo sana:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti Tembo waharibifu wasifike mashambani kwa wananchi hao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kupandisha kiwango cha fidia ya mazao na vifo vinavyosababishwa na tembo hao?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amos G. Makalla Mbunge wa Mvomero lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Maeneo mengi nchini yanakabiliwa na ongezeko la matukio ya Wanyapori waharibifu hususan Ndovu kuvamia mashamba ya wananchi na kuharibu mazao. Kata ya Doma ni miongoni mwa maeneo ambayo wananchi wake wanaathirika na uvamizi wa wanyama hao wanaoleta madhara kwa maisha ya binadamu na mali zao. Katika kukabiliana na tatizo hilo kwenye vijiji vya Kata ya Doma, Wizara ya Maliasili na Utalii imechukua hatua zifuatazo:-

(1) Serikali, kupitia Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania *(TAWIRI)* inafanya utafiti kwa kuwashirikisha wananchi na viongozi wa Vijiji vya Doma, Maharaka na Mikumi, kuhusu matumizi ya njia mbadala za kuzuia Ndovu kuharibu mashamba. Njia hizi ni pamoja na matumizi ya uzio wa kamba iliyopakwa mchanganyiko wa pilipili na oil chafu kuzunguka shamba. Njia nyingine ni matumizi ya matofali ya kinyesi cha Ndovu kilichochanganywa na pilipili ambacho moshi wake ni mkali na hivyo hufukuza wanyama hao. Njia husika zimeonesha mafanikio pale zilipotumika vizuri.

(2) Wizara ya Maliasili na Utalii inawatumia wahifadhi wa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kufukuza wanyama hao kwenye maeneo ya wananchi pale ambapo taarifa zinatolewa kwenye uongozi wa hifadhi hiyo.

(3) Serikali inaandaa utaratibu wa kutambua shoroba na mapito ya wanyamapori ili wananchi wahamasishwe kuepuka kufanya shughuli za kibinadamu ambazo zitaongeza migongano baina ya binadamu na wanyamapori katika maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepandisha viwango vinavyolipwa kwa wananchi ambao wameathiriwa na wanyamapori, kwa mujibu wa kanuni za uhifadhi wa wanyamapori za mwaka 2011 na kutangazwa na Serikali kwa tangazo namba 146 la tarehe 22 Aprili, 2011. Viwango vipya vinavyotumika kwa sasa ni kifuta jasho cha shilingi 100,000 kwa ekari moja kutokana na uharibifu wa shamba unaofanywa na wanyama hadi kiwango cha ekari tano na pia kuna kifuta machozi cha shilingi 1,000,000 pale ambapo binadamu au wananchi wameuawa na wanayama.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada ambazo amezieleza ikiwemo njia ya kupaka pilipili na hizo *oil* chafu, kasi ya ndovu kuendelea kuharibu mazao ni kubwa sana.

(a) Je, Serikali haioni kwamba inatakiwa kuongeza jitihada kuhakikisha kwamba jambo hilo linakwisha?

(b) Kwa kuwa viwango vipya sasa ni kati ya shilingi 100,000 kwa fidia ya mtu ambaye tembo amekula mazao yake na milioni moja kwa mtu ambaye ameuwawa na tembo lakini utafiti uliofanyika ni kwamba tembo mmoja akifa ni sawasawa na dola 3400 ambazo ni sawasawa na shilingi milioni 5,200,000. Hivi inakuaje binadamu akifa wanalipwa milioni moja, ukimua tembo ni milioni 5,200,000?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Makalla kwa ushirikiano ambao amekuwa akitupatia sisi kama Wizara pale ambapo matatizo haya yanatokea, amekuwa akitupigia simu kila wakati na hii imesaidia sana kwa hatua za haraka kuweza kuchukuliwa kupunguza tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tatizo la uharibifu wa wanyama hawa limeongezeka sana miaka ya karibuni kwa sababu mbalimbali zikiwemo ongezeko la binadamu na makazi, lakini vilevile mabadiliko ya tabia nchi yanayofanya wanyama wasipende kukaa kwenye maeneo yao ya asili kwa muda wote. Wizara kwa kulitambua hili kwenye mpango wetu wa bajeti tutakaowakilisha mwezi ujao tumeweka mpango wa kuanzisha *Tanzania Elephant Management Plan* ambao ni mpango wa miaka mitano utakaoshirikisha Wanasayansi wa Tanzania pamoja na wa nchi zingine nchi rafiki katika uhifadhi kuweza kuwa na mpango mpana utakaokuja na majibu ya changamoto hii ambayo inazidi kukua siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe tu pamoja na Bunge lako Tukufu kwamba mtupe nafasi, katika kipindi cha bajeti tutakayowasilisha tutakuwa na mipango ambayo itaweza kuwiana na tatizo lenyewe lilivyo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili la viwango vya fidia au viwango vya kifuta machozi, suala hili tumelizungumza mara kadhaa. Ni kwamba tunachokilipa kwa kweli ni *consolation* siyo fidia, hawa wanyama ni wa kwetu si wa mtu mwingine, ni wa Watanzania. Kwa hiyo, linapotokea tatizo, miaka ya nyuma tulikuwa tunalipa *consolation* ya shilingi 200,000 tumerekebisha Sheria mwaka 2009 na tumerekebisha Kanuni na kwa viwango vya kuanzia ambavyo tulivizungumza na kukubaliana na wadau na sio siku nyingi sana, ni mwezi wa pili Kanuni zimesainiwa, mwezi wa nne tukakubaliana kwamba walau kwa kuanzia tuanzie kulipa *consolation* ya shilingi milioni moja ambayo ni kweli haitoshi lakini kwa kutambua kwamba changamoto hii ni kubwa mimi nakubali kwamba pengine inabidi tena turudi tujaribu kuangalia namna gani tunaweza tukaboresha. Ni *consolation* siyo fidia kwa sababu maisha ya binadamu huwezi ukafidia kwa fedha.

Na. 302

**Matatizo ya Maji – Mbuga ya Wanyama Ruaha**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA** aliuliza:-

Mbuga ya wanyama ya Ruaha imekumbwa na tatizo kubwa la maji ambalo limesababisha wanyama kufa kwa kukosa maji ya kunywa na kufanya kuzorota kwa utalii maeneo hayo na kukosesha Taifa mapato:-

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chrostowaja Gerson Mtinda kama ifuatavyo:-

Ni kweli tatizo la maji ni sugu katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, kwani hutegemea zaidi chanzo kimoja ambacho ni Mto Ruaha Mkuu. Mto huu huwa na maji mengi wakati wa msimu wa mvua na hukauka haraka sana wakati wa msimu wa kiangazi. Chanzo kikubwa cha Mto huu kukauka haraka

wakati wa kiangazi ni shughuli kubwa za umwagiliaji na matumizi yasiyo endelevu ya maji kwenye vyanzo mbalimbali vya Mto huu ambavyo viko nje ya Hifadhi, kwenye maeneo ya Mikoa ya Iringa na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na matatizo haya, mwaka 2008 Hifadhi ya Ruaha ilipanuliwa kwa kuongeza maeneo muhimu kwa ajili ya kutunza Bonde la Usangu. Nia kubwa ni kuhifadhi Bonde la Usangu ili kurejesha uwezo wa Bonde hilo kuhifadhi maji ya kutosha ili kuhakikisha kuwa maji yanatiririka katika Mto Ruaha Mkuu na Mabwawa ya Mtera na Kidatu ikiwezekana kwa kipindi chote cha mwaka. Pamoja na hatua hii bado jitihada zinatakiwa kuchukuliwa ili kuwaelimisha wananchi wanaolima kwenye Nyanda za Juu za Bonde la Usangu ili watunze maji na ikiwezekana watumie kidogo itakavyowezekana. Hata kwa upande Hifadhi, Shirika la Hifadhi la Taifa *TANAPA* limeanza mkakati wa kuweka vyanzo vya maji hifadhini ikiwa ni pamoja na mabwawa ili kuhakikisha kwamba wanyama hawatoki hifadhini. Hatua kibajeti zitaanza kuchukuliwa kwenye bajeti ijayo.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Waziri amekiri wazi kuwa chanzo kikubwa cha kukauka kwa maji ya Mto Ruaha Mkuu ni shughuli za umwagiliaji lakini akasema pia kwamba wananchi waendelee kuelimishwa ili watumie kilimo cha umwagiliaji ambacho kinatumia maji kidogo.

(a) Je, Waziri haoni kwamba anapingana na ushauri wake mwenyewe badala ya kutunza maji wananchi waendelea kutumia maji kwa kumwagilia ambapo ndio sababu kubwa ya kupoteza maji?

(b) Kwa kuwa wanyama kama viboko na ndovu wanapokosa maji wakati wa kiangazi hutoka na kuvamia makazi ya wananchi na kuleta madhara makubwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi wa kuwaelimisha wananchi wa Vijiji vya Chimila, Madibila na Kapunga ambao ndio wakulima wakubwa wa mazao ya mpunga na ambao ndio chanzo kikubwa cha kumaliza maji katika Mto Ruaha ili waweze kutumia maji kiasi kwa umwagiliaji na mengine yaingie katika Mto wa Ruaha Mkuu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Christowaja Mtinda kwa maswali yake. Kimsingi ni kwamba maji yanahitajika kwa shughuli zote, yanahitajika kwa ajili ya kilimo, yanahitajika vilevile kwa ajili ya uhifadhi. Sisi kama Wizara na Serikali tunaona njia muhimu ya kufanya ni kuhakikisha tunakuwa na matumizi ambayo ni *balanced,* kutafuta hatua muhimu za msingi ambazo zitasaidia matumizi ya maji yawe ni yale yanayoendana na utunzaji wake. Yatumike kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini vilevile yanayobaki yaweze kutiririshwa kurudishwa kwenye Mto Mkuu hatimaye yaweze kutiririka kurudi hifadhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kutoa elimu, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuliona hili na ninaamini rafiki yangu Mbunge wa Mbarali, Mheshimiwa Kilufi atakuwa amesikia na wananchi wa Mbarali wamesikia kwamba tunapozungumzia suala la uhifadhi wa maji haya ni la muhimu sana kwa Taifa letu. Tutaendelea kutoa elimu na ninaamini kwamba itafika wakati wananchi wataweza kutuelewa na kutoa ushirikiano.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Sasa naomba nitumie muda huu kutoa matangazo ambayo ninayo mezani. Tangazo la kwanza Waheshimiwa Wabunge, ni wageni waliopo *Speakers Gallery* ambao ni hawa wafuatao:-

Kuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, wa kwanza kabisa ni Mrs. Kudra Maghembe, Mke wa Mheshimiwa Waziri, amefuatana na ndugu Tabu Maghembe, dada wa Mheshimiwa Waziri. Tunaye Mohamed Muya, Katibu Mkuu wa Wizara, Sophia Kaduma, Naibu Katibu Mkuu, Mbogo Futakamba, naye ni Naibu Katibu Mkuu, Emmanuel Achayo, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Ema Isinika, yeye anatoka Shirika la Chakula Duniani *FAO*. Vedasto Chatokonzina, Afisa Mwandamizi Programu katika Ofisi ya *FAO*. Tunaye pia Ndugu Thomas *Hope Good,* yeye ni Mratibu wa Mradi wa *Feed the Future* na Mwenyekiti wa *Donor Support Group* katika sekta ya kilimo. Pia wako Wakuu wa Idara za Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba wasimame wote. Wako Wakuu wa Bodi na Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika wasimame. *(Makofi)*

Vilevile wako wageni wa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Eng. Christopher Kajoro Chiza. Wa kwanza, ni Mrs. Elisafina Chiza, Mke wa Mheshimiwa Chiza, tunashukuru. Yuko Ndugu William Chiza na Goliath Chegeni Chiza. Hao ni watoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri na Mjukuu wake Chejolo Chiza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wako wageni saba wa Mheshimiwa Meshack Olopulukwa Waziri Kivuli wa Kilimo, Chakula na Ushirika ambao ni viongozi wa CHADEMA Wilaya ya Meatu, kwa umoja wao naomba wasimame. *(Makofi)*

Wako Waandishi watano na wafanyakazi watano kutoka *(Tanzania Media Fund),* Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania wakiongozwa na Ernest Sungura. Yupo Meneja Mtendaji na Ndimara Tegambwage, Mbunge Mstaafu, karibuni tunashukuru. *(Makofi)*

Wageni wengine waliofika Bungeni ni wanafunzi 15 kutoka Chuo Kikuu *St. John's Dodoma*, kuna Wanafunzi 60 na Walimu watatu kutoka Shule ya Sekondari Hijra, Dodoma, Wanafunzi 65 na Walimu kutoka Sekondari ya Dodoma, Wanafunzi 40 na Walimu wanne kutoka Shule ya *Silesian Seminar* Dodoma, Wanafunzi 50 na Walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari *City* Dodoma. Waheshimiwa Wabunge hao ndio wageni wetu tuliokuwa nao. *(Makofi)*

Kuna wageni wa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* ambao ni Viongozi wa Taifa wa Mchezo wa *Pull Table,* nao naomba wasimame kwa umoja wao wakiongozwa na Mwenyekiti Issa Togocho. Naomba wasimame kwa umoja wao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea tangazo lingine kutoka kwa Mheshimiwa Idd Azzan, Mwenyekiti wa Bunge *Sports Clubs* kwanza kabisa akitoa pongezi za dhati na za pekee kwa Kamati ya Ufundi inayoongozwa na Mheshimiwa Profesa Majimarefu ikisaidiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Peter Pinda kwa kufanyakazi nzuri siku ya shindano la tarehe 23/7 na matokeo yalikuwa kama ifuatavyo, wakati huohuo Msaidizi wa Kamati ya Ufundi Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa mgeni rasmi kwenye shindano hilo. *(Makofi)*

*Bunge Sports Club* katika bonanza la kwanza ilicheza na *NMB* na wote hawakufungana magoli yalikuwa sifuri kwa sifuri lakini *Bunge Sports Clubs* walipocheza na *Tanzania All Stars Veteran* matokeo yalikuwa ni sifuri kwa sifuri, hawakufungana. *NMB* walipocheza na *Tanzania All Stars* walifungana goli moja moja. Kwa maana hiyo, timu ya Bunge wanaume iliibuka kidedea kwa sababu wao hawakufungwa goli hata moja. *(Makofi)*

Katika Mpira wa Pete, Bunge *Sports Club* Wanawake waliichabanga na kuilaza chini *NMB* kwa magoli 19 kwa 11. Kwa hiyo, *Bunge Sports* Wanawake waliibuka kidedea na mchezaji nyota siku hiyo alikuwa Mheshimiwa Asha Jecha. *(Makofi)*

Hapa naambiwa kwamba pongezi za dhati kwa Kamati ya Ufundi na inaombwa iendelee kwa sababu ilikuwa haijatulia, ilifanya kazi nzuri. Tarehe hiyohiyo Waheshimiwa Wabunge, kulikuwa na mchezo mwingine, Mheshimiwa Said Nkumba, Mwenyekiti wa *Club* ya Wabunge ya kulenga Shabaha, anaomba kutoa matokeo ya mashindano hayo katika viwanja vya shabaha kule JKT Makutupora. Washindi wa kulenga shabaha kwa kutumia pisto walikuwa wafuatao. Wa kwanza ni Mheshimiwa Shaffin Sumar, wa pili ni Mheshimiwa Said Nkumba na wa tatu ni Mheshimiwa Jitu Soni, hao ndio walioongoza kulenga shabaha kwa pisto. Washindi wa kulenga shabaha kwa kutumia *SMG*, wa kwanza ni Muhammad Chomboh, wa pili Shaffin Shomar na wa tatu ni Mheshimiwa Jitu Soni. Waheshimiwa Wabunge hao watu ni hatari lazima kuwaangalia sana hawa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, *weekend* hii Bunge letu lilikuwa na michezo mingi, mchezo wa mwisho hapa ulikuwa ni mchezo wa *Pull Table*. Naomba niwajulishe matokeo ya washindi nyota katika mchezo wa *Pull Table* uliofanyika *Tiger Motel, Area C.* Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo, Mheshimiwa George Simbachawene aliibuka kuwa bingwa wa mchezo huo akifuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba. Sasa wameniomba baada ya kipindi cha maswali na majibu kutafanyika utaratibu wa kukabidhi zawadi zao pale nje, Mheshimiwa George Simbachawene, naomba utaratibu huu ufanyike saa saba. Usije ukavutia sana Wabunge wote wakatoka nje kushuhudia huo ubingwa wenu. Naomba tufanye saa saba kwa mujibu wa utaratibu na Kanuni za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ndio matangazo ambayo nimeyapata hapa Mezani, naomba sasa nimwite Katibu tuendelee na agenda inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo Maji na Mifugo inayohusu Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, sasa lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mwanga, tunaungana na Watanzania wenzetu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine tena kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampa heko Mheshimiwa Rais kwa kuongoza Chama cha Mapinduzi na kupata ushindi mkubwa katika Uchaguzi Mkuu wa Rais kupata asilimia 74 wa Wabunge wote wa Bunge hili na asilimia 84.5 ya Madiwani wote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ushindi huo ni kielelezo cha imani na matumaini waliyonayo Watanzania kwa uwezo alionao wa kuliongoza Taifa letu. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dkt. Ali Mohamed Shein kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.) kwa kuchaguliwa tena na wananchi wa Jimbo la Katavi na kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais na kupitishwa na Bunge hili kuwa Waziri Mkuu. Kuteuliwa kwake kunatokana na uwezo wake mkubwa na umahiri aliouonyesha katika kutenda na kusimamia kazi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Anne Semambo Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge na Spika wa Bunge letu Tukufu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai Mbunge wa Kongwa kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Nawapongeza pia wewe mwenyewe Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa ama kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Wabunge. Kuchaguliwa na kuteuliwa kwao kunatokana na uwezo wao wa kuongoza na kuaminika kwa wananchi waliowachagua na Rais aliyewateua. Katika Uchaguzi Mkuu uliopita, wananchi wamekipa tena Chama cha Mapinduzi (CCM) ridhaa ya kuliongoza Taifa hili kwa kuwachagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Wabunge wengi kutoka Chama cha Mapinduzi. Huu ni ushahidi kuwa Sera za Chama cha Mapinduzi zinakubalika na zinatekelezeka. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuzinadi Sera hizo kwa umahiri mkubwa mpaka CCM ikapata ushindi mkubwa. Kazi iliyo mbele yetu sasa ni kuzitekeleza vizuri sera hizo ili kuhakikisha CCM inaendelea kuongoza Taifa hili kwa miaka mingi ijayo. Aidha, nawapongeza Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa na kupewa madaraka hayo na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru viongozi wa ngazi za juu wa Serikali kwa kukipa kilimo msukumo mpya. Kwa mfano, Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, wakati alipozindua Bunge hili Tukufu tarehe 18 Novemba, 2010 aliainisha maeneo ambayo yataleta mapinduzi katika kilimo. Aidha, katika kipindi hicho kifupi tayari Mheshimiwa Rais alitembelea Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika; Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula; alizindua Kituo Mahiri cha Teknolojia (*Dakawa Center of Excellence);* alizindua Andiko (*Blue Print)* la Mpango wa Kilimo wa Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania- SAGCOT)* Davos, Uswisi na kuwa mgeni rasmi kwenye siku ya Ushirika Duniani. Katika shughuli zote hizo alitoa miongozo na maagizo ambayo yametupa changamoto na mchango mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Vilevile, katika hotuba zake za mwisho wa mwezi, Mheshimiwa Rais amekuwa akifafanua masuala mbalimbali kuhusu kilimo ambayo yametoa hamasa kubwa kwa wadau wa kilimo. Hii inaonyesha namna ambavyo Mheshimiwa Rais anavyotoa kipaumbele katika maendeleo ya kilimo nchini. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake wa karibu kwa Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo, Maji na Mifugo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2011/2012. Naishukuru sana Kamati kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina Taarifa ya Utekelezaji ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2011/2012 katika kikao chake kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 1 na 2 Juni, 2011. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani na pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Mwanga kwa kunichagua tena kuwa Mbunge wao katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwaka 2010. Nawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kuwashirikisha Wanamwanga wote ili kuharakisha maendeleo ya Wilaya yetu. Aidha, napenda kuishukuru familia yangu kwa kunipa ushirikiano na kuwa wavumilivu katika kipindi chote ninapokuwa katika majukumu ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kuwapongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.), Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo (Mb.), Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Stephen Masato Wasira (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, kwa hotuba zao zilizotoa ufafanuzi kuhusu Hali ya Uchumi na Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali na kuelezea kwa muhtasari hali ya kilimo chetu ilivyo hivi sasa na mwelekeo kwa mwaka ujao. Aidha, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliowasilishwa umeainisha kilimo kama mojawapo ya maeneo makuu ya kipaumbele. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge waliotumia mijadala ya hotuba hizo kutoa michango ya namna ya kuendeleza sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchango na Ukuaji wa Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo inatoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi mpana (*Broad Based Growth*) kwa kutoa ajira kwa asilimia 77.5 ya Watanzania wote na kuchangia wastani wa asilimia 95 ya chakula tunachokula nchini. Katika mwaka 2010, Sekta ya Kilimo ilikua kwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na asilimia 3.2 ya mwaka 2009. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta ndogo ya mazao ambayo ilikua kwa asilimia 4.4 mwaka 2010 ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2009. Ukuaji huo ulitokana na kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika msimu wa kilimo wa mwaka 2009/2010; kuimarika kwa miundombinu ya umwagiliaji; jitihada za Serikali za kuongeza ruzuku ya pembejeo za kilimo; na utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme-ASDP*). Ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa kiasi kikubwa ulichangia katika ukuaji wa Pato Halisi la Taifa ambalo lilikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.0 mwaka 2009. Aidha, kilimo kilichangia asilimia 24.1 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 24.6 ya mwaka 2009 ikiashiria kuongezeka kwa shughuli za kilimo zinazolenga biashara zaidi kinyume na kilimo cha kujikimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010, thamani ya mauzo ya bidhaa za mazao makuu ya biashara iliongezeka hadi Dola za Kimarekani milioni 559.0, kutoka Dola milioni 479.6 mwaka 2009, sawa na ongezeko la asilimia 16.6. Ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa lilichangiwa na kuongezeka kwa bei za mazao mbalimbali, hususan tumbaku na korosho. Mazao hayo yalichangia asilimia 41.6 na asilimia 17.3 mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya chakula kwa mwaka 2010/2011 katika mwaka 2010/2011, hali ya chakula nchini ilikuwa ya kuridhisha kutokana na uzalishaji mzuri wa mazao ya chakula katika msimu wa 2009/2010. Tathmini ya uvunaji wa mazao ya chakula kwa mwaka 2009/2010 na upatikanaji wa chakula kwa mwaka 2010/2011, iliyofanywa mwezi Desemba 2010 ilionyesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula kwa ujumla katika msimu huo ulifikia tani milioni 12.32 zikiwemo tani milioni 7.39 za nafaka na tani milioni 4.92 za mazao mengine. Uzalishaji huo ulitosheleza mahitaji ya chakula ya tani milioni 11.15 kwa mwaka 2010/2011 na kuwepo kwa ziada ya tani milioni 1.18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hali hiyo nzuri kulikuwepo na maeneo yenye upungufu. Tathmini ya kina iliyofanyika kati ya mwezi Septemba 2010 na mwezi Mei 2011, ilibaini kuwa jumla ya watu 1,484,190 walihitaji tani 36,970 za chakula cha msaada. Hadi tarehe 30, Juni 2011 jumla ya tani 30,301.9 za mahindi zilikuwa zimechukuliwa na Halmashauri husika kutoka Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* kwa ajili ya kusambazwa kwa walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza makali ya kupanda kwa bei za chakula katika soko, Serikali iliendelea na zoezi la kuuza tani 50,000 za mahindi kutoka *NFRA* kupitia wafanyabiashara wenye mashine za kukoboa na kusaga. Utaratibu huo ulihusisha mikoa 13 ya Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Dodoma, Kilimanjaro, Singida, Morogoro, Mwanza, Mara, Mtwara, Lindi, Shinyanga na Tabora. Hadi tarehe 30 Juni 2011, jumla ya tani 35,334.3 zilikuwa zimeuzwa chini ya utaratibu huo kwa mgawanyo ufuatao; Mkoa wa Dar es Salaam tani 12,196.1; Mtwara tani 2,000.0; Pwani tani 1,914.0; Shinyanga tani 2,045.0; Morogoro tani 970.0; Lindi tani 1,250; Mwanza tani 962.0; Kagera tani 468.2; Arusha tani 2,625.8; Kilimanjaro tani 3,196.6; Mara tani 2,161.8; Singida tani 850.0; na Dodoma tani 5,162.9. Serikali ilipunguza bei ya mahindi yanayouzwa na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kutoka Shilingi 38,000 kwa gunia hadi Shilingi 30,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio ya upatikanaji wa chakula mwaka 2011/2012. Kati ya mwezi Mei na Juni 2011, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya Tanzania Bara ilifanya tathmini ya awali ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula na utabiri wa hali ya chakula kwa mwaka 2011/2012. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonyesha kwamba uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia tani 12,810,818 ikilinganishwa na mahitaji ya chakula yanayokadiriwa kuwa tani 11,499,414 kwa mwaka 2011/2012. Hivyo, Taifa linatarajia kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada ya tani 1,311,404. Tathmini hii ilibaini kuwepo na ziada ya chakula katika Mikoa saba ya Rukwa, Ruvuma, Mbeya, Iringa, Kigoma, Mtwara na Kagera; utoshelezi katika Mikoa nane ya Morogoro, Lindi, Tanga, Dodoma, Singida, Tabora, Kilimanjaro na Manyara; na upungufu katika Mikoa sita ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Arusha, Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa chakula nchini, hususan nafaka kwa msimu wa kilimo 2010/2011 (chakula kinachovunwa sasa) unatarajiwa kufikia tani 6,786,600 wakati mahitaji ni tani 7,200,340 na hivyo kuwa na upungufu Kitaifa wa tani 413,740 za nafaka. Aidha, uzalishaji wa mazao ya chakula yasiyo ya nafaka (viazi, muhogo, ndizi, maharagwe, n.k.) unatarajiwa kuwa tani 6,024,217 wakati mahitaji ya Taifa ni tani 4,299,073, hivyo kuwa na ziada ya tani 1,725,143. Pamoja na ziada hiyo na kwa vile wananchi wengi hutumia zaidi vyakula vya nafaka, ni dhahiri kuwa upungufu wa nafaka wa tani 413,740 unaleta tafsiri ya upungufu wa chakula nchini. Tathmini ya awali ya upatikanaji wa chakula imebainisha pia kuwepo kwa upungufu wa chakula katika Wilaya 56 zilizo katika Mikoa 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mazao ya nafaka katika masoko makuu nchini bado iko juu licha ya kuwa huu ni mwanzo wa mavuno na licha ya juhudi za Serikali kutoa akiba kutoka kwenye maghala ya Taifa ili kukabiliana na kupanda kwa bei hizo. Kwa mfano, bei ya mahindi kwa kilo kwa baadhi ya Miji ni kama ifuatavyo: Musoma ni Shilingi 630, Moshi Shilingi 550, Mwanza Shilingi 600, Singida Shilingi 485, Arusha Shilingi 465, Tabora Shilingi 420, Dar es Salaam Shilingi 430 na Shinyanga Shilingi 500. Bei ya wastani ya mahindi ya tarehe 30 Juni ilikuwa Shilingi 430 kwa kilo, bei ya mchele kwa kilo iliongezeka kutoka Shilingi 1,040 mwezi Januari hadi Shilingi 1,225 mwezi Juni 2011 wakati bei za mazao mengine hususan maharagwe nazo zimeendelea kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya chakula Duniani na nchi jirani. Taarifa ya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* iliyotolewa mwezi Mei 2011, inaonyesha kuwa katika mwaka 2010/2011, uzalishaji wa nafaka duniani unatazamiwa kushuka kwa asilimia 1.2. Kutokana na kushuka huko takriban nchi 30 duniani zinatazamiwa kukabiliwa na upungufu wa chakula na zitahitaji chakula cha msaada.

Nyingi ya nchi hizo ziko katika kundi la nchi maskini zenye kipato kidogo za Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla mavuno pungufu hasa kwa mazao ya nafaka yanayotazamiwa katika msimu wa 2010/2011, yataathiri hali ya chakula hususan miongoni mwa jamii za wafugaji katika nchi za Afrika Mashariki. Aidha, baadhi ya nchi jirani hususan Burundi, Somalia, Kenya, Uganda, Congo (DRC), Sudan ya Kusini, Madagascar na Msumbiji zinatazamiwa kuwa na maeneo yatakayokabiliwa na upungufu wa chakula kutokana na sababu mbalimbali hasa ukame na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu huo, bei za nafaka katika maeneo hayo hususan, Kenya, Uganda, Somalia ya Kusini na Sudan ya Kusini zimeendelea kupanda kuanzia kipindi cha Januari hadi Mei 2011. Bei za juu zaidi zimeripotiwa katika masoko ya Kampala, Mogadishu, Juba na Nairobi ambako kwa ujumla bei za sasa za mahindi zimepanda kwa zaidi ya asilimia 120 ikilinganishwa na viwango vya mwezi Aprili 2011. Kwa mfano, katika soko la Nairobi bei ya mahindi imepanda kutoka Dola za Kimarekani 215 kwa tani au Shilingi 323 za Kitanzania kwa kilo, mwezi Januari hadi kufikia Dola za Kimarekani 465 kwa tani au Shilingi 744 za Kitanzania kwa kilo mwezi Juni 2011 sawa na ongezeko la asilimia zaidi ya 130. Kwa upande wa Kenya tatizo hilo limeongezeka kutokana na kuporomoka kwa thamani ya Shilingi ya Kenya na hivyo bei ya mahindi kupanda sana kwa walaji. Aidha, Serikali ya nchi hiyo imetangaza kushuka kwa uzalishaji wa mahindi kwa magunia milioni 14.8 au tani milioni 1.32. Hali hiyo ya ongezeko la bei ya mazao ya chakula hususan yale ya nafaka imechochea kwa kiwango kikubwa ongezeko la biashara ya mazao ya chakula kutoka nchini kwenda nchi hizo zenye uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na hali ya upungufu wa chakula, hususan nafaka katika mwaka 2011/2012 na kuendelea kupanda kwa bei za vyakula, Serikali inachukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuhamisha tani 115,000 za akiba ya nafaka iliyopo kwenye maghala yaliyopo Sumbawanga, Makambako na Songea kwenda kwenye maghala yaliyo karibu na maeneo yenye upungufu wa chakula ya Dar es Salaam, Dodoma, Shinyanga na Arusha. Hatua hiyo itaiwezesha Serikali kukabiliana na upungufu wa chakula na mahitaji mengine ya soko kwa haraka zaidi na pia itatoa nafasi ya kuhifadhi nafaka zitakazonunuliwa msimu wa ununuzi wa 2011/2012;

(ii) Kuiwezesha *NFRA* kununua tani 200,000 za nafaka kutoka kwa wakulima wa Mikoa ya Rukwa, Iringa, Mbeya na Ruvuma;

(iii) Kuiwezesha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kununua tani 16,000 za mazao (kwa kuanzia) kutoka kwa wakulima wa mikoa ya Rukwa, Kigoma, Iringa, Mbeya, Ruvuma na Morogoro na kuyauza katika Mikoa yenye upungufu wa chakula. Manunuzi hayo yatatumia fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012 na mikopo kupitia taasisi za fedha;

(iv) Kuhimiza wananchi kutumia aina mbalimbali za vyakula ikiwa ni pamoja na muhogo, viazi vitamu, viazi mviringo, ndizi na vyakula vingine ambavyo vinapatikana kwa wingi katika maeneo yao; na

(v) Serikali imeagiza Mikoa na Halmashauri za Wilaya zenye upungufu wa chakula kuongeza upatikanaji wa chakula katika maeneo yao kwa kuhamasisha wafanyabiashara wenye uwezo wa kununua chakula kutoka Mikoa yenye ziada na kuuza kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na bei nzuri ya mahindi na mpunga na mazao mengine ya chakula kwa wakulima, wakulima wengi wanauzia mazao yao shambani na kuna hatari ya kuuza mavuno yote bila ya kujiwekea akiba. Hivyo, Serikali inawahimiza wananchi wote katika ngazi ya kaya hususan wakulima kujiwekea akiba ya chakula cha kutosha kwa ajili ya mahitaji ya kaya zao mpaka msimu ujao. Aidha, ili kuepuka hatari ya Taifa kukumbwa na tatizo la upungufu wa chakula, Serikali imefuta vibali vyote ambavyo vilikwishatolewa kwa ajili ya kusafirisha mazao ya chakula nje ya nchi na kusitisha uuzaji wa mazao hayo nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 6, kuanzia tarehe 1 Julai, 2011 hadi tarehe 31 Desemba, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ushirika nchini, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kuimarisha Ushirika kupitia utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini (*Cooperative Reform and Modernization Program –CRMP)*. Vyama vya Ushirika viliendelea kufanya vizuri kwa kutoa huduma mbalimbali zikiwemo ununuzi wa mazao na usambazaji wa pembejeo kwa wanachama wake na jamii kwa ujumla. Hadi kufikia Machi 2011, kulikuwa na jumla ya Vyama vya Ushirika 9,397 vikiwemo Vyama vya Msingi 9,316, ambavyo vipo katika mchanganuo ufuatao: Ushirika wa Mazao *(Agricultural Marketing Cooperative Societies - AMCOS)* 2,811, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) 5,251, Umwagiliaji 108, Mifugo 158, Uvuvi 112, Nyumba 30, Madini 58, Viwanda 178, Walaji 102, Huduma 214 na aina nyingine za Vyama vya Ushirika 293. Aidha, kuna Vyama Vikuu 41, Benki za Ushirika mbili, Chama Kilele kimoja, Shirikisho la Vyama vya Ushirika na miradi 36 ya Pamoja ya Ushirika (*Joint Enterprises*). Idadi ya wanachama wa vyama vyote hivyo iliongezeka kutoka wanachama 2,100,000 mwaka 2009/2010 na kufikia 2,244,727 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, mitaji ya Vyama vya Ushirika kwa ujumla ukiondoa *SACCOS* ilifikia Shilingi bilioni 7.01 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 4.32 za mwaka 2009/2010. Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo vilikuwa na mtaji wa kukopesha (hisa, akiba na amana) wa Shilingi bilioni 236.80 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 211.30 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 12. Aidha, mikopo iliyotolewa kwa wanachama iliongezeka kutoka Shilingi bilioni 463.40 hadi Shilingi bilioni 539.20 katika kipindi hicho ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 16. Mikopo iliyotolewa ilitumiwa katika shughuli za biashara, kilimo, viwanda vidogovidogo, ufugaji, ujenzi wa nyumba, karo za shule, ununuzi wa matrekta madogo (*power tillers*), matrekta makubwa na pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji mwaka 2010/2011, Fungu 43, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kwa mwaka 2010/2011, ilikadiria kukusanya mapato ya kiasi cha Shilingi bilioni 1.438 kutokana na vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na malipo ya hati za ukaguzi wa usafi wa mazao ya kuuzwa nje ya nchi na yanayoingizwa nchini; uandikishaji wa madawa ya kilimo; na malipo ya zabuni mbalimbali. Hadi tarehe 30 Juni, 2011, kiasi cha Shilingi bilioni 2.234 sawa na asilimia 155 ya makadirio kilikuwa kimekusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kupitia Fungu 43 ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 253.35. Aidha, Wizara ilipokea fedha za nyongeza kutoka Hazina Shilingi bilioni 57 kwa ajili ya ununuzi na usafirishaji wa nafaka kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula na Shilingi bilioni 4.337 kwa ajili ya deni la mbolea ya Minjingu na hivyo kufanya bajeti ya Fungu 43 kufikia jumla ya Shilingi bilioni 314.690. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 210.738 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni 103.952 ni fedha za Maendeleo. Kati ya fedha za Maendeleo, Shilingi bilioni 3.416 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 100.535 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi tarehe 30 Juni, 2011 fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa kutoka Hazina ni Shilingi bilioni 179.76 sawa na asilimia 85.30 ya kiasi kilichoidhinishwa. Matumizi yalifikia Shilingi bilioni 178.57 sawa na asilimia 99.35 ya kiasi cha fedha kilichotolewa. Aidha, fedha za Bajeti ya Maendeleo zilizotolewa ni Shilingi bilioni 93.88 sawa na asilimia 90.30 ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa. Jumla ya Shilingi bilioni 90.59 zilitumika sawa na asilimia 96.49 ya fedha zilizotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa azma ya Kilimo Kwanza. Azma ya Kilimo Kwanza katika Sekta ya Kilimo inatekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP)* na Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika *(CRMP).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo inatekelezwa katika ngazi ya Wilaya kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Plans-DADPs*) na katika ngazi ya Kitaifa kupitia Wizara za Sekta ya Kilimo na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya – *DADPs*. Katika mwaka 2010/2011, Wizara za Sekta ya Kilimo ziliendelea kuimarisha utekelezaji wa *ASDP* katika ngazi ya Wilaya kwa kuboresha Mwongozo wa kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) kwa kuongeza masuala yanayohusu mazingira, elimu ya biashara, matumizi na usimamizi wa fedha za Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya (*District Irrigation Development Fund – DIDF*).

Aidha, mafunzo yalifanyika kwa Timu za Wawezeshaji wa Wilaya na Waratibu wa *ASDP* wa Mikoa kwa ajili ya kuboresha uandaaji wa *DADPs*. Moja ya mafanikio ya mafunzo hayo ni ongezeko la miradi ya umwagiliaji iliyoombewa fedha kutoka *DIDF* kutoka miradi 262 mwaka 2010/2011 hadi 358 mwaka 2011/2012. Kati ya miradi 358 iliyoombewa fedha, miradi 136 imetengewa fedha katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilisimamia utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji iliyoibuliwa na wakulima na kujumuishwa katika *DADPs*. Aidha, wataalam katika Kanda za Umwagiliaji waliendelea kutoa ushauri wa kitaalam wa utayarishaji, usanifu na usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji iliyojumuishwa kwenye mipango hiyo. Kutokana na ushauri huo skimu 113 zilizosanifiwa zilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 31.107 kutoka *DIDF* kwa utekelezaji. Hivi sasa miradi hiyo ya *DADPs* iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi mingine iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kilometa 150 za barabara za vijijini; mabwawa 18; masoko 10 ya mazao na masoko matatu ya mifugo; maghala 31 ya kuhifadhi mazao; machinjio matano na mabanda matatu ya kuanikia ngozi. Vilevile, mashine za kukoboa nafaka 26, kahawa tatu na 31 za kukamulia mafuta zilitolewa kwa wakulima kwa mfumo wa kuchangia gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya matrekta madogo ya mkono (*power tiller*) 430 na matrekta makubwa 42 yalinunuliwa na Halmashauri na kusambazwa kwa vikundi vya wakulima kwa utaratibu wa uchangiaji wa asilimia 20 ya gharama (*cost sharing arrangement*). Aidha, mafunzo mbalimbali kwa wakulima na wafugaji yalitolewa ikiwa ni pamoja na mafunzo ya uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa Wakulima 34,685; ufugaji bora kwa wafugaji 5,590 na masuala ya masoko na usindikaji kwa wakulima na wafugaji 39,158. Vilevile, mashamba darasa 1,630 na vituo vya mafunzo tisa (9) viliendelezwa. Pia Vituo vya Taaluma vya Kata (*Ward Agricultural Resource Centres – WARCs*) 21 vilijengwa na Maafisa Ugani 5,814 walipatiwa mafunzo mbalimbali ili kuboresha utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara za Sekta ya Kilimo ziliendelea kuboresha Takwimu za Kilimo (*Agricultural Routine Data System*) kwa kufanya majaribio katika Wilaya za Morogoro Vijijini na Kilosa Mkoa wa Morogoro na Wilaya za Mpwapwa na Kondoa katika Mkoa wa Dodoma na kuunganishwa na mtandao wa kompyuta wa *Local Government Monitoring Database System - LGMD2.* Lengo ni kuwezesha upatikanaji wa takwimu na taarifa za kupima utekelezaji wa *ASDP*. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa Maafisa Ugani 546 wa Vijiji na Kata, 29 wa Wilaya na wanne wa Sekretarieti za Mikoa hiyo ili waweze kutumia mfumo huo. Mfumo huo ukionyesha mafanikio utaenezwa katika Mikoa na Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo Wilayani (*District Agricultural Sector Investment Project – DASIP)* ambao unatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya 28 za Mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga unatumia mfumo wa *DADPs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Mradi wa *DASIP* ulitoa mafunzo kwa wataalam 168 wa Wilaya na 10 wa Mikoa kuhusu kuandaa na kutekeleza *DADPs* yaliyowezesha Vijiji 780 kuibua miradi na kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Vijiji hivyo. Kutokana na mafunzo hayo, jumla ya miradi 291 ya kilimo iliibuliwa na jamii. Miradi hiyo ni pamoja na majosho 24, mabanio ya mifereji nane, maghala 23, masoko 23, Malambo 18, barabara za Vijijini 45 zenye jumla ya urefu wa kilomita 110. Miradi mingine iliyotekelezwa ni pamoja na machinjio 21, mabwawa ya kufugia samaki 17, mabirika ya kunywea maji mifugo 11, pampu ya kusukuma maji kwa njia ya upepo moja, vituo vya kukobolea kahawa 13, vituo vya afya na huduma za mifugo vitatu, Vituo vya Taaluma vya Kata vitatu, vituo vya kufundishia wanyamakazi vinne, pampu za umwagiliaji 28, zana za kupandia na kupalilia 25, vituo vya uhamilishaji vitatu na miradi ya hifadhi ya mazingira 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, jumla ya matrekta madogo *(power tillers)* 300 yalinunuliwa na kusambazwa kwa vikundi 300 vya wakulima katika Wilaya 17 ambavyo vilichangia asilimia 20 ya gharama. Katika kuhakikisha matrekta hayo yanaendeshwa kwa ufanisi na kwa faida, mafunzo yalitolewa kwa wataalam 35 wa zana za kilimo katika Wilaya zilizopata matrekta hayo kwa lengo la kuelimisha wanavikundi walionufaika na matrekta hayo. Mafunzo pia yalitolewa kwa ajili ya kuandaa mipango biashara kwa vikundi hivyo ili matrekta hayo yarudishe gharama za ununuzi na kuzalisha faida. Vilevile, vikundi 3,007 vilivyohitimu mafunzo ya shamba darasa msimu wa 2009/2010, vilipatiwa mafunzo ya kuandaa mipango biashara ili kuviwezesha kuzalisha kwa ufanisi na kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia *DASIP*, jumla ya skimu za umwagiliaji 27 zilifanyiwa usanifu wa awali mwaka 2010/2011. Kati ya skimu hizo, skimu 23 zilifanyiwa usanifu wa kina na skimu 20 kati ya hizo ujenzi utaanza mwaka 2011/2012. Skimu hizo ni Ishololo (Shinyanga Vijijini), Kahanga (Kahama), Mwasubuya (Bariadi), Mwagwila (Meatu), Nyenze (Kishapu), Masinono (Musoma), Nyamitita (Serengeti), Kisangwa (Bunda), Lutubiga (Magu), Sukuma (Sengerema), Miyogwezi (Ukerewe), Lwenge (Geita), Luhala (Kwimba), Nyisanzi (Chato), Mwiruzi (Biharamulo), Kyakakera (Misenyi), Kyamyorwa (Muleba), Kabanga (Kasulu), Mgondogondo (Kibondo) na Mkuti (Kigoma Vijijini). Skimu zote 20 zitakapokamilika zitakuwa na uwezo wa kumwagilia hekta 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji (*National Irrigation Master Plan*) wa mwaka 2002. Mkazo uliwekwa katika utayarishaji, usanifu, usimamiaji wa ujenzi, ukarabati wa skimu za umwagiliaji na mabwawa. Aidha, uhamasishaji wa matumizi ya maji chini ya ardhi na teknolojia za umwagiliaji zenye ufanisi katika matumizi ya maji zilipewa msukumo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya umwagiliaji na ujenzi wa mabwawa. Katika mwaka 2010/2011, Wizara ilijenga na kukarabati skimu 47 zenye eneo la hekta 14,200 ikilinganishwa na lengo la hekta 18,000 na hivyo kuongeza eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 331,490 mwaka 2009/2010 hadi hekta 345,690 mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Juni 2011, ujenzi wa mabwawa mawili ya Kahama Nhalanga (Nzega) yenye uwezo wa kumwagilia hekta 500 na Maliwanda (Musoma Vijijini) hekta 100 ulikamilika. Mabwawa mengine sita ya Lwanyo (Mbarali) hekta 1,000; Inala (Tabora Manispaa) hekta 400; Misozwe (Muheza) hekta 100; Mahiga (Kwimba) hekta 242; Mwangeza Iramba hekta 400; na Mesaga (Serengeti) hekta 250 yanaendelea kujengwa na yanatarajiwa kukamilika mwaka 2011/2012. Matarajio kutoka ujenzi wa skimu hizo na mabwawa hayo ni kuongeza eneo la umwagiliaji na uzalishaji wa mpunga, mahindi na mazao ya bustani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ililenga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu za umwagiliaji zenye ukubwa wa hekta 95,000 kwenye kanda zote saba za umwagiliaji nchini. Hadi kufikia mwezi Juni 2011, usanifu ulikamilika katika skimu 25 zenye eneo la hekta 54,010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia za umwagiliaji zenye ufanisi na tija. Katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kuwahamasisha wadau katika matumizi ya teknolojia za umwagiliaji kwa njia ya matone (*drip irrigation systems*) katika maeneo yote yenye maziwa, mito na yenye uwezekano wa kupata maji chini ya ardhi. Vilevile, uhamasishaji ulihusu matumizi ya pampu za kusukuma maji kwa miguu, upepo, mionzi ya jua na nishati ya mafuta kwa ajili ya kusukuma maji kwa matumizi ya umwagiliaji. Aidha, Wizara iliendelea kusimamia uanzishaji na upanuzi wa mashamba yanayotumia teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone kwa kutumia maji chini ya ardhi katika skimu ya Kisasida (Singida Mjini) yenye hekta 150 kwa kilimo cha mbogamboga na Chinangali (Chamwino) yenye hekta 120 kwa kilimo cha mizabibu. Umuhimu zaidi unatolewa katika kutumia kilimo cha umwagiliaji kwa njia ya matone kutokana na maji yanayosukumwa kwa kutumia nishati ya jua. Aidha, faida ya teknolojia hizo za umwagiliaji ni kutumia maji kwa ufanisi zaidi; kuongeza tija na uzalishaji; kuongeza misimu ya kilimo kwa mwaka; na kuweza kulima mazao mengi kwa mzunguko (*crop rotation*). Utaratibu huo unawahakikishia wakulima usalama wa chakula na kuongeza pato la kaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilihamasisha matumizi bora na endelevu ya maji kwa umwagiliaji kupitia maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Sabasaba na Sikukuu ya Wakulima (Nane Nane). Lengo lilikuwa kuonesha aina mbalimbali za mifumo ya umwagiliaji yenye kutumia maji kwa ufanisi zaidi na tija katika uzalishaji wa mazao. Kadhalika fursa za kutumia nishati mbadala za upepo na jua katika kuendesha pampu za kusukuma maji kwa ajili ya umwagiliaji zilioneshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kuratibu na kutoa huduma za kitaalam kwa Halmashauri za Wilaya katika kuandaa na kusimamia utekelezaji na uendeshaji wa skimu 113 za umwagiliaji zilizotengewa fedha kutoka Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji Ngazi ya Wilaya (*DIDF*) na 47 zilizotengewa fedha kutoka Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji Ngazi ya Taifa (*NIDF*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilishirikiana na Taasisi zinazotoa elimu ya juu ambazo ni Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji (*Water Development Management Institute - WDMI*) na Chuo cha *St. Joseph College of Engineering (SJCE)* kuandaa mitaala ya ufundishaji wa kozi za umwagiliaji ngazi za Vyeti, Stashahada na Shahada. Kukamilika kwa mitaala hiyo kutawezesha taasisi hizo kutoa wataalam wenye uelewa wa kina wa fani ya umwagiliaji. Chuo cha Ufundi cha Arusha tayari kimeanza kufundisha wanafunzi 25 ngazi ya Shahada baada ya kukamilika kwa mitaala ya ufundishaji wa kozi za umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili ya mradi wa ushirikiano wa kitaalam kati ya Tanzania na Japan (*Tanzania Japan Technical Cooperation Project-TCP*) itakayokuwa ya muda wa miaka mitatu imeanza kutekelezwa. Mradi huo umefuatia kukamilika kwa awamu ya kwanza iliyowezesha uandaaji wa miongozo ya kitaalam ya kutekeleza miradi ya umwagiliaji kupitia *DADPs*. Awamu ya pili itahusisha kufundisha namna ya kutumia miongozo hiyo kwa kutumia skimu saba za umwagiliaji za mfano zilizochaguliwa kutoka kila kanda ya umwagiliaji. Skimu hizo ni Mvumi (Kilosa); Kivulini (Mwanga); Bahi-Sokoni (Bahi); Inala (Tabora Manispaa); Mahiga (Kwimba); Mshewe (Mbeya); na Narunyu (Lindi Vijijini).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilianza kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais kupitia tamko alilolitoa tarehe 2 Februari 2011 la kuundwa kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itakayokuwa chombo maalum cha kuendeleza na kusimamia masuala ya umwagiliaji nchini. Katika mwaka 2010/2011, Wizara ilikusanya maoni ya wadau mbalimbali kuhusu muundo, majukumu na vipengele muhimu vitakavyotumika katika kuandaa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya kuanzisha Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa kilimo katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kuimarisha huduma za utafiti ambazo ziliwezesha kubuni teknolojia bora za kumwezesha mkulima kuongeza uzalishaji wa mavuno na tija. Utafiti huo ni pamoja na mbegu bora, rutuba ya udongo na ushauri wa mifumo ya kilimo na uchumi jamii. Wizara kupitia *ASDP* iliimarisha Mifuko ya Utafiti na Maendeleo ya Kanda *(Zonal Agricultural Research Development Fund-ZARDEFs*) na usimamizi wa utafiti kwa kutumia mfumo unaowalenga wadau *(Client Oriented Research and Development Management Approach-CORDEMA)*. Katika mwaka 2010/2011, kupitia *ZARDEFs*, miradi 123 ya utafiti iliendelea kutekelezwa. Kati ya hiyo, miradi 12 ilikamilika na usambazaji wa matokeo kwa walengwa unaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kupitia vituo vyake vya utafiti ilitoa aina mpya 21 za mbegu za mazao zenye sifa zaidi ya zile zinazotumiwa na wakulima kwa sasa. Mbegu hizo ni kahawa Robusta (4) na Arabica (1), viazi vitamu (2), dengu (4), soya (1), nyanya (2), figiri (2), mnavu (2), ngogwe (1) na mchicha (2). Mbegu hizo ziliidhinishwa kitaifa kwa ajili ya matumizi ya wakulima. Aidha, kampuni binafsi iitwayo *Pioneer Hybrid Seed Ltd.* ilifanya majaribio ya mbegu ya mahindi aina ya P2859 kuhusu ustawi wa mbegu hiyo katika mazingira ya Kitanzania ambapo Kamati ya Taifa ya Mbegu iliridhika na matokeo na kuidhinisha matumizi yake nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilizalisha jumla ya tani 25.92 na vipingili 450,000 za mbegu mama *(Breeders' seed*) za mbegu bora ili kukidhi mahitaji ya Wakala wa Mbegu za Kilimo (*Agricultural Seed Agency - ASA*) kuweza kuzalisha mbegu za msingi. Hatua hiyo inalenga kuhakikisha kuwa mbegu bora zinawafikia wakulima. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya katika Mikoa ya Mtwara na Lindi kupitia vikundi vya wakulima, ilizalisha tani 65 za mbegu za Daraja la Kuazimiwa (*Quality Declared Seeds - QDS*). Kati ya hizo tani 35 ni za karanga na tani 30 za ufuta. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Lushoto na Babati kupitia vikundi vya wakulima ilizalisha mbegu za maharagwe aina ya Lyamungo85 tani 3 na Lyamungo90 tani 2.45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilifanikiwa kubuni mbinu za uzalishaji wa mazao ambazo zitaongeza tija. Teknolojia hizo ni pamoja na zile za kutumia mbinu endelevu za kupunguza matawi na kuelekeza mizabibu (*pruning and training of grapes*) na kupelekwa kwa wakulima wa Kanda ya Kati. Katika zao la korosho utafiti umependekeza kwa wakulima dawa aina ya *Weedall* na *Kalachi* zenye nguvu za kuua magugu aina zote katika mashamba ya mikorosho. Aidha, Wizara imetathmini na kupendekeza aina tatu za dawa ya *Bayfidan, Timefon na Falmenol* pamoja na Salfa ya maji aina ya *Uganoll 580 WP.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa wakulima wa zao la migomba wanakuwa na ndizi katika kipindi chote wakati wanaendelea kudhibiti ugonjwa wa mnyauko, utafiti umependekeza utaratibu wa kung'oa migomba yenye ugonjwa na kupandikiza migomba mipya kwa awamu (*Sequential Uprooting and Replanting)* ambao umeonyesha kuwa unarudisha uhai wa shamba la migomba bila kukosa mazao kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti magugu, magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea na mazao, Wizara ilitoa teknolojia za matumizi ya madawa ya asilia, madawa ya madukani na udhibiti husishi. Baadhi ya matokeo ya utafiti huo ni matumizi ya Muarobaini na Dawa ya *Carbofuran 5G* katika kupunguza mashambulizi ya fukuzi kwenye migomba na matumizi ya dawa aina ya '*Amistar 330EC'* kudhibiti magonjwa ya majani kwenye ngano na shayiri. Vilevile, utafiti uliofanyika katika zao la korosho ulionyesha kuwa dawa aina ya *Weedall* na *Kalachi* zina nguvu za kuuwa magugu aina zote katika mashamba ya mikorosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, ili kupunguza matumizi ya madawa ya viwandani, gharama za matumizi ya madawa pamoja na kuhifadhi mazingira, utafiti umetathmini na kupendekeza matumizi ya manyigu (*Diadegma sp*.) ili kudhibiti nondo mwenye mgongo wa almasi (*Diamond back moth)* ambaye anashambulia zao la kabeji. Teknolojia hiyo imepokelewa na kuleta mafanikio kwa wakulima wa Arumeru na Lushoto. Aina mpya 361 za nasaba za mimea zilikusanywa ambazo ni pamoja na aina 200 za migomba, aina 24 za muhogo, aina 50 za kunde, aina 20 za mbaazi na aina 17 za soya. Pia aina 50 za nasaba za viungo zilihifadhiwa. Aidha, aina mpya ya mgomba ijulikanayo kama *East African Highland Bananas* '*Sensu Lato'* ambayo ni tofauti na aina zingine za "*East African Highland Banana* '*Sensu Stricto'* ilitambuliwa na hivyo kuongeza idadi ya nasaba zinazojulikana duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa mifumo ya kilimo na uchumi sayansi jamii, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kufanya utafiti wa kutathmini gharama na mapato yanayoweza kupatikana katika kilimo cha mazao mbalimbali katika maeneo tofauti. Matokeo yanaonesha kuwa faida anayopata mkulima inaongezeka kama akitumia pembejeo kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo. Kwa mfano, wakulima wa mpunga wa Kanda ya Ziwa waliopanda mbegu bora za mpunga na kufuata ushauri wa kilimo bora, walipata faida ya Shilingi 1,407,000 kwa hekta wakati wale ambao hawakutumia mbegu bora na bila kufuata kanuni bora walipata faida ya Shilingi 639,200 tu ikiwa ni pungufu kwa Shilingi 767,800 ambayo ni pungufu zaidi ya asilimia 100. Kwa upande wa kilimo cha mahindi faida inayoweza kupatikana ni Shilingi 516,100 kwa hekta kwa kutumia pembejeo zilizopendekezwa, ikilinganishwa na Shilingi 367,000 kwa wale wasiotumia pembejeo zilizopendekezwa kikamilifu. Mwelekeo huo unaonekana kwenye mazao mengine kama pamba, kahawa, mtama, korosho, ufuta na alizeti. Matokeo hayo yanaonyesha kuwa matumizi ya teknolojia bora na kuzingatia kanuni za kilimo bora yana faida kubwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha Vituo na kuimarisha uwezo wa Watafiti katika mwaka 2010/2011, Wizara ilifanya ukarabati wa nyumba 13 za watumishi katika Vituo vya Makutopora, Ukiriguru, Uyole, Naliendele, Tumbi, Ilonga na Maruku na ujenzi wa nyumba mpya Seliani. Aidha, vituo vitano vya Utafiti vya Tumbi, Mikocheni, Uyole, Naliendele, Selian na Makutopora, vilipatiwa samani za ofisi ikiwa ni pamoja na viti, meza na kabati. Vilevile, ulifanyika ununuzi wa magari matatu kwa ajili ya Vituo vya Mlingano na Makao Makuu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ilikamilisha ujenzi wa Kituo cha Utafiti na Mafunzo kwa Wakulima Dakawa, Morogoro. Kituo hicho kilifunguliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 2 Aprili, 2011. Kituo kitakuwa na kazi zifuatazo: kuonyesha teknolojia za Kitanzania na Kichina; kutoa mafunzo kwa wakulima ikiwa ni pamoja na ujasiriamali kwenye kilimo cha mbogamboga, mahindi na ufugaji wa kuku wa kisasa; kuzalisha miche kwa njia ya Tishu (*Tissue Culture);* na kufanya utafiti kwa mazao ya mahindi, mpunga na mazao ya mbogamboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kuimarisha Kituo cha KATRIN ili kukipandisha hadhi ya kuwa Kituo Mahiri cha Utafiti (*Centre of Excellence*) kwa zao la mpunga. Kituo hicho kimepatiwa vitendea kazi kupitia Programu ya Kilimo ya Kuendeleza Tija na Uzalishaji katika Afrika ya Mashariki (*Eastern Africa Agricultural Productivity Programme*). Aidha, kupitia programu hiyo, Vituo vya Dakawa, Uyole, Ukiriguru na Mikocheni vimenufaika kwa kupatiwa vitendea kazi vikiwemo magari manne, mashine

za kurudufia 13 na kompyuta 29. Serikali itawekeza zaidi katika vifaa vya maabara, mafunzo kwa wataalam na nyenzo za utafiti katika kukitayarisha Kituo cha KATRIN ili kifikie matarajio ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara iligharamia mafunzo kwa watafiti kwa lengo la kuwajengea uwezo. Jumla ya watafiti 20 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Shahada ya Uzamili na Uzamivu. Kati ya hao watafiti 11 ni wa Shahada ya Uzamili (*MSc*) na watafiti tisa (9) ni wa Shahada ya Uzamivu (*PhD*). Vilevile, Watafiti 45 walipata ufadhili wa mafunzo kupitia fedha zilizotengwa kuimarisha uwezo wa Watafiti kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*). Kati ya hao Watafiti 33 ni wa Shahada ya Uzamili na 12 ni wa Shahada ya Uzamivu. Watafiti wengine 20 walipata mafunzo ya muda mfupi ya mbinu za utafiti (*research methodologies*) na wengine 40 walipata mafunzo katika fani ya Uandishi wa Tungo (*Winning Proposal Writing*). Pia, Watafiti Wachumi 35 walipata mafunzo ya wiki moja ya jinsi ya kufanya uchambuzi wa mnyororo wa thamani ya mazao (*value chain analysis*) na jinsi ya kufanya uchambuzi wa upokeaji wa teknolojia na matokeo yake (*Adoption and impact analysis*) kwa kutumia programu ya kompyuta ijulikanayo kama *Data Analysis and Statistical Software (STATA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ikishirikiana na TAMISEMI iliendelea kuimarisha Huduma za Ugani kwa wakulima kwa kutumia mbinu shirikishi jamii katika kilimo, hususan Shamba Darasa. Wizara ilitoa mafunzo rejea ya Wakufunzi Wawezeshaji (*Training of Trainers-TOT*) wa Shamba Darasa kwa Maafisa Ugani 73 kutoka Halmashauri 40 za Mikoa ya Mara, Mwanza, Kigoma, Kagera, Tabora na Shinyanga. Aidha, kupitia Programu ya Kilimo ya Kuendeleza Tija na Uzalishaji (*Eastern Africa Agricultural Productivity Programme- EAAPP*), Tanzania ikiwa ni kinara katika kilimo cha mpunga, Wizara ilitoa mafunzo ya Wakufunzi Wawezashaji katika kilimo cha mpunga kwa Maafisa Ugani 100 kutoka Halmashauri 20 za Igunga, Nzega, Bahi, Bagamoyo, Rufiji, Kilombero, Mvomero, Kilosa, Kahama, Shinyanga, Sengerema, Misungwi, Kwimba, Bukombe, Maswa, Kibondo, Magu, Mbarali, Kyela na Iringa ambayo yalifanyika *Kilimanjaro Agricultural Trainning Center (KATC)*. Pia ziara za mafunzo zilifanyika kwa wakulima 40 na Maafisa Ugani wanne kutoka Halmashauri za Mvomero, Mwanga na Moshi. Wakulima kutoka Kilombero na Mwanga walitembelea wakulima wenzao katika skimu za umwagiliaji za Mkindo na Lower Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliboresha Mwongozo wa kuanzisha na kuendesha Vituo vya Taaluma vya Kata (*Ward Agricultural Resource Center - WARC)* na kutoa toleo la pili ambalo lilifafanua zaidi matumizi ya *WARCs* na namna ya uendeshaji wa vituo hivyo kwa kushirikisha Sekta binafsi. Aidha, Wizara iliwezesha wakulima 593,400 kupata mafunzo ya kilimo bora na taarifa mbalimbali zikiwemo bei za mazao katika vituo hivyo kwa kuandaa mashamba ya majaribio na kutoa machapisho kupitia Ofisi za Kiungo za Kanda za Utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kuimarisha mfumo wa mkulima kufundisha mkulima (*Farmer-to-Farmer Extension*) kwa kutoa mafunzo kwa wakulima 26,400 ambao wanaendelea kuwafundisha wakulima wenzao mbinu bora za kilimo. Aidha, elimu ilitolewa kwa wakulima kupitia vipindi vya redio, vijitabu, machapisho, vipeperushi, mabango na kuonyesha sinema Vijijini kwa kuzingatia kanda za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI iliajiri vijana ambao ni Wagani tarajali 742 na hivyo kufanya idadi ya Maafisa Ugani kufikia 5,181. Kati ya hao, wataalam 64 wana Shahada ya Uzamili (MSc.), 475 wana Shahada ya Kwanza (BSc.), 4,100 wana Astashahada (Diploma) na 542 wana Cheti (*Certificate*). Mahitaji ya wataalam katika ngazi ya Kata na Vijiji ni 15,082. Pia, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI ilianzisha mchakato wa kuweka vigezo vya kupima utendaji kazi wa Maafisa Ugani wa ngazi ya Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliratibu na kushiriki maadhimisho ya Nane Nane ambayo yalifanyika kitaifa Mkoani Dodoma kwenye Uwanja wa Nzuguni. Kauli mbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa "*Kilimo Kwanza*, *Mapinduzi ya Kijani, Uhakika wa Chakula na Kipato*". Katika maadhimisho hayo, Wizara ilitoa zawadi mbalimbali kwa washindi ambapo mkulima bora kitaifa alitoka Halmashauri ya Kongwa ambaye alizawadiwa trekta lenye jembe la thamani ya Shilingi 27,000,000, madawa yenye thamani ya Shilingi 12,000, fedha taslim Shilingi 350,000 na Cheti. Mshindi wa pili alitoka Halmashauri ya Manyoni ambaye alizawadiwa trekta dogo la mkono (*power tiller*) lenye thamani ya Shilingi 7,000,000, madawa ya Shilingi 12,000, fedha taslim Shilingi 300,000 na Cheti. Mshindi wa tatu alitoka

Halmashauri ya Wilaya ya Iramba na kuzawadiwa jembe la kukokotwa na ng'ombe, mbolea na mbegu vyenye thamani ya Shilingi 1,921,400 na Cheti. Washindi kutoka makundi ya Vyama vya Ushirika akiwemo mshindi wa kwanza, wa pili na wa tatu walipewa zawadi mbalimbali zenye thamani ya Shilingi 5,675,000. Vilevile, washindi watatu kutoka Bodi za Mazao ya Kahawa na Chai walipewa zawadi zenye thamani ya Shilingi 3,750,000 na mshindi kutoka sekta binafsi alipewa zawadi ya Shilingi 10,000,000. Katika kuhamasisha matumizi bora na endelevu ya maji, washindi bora watatu wa kilimo cha umwagiliaji walipewa vifaa vya umwagiliaji vyenye thamani ya Shilingi 7,500,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwatambua wadau 15 wa kilimo waliochangia katika kutoa zawadi hizo kama ifuatavyo: *Kihelya Auto Tractor-Mwanza*, *Suba Agro*, *NMB*, *INCAR* Dar es Salaam, *AGRICOM, Tanzania Farmers Service Center (TFSC)* Arusha, YARA (CHAPA MELI), *Tanzania Fertilizer Company Ltd. (TFC), Export Trading*, *Minjingu Company* Ltd., *Pannar Seed Company Ltd.,* PASS, Bodi ya Chai, Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai–*Tanzania Smallholder Tea Development Agency - TSHTDA* na Bodi ya Kahawa. Napenda kutumia nafasi hii kuwaomba wadau hawa na wengine kuendelea kuchangia katika kutoa zawadi kwa washindi watakaopatikana katika maadhimisho ya mwaka huu yatakayofanyika Nzuguni, Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo kwa wakulima, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI na Shirika la Maendeleo la Japan - *JICA* kupitia *DADPs* ilitoa mafunzo ya msingi (*standard training*) ya kilimo bora cha uzalishaji wa zao la mpunga kwa njia ya umwagiliaji. Mafunzo yalitolewa kwa wakulima 3,072 katika skimu 12 za Tungamalenga (Iringa Vijijini), Kasyabone/Kisegese (Rungwe), Mshewe (Mbeya Vijijini), Mfumbi (Makete), Madaba (Tunduru), Mvumi (Kilosa), Lupilo (Ulanga), Mbarangwe (Morogoro), Ngongowele (Liwale), Sawenge (Magu), Chereche (Rorya) na Ngage (Simanjiro). Aidha, mafunzo ya uzalishaji wa mpunga aina ya NERICA inayolimwa kwenye maeneo ya juu *(Upland*) yalifanyika kwa wakulima katika wilaya za Muheza, Kyela, Makete, Morogoro Vijijini, Ulanga, Bagamoyo, Bukombe, Lindi Vijijini na Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya kilimo kwa wataalam, katika mwaka 2010/2011, Wizara iligharamia mafunzo ya wanafunzi 5,557 ngazi ya Stashahada (Diploma) na Astashahada (Cheti). Aidha, wanafunzi 1,942 walihitimu masomo mwezi Novemba 2010 na wengine 2,588 wamehitimu mafunzo yao mwezi Juni 2011. Wizara pia ilidahili wanafunzi 1,072 katika Vyuo vya Kilimo ambao watahitimu mwezi Juni 2012. Wakufunzi wa kilimo 57 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi kuhusu mbinu sahihi za ufundishaji pamoja na usimamizi na uendeshaji wa Vyuo. Mafunzo ya Astashahada ya Kilimo yameanza kutolewa kwa wanafunzi 45 katika Chuo cha Mtakatifu Maria Goreti (Ilula- Iringa) kupitia mfumo wa *Public-Private Partnership (PPP)* kuanzia Aprili 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilitoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi ili kuimarisha utendaji kazi. Jumla ya wataalam watatu waliendelea kupata mafunzo ya Shahada za Uzamivu (*PhD.*), 25 katika Shahada ya Uzamili (*MSc.*) na 23 Shahada ya Kwanza (*BSc.*). Mafunzo hayo yalihusu Uhandisi wa Kilimo, Uchumi Kilimo, Umwagiliaji, Kanuni Bora za Kilimo na Usimamizi wa Fedha. Wizara pia ilitoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi katika fani mbalimbali. Jumla ya watumishi 149 walipatiwa mafunzo kuhusu uchambuzi wa sera; uandaaji wa bajeti; usimamizi wa fedha; matumizi ya zana za kilimo; usindikaji wa mazao; uchumi; matumizi bora ya maji; uendeshaji, utunzaji, usanifu, usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji; na matumizi ya teknolojia ya kuvuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, makadirio ya mahitaji ya mbolea yalikuwa tani 385,000 zikiwemo tani 200,000 za mbolea ya ruzuku na tani 185,000 za mbolea isiyo ya ruzuku. Jumla ya tani 275,684.8 za mbolea sawa na asilimia 72 zilipatikana. Kati ya hizo, tani 201,050 zilikuwa ni mbolea ya ruzuku ikiwemo mbolea ya kupandia tani 100,525 na mbolea ya kukuzia tani 100,525 ikilinganishwa na tani 150,000 ambazo zilitolewa mwaka 2009/2010. Mbolea ya ruzuku ilinufaisha wakulima 2,011,000 ikilinganishwa na wakulima 1,500,000 walionufaika mwaka 2009/2010. Wakulima walioongezwa walitoka katika Wilaya za Sikonge, Urambo na Igunga (Tabora); Tarime, Serengeti, Rorya na Bunda (Mara); Kahama na Bukombe (Shinyanga); Chato na Karagwe (Kagera); Geita na Sengerema (Mwanza); Mtwara, Newala na Masasi (Mtwara); Lindi (V), Nachingwea na Ruangwa (Lindi); Korogwe, Lushoto, Kilindi, Handeni na Muheza (Tanga); Mpwapwa, Kongwa na Bahi (Dodoma); Bagamoyo na Rufiji (Pwani); Singida (V), Manyoni na Iramba (Singida).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, upatikanaji wa mbegu bora ulifikia tani 26,545 ikilinganishwa na tani 16,148.20 mwaka 2009/2010. Mbegu hizo zinajumuisha mbegu za mazao ya mahindi tani 22,725; mpunga tani 896; mbegu za mafuta tani 676; mikunde tani 486; ngano tani 138; na mtama tani 1,624. Mbegu hizo zilitokana na sekta binafsi na sekta ya umma ambapo sekta ya umma ilizalisha tani 5,678.6, kati ya hizo tani 1,881 ni kutoka *ASA*; tani 1,489.1 kutoka Magereza na JKT na wakulima wadogo walizalisha tani 2,308 za mbegu za Daraja la Kuazimiwa (*Quality Declared Seed – QDS)*. Aidha, sekta binafsi ilichangia jumla ya tani 20,866.4. Kati ya hizo tani 8,149.4 zilizalishwa nchini na tani 12,717 ziliagizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilitoa ruzuku ya tani 20,357.86 za mbegu bora za mahindi na mpunga ikilinganishwa na tani 15,150 zilizotolewa mwaka 2009/2010. Aidha, Wizara ilitoa tani 15,375 za mbegu ya pamba kwa utaratibu wa vocha. Mbegu za mahindi na mpunga zilisambazwa katika Mikoa 20 inayozalisha mazao hayo kwa wingi na mbegu za pamba zilisambazwa katika Mikoa tisa inayozalisha zao hilo. Vilevile, Wizara ilitoa ruzuku ya mbegu bora za mtama tani 356.25 na alizeti tani 50 nje ya utaratibu wa vocha ikilinganishwa na tani 289.8 za mtama na tani 85.4 za alizeti mwaka 2009/2010 ambazo zilisambazwa kwenye Mikoa ya Singida, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Dodoma na Morogoro. Jumla ya wakulima 110,600 wa zao la mtama na wakulima 10,392 wa zao la alizeti walinufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Taasisi ya Zao la Kahawa (*Tanzania Coffee Reserach Institute-TaCRI*) ilizalisha miche bora ya kahawa 14,430,000 sawa na asilimia 96.2 ya lengo la kuzalisha miche 15,000,000. Aidha, kupitia Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai, wakulima 2,227 katika vikundi 178 walizalisha miche bora ya chai 10,141,000 na Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania (*Tea Research Institute of Tanzania- TRIT*) ilizalisha miche 3,200,000 na hivyo kufanya uzalishaji wa miche kufikia 14,341,000. Uzalishaji huo ni sawa na asilimia 96 ya lengo la kuzalisha miche 15,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilitoa ruzuku ya madawa ya pamba na korosho ambapo jumla ya *acrepack* 4,653,159 za madawa ya pamba zilizotosheleza ekari 1,537,500 zilitolewa. Madawa hayo yalinufaisha wakulima 576,710 wa Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Tabora, Singida, Kigoma, Morogoro, Manyara na Pwani. Aidha, jumla ya tani 148 na lita 153,395 za madawa ya korosho zilisambazwa kwa wakulima wa Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, Ruvuma na Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na taasisi ya *Citizen Network for Foreign Affairs (CNFA)* ilitoa mafunzo kwa Mawakala 3,855 wa Pembejeo za Kilimo (*Rural agro-dealers*). Mafunzo hayo yalihusu uendeshaji wa biashara, matumizi na hifadhi salama ya pembejeo. Mawakala hao walitoka katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Manyara, Kigoma, Tabora, Mara, Tanga, Shinyanga, Kagera, Mwanza, Lindi, Singida, Dodoma, Pwani na Mtwara. Aidha, kati ya hao, Mawakala 511 walidhaminiwa kupata mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 6.7 kutoka NMB.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa utoaji wa pembejeo kwa kutumia vocha, Wizara ilifanya tathmini kuanzia mwezi Oktoba 2010 hadi Aprili 2011 katika Mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara, Tabora, Shinyanga, Kigoma, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Singida, Dodoma, Pwani, Lindi na Mtwara. Tathmini hiyo ilibaini kuwa wakulima walionufaika na pembejeo kuanzia mwaka 2010/2011 wanatarajia kuongeza mavuno kwa ekari kutoka wastani wa tani 0.7 hadi wastani wa tani 2 kwa ekari kwa zao la mahindi na kutoka wastani wa tani 0.4 hadi wastani wa tani 2.5 kwa ekari kwa zao la mpunga. Aidha, Wakulima walionufaika na utaratibu huo kuanzia miaka ya nyuma tangu mpango uanze, wanatarajia kuongeza uzalishaji kuanzia wastani tani 2 hadi tani 2.7 kwa ekari kwa zao la mahindi na mpunga kwa wastani wa tani 2.5 mpaka tani 3.5 kwa ekari. Aidha, uelewa wa wakulima kuhusiana na matumizi ya pembejeo, hususan mbegu bora na mbolea umeongezeka. Hii inadhihirishwa na wakulima kununua pembejeo hizo nje ya mfumo wa ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, tathmini hiyo ilibaini mapungufu yafuatayo:-

(i) Kushindwa kukidhi mahitaji ya ruzuku ya pembejeo ambayo ni makubwa kuliko uwezo wa Serikali;
(ii) Usimamizi hafifu wa ruzuku ya pembejeo katika baadhi ya Wilaya, Kata na Vijiji;
(iii) Uteuzi wa Mawakala wa Pembejeo wasiokuwa na sifa katika baadhi ya Kamati za Pembejeo za Wilaya;
(iv) Baadhi ya wakulima kutoelewa umuhimu wa kutumia pembejeo za kilimo; na

(v) Baadhi ya wakulima kutouelewa vizuri utaratibu wa ruzuku na hivyo kurubuniwa na Mawakala wa Pembejeo ambao hushirikiana na Watendaji wa Vijiji kuwaibia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu huo, Serikali ilichukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuagiza Wakuu wa Mikoa walete taarifa inayoainisha yafuatayo: orodha ya pembejeo zilizopelekwa katika kila Wilaya, Kata na katika kila Kijiji majina ya wakulima waliopewa pembejeo kwa utaratibu wa vocha;

(ii) Kwa kushirikiana na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali inaandaa Ukaguzi Maalum (*Special Audit*) kuhusu utekelezaji wa mfumo wa pembejeo kwa utaratibu wa vocha kwa lengo la kubaini waliokiuka utaratibu na kuwachukulia hatua za kisheria;

(iii) Kuhimiza usimamizi wa karibu wa utoaji wa ruzuku kwa kushirikiana na Kamati za Vocha za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji katika kutekeleza Waraka wa Serikali uliotolewa kuhusiana na usimamizi wa utaratibu huo; na

(iv) Kutoa elimu kwa wakulima kuhusu umuhimu wa pembejeo katika kilimo na Mfumo wa Vocha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya zana bora za kilimo yameanza kuongezeka kutokana na jitahada za Serikali za kuhamasisha matumizi ya zana hizo. Takwimu zinaonyesha kuwa matumizi ya trekta yameongezeka kutoka asilimia 10 mwaka 2005 hadi asilimia 12 mwaka 2010. Aidha, matumizi ya jembe la kukokotwa na wanyamakazi yameongezeka kutoka asilimia 20 mwaka 2005 hadi asilimia 24 mwaka 2010. Kutokana na ongezeko la matumizi ya zana hizo, matumizi ya jembe la mkono yamepungua kutoka asilimia 70 mwaka 2005 hadi asilimia 64 mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, sekta binafsi iliingiza nchini matrekta makubwa 986, matrekta madogo ya mkono 991 na majembe ya kukokotwa na wanyamakazi 103,343. Aidha, Wizara ilitoa matrekta madogo ya mkono 35 kwa vikundi vya wakulima 35 vyenye wakulima 880 kwa utaratibu wa vikundi kuchangia asilimia 20 kufuatana na mwongozo wa *DADPs*. Matrekta hayo yalitolewa kwenye vikundi vilivyoko kwenye skimu za umwagiliaji za Ruvu (Bagamoyo), Mkula na Njagi (Kilombero), Minepa (Ulanga), Bahi na Matajira (Bahi), Lumuma (Mpwapwa), Mwangeza (Iramba), Kisasida (Singida Mjini) Chikuyu (Manyoni), Nyanzwa na Irindi (Kilolo), Mlenge (Iringa Vijijini), Mpitimbi (Songea), Lekindo (Tunduru), Kasyabone (Rungwe), Mshewe (Mbeya Vijijini), Ngana (Kyela), Mbebe (Ileje), Naming'ongo (Mbozi) Sakalilo (Sumbawanga), Uruira (Mpanda), Ochuna na Chereche (Rorya), Buswahili (Musoma Vijijini), Nyatwali (Bunda), Rungwe Mpya (Kasulu), Rumashi na Ruhwiti (Kibondo), Kitivo (Lushoto), Mombo (Korogwe), Ngage na Lemkuna (Simanjiro), Lekitatu (Meru) na Kitere (Mtwara Vijijini).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, matrekta mengine madogo ya mkono matano yalitolewa kwa utaratibu huo ili kuendeleza Kilimo Hifadhi kwenye Mikoa ya Arusha na Kilimanjaro kwa vikundi vya: Kilimapunda na Merikinoi (Meru), Mwangaza B (Karatu), Lukundo na Jitegemee (Moshi Vijijini). Aidha, Wizara ilianzisha mashamba darasa yenye ukubwa wa ekari moja katika skimu hizo ambapo wakulima walipatiwa mafunzo kuhusu kilimo bora cha mpunga na matumizi bora ya matrekta madogo ya mkono. Vilevile, mafunzo kuhusu matumizi na huduma ya matengenezo ya matrekta madogo ya mkono yalitolewa kwa maopereta 72 kutoka skimu hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilitayarisha mwongozo kwa ajili ya watumiaji wa matrekta makubwa na matrekta madogo ya mkono (*powertiller*) ili kuwawezesha watumiaji hao kuyatumia matrekta hayo kwa usahihi kwa lengo la kuongeza tija. Vilevile, Wizara ilitoa viwango vya ufundi (*technical specifications*) kwa ajili ya matrekta madogo ya mkono, mitambo ya kukobolea mpunga na mashine za kukamulia mafuta. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na ya Kusini ilifanya ukaguzi wa matrekta ya mkono kabla ya kupokelewa (*pre-delivery inspection*) kwa lengo la kudhibiti ubora wa matrekta yanayotolewa na makampuni yaliyoshinda zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilitoa mafunzo kwa wakulima na maopereta 215 juu ya matumizi na matunzo ya zana mbalimbali ikiwa ni pamoja na matrekta makubwa na madogo, mashine za kupandikiza mpunga (*rice transplanters*), mashine za kunyunyizia dawa (*boom sprayers*), mashine ya

kupukuchua mahindi na mashine ya kupura mpunga. Wakulima hao walitoka katika Wilaya za Korogwe, Muheza, Tunduru, Njombe, Kongwa, Babati, Morogoro, Mbozi, Ileje, Mbeya Vijijini, Kyela, Sumbawanga, Nkasi, Mpanda na Simanjiro. Aidha, mafunzo kuhusu kuendesha, kufanya matengenezo madogo na kutunza mashine za kuchakata muhogo na kusindika mbegu za mafuta kwa wakulima 53 yalitolewa katika Wilaya za Kisarawe, Mkuranga na Rufiji. Vilevile, Wizara iliandaa na kutoa mafunzo kwa wakulima 85 katika fani za matumizi bora ya maji, uendeshaji, utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji na matumizi ya teknolojia ya kuvuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashamba Darasa 94 yenye wakulima 8,612 yaliendelezwa katika Wilaya za Meru, Arusha, Karatu, Babati, Hanang na Moshi Vijijini ambapo wakulima waliendelea kujifunza kwa vitendo juu ya matumizi ya zana bora za kilimo hifadhi kama vile ripa na mashine za kupanda bila kukatua (*direct seeders)*. Aidha, wakulima wengine 527 walipata mafunzo katika Mashamba Darasa hayo na kuwezeshwa kuanzisha mashamba ya mfano ya nusu eka kila moja katika mashamba yao binafsi. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Mtandao wa Kilimo Hifadhi Afrika (*African Conservation Tillage Network* - ACT) na Halmashauri za Wilaya za Kiteto, Kongwa, Kilosa na Mvomero ilianzisha Mashamba Darasa 20 ya matumizi ya zana bora za kilimo hifadhi zinazokokotwa na matrekta. Mashamba Darasa hayo yana ukubwa wa eka tano kila moja na yanasimamiwa na wakulima wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo wa masharti nafuu kutoka India, katika mwaka 2010/2011, Serikali ilipata mkopo wenye masharti nafuu (*line of credit*) kutoka India wa Dola za Kimarekani milioni 40 uliowezesha kuingiza nchini matrekta makubwa 1,860 na zana zake, matrekta madogo ya mkono 400 na pampu za kusukuma maji 1,100 ambayo yanauzwa na SUMA JKT. Wakulima wanashauriwa kutumia fursa ya mikopo inayotolewa na Dirisha la Kilimo katika Benki ya Rasilimali (*Tanzania Investment Bank-TIB*), Mfuko wa Taifa wa Pembejeo na taasisi zingine za fedha zitakazowawezesha kununua matrekta hayo na pembejeo nyingine za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Pembejeo za Kilimo, katika mwaka 2010/2011, Mfuko wa Pembejeo ulitengewa jumla ya Shilingi bilioni 3.8 kwa ajili ya kutoa mikopo ya kununulia na kusambaza pembejeo na zana za kilimo. Aidha, Mfuko ulikusanya marejesho ya madeni ya nyuma ya kiasi cha Shilingi bilioni 3.94. Hadi mwezi Juni, 2011 Mfuko ulipata jumla ya Shilingi 6,484,738,294 kwa ajili ya kutoa mikopo na matumizi ya ofisi. Kati ya kiasi hicho Shilingi 2,540,002,000 zilitoka Serikalini na Shilingi 3,944,736,294 ni marejesho ya mikopo. Mfuko ulitoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 4,516,770,056 ikiwa Shilingi 3,498,768,556 kwa ajili ya ununuzi wa matrekta makubwa 96, Shilingi 217,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa matrekta madogo 19, ununuzi wa pembejeo za kilimo na mifugo yenye thamani ya Shilingi 717,001,500, kukarabati matrekta makubwa manne Shilingi 34,000,000 na kununua zana za umwagiliaji zenye thamani ya Shilingi 50,000,000. Mikopo hiyo ilitolewa kwa wakulima binafsi, wasambazaji wa pembejeo za kilimo na mifugo na zana za kilimo kupitia Benki ya Biashara na Uchumi ya Mkoa wa Kilimanjaro, Benki ya Wananchi Mbinga, Benki ya Ushirika Kagera na Benki ya Wananchi Tandahimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi bora ya ardhi, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilipima maeneo ya ardhi ya Wizara katika Kituo cha Utafiti cha KATRIN (Kilombero) na shamba la mbegu la Bugaga (Kasulu). Aidha, upimaji unaendelea katika shamba la mbegu la Dabaga (Kilolo) na eneo la utafiti wa kilimo ARI-Seliani (Arusha). Lengo ni kupata hatimiliki ya ardhi ya Serikali na kupunguza migogoro inayotokana na uvamizi unaojitokeza mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilitoa mafunzo kwa wataalam 31 waliopo kwenye Vituo vya Kanda na Halmashauri 23. Mafunzo hayo yalihusu teknolojia mbalimbali za hifadhi ya udongo na maji mashambani; utambuzi wa aina za udongo na virutubisho vyake; tathmini ya ubora wa udongo kwa kilimo; uchukuaji wa sampuli za udongo kwa ajili ya tathmini kwenye maabara za udongo; uandaaji wa kina wa mipango ya matumizi bora ya ardhi; kilimo mseto; na ukusanyaji na utunzaji wa takwimu za rasilimali ardhi. Lengo lilikuwa kupata taarifa sahihi za kutumia wakati wa utoaji wa huduma za matumizi bora ya ardhi kwa wakulima. Halmashauri zilizohusika ni Mufindi, Mbeya, Sumbawanga Vijijini, Sumbawanga Mjini, Iringa, Mbarali, Ileje, Mpanda, Tarime, Kishapu, Magu, Bunda, Musoma, Maswa, Bukoba, Kondoa, Iramba, Singida Vijijini, Hanang, Mbulu, Chamwino, Dodoma Mjini na Dodoma Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe ilianza kutekeleza Mpango wa Usimamizi na Matumizi Bora ya Ardhi ya Kilimo (*Agricultural Land Use Management Plan*) katika kijiji cha Zegero kilichoteuliwa kama kijiji cha mfano kwa kukusanya sampuli za udongo kwa ajili ya kutathmini ubora wake. Wakulima 50 wa kijiji hicho walifundishwa kuandaa mipango ya kina ya usimamizi na matumizi bora ya ardhi ya kilimo ambao wamekuwa chachu kwa wakulima wenzao katika kuhimiza matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo. Kazi nyingine zilizofanyika ni kupima eneo la kila mkulima na kukusanya takwimu zinazohusu uwepo wa rasilimali za asili, uzalishaji wa mazao ya kilimo na vyanzo vya upatikanaji wa kipato kwa wakulima. Wizara itatumia matokeo ya kazi hiyo katika kuimarisha na kusimamia matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya mazingira, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kutathmini athari za shughuli za kilimo kwenye mazingira katika Halmashauri 10 za Wilaya za Hanang, Babati, Mbulu, Kilolo, Iringa Vijijini, Kisarawe, Kibaha, Lindi Vijijini, Ruangwa na Kondoa. Tathmini hiyo ilibaini uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji na ardhi, ukataji na uchomaji ovyo wa misitu, mifugo mingi kuliko uwezo wa malisho pamoja na uchafuzi wa maji kutokana na matumizi mabaya ya mbolea na madawa ya kuua wadudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilitoa mafunzo ya Tathmini ya Mazingira Kimkakati kwa wataalam wa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika waliopo katika ngazi ya Kanda. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wataalam 57 kutoka Kanda za Umwagiliaji, Idara ya Matumizi Bora ya Ardhi, Vituo vya Utafiti, Vyuo vya Mafunzo na Vituo vya Afya ya Mimea. Aidha, Wizara iliandaa Mpango Kazi wa Mazingira wa Miaka Mitano (5) utakaotumika kutekeleza shughuli za mazingira katika sekta ya kilimo kwa lengo la kupunguza uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za kilimo na uelewa mdogo wa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao ya kilimo, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilidhibiti kikamilifu Nzige Wekundu makundi yapatayo 400 yenye ukubwa wa kuanzia nusu eka mpaka eka 50 kwa kila kundi katika Mbuga za Katavi, Ikuu, Bonde la Ziwa Rukwa na Wembere. Nzige hao walidhibitiwa katika eneo la hekta 19,778. Kutokana na udhibiti huo katika maeneo ya mazalia zaidi ya eka 800,000 za mazao ya nafaka katika Mikoa ya Rukwa, Tabora na Kigoma zilisalimika kutokana na mashambulizi ya nzige hao. Hivyo, wananchi katika maeneo hayo waliweza kuvuna mpunga, mahindi, mtama na ndizi pasipo kuathirika. Aidha, kutokana na kazi nzuri inayofanyika ya udhibiti wa nzige wananchi wengi hawajui kuwa Tanzania kuna nzige wengi kuliko nchi nyingine yoyote ile Kusini na Kati mwa Afrika na mlipuko mkubwa uliotokea kwa mara ya mwisho mwaka 1944 haujatokea tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani ilidhibiti ndege aina ya Kwelea Kwelea milioni 110.4 na hivyo kuokoa tani 1,104 kwa siku za mazao ya nafaka ikiwa ni pamoja na mpunga, mtama, uwele, ulezi na ngano. Ndege hao walidhibitiwa katika Halmashauri za Wilaya za Same, Chamwino, Bahi, Kongwa, Mpwapwa, Dodoma Vijijini, Kondoa, Igunga, Misungwi, Bunda, Musoma Vijijini, Singida Vijijini, Mvomero, Kilosa, Mbarali na Mbulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2010/2011, Wizara ilitoa mafunzo ya utabiri shirikishi na udhibiti wa Viwavijeshi kwa wakulima 160 katika Wilaya za Bahi, Kongwa, Mvomero na Kilosa. Vilevile, wakulima 391 wa pamba kutoka Mikoa ya Mara, Shinyanga na Mwanza walipatiwa mafunzo kuhusu udhibiti husishi. Aidha, uzalishaji na usambazaji wa viumbe vya kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao kibiolojia uliendelea katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Morogoro, Arusha, Dar es Salaam, Ruvuma, Dodoma, Kigoma, Mwanza, Kagera na Mara. Vilevile, ili kupunguza athari katika mazingira na kwa afya ya binadamu zinazosababishwa na matumizi mabaya ya viuatilifu, mafunzo ya matumizi sahihi ya viuatilifu yalitolewa kwa wadau 35 katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, jumla ya Hekta 4,836.9 za mazao ya nafaka zilizovamiwa na Viwavijeshi katika Wilaya za Newala, Masasi, Morogoro Vijijini, Mvomero, Lindi Mjini, Lindi Vijijini, Moshi Vijijini, Korogwe, Handeni na Arusha Mjini ziliokolewa. Aidha, kutokana na jitihada za kushirikisha jamii, utabiri na udhibiti hufanyika mapema na hivyo, milipuko mikubwa ilipungua kutoka Wilaya 19 mwaka 2009/2010 hadi kufikia Wilaya 10 zilizovamiwa katika mwaka 2010/2011. Milipuko ya panya ilidhibitiwa katika vijiji 636 katika Mikoa ya Kilimanjaro, Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro, Mtwara, Pwani, Lindi, Mbeya, Arusha, Ruvuma na Shinyanga kwa kutumia chambo chenye sumu ambapo kilo 160,252 za sumu hiyo zilitumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa nzi wa matunda anayeitwa *Bactrocera Invadens* ulifanyika katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Tabora na Tanga. Katika udhibiti huo wakulima walifundishwa na kuhimizwa kutumia mbinu za Udhibiti Husishi (*Integrated Pest Management - IPM*) ikiwa ni pamoja na usafi wa mashamba na kutumia kivutia wadudu (*pheromone*) aina ya *Methyl Euginol* na kutumia nyigu aitwaye *fopius arisanus* anayekula nzi hao. Serikali imewaleta mabuu (*pupa*) wa nyigu huyo 30,000 kutoka *International Center for Insect Physiology and Ecology – ICIPE* ili wazalishwe kwa wingi na kusambazwa kote nchini kwa ajili ya kuwadhibiti nzi hao. Aidha, wakulima 300 kutoka Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani walipatiwa mafunzo husika kwa njia ya vikundi shirikishi. Kutokana na udhibiti wa Nzi wa Matunda, wakulima waliweza kuongeza mavuno hususan wilaya ya Muheza (Tanga) ambapo inakisiwa walipata Shilingi bilioni 2.16 kwa kuvuna tani 72,000 za machungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilifanya ukaguzi wa mazao yanayoingia nchini na yanayosafirishwa nchi za nje katika vituo vya mipakani ili kudhibiti ueneaji wa visumbufu vya mimea na kurahisisha biashara ya mazao ndani na nje ya nchi. Jumla ya tani 447,738.82 za mazao mbalimbali zilikaguliwa na kusafirishwa nchi za nje ambapo vyeti 8,952 vya usafi vilitolewa. Aidha, jumla tani 750,251.32 za mazao ziliingizwa nchini na vibali 511 vya kuingiza mazao vilitolewa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Chakula na Kilimo *(Food and Agriculture Organization-FAO)* ilitoa mafunzo kwa wakaguzi 22 wa mazao na Afisa Maabara sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa mazao ya kilimo, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara, katika mwaka 2010/2011, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara ya kahawa, chai, korosho, miwa, pamba, mkonge, pareto na tumbaku ulikua kwa viwango tofauti. Kwa ujumla kulikuwa na ongezeko la uzalishaji kwa mazao ya tumbaku, pareto, mkonge, kahawa na korosho na kupungua kwa uzalishaji wa pamba, chai na sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, uzalishaji wa chai ulipungua kutoka tani 33,160 mwaka 2009/2010 hadi tani 32,000 ikilinganishwa na lengo la kuzalisha tani 35,000. Upungufu huo ulitokana na ukame na kufungwa kwa Kiwanda cha Chai Lupembe ambacho kilisababisha chai katika shamba la Mlangali lenye ukubwa wa hekta 200 kutovunwa. Aidha, Serikali inaendelea kusuluhisha mgogoro kati ya Chama cha Wakulima Wadogo wa Chai Rungwe (*RSTGA*) na waliokuwa wanachama wa Chama cha Ushirika wa Chai Rungwe (*RUTECO*) ambacho kilifutiwa usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, uzalishaji wa sukari ulipungua kutoka tani 279,850 mwaka 2009/2010 hadi tani 263,460.69 mwaka 2010/2011. Lengo la uzalishaji wa sukari kwa mwaka huo lilikuwa tani 317,000. Upungufu huo ulitokana na ukame ulioyakumba maeneo yanayozalisha miwa. Maeneo yaliyoathirika zaidi ni yale ya viwanda vya *Tanganyika Planting Company Ltd. (TPC)* na Kagera hali iliyosababisha kufungwa kwa viwanda mapema kutokana na kukosekana kwa malighafi ya miwa ya kutosha. Aidha, kuharibika kwa mtambo wa kusindika sukari katika Kiwanda cha *TPC* kumechangia kushuka kwa uzalishaji wa sukari katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, uzalishaji wa tumbaku uliongezeka hadi tani 130,000 ikilinganishwa na tani 60,900 mwaka 2009/2010 ikiwa ni ongezeko la asilimia 113. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa bei ya tumbaku katika soko la dunia kulikotokana na kupungua kwa uzalishaji wa tumbaku nchini Brazil uliosababishwa na mafuriko yaliyotokea msimu wa 2009/2010. Hali hiyo ilisababisha bei ya tumbaku nchini kupanda kutoka wastani wa Shilingi 1,100 hadi Shilingi 3,100 kwa kilo ya tumbaku ya mvuke na Shilingi 682 hadi 2,000 kwa kilo ya tumbaku ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mafuriko nchini Brazil, uzalishaji wa tumbaku nchini humo katika msimu wa 2010/2011 uliongezeka kuliko hali ya kawaida. Ongezeko hilo pamoja na ongezeko la uzalishaji hapa nchini lilisababisha uhaba wa soko la tumbaku yetu. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara inafanya jitihada ya kutafuta masoko mengine kwa ajili ya kuuza ziada ya tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, uzalishaji wa pamba mbegu ulipungua kutoka tani 267,004 mwaka 2009/2010 hadi tani 163,644, ikiwa ni chini ya lengo la kuzalisha tani 260,000. Sababu kuu iliyochangia kushuka kwa uzalishaji wa pamba ni bei ndogo iliyotolewa katika msimu uliotangulia ambayo ilisababisha wakulima kulima mazao mengine. Sababu nyingine ni ukame ulioyakumba maeneo

yanayolimwa pamba hususan katika Kanda ya Magharibi kati ya mwezi Desemba 2009 na Machi 2010; mvua kubwa kupita kiasi iliyonyesha katika baadhi ya maeneo ya Kanda ya Magharibi kati ya mwezi Aprili na Juni 2010; na kutoeleweka vyema kwa utaratibu wa ruzuku ya pembejeo ambako kulisababisha watoa huduma wa pembejeo hususan madawa kutoratibiwa ipasavyo na hivyo kutoa madawa yasiyokidhi viwango. Suala hilo sasa limepatiwa ufumbuzi ambapo ruzuku ya pembejeo kwa zao la pamba kuanzia msimu ujao itatolewa kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Zao la Pamba ambapo uratibu wa watoa huduma utaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, uzalishaji wa pareto uliongezeka kutoka tani 3,320 mwaka 2009/2010 hadi tani 5,000. Ongezeko hilo lilichangiwa na kupanda kwa bei ya pareto kutoka wastani wa Shilingi 1,200 kwa kilo mwaka 2009/2010 hadi wastani wa Shilingi 1,700 kwa kilo mwaka 2010/2011. Kutokana na hali hiyo, uuzaji nje sumu ghafi (*crude extracts*), *pyrethrum grist* na unga (*powder*) wa pareto uliliingizia Taifa wastani wa Dola za Kimarekani milioni tano (5) ikilinganishwa na Dola za Kimarekani milioni 4.8 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mkonge uliongezeka kutoka tani 26,363 mwaka 2009/2010 hadi tani 35,000 mwaka 2010/2011. Ongezeko hilo lilitokana na kupanda kwa bei ya mkonge kutoka wastani wa Dola za Kimarekani 820 kwa tani mwaka 2009/2010 hadi Dola za Kimarekani 1,200 kwa tani mwezi Machi, 2011 kwa mkonge wa daraja la UG. Aidha, ongezeko la bei lilisababishwa na kuongezeka kwa mahitaji ya mkonge na bidhaa zake katika soko la dunia, hususan kwenye nchi za China, Saudi Arabia, India, Hispania, Uingereza, Ujerumani, Kenya, Uganda na Nigeria. Pamoja na ongezeko kubwa la bei, bado kasi ya kufufua mashamba ya mkonge ni ndogo. Serikali inaendelea kujadiliana na wadau na kuhimiza Bodi ya Mkonge kuongeza uzalishaji na mauzo ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa kahawa uliongezeka kutoka tani 40,000 mwaka 2009/2010 hadi tani 60,575 mwaka 2010/2011. Ongezeko hilo lilichangiwa na hali nzuri ya hewa na tabia ya zao la kahawa kuongeza tija msimu unaofuatia msimu wa uzalishaji mdogo (*biannual bearing*). Aidha, bei ya kahawa katika msimu wa 2010/2011 iliendelea kuwa nzuri na kufikia Shilingi 7,000 kwa kilo ya kahawa safi ya Arabica kutoka wastani wa Shilingi 5,000 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa korosho uliongezeka kutoka tani 74,169 mwaka 2009/2010 hadi tani 121,070 mwaka 2010/2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 63.2. Ongezeko hilo kwa kiasi kikubwa lilitokana na bei nzuri waliyopata wakulima kutokana na kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Maghala. Kupitia Mfumo huo, wakulima walipata malipo ya ziada (majaliwa) na kuweza kupandisha bei ya kilo ya korosho kati ya Shilingi 1,420 na 1,660.70 ikilinganishwa na bei waliyokuwa wakipata kabla ya Mfumo, ya kati ya Shilingi 200 na 350 kwa kilo. Aidha, mfumo huo umeepusha ununuzi holela usiomnufaisha mkulima. Sababu nyingine zilikuwa ni hali nzuri ya hewa na utoaji wa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima, hususan madawa ya kuua wadudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilishirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo Halmashauri za Wilaya, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na makampuni binafsi katika kuendeleza uzalishaji na usindikaji wa mazao ya alizeti, ufuta, karanga, michikichi, mbegu za pamba na soya. Uzalishaji huo umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, uzalishaji wa alizeti uliongezeka kutoka tani 348,877 mwaka 2009/2010 hadi tani 786,902 mwaka 2010/2011. Ongezeko la uzalishaji wa mbegu za mafuta lilitokana na kupanuka kwa soko la ndani kufuatia kuenea kwa teknolojia ya usindikaji wa mbegu za mafuta na kilimo cha mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mazao ya bustani, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilitunza bustani za Mpiji (Bagamoyo), Jaegetal (Lushoto), Songa na Kizugu (Muheza), Igurusi (Mbarali) na Bugaga (Kasulu) kwa ajili ya kupata vikonyo vya mazao ya bustani ili kuzalisha miche bora. Miche 365,000 ya matunda ilizalishwa katika bustani hizo na kusambazwa kwa wakulima. Aidha, Wizara kwa kushirikana na Baraza la Kuendeleza Mazao ya Bustani (*Horticulture Development Council of Tanzania - HODECT*) na wadau wengine iliandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Mazao ya Bustani (*National Horticulture Development Strategy*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kimkakati yatakayozingatiwa katika utekelezaji wa programu ya kuendeleza sekta ya mazao ya bustani ni pamoja na: kuongeza uwekezaji na ugharamiaji wa muda mrefu katika sekta ya mazao ya bustani; kuainisha na kushughulikia changamoto na vikwazo vya

miundombinu katika sekta ndogo ya mazao ya bustani; kuwezesha upatikanaji wa masoko ya mazao ya bustani; kuongeza uzalishaji wenye tija na ubora; na kujenga uwezo wa rasilimali watu ili kutekeleza kwa mafanikio mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika kilimo, mwezi Julai, 2010, Serikali ilisaini makubaliano ya kutekeleza Programu Kabambe ya Maendeleo ya Kilimo Afrika (*Comprehensive Africa Agriculture Development Programme - CAADP).* Makubaliano hayo yataiwezesha Tanzania kunufaika na fursa zilizopo katika Umoja wa Afrika za kuendeleza kilimo hususan kuimarisha usalama wa chakula. Makubaliano hayo yatatekelezwa kupitia mfumo wa utekelezaji wa *ASDP* utakaoboreshwa kuhusisha wadau wengi zaidi. Tayari Wizara za Sekta ya Kilimo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zinakamilisha uandaaji wa Mpango wa Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilishiriki katika kuandaa Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania (*Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT*) ambao utatekelezwa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa. Aidha, Mpango utatekelezwa pia Zanzibar. Mpango huo ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2010 (*Public-Private Partnership Policy 2010*). Kwa upande wa Serikali, Mpango huo utasimamiwa na Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji (*Rufiji Basin Development Authority- RUBADA*). Mamlaka hiyo itafanyiwa maboresho ili iweze kumudu majukumu hayo mapya. Wizara pia kwa kushirikiana na wadau imekamilisha maandalizi ya miradi ya *Bread Basket* na *Feed the Future* ambayo nayo inalenga kuongeza usalama wa chakula na kuzalisha ziada kwa ajili ya kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi RUBADA imeendelea kutekeleza makubaliano ya ubia na kampuni ya *Agrica* ya Uingereza katika kuendeleza kilimo cha mpunga katika shamba la Mngeta kwa kushirikiana na Kampuni ya ubia ya *Kilombero Plantations Ltd.* Ubia huo umewezesha uwekezaji wa Dola za Kimarekani milioni 25 na kuendeleza eneo la hekta 4,150 za kilimo cha mpunga. Hadi tarehe 30 Juni, 2011 jumla ya tani 12,000 za mpunga zilikuwa zimevunwa katika eneo la hekta 3,000. Matarajio ya mavuno kwa hekta zote 4,150 ni kati ya tani 15,000 hadi tani 16,000 za mpunga. Aidha, ili kuongeza tija, kampuni imeanza kujenga miundombinu ya umwagiliaji na eneo lote la hekta 5,000 litalimwa msimu ujao. Vilevile, kampuni imetoa ajira mpya 172 ya wafanyakazi wa kudumu na vibarua 650. Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa namna hiyo katika maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha iliendelea kupitia kodi mbalimbali zinazohusu Sekta ya Kilimo katika kuhamasisha uwekezaji katika sekta hiyo. Kutokana na mapitio hayo, Serikali imefanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* kwenye zana za kilimo kama ifuatavyo:-

(i) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mashine za kupura (*threshers*), mashine za kukaushia na kukoboa mpunga (*rice dryers and mills*), mashine za kupandia mbegu (*planters*) na matrekta ya kukokota kwa mkono (*power tiller*); na

(ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vipuri vya mashine za kunyunyizia na kutifua udongo (*Sprayers and Harrows*) na mashine za kupandishia nafaka (*Grain Conveyors).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010, Wizara pia ilishiriki katika utekelezaji wa *Roadmap* ya maboresho ya mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara kupitia viashiria vilivyoainishwa katika ripoti ya Benki ya Dunia (*World Bank Doing Business Report 2010)*, kwa kuandaa kanuni za Bodi za Mazao na kupendekeza marekebisho katika Sheria ya Hifadhi ya Mimea (*The Plant Protection Act, 1997*) kwa lengo la kuondoa kero zinazokwaza wawekezaji na wafanyabiashara katika mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa chakula, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilifanya mafunzo kwa watoa taarifa na takwimu za mvua na hali ya mazao mashambani wapatao 284. Watoa taarifa hao walitoka katika Halmashauri za Wilaya 73 za Mikoa ya Kanda ya Mashariki (Morogoro, Tanga, Pwani na Dar es Salaam); Kanda ya Kati (Dodoma na Singida); Kanda ya Ziwa (Shinyanga, Mwanza, Mara na Kagera); na Kanda ya Kusini (Mtwara na Lindi). Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuboresha ukusanyaji wa taarifa na takwimu hizo kwa kutumia mfumo wa moja kwa moja wa kutumia simu za viganjani na

kompyuta (*Automation)*. Pia, ukaguzi na ukarabati wa vituo vya kutoa taarifa za mvua na hali ya mazao mashambani ulifanyika katika mikoa ya Kilimanjaro, Manyara, Mwanza na Kagera ili viweze kutoa taarifa na takwimu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya chakula na usindikaji, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliainisha wasindikaji wa mazao mbalimbali ya nafaka, mbegu za mafuta, matunda na mbogamboga katika Halmashauri za Wilaya za Kilosa, Tunduru na Korogwe ambapo jumla ya wasindikaji 30 waliainishwa. Lengo lilikuwa ni kuwatambua, kubaini shughuli zao na kubuni utaratibu wa kuanzisha ubia wa usindikaji kati ya Serikali na wakulima/wajasiriamali *(Public Private Partnership –PPP)*. Katika kuhakikisha kuwa wakulima wanapata bei nzuri kwa zao la mpunga, Wizara ilitoa mafunzo kwa wakulima 150 wa zao hilo kuhusu usindikaji na upangaji wa madaraja. Mafunzo hayo yalitolewa katika skimu za umwagiliaji za Mbarali, Lower Moshi na Mkindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi na ununuzi wa chakula kupitia *NFRA*, katika mwaka 2010/2011, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*National Food Reserve Agency - NFRA*) ilipanga kununua jumla ya tani 200,000 za mahindi. Hadi tarehe 30 Juni 2011, *NFRA* ilikuwa imenunua tani 181,019 za mahindi sawa na asilimia 90.5 ya lengo. Hata hivyo, lengo la ununuzi halikufikiwa kutokana na kupungua kwa mahindi katika maeneo ya ununuzi na kupanda kwa bei ya mahindi katika kipindi hicho. Ununuzi huo ukijumuishwa na akiba iliyokuwepo mwanzoni mwa msimu ya tani 47,685.6 za mahindi na tani 9.2 za mtama, ulifanya akiba ya chakula kufikia tani 228,713.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kurekebisha na kuhuisha Sera na Sheria, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilisambaza nakala za vitabu vya Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010 kwa wadau. Wizara pia iliandaa mapendekezo ya kuhuisha Sheria ya Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (*The Agricultural Inputs Trust Fund Act,* 1999) na Sheria ya Hifadhi za Mimea (*Plant Protection Act, 1997).* Vilevile, Wizara iliandaa mapendekezo ya Miswada ya Sheria za Kusimamia Rasilimali za Kilimo *(The Agricultural Resource Management Legislation*); Sheria ya Nasaba kwa ajili ya Kilimo na Chakula (*The Plant Genetic Resource for Food and Agriculture Legislation*); na Sheria ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika (*The Cooperative Development Commission Legislation*). Pia Kanuni za Sheria ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko; Sheria ya Mbolea *(The Fertilizer Regulations*); na kanuni za Sheria za Mazao ya Pareto, Chai, Sukari, Korosho, Tumbaku, Pamba, Kahawa na Mkonge ziliandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya watumishi, katika mwaka 2010/2011, watumishi 234 walipandishwa na kubadilishwa cheo katika madaraja mbalimbali kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma. Aidha, Watafiti Wastaafu 36 walipewa mikataba mipya ya kazi. Wizara ilikamilisha mapitio ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja kwa ajili ya kuboresha huduma zake. Katika utekelezaji wa malengo ya utawala bora, Wizara ilisimamia Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji kazi (*Open Performance Review Appraisal System - OPRAS*) ambapo asilimia 73 ya watumishi wote walifanyiwa tathmini katika mfumo huo. Watumishi wengine waliendelea kufanyiwa mafunzo ya *OPRAS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kupunguza makali ya UKIMWI, Wizara iliendelea kuwapatia vyakula vyenye virutubisho pamoja na matibabu watumishi 17 wanaoishi na virusi vya UKIMWI na kuhamasisha upimaji wa afya wa hiari miongoni mwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kujenga uwezo wa Kamati ya Jinsia ya Wizara kwa kutoa mafunzo kwa wajumbe sita wa Kamati hiyo katika Chuo cha *Eastern and Southern Africa Management Institute (ESAMI).* Aidha, rasimu ya Mwongozo wa Jinsi ya Kuingiza Masuala ya Jinsia kwenye Sekta ya Kilimo iliwasilishwa kwa wadau ili kupata maoni yao kabla ya kukamilishwa. Wizara inaendelea kukamilisha mwongozo huo baada ya kupata maoni ya wadau na utakuwa tayari kwa matumizi katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 24, katika mwaka 2010/2011, Wizara kupitia Fungu 24 ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 6.708. Kati ya hizo, Shilingi bilioni 6.608 ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi milioni 100.0 ni Fedha za Maendeleo. Hadi tarehe 30 Juni, 2011, Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizopokelewa kutoka Hazina zilikuwa Shilingi bilioni 5.576 sawa na asilimia 83.13 ya kiasi kilichoidhinishwa. Matumizi yalifikia Shilingi bilioni 5.497 sawa na asilimia 98 ya kiasi cha fedha kilichotolewa. Aidha, hadi

tarehe 30 Juni, 2011, Fedha za Bajeti ya Maendeleo zilizopokelewa ni Shilingi milioni 30.0 sawa na asilimia 30 ya fedha zilizoidhinishwa ambazo zote zilitumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliimarisha Ushirika kupitia utekelezaji wa Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika nchini. Maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na kuimarisha uongozi wa Vyama vya Ushirika; kuwahamasisha wananchi kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Ushirika; kuimarisha masuala ya mazao ya wakulima kwa kueneza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala; kufufua na kuimarisha Vyama vya Ushirika; kuimarisha uendeshaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo - (*Savings and Credit Cooperative Society - SACCOS*) na Benki za Ushirika; kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika; kuimarisha taasisi za ushirika; na kuendelea na mchakato wa kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha uongozi wa Vyama vya Ushirika, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI ilisimamia chaguzi za theluthi moja ya wajumbe wa Bodi katika maeneo ya Vyama Vikuu ambao muda wao uliisha. Vyama hivyo ni Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (*Savings and Credit Cooperative Union League of Tanzania Ltd. – SCCULT*), *Biharamulo Cooperative Union Ltd.* (BCU) (1986) Ltd., Mradi wa Ushirika wa pamoja Kanyovu (Kanyovu *Cooperative Joint Enterprise),* Chama Kilele cha Tumbaku *(Tanzania Tobacco Cooperative Apex - TTCA)* na *Central Tobbacco Cooperative Union Ltd.* (CETCU).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilisimamia na kufuatilia kwa karibu hatua za ujenzi wa mitaji ya Benki za Kilimanjaro *Cooperative Bank Limited* (KCBL) na *Kagera Farmers Cooperative Bank Limited (KFCB)* kwa ajili ya kuimarisha Benki hizo. Wizara pia iliendelea na usuluhishi wa migogoro mbalimbali ya Vyama vya Ushirika vikiwemo Rusaba, Matiazo na Mkabogo Cooperative Society (RUMAKO), *Coast Region Cooperative Union (1984) Ltd.* (CORECU), Chama cha Mazao RUARUKE, *Mosemo Cooperative Marketing* (MCM) SACCOS, Buguruni Traders SACCOS, Luiche SACCOS na *Dar es Salaam Airport Tax Drivers Cooperative Society*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara iliendelea na uhamasishaji na uimarishaji wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Mara (WAMACU) na ilishughulikia ufilisi wa Vyama vya Ushirika vya *Vumilia Producers Cooperative Societies* (VUPO), TUKE *Consumers Cooperative Society, Mbinga Cooperative Union Ltd. (MBICU)* na ufufuaji wa *Mbinga Farmers Cooperative Union Ltd. (MBIFACU).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha utendaji wa viongozi wa Vyama vya Ushirika, mafunzo ya uendeshaji wa Vyama vya Ushirika yalitolewa kwa viongozi 40 kutoka Chama Kikuu cha Ushirika cha Igembensabo *Cooperative Union Ltd. (ICU*), Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (*Tanzania Federation of Cooperatves Ltd. - TFC*), *SCCULT*, *Kilimanjaro Native Cooperative Union Ltd.* (KNCU), *KCBL*, *Vuasu Cooperatve Union Ltd.* (VCU) na *Arusha Cooperative Union Ltd.* (ACU) kwa lengo la kuviwezesha vyama hivyo kuzingatia misingi ya utawala bora. Aidha, mafunzo ya cheti yalitolewa kwa watendaji wa *SACCOS* kutoka Mikoa ya Arusha, Tabora na Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi kujiunga na Vyama vya Ushirika, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilihamasisha wananchi ama kuanzisha au kujiunga na Vyama vya Ushirika kupitia maadhimisho ya Nane Nane na Siku ya Ushirika Duniani. Siku ya Ushirika Duniani ilijikita katika kuhamasisha wanawake kushiriki katika ushirika, kaulimbiu ikiwa "*Ushirika Hujasirisha Wanawake*". Siku ya SACCOS duniani ililenga katika kuhamasisha wanachama na kuzitaka jamii kujiunga kwa wingi kupitia kaulimbiu ya *"SACCOS zetu ni Tegemeo kwa Maendeleo ya Jamii"*. Katika maadhimisho hayo vyama vilivyoshiriki ni pamoja na TFC, KNCU, *Karagwe District Cooperative Union Ltd. (KDCU),* BCU, KFCB, KCBL, *Kagera Cooperative Union Ltd.* (KCU), *Tanga Diary Cooperative Union Ltd.* (TDCU), *Western Zone Tobacco Growers Cooperative Union Ltd. (*WETCU), Masasi Mtwara Cooperative Union Ltd. (MAMCU), *Tunduru Agricultural Marketing Cooperative Union Ltd. (TAMCU), Dar es Salam Region Cooperative Union Ltd. (DARECU), Tandahimba Newala Cooperative Union Ltd. (TANECU), ICU, ACU, Riftvalley Cooperative Union Ltd. (RIVACU), Songea Namtumbo Agriculture Marketing Cooperative Union Ltd. (SONAMCU), Kigoma Tobacco Growers Cooperative Union Ltd. (KTCU), Central Zone Tobacco Growers Cooperative Union Ltd. (CETCU), SCCULT* na *Chunya Tobacco Growers Cooperative Union Ltd. (CHUTCU).* Vilevile, Vyama vya Msingi vya mazao 20, Ufugaji/Maziwa vitano, *SACCOS* 35 pamoja na vikundi 20 navyo vilishiriki kwenye maadhimisho hayo.

Kutokana na uhamasishaji huo vyama vyenye mitaji na uwezo mdogo wa kujiendesha vilihamasishwa kuungana. Kutokana na jitihada hizo idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika imeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilieneza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika Mikoa inayozalisha korosho, kahawa, pamba na alizeti. Kupitia Mfumo huo, Vyama vya Ushirika vya Korosho katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Ruvuma (Tunduru) viliwalipa wakulima malipo ya ziada (majaliwa) na kuwezesha kupata bei nzuri ya korosho. Aidha, mfumo huo umewezesha Vyama vya Ushirika kukopesheka, kuongeza ubora na thamani ya zao, matumizi ya vipimo sahihi, upatikanaji wa ushuru wa Halmashauri za Wilaya na uchangiaji wa huduma za kijamii kama shule na zahanati. Kwa mfano wakulima wanaohudumiwa na Chama cha TANECU wameweza kuchangia ushuru wa Halmashauri Shilingi bilioni mbili (bilioni 2), Vyama vya Ushirika vya Msingi Shilingi bilioni 2.5, mchango wa madawati shuleni Shilingi milioni 360 na ujenzi wa maghala Shilingi milioni 900. Pia mfumo huo umewasaidia kuepuka ununuzi holela usiomnufaisha mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ilifanya tathmini ambayo ilibaini kuwa baadhi ya gharama za masoko na uendeshaji wa Mfumo huo zilikuwa kubwa na hivyo kushauri kupunguza gharama hizo kwenye usafirishaji, ushuru wa Vyama na Halmashauri za Wilaya ili kumwezesha mkulima kupata malipo mazuri zaidi. Aidha, Wizara ilihamasisha matumizi ya Mfumo huo kwenye mazao ya kahawa katika Wilaya za Mbinga na Tarime; pamba katika Wilaya za Igunga, Nzega, Musoma na Bunda; ufuta kwenye Wilaya zote za Mikoa ya Lindi na Mtwara; na alizeti katika Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufufua na kuimarisha Vyama vya Ushirika, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kulipa madeni ya Vyama vya Ushirika ambapo jumla ya Shilingi 745,925,000 zilitumika kwa ajili ya kulipa mafao ya watumishi na madeni ya Vyama vya *Nyanza Cooperative Union Ltd.* (NCU), ACU, Mbeya *Ileje Cooperative Union Ltd.* (MICU) na *Kyela Cooperative Union Ltd.* (KYECU). Aidha, baadhi ya Vyama vya Ushirika vilivyofutiwa madeni vya *KCU, KNCU, ICU* na *TDCU* vimeonesha mafanikio makubwa. Kwa mfano, Chama Kikuu cha KCU (1991) Ltd. kimeweza kuongeza uzalishaji wa Kahawa Hai (*Organic Coffee*) aina ya Robusta kwa kuuza na kuwalipa wakulima Shilingi 3,600 kwa kilo ikilinganishwa na kahawa ya kawaida Shilingi 1,800 kwa kilo ya kahawa safi. Vilevile, *KNCU* (1984) Ltd. iliwalipa wakulima Shilingi 3,200 kwa kilo ya kahawa aina ya Arabica ikilinganishwa na malipo ya awali ya Shilingi 3,000 kwa kilo. Vyama hivyo viliajiri Maafisa Ugani 77 (45 *KCU* na 32 *KNCU*) wanaohudumia wakulima katika vyama wanachama. Aidha, *TDCU* iliwezesha idadi ya wafugaji katika Vyama vya Msingi kuongeza upatikanaji wa maziwa kutoka lita 6,200,000 hadi lita 7,750,000 ikiwa ni ongezeko la asilimia 25. Vilevile, wafugaji walipata bei nzuri ya maziwa kutoka wastani wa Shilingi 350 kwa lita mwaka 2009/2010 hadi Shilingi 550 kwa lita mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuviongezea nguvu Vyama vya Ushirika, baadhi ya Vyama viliungana kwa kuunda miradi ya pamoja na hivyo kuweza kuuza mazao nje ya nchi. Kwa mfano, mradi wa pamoja wa ushirika wa KANYOVU (Kigoma) uliuza kahawa aina ya Arabica kwenye soko maalum la *fair trade* ambapo wakulima walilipwa hadi Shilingi 5,600 kwa kilo ikilinganishwa na malipo ya Shilingi 3,400 kwa kilo mwaka 2009/2010. Chama hicho kilipewa tuzo ya kahawa bora Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kuimarisha Vyama vya Ushirika vinavyolima tumbaku vya *WETCU*, *Kahama Cooperative Union Ltd. (KACU), CETCU SONAMCU, Lake Tobacco Growers Cooperative Union Ltd. (LATCU), CHUTCU, KTCU* na Vyama vya Msingi vya wakulima wa tumbaku wa Iringa vya Mfyome, Magubike, Mhanga na Kiwemu ili viweze kukopesheka. Vyama hivyo vilipata mikopo ya jumla ya Shilingi bilioni 123.6 (sawa na Dola za Kimarekani 85,802,212 wakati mkopo ulipochukuliwa) kutoka benki za *CRDB plc*. na *NMB* kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa pembejeo kwa wakulima. Pembejeo zilizonunuliwa ni pamoja na mbolea aina ya *NPK* 10:18:24 mifuko 925,683, *CAN* 27% mifuko 233,221, *NPK* 20:10:10 mifuko 57,600 na *UREA* mifuko 237,619. Madawa ya *Confidor* 70 WG (30gm) paketi 531,939, *Yamaotea* lita 108,182, *Actara* 25 WG ( 4gm) paketi 84,884, *Bill dock* kilo 2,691, *Decis* vidonge 873,413, vifungashio aina *ya New hessian cloth* marobota 6,222, *Jute twine* marobota 3,865 na *Cotton twine 1.5 kilo spool*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Vyama Vikuu 41 na Chama Kilele vinavyojishughulisha na mazao ya kahawa, korosho, tumbaku, pamba na mazao mchanganyiko viliweza kupata mikopo kutoka *NMB* na *CRDB plc*. Mikopo ilitolewa kwa zao la kahawa Shilingi bilioni 18.6; korosho Shilingi bilioni 16.6; pamba Shilingi bilioni 6.6; tumbaku Shilingi bilioni 123.6 na mazao mchanganyiko Shilingi milioni 500. Vyama hivyo vilitoa huduma kwa wanachama na wasio wanachama ambapo kwa kipindi hicho viliweza kutoa huduma kwa wakulima zaidi ya milioni sita (milioni 6).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha uendeshaji wa *SACCOS* na Benki za Ushirika, katika mwaka 2010/2011, Wizara ilitoa mafunzo kwa Maafisa Ushirika 42 wa Mikoa ya Iringa, Mbeya, Lindi, Mtwara, Rukwa na Ruvuma kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kusimamia na kukagua *SACCOS* ili ziweze kuendeshwa kwa kuzingatia sheria, taratibu na viwango vinavyotakiwa. Aidha, Wizara ilichambua na kuidhinisha Mipango ya muda wa mwaka mmoja ya Vyama Vikuu vya Ushirika 23, benki za ushirika mbili na *SACCOS* 10 zenye mahitaji ya mikopo zaidi ya Shilingi milioni 500 na kuvipatia hati ya ukomo wa madeni (*maximum liability certificates)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika, katika mwaka 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI ilifanya ukaguzi maalum wa *SCCULT*, *WETCU, MBIFACU, SONAMCU, TAMCU, ICU, NCU, KNCU, MBOCU, RUCU, MICU, KYECU, RIVACU, G32, RUARUKE, MCU, VUPO* (chini ya Ufilisi) na Vyama 119 vya Ushirika vya Msingi ambavyo wanachama wa vyama hivyo waliwasilisha maombi kwa lengo la kubaini hali ya uendeshaji wa vyama husika. Matokeo yalionyesha kuwepo dosari mbalimbali kwa baadhi ya vyama ikiwa ni pamoja na uandishi mbovu wa vitabu, kutotunza vizuri daftari la wanachama na daftari la mali za chama, ucheleweshaji wa marejesho ya mikopo, matumizi makubwa kuliko mapato, ubadhirifu wa fedha za vyama na kutozingatiwa kwa utekelezaji wa baadhi ya vifungu vya sheria. Wizara imetoa maelekezo kwa wanachama kuwawajibisha viongozi wa Bodi na Watendaji kupitia Mikutano Mikuu na kuchukua hatua za kisheria pale inapostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha taasisi za ushirika, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kuimarisha taasisi za ushirika kwa kufanya maboresho ya uongozi, usimamizi na utendaji. Maboresho hayo yalifanywa katika Shirikisho la Vyama vya Ushirika pamoja na *SCCULT* ili kuwezesha vyama hivyo kutoa huduma zinazotarajiwa na wanachama. Aidha, Wizara iliendelea kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ushirika na Stadi za Biashara (*Moshi University College of Cooperative and Business Studies - MUCCoBS*) katika kufanya utafiti wa maendeleo ya ushirika na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Idara ya Maendeleo ya Ushirika, viongozi pamoja na watendaji wa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kulipatia ruzuku Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*) ili kuimarisha shughuli za ukaguzi wa vyama. Kwa mwaka 2010/2011, Shirika lilifanya ukaguzi katika Vyama 1,419. Vyama vilivyokaguliwa ni pamoja na *AMCOS* 644; *SACCOS* 711 na Vyama 64 vya aina nyingine. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa watumishi 30, kati yao watumishi 10 waliendelea kupata mafunzo ya uzamili, saba mafunzo ya stashahada, mmoja mafunzo ya cheti na 12 walipata mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi. Vilevile, Idara ilipatiwa vitendea kazi mbalimbali yakiwemo magari mawili ili kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea na mchakato wa uanzishaji wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais kwa lengo la kuleta msukumo mkubwa katika uhamasishaji, uanzishaji, uendelezaji, uimarishaji na usimamizi wa ushirika nchini. Baadhi ya majukumu ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika yameanza kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uendelezaji wa maendeleo ya ushirika hususan katika ushirika wa masoko (*Cooperative Marketing*), Ushirika wa fedha (*Cooperative Microfinance*), Benki za Ushirika (*Cooperative Banks*) na usimamizi wa biashara ya vyama vya ushirika ili viweze kununua na kuuza mazao pamoja na kuwafikishia pembejeo wakulima. Aidha, mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika yameandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa mwaka 2011/2012, malengo ya Wizara, mpango na bajeti ya mwaka 2011/2012 umelenga katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia 2011/2012 hadi 2015/2016 wenye lengo la kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo (*Tanzania Development Vision - TDV 2025*). Aidha, mpango na bajeti utaendelea kutekeleza Malengo ya Maendeleo ya Milenia; MKUKUTA II; Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka

2010; Azma ya Kilimo Kwanza; na Maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipotembelea Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia itatekeleza Programu Kabambe ya Maendeleo ya Kilimo Afrika (*Comprehensive Africa Agriculture Development Programme - CAADP*) kupitia Mpango wa Uwekezaji ulioandaliwa na wadau (*Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan - TAFSIP*); Mpango wa Ukanda wa Kilimo wa Kusini mwa Tanzania (*SAGCOT*); na Miradi ya *Feed the Future* na *Bread Basket.* Mipango hiyo inayolenga katika kuongeza tija na uzalishaji, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza kipato cha mkulima itatekelezwa chini ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mipango hiyo, Wizara inalenga kukabiliana na vikwazo vinavyokwamisha ukuaji wa Sekta ya Kilimo kama vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Baadhi ya vikwazo hivyo ni pamoja na kilimo cha kutegemea mvua pekee; uwekezaji mdogo; upatikanaji mdogo wa mikopo; tija ndogo; masoko duni; mabadiliko ya tabianchi (ukame na mafuriko); na uthamanishaji mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa vikwazo hivyo, Wizara itatekeleza maeneo ya kipaumbele yafuatayo: kupanua eneo la umwagiliaji; kuhimiza na kuongeza matumizi ya pembejeo na zana bora za kilimo; kuimarisha huduma za kitaalam (utafiti, ugani na mafunzo); kuhimiza matumizi bora ya ardhi ya kilimo; kuimarisha ushirika nchini; kuhimiza kilimo cha kibiashara na uongezaji thamani ya mazao; na kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo yatatekelezwa kupitia *ASDP* ambayo hutekelezwa katika ngazi ya Taifa na Wizara za Sekta ya Kilimo na katika ngazi ya Halmashauri kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs).* Utekelezaji wa *DADPs* unaimarisha sera ya ugatuaji wa madaraka kwenda ngazi ya Halmashauri (*Decentralization by Devolution – D-by-D*) hivyo kuwawezesha wakulima kuibua, kupanga, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo yao katika kilimo na ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itasimamia na kuratibu utekelezaji wa *ASDP* katika ngazi ya Kitaifa na ngazi ya Halmashauri. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo, Wabia wa Maendeleo pamoja na wadau wengine itafanya tathmini ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya *ASDP*. Matokeo ya tathmini hiyo yatatumika katika kuandaa awamu ya pili ya *ASDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 43, Kilimo cha Umwagiliaji, maji ndiyo pembejeo ya umuhimu wa kwanza katika kilimo. Kulingana na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010, lengo ni kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia hekta 1,000,000 ili kujitosheleza kwa chakula na kuuza ziada ifikapo mwaka 2015. Eneo la umwagiliaji lililoendelezwa hadi sasa ni hekta 345,690. Kutokana na ufinyu wa rasilimali tulizonazo itachukua muda mrefu kufikia lengo la hekta 1,000,000 kwa utaratibu ambao umekuwa ukitumika wa kutegemea miundombinu mikubwa peke yake ambayo ina gharama kubwa. Hivyo, msukumo mkubwa utawekwa katika kutumia teknolojia mbalimbali zikiwemo zenye ufanisi, gharama nafuu na kuhusisha sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzisha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itatekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete la kuunda Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itakayosimamia kwa ukamilifu shughuli za umwagiliaji kwa kuandaa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya kuanzisha Tume hiyo. Aidha, kufuatia kukamilika kwa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji, Wizara itaitafsiri Sera hiyo kwa lugha ya kiswahili na lugha nyepesi kwa ajili ya kuifikisha kwa umma; kukamilisha uandaaji wa Mkakati wa Umwagiliaji; na kuandaa mapendekezo ya Muswada wa Sheria ya Umwagiliaji. Jumla ya Shilingi milioni 51.88 zimetengwa kwa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, utekelezaji wa maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji utazingatia Sera ya Taifa ya Umwagiliaji (2010) na Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji (2002). Katika utekelezaji huo, maeneo yanayolengwa ni: uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji; matumizi bora ya teknolojia za umwagiliaji zenye ufanisi na tija; kutoa huduma za kitaalam kwa Halmashauri; kuandaa Mkakati na Sheria ya Umwagiliaji; na kukamilisha uanzishaji wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Jumla ya Shilingi milioni 409.85 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji, Wizara itaendeleza miradi ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 40,000 na hivyo kufanya eneo la umwagiliaji kuongezeka kutoka hekta 345,690 mwaka 2010/2011 hadi hekta 385,690 mwaka 2011/2012. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 24, mabwawa nane na mashamba mawili ya Wakala wa Mbegu za Kilimo ya Kilangali na Msimba (Kilosa) kwa kutumia fedha za Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Taifa (*National Irrigation Development Fund – NIDF*) ambapo Shilingi bilioni 10.60 zimetengwa katika kutekeleza kazi hizo. Aidha, skimu 136 zitaendelezwa kwa kutumia fedha za *DADPs* na Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji ngazi ya Wilaya (*District Irrigation Development Fund – DIDF*) ambapo Shilingi bilioni 32.89 zitatumika. Aidha, mitambo mikubwa 13 ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji iliyopo katika kanda za umwagiliaji itakarabatiwa kwa lengo la kuzipa kanda hizo uwezo zaidi wa kuongeza eneo la umwagiliaji. Jumla ya Shilingi milioni 140.62 zimetengwa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya umwagiliaji 95 yenye jumla ya hekta 70,500. Miradi hiyo itatoka katika kanda zote saba za umwagiliaji kama ifuatavyo: Morogoro (27); Tabora (9); Mwanza (8); Kilimanjaro (5); Mbeya (13); Mtwara (15); na Kanda ya Kati (18). Miradi ambayo tayari imefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu na kuwa kwenye hatua mbalimbali ni 122 yenye eneo la hekta 81,182. Miradi hiyo ikijumuishwa na ile itakayofanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2011/2012 itafanya jumla ya miradi iliyofanyiwa upembuzi yakinifu kufikia 217 na hivyo kufanya eneo lote lililofanyiwa upembuzi yakinifu kufikia hekta 151,682. Jumla ya Shilingi bilioni 1.036 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza eneo la umwagiliaji Wizara pia itaweka msukumo zaidi katika kutumia teknolojia za umwagiliaji zenye uwezo na ufanisi mkubwa katika matumizi ya maji. Teknolojia hizo ni pamoja na utumiaji wa mabomba kwa ajili ya kupitisha maji kutoka kwenye vyanzo; matumizi ya maji chini ya ardhi; matumizi ya pampu zinazotumia umeme na nishati mbadala ya jua na upepo; na umwagiliaji kwa njia ya matone na unyunyiziaji ambao utawezesha kwa kiasi kikubwa kuzalisha mazao yenye thamani kubwa (mbogamboga, zabibu, viungo, maua n.k.).

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya teknolojia hizo ni pamoja na kutumia maji kwa ufanisi zaidi; kuongeza tija na uzalishaji; kuongeza misimu ya kilimo kwa mwaka; na kuweza kulima mazao ya aina nyingi kwa mzunguko kwa mwaka (*crop rotation*). Utaratibu huo unawahakikishia wakulima usalama wa chakula na kuongeza pato la kaya. Mfano wa miradi ya aina hiyo ni pamoja na Misufini/Kochakindo hekta 50, Kyomu hekta 50 na Miwaleni hekta 100 (Moshi Vijijini); Kirya hekta 640 (Mwanga); Kisasida hekta 150 (Singida Manispaa); Chinangali hekta 200 (Chamwino); Mgama hekta 300, Wangama hekta 150, Tanangozi hekta 50 na Igingilanyi hekta 10 (Iringa Vijijini); Msoga hekta 200 (Bagamoyo); Nyatwali-Green Triangle Group hekta 5 (Bunda); Shirati-Bubombi Group hekta 5 (Rorya) na Gollan-Shuta-Shuta hekta 30 (Jiji la Tanga). Aidha, Wizara itatuma timu ya wataalam kwenda India kujifunza namna nchi hiyo ilivyoweza kuendeleza kilimo kwa kutumia teknolojia rahisi za umwagiliaji ikiwemo umwagiliaji kwa kutumia njia ya matone na matumizi ya nishati ya jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Taifa wa Umwagiliaji, Wizara yangu itafanya mapitio ya Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 ili kuuboresha kulingana na hali halisi na malengo ya Taifa ambayo ni pamoja na kupanua eneo la umwagiliaji kufikia hekta 1,000,000 na kujitosheleza kwa chakula (mpunga na mahindi) kwa kiwango cha asilimia 120 ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara itafanya utafiti katika masuala ya teknolojia mbalimbali za umwagiliaji zenye kuongeza na kuboresha uzalishaji na tija kwa mazao kutokana na matumizi ya maji ya umwagiliaji kwa ufanisi. Lengo ni kuhakikisha kuwepo kwa ufanisi na tija katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Pamoja na hatua hizi, Wizara itaanzisha Kituo cha Utafiti na Mafunzo mkoani Morogoro kwa ajili ya utafiti wa teknolojia za umwagiliaji. Lengo ni kuongeza uzalishaji na tija na matumizi ya maji ya umwagiliaji kwa ufanisi. Vilevile, Wizara itawezesha kufanyika tathmini ya mazingira (*Environmental and Social Impact Assessment-ESIA*) katika miradi 13 ya umwagiliaji katika kanda zote saba za umwagiliaji. Jumla ya shilingi milioni 400.58 zimetengwa kutekeleza kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza tija katika skimu za umwagiliaji, Wizara imedhamiria kuongeza tija katika uzalishaji wa mpunga kwa kiwango cha kati ya asilimia 75-100 kwa kuanza na skimu 27 za umwagiliaji katika awamu ya kwanza zenye jumla ya hekta 10,159. Skimu hizo zitakarabatiwa na ujenzi wake kukamilishwa kwa kutumia fedha za DIDF ambazo zimetengwa moja kwa moja katika bajeti za

Halmashauri na fedha za *NIDF*. Wakulima katika skimu hizo watawezeshwa kupitia ruzuku ya pembejeo na *DADPs* kupata mbolea, mbegu bora, huduma za ugani, zana za kilimo na elimu ya matumizi bora ya ardhi na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza thamani ya zao la mpunga, Wizara kwa msaada wa Serikali ya Japan, (*Japan Policy and Human Resource Development – PHRD Grant P125484)* itaongeza tija na uzalishaji wa zao la mpunga kwa kuwezesha wakulima katika skimu za umwagiliaji 20 zenye hekta 15,431 kuanza kulima zao hilo kibiashara. Wakulima wapatao 33,108 wa skimu hizo watawezeshwa kuongeza thamani ya zao la mpunga kwa kutumia mashine bora za kuvuna, kukoboa, kuchambua mawe na kupanga mchele kulingana na madaraja mbalimbali. Kiasi cha shilingi bilioni 10.945 zitatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo ya umwagiliaji kwa wataalam na wakulima, katika mwaka 2011/2012, Wizara itawezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 20 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 45 katika fani mbalimbali za umwagiliaji. Aidha, wakulima wa umwagiliaji 105 watapatiwa mafunzo kwa lengo la kuwawezesha kuzitambua na kuzitumia teknolojia mbalimbali zenye kutumia maji ya umwagiliaji kwa ufanisi na uzalishaji wa mazao wenye tija. Ili kufikia lengo hilo, Wizara itawawezesha Wahandisi wa umwagiliaji na Mafundi Sadifu (*Irrigation Technicians*) wa umwagiliaji kupata mafunzo katika Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji (*Water Development and Management Institute – WDMI*), Chuo cha Ufundi cha Arusha (*Arusha Technical College - ATC*), Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (*SUA*) na MATI Igurusi – Mbeya. Lengo ni kuongeza upatikanaji wa watumishi wa fani hiyo kwa ajili ya kusimamia ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na matumizi bora ya maji ya umwagiliaji. Jumla ya shilingi milioni 613.25 zimetengwa kwa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kupunguza tatizo la upungufu wa wataalam wa umwagiliaji, Wizara inatarajia kupata wataalam 18 kutoka Vietnam kupitia mpango wa *South South Cooperation*. Kati ya wataalam hao, Wahandisi wa Umwagiliaji watakuwa sita na Mafundi Sadifu 12. Hatua hiyo ni ya muda mfupi wakati Wizara inaendelea kujenga uwezo. Jumla ya Shilingi milioni 61.47 zimetengwa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano kati ya Tanzania na Japan, Wizara itaendelea kutekeleza awamu ya pili ya Mradi wa Ushirikiano wa Kitaalam kati ya Tanzania na Japan (*Tanzania Japan Technical Cooperation Project-TCP*). Katika awamu hii, utekelezaji utahusisha kufundisha wataalam wa umwagiliaji na wakulima namna ya kutumia miongozo ya umwagiliaji iliyoandaliwa katika awamu ya kwanza. Mafunzo hayo yatatolewa katika skimu saba za umwagiliaji za mfano zilizochaguliwa kutoka katika kila kanda ya umwagiliaji. Skimu hizo ni Mvumi (Kilosa); Kivulini (Mwanga); Bahi-Sokoni (Bahi); Inala (Tabora Manispaa); Mahiga (Kwimba); Mshewe (Mbeya); na Narunyu (Lindi Vijijini). Wataalam wa kanda za umwagiliaji na Halmashauri husika pamoja na wakulima 13,468 watanufaika na mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo na zana za kilimo, katika kuharakisha mapinduzi ya kijani, matumizi ya pembejeo na zana bora za kilimo ni muhimu katika kuongeza uzalishaji na tija. Hata hivyo, matumizi ya pembejeo na zana za kilimo ni madogo hapa nchini kutokana na sababu mbalimbali hususan gharama kubwa ya pembejeo na zana na hivyo kufanya mkulima mdogo kushindwa kumudu gharama hizo. Kutokana na hali hiyo Serikali ilianzisha utaratibu wa kutoa ruzuku mwaka 2003/2004 ili kumwezesha mkulima kupata pembejeo na zana kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Ruzuku. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kugharamia ruzuku ya mbolea, mbegu bora, miche bora ya kahawa na chai pamoja na madawa ya pamba na korosho. Idadi ya wakulima watakaonufaika na mpango wa ruzuku kwa mazao ya chakula kwa utaratibu wa vocha ni 1,800,000. Aidha, jumla ya mbolea itakayotolewa kwa utaratibu wa ruzuku ni tani 180,000 na mbegu bora kwa mazao ya mpunga na mahindi ni tani 18,157. Idadi ya wakulima wanufaika kwa mazao ya chakula itapungua ikilinganishwa na idadi ya wakulima 2,000,000 wa mwaka 2010/2011 kutokana na ufinyu wa bajeti. Aidha, wakulima 737,000 walioanza kupata ruzuku tangu mwaka 2008/2009 kwa utaratibu wa vocha wametimiza miaka mitatu ya kupata ruzuku na hivyo, tunaamini kuwa wakulima hao wana uwezo wa kununua pembejeo bila kutegemea tena ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia itaendelea kutoa ruzuku kwa mbegu bora za mtama tani 356, ambapo wakulima wapatao 127,300 kutoka Mikoa yenye ukame ya Dodoma, Shinyanga, Singida, Tabora, Mwanza na Mara watanufaika. Aidha, mikoa ya Shinyanga na Singida itapata mbegu za alizeti tani 50 kwa utaratibu wa ruzuku. Wizara pia itatoa ruzuku kwenye miche ya chai na kahawa. Jumla ya miche

milioni 10 ya kahawa na milioni 10 ya chai itazalishwa na kusambazwa. Aidha, ruzuku itatolewa kwa ajili ya tani 19,475 za mbegu za pamba na *acrepack* 3,324,200 za madawa ya pamba. Ruzuku pia itatolewa kwa madawa ya korosho tani 64,000. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa mpango wa ruzuku ni Shilingi bilioni 136.67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa Mbegu Bora. Kwa ujumla mahitaji ya mbegu bora nchini ni makubwa. Mahitaji ya mbegu bora za nafaka, mikunde na mbegu za mafuta iwapo kila mkulima atatumia mbegu bora (*potential demand*) ni tani 120,000 kwa mwaka. Aidha, mahitaji halisi (*actual demand*) ya mbegu yanakadiriwa kuwa tani 60,000 kwa mwaka. Hata hivyo, uzalishaji wa mbegu bora nchini kwa sasa ni tani 13,828 tu, hivyo Wizara itatekeleza mpango wa kuongeza uzalishaji wa mbegu bora nchini kwa lengo la kufikia angalau tani 60,000 kwa mwaka katika kipindi cha miaka mitatu. Maeneo ya utekelezaji yatakayozingatiwa ni pamoja na kuongeza uwezo wa *ASA* wa kuzalisha mbegu kwa wingi kwa kufufua mashamba ya mbegu ya Serikali ikiwa ni pamoja na kupanua eneo linalolimwa na kuweka miundombinu ya umwagiliaji ili kuwezesha uzalishaji wa mbegu kufanyika mpaka mara tatu kwa mwaka; kuiwezesha *ASA* kuingia mikataba na makampuni ya mbegu ya Tanzania ili kuzalisha mbegu za msingi; kuhamasisha na kuyawezesha makampuni binafsi ya Tanzania kuanzisha mashamba ya mbegu au kuingia ubia na Serikali; na kuruhusu Sekta binafsi (Makampuni Binafsi) kuzalisha mbegu za msingi kwa kutumia mbegu mama zinazozalishwa na Vituo vya Utafiti vya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo itaongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 1,881 msimu wa 2010/2011 hadi tani 4,000. Pia, kwa kupitia utaratibu wa makubaliano yaliyopo kati ya *ASA* na Jeshi la Magereza/Jeshi la Kujenga Taifa *(JKT)*, jumla ya tani 3,000 za mbegu bora zitazalishwa. Sekta binafsi inatarajiwa kuzalisha tani 15,000. Hivyo, uzalishaji wa mbegu bora nchini unatarajiwa kufikia tani 22,000. Miche ya matunda 200,000 na vipando vya mihogo 25,000,000 vitazalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa mashamba matatu ya mbegu ya Arusha (hekta 50), Msimba (hekta 100) na Kilangali (hekta 200) utaendelea ambapo ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji utafanyika ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mbegu katika msimu wa uzalishaji. Jumla ya Shilingi bilioni 7.28 zimetengwa kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu (*Tanzania Official Seed Certification Institute- TOSCI*) itakagua jumla ya hekta 6,000 za mashamba ya mbegu za mazao mbalimbali ya makampuni binafsi, ASA na wakulima wanaozalisha Mbegu za Daraja la Kuazimiwa (*QDS*). Aidha, kazi nyingine zitakazofanyika ni pamoja na kupima ubora wa mbegu zinazozalishwa nchini na zinazoingizwa nchini kiasi cha takriban tani 18,000; kuthibitisha uhalisia wa aina 30 za mbegu mpya; na kukamilisha maandalizi ya taratibu za kujiunga na mashirika ya *Organisation for Economic Cooperation and Development (OECD), International Seed Testing Agency (ISTA)* na *The International Union for the Protection of New Varieties of Plants - UPOV* ili mbegu zinazozalishwa nchini ziweze kufikia viwango vya ubora vinavyokubalika Kimataifa. Katika kufanikisha hilo, Wizara itaijengea uwezo *TOSCI* kwa kununua vifaa vya maabara, madawa na jenereta ili kuiwezesha kutekeleza wajibu wake wa ukaguzi wa ubora wa mbegu zilizoko sokoni katika Halmashauri za Wilaya 40 ili kukabiliana na tatizo la mbegu zisizo na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zana za kilimo. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuhamasisha matumizi ya zana bora na mashine za usindikaji mazao ya kilimo kibiashara. Aidha, kwa kushirikiana na *Center for Agricultural Mechanization and Rural Technology (CAMARTEC), Tanzania Automotive Technology Center (TATC)* na *Mzinga Corporation* itaendeleza teknolojia zilizobuniwa kwenye Taasisi za utafiti katika Halmashauri 10. Halmashauri hizo ni Korogwe, Muheza, Handeni, Morogoro Vijijini, Kilosa, Newala, Tandahimba, Masasi, Nanyumbu na Lindi Vijijini. Mashine sita za kuchuna katani (*decorticator*) na mashine 30 za kubangua korosho zitanunuliwa na mafunzo juu ya uendeshaji wa mashine hizo yatatolewa katika Halmashauri husika; kazi hiyo imetengewa Shilingi milioni 36.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, *CAMARTEC, SUA, TATC, MZINGA*, Shirika la Viwanda Vidogo na Tume ya Sayansi na Teknolojia kuandaa taratibu za usimamizi wa ubora wa mashine za kilimo zinazoingizwa nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Mtwara Vijijini, Kibaha, Mbarali na Singida itaanzisha na kuendeleza viwanda vinne vidogo vyenye uwezo wa kusindika tani 10 za muhogo kwa siku. Fedha iliyotengwa kwa kazi hiyo ni Shilingi milioni

119. Vilevile, Wizara itahamasisha matumizi ya zana zinazoendeshwa na matrekta madogo ya mkono kwa kutoa mafunzo kwa wakulima katika skimu 40 za umwagiliaji. Mafunzo hayo yatahusu matumizi ya mashine za kukata mpunga; kupura mpunga na za kunyunyizia dawa. Fedha iliyotengwa kwa kazi hiyo ni Shilingi milioni 81.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara, itaendeleza na kutoa msukumo wa matumizi ya zana za kilimo hifadhi zinazokokotwa na trekta dogo la mkono (kipandio na tindo) kwenye Halmashauri 10 na kuhamasisha utengenezaji wa zana hizo hapa nchini. Halmashauri zitakazohusika ni Karatu, Arusha, Meru, Babati, Hanang, Handeni, Kiteto, Kongwa, Kilosa na Mvomero. Fedha iliyotengwa kwa kazi hiyo ni Shilingi milioni 105. Aidha, Wizara itatathmini mahitaji ya nguvu za mashine za kilimo kwenye kanda nne za kilimo za Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kati na Kanda ya Magharibi ikijumuisha kukusanya takwimu, kuzihakiki na kuzihifadhi. Fedha iliyotengwa kwa kazi hiyo ni Shilingi milioni 37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itatoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wataalam 15 wa zana kuhusu mashine za kilimo, usindikaji mazao ya kilimo na nishati jadidifu *(renewable energy)*. Fedha iliyotengwa kwa kazi hiyo ni Shilingi milioni 106.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Pembejeo. Katika mwaka 2011/2012, Mfuko wa Pembejeo utatoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 6.7 ikiwemo mikopo ya matrekta mapya makubwa 119 yenye thamani ya Shilingi bilion 4.76; matrekta madogo ya mkono (*power tiller*) yenye thamani ya Shilingi milioni 900; pembejeo za kilimo na mifugo (mbolea, mbegu, vifungashi, sumu na madawa ya mimea na mifugo) kwa wasambazaji 65 yenye thamani ya Shilingi milioni 744.74; vifaa vya umwagiliaji vyenye thamani ya Shilingi milioni 160; na vifaa vya usindikaji vyenye thamani ya Shilingi milioni 180.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Kitaalam. Utafiti wa Kilimo. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kupitia vituo vyake vya utafiti itaendelea kutafiti aina za mbegu mpya za mazao zenye sifa za kuzaa sana, kukomaa mapema, kustahimili ukame, zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea na zinazokidhi viwango vya ubora na matakwa ya wadau na soko. Lengo ni kupata mbegu bora ambazo mkulima akizitumia atavuna mazao mengi hivyo kujitosheleza kwa chakula na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara inatarajia kutoa angalau aina tano za mbegu bora za mazao mbalimbali ya nafaka, jamii ya mikunde, mbogamboga na matunda. Vilevile, Wizara itaendelea kutafiti mbinu bora za kilimo cha uzalishaji wa mazao mbalimbali katika maeneo husika kufuatana na ikolojia yanapolimwa katika kanda zote saba ili kuweza kupata angalau teknolojia bora tano za agronomia. Wizara inategemea kupata angalau teknolojia aina tatu za kudhibiti visumbufu vya mimea pamoja na madawa ya asilia na ya viwandani. Katika kutekeleza hayo mbinu za ushirikishwaji wa wadau zitatumika ikiwa ni pamoja na kufanya utafiti kwa kutumia mashamba ya wakulima (*on-farm research*); shilingi milioni 902.76 zitatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuzalisha Mbegu Mama (*Breeder's Seeds*). Wizara itaendelea kuhifadhi na kuzalisha mbegu mama tani 30 za mazao ya jamii za nafaka, mikunde, mbegu za mafuta na vipingili 1,000,000 vya mazao ya mizizi. Mbegu mama ni chanzo cha mbegu bora ambazo zikizalishwa katika daraja la mbegu za msingi, zitawezesha kuzalisha mbegu zilizothibitishwa na kuweza kumpatia mkulima mbegu bora. Jumla ya Shilingi milioni 152.38 zimetengwa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa udongo na rutuba ya ardhi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara, kupitia vituo vya utafiti vya Mlingano, Uyole, Selian na Ukiriguru itahakiki na kupendekeza teknolojia angalau tano za urutubishaji husishi wa udongo (*Integrated Soil Fertility Management options*) kulingana na ikolojia za kilimo zilizoko katika Wilaya 53 ambazo zinapata ruzuku ya pembejeo. Lengo ni kuwezesha wakulima kutumia aina na viwango sahihi vya mbolea kulingana na aina ya udongo katika maeneo yao. Aidha, Wizara itaendelea kutathmini hali ya udongo wa maeneo mbalimbali na kutoa ushauri wa matumizi sahihi ikiwa ni pamoja na kuhakiki na kutoa mapendekezo kuhusu viwango vya matumizi ya mbolea. Jumla ya Shilingi milioni 486.13 zitatumika kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji wa uratibu wa utafiti nchini. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendeleza mchakato wa uanzishwaji wa Taasisi inayojitegemea ya Utafiti wa Kilimo ili kuboresha utafiti na kuhakikisha kuwa teknolojia zinamfikia mkulima. Jumla ya Shilingi milioni 91.70 zimetengwa ili kutekeleza mchakato huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa mifumo ya kilimo na Sayansi ya Jamii. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kufanya uchambuzi wa gharama na mapato (*farm budgets*) inayopatikana katika kilimo kwenye ngazi ya wakulima vijijini ili kuwaonesha wakulima faida ya matumizi bora ya teknolojia kwa lengo la kuwawezesha kuchagua aina ya teknolojia zinazowafaa. Ili kujua kiwango na mafanikio yanayopatikana katika teknolojia zilizopelekwa kwa wakulima, Wizara itafanya tathmini za mafanikio ya upokeaji wa teknolojia. Shilingi milioni 367.00 zimetengwa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha Vituo na Kuimarisha Uwezo wa Watafiti. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia ASDP na Programu ya Kilimo ya Kuendeleza Tija na Uzalishaji katika Afrika ya Mashariki (*Eastern Africa Agricultural Productivity Programme – EAAPP*), itaendelea kukarabati baadhi ya nyumba za kuishi wafanyakazi wa vituo vya Selian kwa kujenga nyumba mpya moja, kufanya ukarabati wa nyumba moja kituo cha Ilonga na kujenga miundombinu ya vituo vya KATRIN pamoja na Ukiriguru ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi watafiti. Katika kuhakikisha teknolojia zinapatikana haraka kwa muda mfupi, vituo vya KATRIN, Ukiriguru na Dakawa vitajengewa mifumo ya umwagiliaji katika mashamba ya majaribio. Vilevile, Wizara itaendelea kupunguza matatizo ya vitendea kazi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa magari matano, pikipiki 15 na ukarabati wa nyumba mbili. Aidha, watafiti 11 wakiwemo tisa wa shahada za uzamili na wawili wenye shahada ya uzamivu watahitimu masomo yao. Pamoja na hao, jumla ya watafiti 60 watajengewa uwezo katika mafunzo ya muda mrefu. Kati ya hao watafiti 46 watapata ufadhili kutoka fedha zilizotengwa na Serikali kupitia *COSTECH*. Vilevile, watafiti na watumishi wengine wapatao 100 watapatiwa mafunzo mbalimbali kulingana na fani zao. Jumla ya Shilingi bilioni 2.54 zimetengwa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kufanya marekebisho ya kanuni za kusimamia matumizi salama ya bayoteknolojia (*biotechnology*) ili kuweka mazingira mazuri ya kuhawilisha na kuendeleza utafiti na matumizi ya taaluma ya uhandisi jeni (*Genetic Engineering*) katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za Ugani. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itashirikiana na TAMISEMI kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima kwa kuboresha uenezaji wa teknolojia kwa kutumia mbinu shirikishi jamii katika kilimo. Mbinu shirikishi katika kilimo zitaongeza matumizi ya Shamba Darasa kutoka mashamba 6,393 yenye wakulima 157,782 mwaka 2010/2011 hadi 9,500 yenye wakulima 237,500 katika Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Programu ya Kilimo ya Kuendeleza Tija na Uzalishaji katika Afrika ya Mashariki itatoa mafunzo kwa wakulima 280 na wataalam wa ugani 150 katika maeneo yanayozalisha mpunga, muhogo na ngano; na pia itahamasisha uanzishaji na uendelezaji wa vikundi vya usindikaji 10 katika mazao hayo katika mikoa ya Kanda ya Kusini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Mashariki na Kanda ya Kaskazini. Aidha, Wizara itaboresha uandaaji na uenezaji wa teknolojia sahihi katika kilimo hususan kwa mazao ya mpunga, muhogo na ngano kwa kutumia vipindi 36 vya redio na vipindi vinane vya *TV*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaboresha Kitengo cha Ukulima wa Kisasa ili kiweze kutoa elimu bora kwa wadau kwa njia ya redio, *TV* na machapisho na kusambaza teknolojia 20 za mazao mbalimbali hususan mpunga, mahindi, mtama, muhogo, mbegu za mafuta, mbogamboga na matunda katika Vituo vya Taaluma vya Kata 127 na Ofisi Kiungo za Mawasiliano za Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa kutumia mkulima kiongozi kuwafundisha wakulima wenzake (*Farmer-to-Farmer Extension*) utaimarishwa kwa kutoa mafunzo kwa wakulima ili waweze kusimamia uzalishaji wa mpunga katika skimu 27 za umwagiliaji katika mikoa 17 na wakulima wa mazao ya mahindi, muhogo, matunda, mbogamboga na mazao ya mbegu za mafuta. Vilevile, elimu kwa wakulima itatolewa kupitia vipindi vya redio, vijitabu, machapisho, vipeperushi, mabango na sinema vijijini kwa kuzingatia kanda za kilimo kwa kutumia Ofisi Kiungo za Mawasiliano za Kanda. Pia, Wizara itawezesha maonyesho ya teknolojia mbalimbali katika maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nane Nane na Siku ya Chakula Duniani na Miaka 50 ya Uhuru. kupitia mpango huo, kazi hizo zimetengewa kiasi cha Shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itadahili na kufundisha vijana 3,500 ngazi ya Stashahada na Astashahada kwa ajili ya kuongeza idadi ya Maafisa Ugani. Kazi hiyo itagharimu Shilingi bilioni 3.59. Aidha, Wizara itakarabati mabweni mawili ya Chuo cha Mbondo (Kigoma) ili kuweza kupokea wanafunzi 80 kuanzia Novemba - Desemba 2011. Kazi hiyo itagharimu Shilingi milioni 139.94. Vilevile, Wizara itanunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuboresha mazingira ya mafunzo kwenye chuo cha *MATI* Igurusi kwa kununua vifaa vya teknolojia ya kisasa vya kufundishia somo la umwagiliaji na matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itawajengea uwezo wafanyakazi wa kilimo kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ambapo watumishi 150 watapata mafunzo katika fani mbalimbali. Kazi hiyo itagharimu Shilingi milioni 287. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI itatoa mafunzo ya kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima wa zao la mpunga katika skimu 12 za umwagiliaji. Lengo ni kuongeza tija ya uzalishaji wa mpunga kufikia tani 5 kwa hekta; kazi hiyo imetengewa Shilingi milioni 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea na udhibiti wa milipuko ya visumbufu mbalimbali ikiwemo ya nzige wekundu, kwelea kwelea, viwavijeshi na panya. Jumla ya Shilingi bilioni 2.99 zimetengwa kwa kazi hiyo. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha uwezo wake wa kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Mimea kwa kutoa mafunzo kwa wakaguzi na kuajiri wakaguzi 52 wa mazao na madawa ya mimea ili wasimamie ipasavyo utekelezaji wa sheria hiyo kwa ufanisi zaidi. Aidha, Wizara itatoa huduma ya karantini ya mimea na mazao ili kuepukana na athari ya kuenea kwa visumbufu. Ili kukidhi viwango vya ubora unaotakiwa na masoko ya nje na kudhibiti uingizaji wa magonjwa ya mazao nchini, Wizara itaimarisha huduma ya ukaguzi wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa mazao ya kilimo. Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Biashara. Wizara kupitia Bodi za Mazao Makuu ya Biashara itatekeleza mikakati inayolenga kuongeza tija, uzalishaji na ubora wa mazao. Juhudi maalum zitaelekezwa katika kuhakikisha wakulima wanapata bei ya haki kulingana na nguvu ya soko, na gharama za uzalishaji, hivyo Wizara itafanya tathmini ya makato yote yanayofanyika wakati wa kukokotoa bei za wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Bodi za Mazao zitaendelea kutoa huduma za elimu ya kilimo bora cha mazao hayo moja kwa moja kwa wakulima au kupitia kwa wataalam wa ugani katika Halmashauri zinazozalisha mazao hayo, kusimamia sheria na kanuni za uzalishaji na biashara ya mazao hayo na kuwapatia wakulima taarifa za bei dira za mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha mfumo wa masoko wa mazao, Wizara itashirikiana na Wizara za Kisekta, Wizara ya Fedha na wadau wengine kuandaa utaratibu utakaohakikisha kunakuwepo na mfumo rasmi wa masoko ya mazao ya wakulima kwa kutumia utaratibu wa *Commodity Exchange Markets*. Mfumo huo utaanza kutekelezwa katika mazao ambayo tayari yana mifumo ya ushirika na utaratibu wa kuuza mazao kupitia Stakabadhi za Maghala. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya Bodi za Mazao ili kutekeleza majukumu hayo ni Shilingi bilioni 8.19. Pamoja na hatua hizi Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imeanzisha kikosi kazi cha kuharakisha mchakato wa uanzishaji wa mfumo wa kuuza mazao kupitia *Commodity Exchange.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba, matarajio ya uzalishaji wa pamba msimu wa 2011/2012 ni tani 250,000 za pamba mbegu kutoka katika hekta 469,345 zilizolimwa. Ongezeko la uzalishaji unaotarajiwa utachangiwa na bei waliolipwa wakulima msimu 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti. Tumbaku, katika mwaka 2011/2012, tani 93,000 za tumbaku zinatarajiwa kuzalishwa ikilinganishwa na tani 130,000 zilizozalishwa mwaka 2010/2011. Hali hiyo inatokana na kuwepo kwa tumbaku nyingi katika masoko asilia ya tumbaku ya Tanzania hususan masoko ya Ulaya, Marekani na Japan ikilinganishwa na mahitaji. Kutokana na tatizo hilo la soko, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara itaendelea kutafuta masoko mengine duniani ili kupanua wigo wa soko la tumbaku ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pareto, lengo la uzalishaji wa pareto katika mwaka 2011/2012 ni tani 5,600. Lengo hilo linatarajiwa kufikiwa kutokana na upatikanaji wa miche bora, kuimarisha huduma za ugani, kuimarisha utafiti katika Kituo cha Uyole na kuongeza ubora wa maua. Aidha, wastani wa tani 4,000

za pareto zinatarajiwa kusindikwa na kutoa wastani wa kilo 160,000 za sumu ghafi zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 9.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chai, katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa chai unatarajiwa kufikia tani 35,000. Uzalishaji huo utachangiwa na ujenzi wa Kiwanda cha Kusindika majani mabichi ya chai katika Tarafa ya Lupembe unaofanywa na Kampuni ya Chai na Kahawa ya Mufindi (*Mufindi Tea and Coffee Company Limited*), kufufuliwa kwa mashamba ya Mlangali ambayo huchangia tani 300 za chai kwa mwaka na kuhamasisha matumizi ya pembejeo kwa wakulima wadogo wa chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari, katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa miwa unatarajiwa kufikia tani milioni 3.28 ikiwa ni sawa na tani 317,000 za sukari. Ongezeko hilo litafikiwa kutokana na uhamasishaji wa uzalishaji wa mashamba makubwa (*block farming*), kuimarisha utafiti wa mbegu mpya za miwa zilizoagizwa kutoka Afrika ya Kusini, Mauritius na Reunion chini ya usimamizi wa Kituo cha Utafiti wa Miwa (*Sugar Research Institute-SRI*) na kuhamasisha matumizi endelevu ya zao la miwa ili liweze kutumika katika kuzalisha nishati mbadala ya *ethanol* pamoja na umeme (*co-generation*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa, katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa kahawa unatarajiwa kupungua kutoka tani 60,575 za mwaka 2010/2011 hadi tani 45,000. Upungufu huo unatokana na tabia ya zao la kahawa kupungua uzalishaji katika msimu unaofuatia msimu wa uzalishaji ulioongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkonge, katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa zao la mkonge unatarajiwa kuwa tani 35,000 sawa na msimu wa 2010/2011 kutokana na tatizo la umeme katika viwanda vya usokotaji wa mkonge. Aidha, uzalishaji wa mbegu za mkonge kwa kutumia teknolojia ya vikonyo (*meristematic tissue culture*) utaimarishwa; kuendeleza soko la mkonge na bidhaa zake ndani na nje ya nchi, kushirikiana na vituo vya utafiti na vyuo vikuu ili kuongeza teknolojia na utaalam katika hatua za uzalishaji (upandaji, palizi, uvunaji) na uzalishaji wa bidhaa za mkonge na kuendeleza kilimo cha mkataba kati ya wakulima wadogo na Kampuni ya Katani *Ltd*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho, katika msimu wa 2011/2012, matarajio ni kuongeza uzalishaji kutoka tani 121,070 za msimu 2010/2011 hadi tani 127,000 za korosho ghafi. Lengo hilo linatarajiwa kufikiwa kutokana na kuongezeka kwa bei ya korosho msimu uliopita iliyosababishwa na matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala na uhamasishaji wa matumizi ya korosho na mazao yake nchini na nje ya nchi. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha ongezeko la uwezo wa ubanguaji korosho nchini hadi kufikia wastani wa asilimia 40 mpaka 45 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 30 hadi 40 kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa mazao ya bustani. Mazao ya bustani yana umuhimu mkubwa katika kuboresha lishe na katika kuongeza kipato kwa wakulima na kulipatia Taifa fedha za kigeni hasa kwa sababu mazao hayo yana thamani kubwa. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaandaa Programu ya Kitaifa ya kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Mazao ya Bustani na kusimamia utekelezaji wake. Aidha, Wizara itaimarisha bustani za Mpiji, Bugaga, Igurusi, Jaegetal, Kizugu na Songa ili kuhifadhi vinasaba vya mazao ya bustani kwa ajili ya utafiti na uzalishaji wa miche bora. Vilevile, Wizara itaendelea kuingiza nchini vinasaba bora zaidi vya mazao ya bustani kwa ajili ya kuboresha vinasaba vilivyopo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia itaendelea kuainisha na kuwasajili wazalishaji wa miche ya mazao ya bustani na kuwajengea uwezo kimafunzo ili wazalishe miche bora itakayoongeza uzalishaji na ubora wa mazao. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuendeleza mazao ya bustani katika nyanja mbalimbali zikiwemo: kuanzisha vituo vya ukusanyaji na uhifadhi wa mazao ya bustani; kuimarisha mfumo wa upatikanaji na usambazaji wa taarifa za masoko na bei ya mazao ya bustani; kuimarisha uwezo wa Chuo cha *HORTI* - Tengeru ili kitoe mafunzo yanayolingana na mahitaji ya wadau kwa mazingira ya sasa; na kushiriki katika maonyesho mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kutangaza na kupanua wigo wa soko la bidhaa za Tanzania za mazao ya bustani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu za mafuta. Wizara inatambua umuhimu wa kuendeleza mazao ya mbegu za mafuta ili kuzalisha mafuta ya kula kwa lengo la kukidhi mahitaji ya soko la ndani na hivyo kupunguza uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi na ikiwezekana kuuza ziada nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kusimamia utafiti na kuhamasisha uzalishaji wa mbegu za mafuta. Aidha, itaratibu na kuwaunganisha wadau wote wa sekta ndogo ya mazao ya mbegu za mafuta za ufuta, alizeti, karanga, kartamu *(safflower),* pamba, michikichi na soya pamoja na kusaidia katika kuanzisha umoja kati yao ili kuwa na uzalishaji endelevu na wa kibiashara kwa mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa chakula. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itafanya savei tatu za utabiri wa uzalishaji wa mazao ya chakula ili kubaini hali ya chakula nchini na hatua za kuchukuliwa. Aidha, kwa kushirikiana na wadau wa usalama wa chakula itafanya tathmini za kina za hali ya chakula kwa lengo la kutambua kaya zenye upungufu wa chakula na kupendekeza hatua za kukabiliana na upungufu huo. Wizara itakusanya takwimu za hali ya mazao na mvua katika vituo 600 na kutoa ushauri na pia itaainisha na kusambaza teknolojia mbalimbali za kuhifadhi mazao ya chakula. Shilingi milioni 550 zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya chakula. Katika mwaka 2011/2012, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula imepanga kununua tani 200,000 za nafaka kutoka Mikoa ya Rukwa, Iringa, Mbeya, Ruvuma na Kigoma na kuzihifadhi katika maghala yake ili kukabiliana na upungufu wa chakula utakaoweza kujitokeza. Jumla ya Shilingi bilioni 17.6 zimetengwa katika bajeti kwa ajili ya kazi hiyo. Aidha, fedha nyingine zinategemewa kutokana na mauzo ya mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi bora ya ardhi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itatoa mafunzo ya kitaalam kwa maafisa 10 wa Kanda na 44 kutoka Halmashauri za Wilaya za Moshi Vijijini, Bahi, Kongwa, Kondoa, Chamwino, Kishapu, Meatu, Bariadi, Maswa, Igunga, Iramba na Singida Vijijini. Nyingine ni Kisarawe, Kilwa, Kilosa, Mvomero, Morogoro Vijijini, Handeni, Kilombero, Ngara, Karagwe na Misenyi. Mafunzo hayo yatahusu teknolojia za hifadhi ya udongo na maji mashambani na jinsi ya kuibua miradi ya matumizi bora ya ardhi ya kilimo katika Halmashauri hizo. Kazi hiyo imetengewa Shilingi milioni 114.28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na *FAO* kutekeleza mradi wa *Globally Important Agricultural Heritage Systems* unaolenga kuainisha mifumo mbalimbali asilia ya kilimo na ufugaji endelevu katika Mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro na Ruvuma. Katika mwaka 2011/2012, shughuli za mradi huo zitatekelezwa katika Wilaya za Moshi Vijijini, Kata ya Uru, Kijiji cha Uru Shimbwe na Ngorongoro katika Kijiji cha Engarasero ambapo mafunzo yatatolewa kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya teknolojia za kilimo mseto, matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo na mbinu za kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha kuongezeka kwa joto duniani. Jumla ya Shilingi milioni 28.51 zimetengwa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuchochea kasi ya uwekezaji katika kilimo cha kibiashara, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Sekretarieti za Mikoa na Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi itaendelea kutambua na kupima maeneo yanayofaa kwa kilimo cha kibiashara katika vijiji 10 vya mikoa ya Morogoro na Pwani vilivyoandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili hatimaye yajumuishwe kwenye benki ya ardhi (*Land Bank*). Aidha, mipaka ya maeneo ya kituo cha Mabogini (Moshi Vijijini), kituo cha majaribio Magugu (Babati), shamba la majaribio Ngaramtoni (Arusha Mjini), Shamba la mbegu Dabaga (Kilolo), shamba la Mpiji (Bagamoyo) na Taasisi ya Utafiti wa Madawa ya Visumbufu vya Tropiki (*Tropical Pesticides Research Institute-TPRI)* (Arusha), itahuishwa na kupimwa ili yapatiwe hati miliki ya ardhi ya Serikali. Fedha zilizotengwa kwa kazi hiyo ni Shilingi milioni 84.63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi ya mazingira. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuratibu, kudhibiti na kuhamasisha shughuli za hifadhi ya mazingira katika maendeleo ya kilimo. Wizara pia itatoa mafunzo kwa Halmashauri kuhusu masuala ya hifadhi ya mazingira katika kilimo kwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Vilevile, Wizara itafanya tathmini ya athari za shughuli za kilimo kwenye mazingira katika skimu za umwagiliaji zilizopo katika Wilaya za Kwimba, Nzega, Mpwapwa, Mbarali, Kilolo, Mtwara Vijijini, Kilosa na Moshi Vijijini. Jumla ya Shilingi milioni 47.56 zimetengwa kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya rasilimali watu. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itapandisha cheo watumishi 290 katika madaraja mbalimbali na kuajiri watumishi wapya 588 wa kada mbalimbali. Kati yao 142 ni Wahandisi wa Umwagiliaji, 52 ni Wakaguzi wa mazao, 60 ni Watafiti, 15 ni Wahandisi wa zana za kilimo na waliobaki 319 ni wa kada nyingine. Aidha, Wizara itashirikiana na TAMISEMI

kuajiri wagani 5,089 (wakiwemo 4,291 wa Astashahada na Stashahada; na 798 wa Shahada) na Maafisa Ushirika 435 waliohitimu mwaka 2010 na 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kuwawezesha watumishi 17 wanaoishi hivi sasa na VVU na watakaojitokeza kupata lishe bora na matibabu. Kazi hiyo itagharimu Shilingi milioni 30. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia Mfumo wa Wazi wa Tathmini ya Utendaji Kazi *(OPRAS)* katika vituo vyote vya Wizara. Kazi hiyo itagharimu Shilingi milioni 30. Vilevile, Wizara itaendelea kufanya ukaguzi wa watumishi (*Human Resources Audit*) ili kuiwezesha Wizara kusimamia vyema ankara ya mishahara na kupanga matumizi bora ya rasilimali watu; kazi hiyo itagharimu Shilingi milioni 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio ya Sekta ya Ushirika, sekta hiyo inaendelea kukabiliwa na vikwazo vingi ikiwa ni pamoja na idadi ndogo ya Maafisa Ushirika ikilinganishwa na idadi ya Vyama vya Ushirika. Kwa sasa Afisa Ushirika mmoja anasimamia vyama 17 ikilinganishwa na uwiano unaotakiwa wa Afisa Ushirika mmoja kusimamia vyama saba. Pia, baadhi ya viongozi na watendaji wa Vyama vya Ushirika kukosa uaminifu na kutokuwajibika katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo; vyama vingi kukosa watendaji wenye sifa; na mitaji midogo katika kuendesha shughuli za vyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na vikwazo hivyo, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kutekeleza Programu Kabambe ya Mageuzi na Modenaizesheni ya Ushirika ikiwa ni pamoja na kutekeleza Sera, Sheria, Mikakati na usimamizi katika sekta ya Ushirika; kuimarisha na kuwezesha Asasi za Wananchi katika Ushirika; kuanzisha na kuijengea uwezo Tume ya Maendeleo ya Ushirika ikiwa ni pamoja na kuajiri maafisa ushirika 20 ili kutekeleza majukumu yake; kuimarisha Mfumo wa Ukusanyaji, Uhifadhi, Uchambuzi na Usambazaji wa takwimu na taarifa za Vyama vya Ushirika; kuimarisha utekelezaji endelevu wa Mkakati wa Taifa wa kupambana na rushwa; na kuboresha huduma na kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera, Sheria, Mikakati na Usimamizi katika Sekta ya Ushirika. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Ushirika kwa kuhamasisha wananchi wengi kujiunga na Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za uchumi; kuandikisha Vyama vya Ushirika imara kiuchumi na vyenye uwezo wa kujiendesha kibiashara; kuimarisha usimamizi na utawala wa fedha katika vyama vya ushirika wa akiba na mikopo *(SACCOS)* na mabenki ya Ushirika; kusimamia na kuendeleza maadili, misingi ya ushirika, utawala bora; na kusimamia manufaa yatokanayo na ushirika kwa wanachama wake na jamii. Aidha, Wizara itachukua hatua zenye lengo la kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Jumla ya vyama 100 vitasajiliwa; mafunzo yatatolewa kwenye vyama vya ushirika 350; na ukaguzi utafanyika kwenye Vyama vya Ushirika 3,900 na Benki mbili za Ushirika. Vilevile, miongozo mitatu ya ukaguzi na 14 ya usimamizi wa vyama vya ushirika itakamilishwa na kusambazwa kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya utekelezaji wa mpango huu ni kuwa na Vyama vya Ushirika imara kiuchumi vinavyojitegemea na vinavyoendeshwa kibiashara, kuweka nidhamu katika uendeshaji; kuimarisha uongozi; kuwepo kwa utawala bora; kudhibiti ubadhirifu ndani ya vyama kwa kuzingatia maadili ya uongozi; na kuwepo kwa taasisi imara za fedha za kiushirika. Aidha, kuunganisha au kufuta vyama dhaifu na kuondoa utitiri wa vyama vidogo vidogo katika kujenga vyama vikubwa vyenye nguvu na vitakavyokidhi mahitaji ya soko. Fedha iliyotengwa kwa kazi hiyo ni Shilingi bilioni 1.357.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga uwezo wa Asasi za Wananchi za Ushirika. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaendelea kuimarisha asasi za wananchi za ushirika kwa kuwezesha kuwepo kwa weledi, utaalam wa masoko na uongezaji wa thamani ya mazao katika Vyama vya Ushirika. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa Vyama vya Ushirika vya mazao 400, *SACCOS* 300 na Benki za Ushirika mbili. Mafunzo hayo yatahusu uzalishaji na masoko na utawala wa fedha ikiwemo ujenzi wa mitaji ya vyama na mikopo. Pia, vijana wanaoshiriki katika kilimo watahamasishwa kuunda Vyama vya Ushirika vya uzalishaji na kusaidiwa kupata mitaji na masoko. Fedha iliyotengwa kwa kazi hiyo ni Shilingi milioni 349.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itakamilisha mapendekezo ya Muswada wa kutunga Sheria ya kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika na kuijengea uwezo Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu na Taarifa za Vyama vya Ushirika. Katika mwaka 2011/2012, kwa kutambua umuhimu wa kuwa na takwimu sahihi katika kuendeleza ushirika, Wizara itaendelea kuboresha utaratibu wa kukusanya, kuchambua na kusambaza takwimu za ushirika kwa wadau. Mafunzo yatatolewa kwa Maafisa Ushirika 84 kutoka mikoa ya Arusha, Manyara, Kigoma, Singida, Tabora na Dodoma. Mafunzo hayo yatahusu ukusanyaji wa takwimu, kuzitumia na kuzihifadhi. Aidha, kompyuta moja itatolewa kwa kila mkoa kwa ajili ya kuhifadhi takwimu zitakazokusanywa. Fedha iliyotengwa kwa kazi hiyo ni Shilingi milioni 169.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa. Katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Rushwa, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa Watumishi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Wanaushirika wa vyama 15 kuhusu mkakati wa kuzuia rushwa. Katika kutekeleza mkakati huo, vijarida na vipeperushi vinavyoonesha madhara ya rushwa vitachapishwa na kusambazwa kwa watumishi na Wanaushirika. Fedha iliyotengwa kwa kazi hiyo ni Shilingi milioni 14.67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, UKIMWI. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itatoa elimu kwa watumishi 150 kuhusu kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI na itawahamasisha kupima kwa hiari. Aidha, wale watakaojitokeza kuhitaji huduma za lishe na matibabu watasaidiwa; kazi hiyo itagharimu Shilingi milioni 33.45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Kwanza, napenda kuzishukuru nchi za Japan, Ireland, China, India, Israel, Indonesia, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Ubelgiji na Uholanzi. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, CFC, AVRDC, AGRA, WARDA*, *Rockfeller Foundation* na *Bill and Melinda Gates Foundation*. Ushirikiano na misaada ya Nchi na Mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na mazingira magumu waliyonayo. Napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Buyungu; Katibu Mkuu Bwana Mohamed Said Muya; Naibu Katibu Mkuu Bibi Sophia Elias Kaduma; Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Mbogo Futakamba; Wakurugenzi wa Idara; Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; watumishi wote wa Wizara; na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2010/2011 kama nilivyofafanua katika hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2011/2012. Mwisho, natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kufanikisha kuchapishwa kwa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha za mpango kwa Mwaka 2011/2012. Kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe Shilingi 258,350,877,100 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Fungu 43. Kati ya fedha hizo, Shilingi 152,406,152,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 105,944,725,100 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Kati ya fedha za bajeti ya Maendeleo, Shilingi 14,260,042,000 ni fedha za ndani na Shilingi 91,684,683,100 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kupitia Fungu 24 inaomba Shilingi 6,660,012,000 kwa ajili ya shughuli za kuendeleza ushirika nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruksa yako, naomba nitoe Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na

Maji, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa mwaka wa Fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 1 na 2 Juni, 2011, Kamati ilikutana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar-es-salaam ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, maoni na ushauri wa Kamati kwa makisio ya mwaka wa fedha wa 2010/2011 pamoja na malengo na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 ambayo yaliambatana na maelezo ya maeneo ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ikiwa msimamizi wa Wizara hii, ilitoa maoni na ushauri wa kuzingatiwa wakati wa kujadili na kuchambua bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 kwa lengo la kuboresha sekta hii muhimu. Wizara imejitahidi kuyafanyia kazi maoni na ushauri wa Kamati. Baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo Kwanza. Katika kutekeleza dhana ya Kilimo kwanza, Wizara inatekeleza Kilimo Kwanza kupitia *Agricultural Sectoral Development Program (ASDP)* na utekelezaji wake umekuwa ukifanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa mwaka 2010/2011, Wizara ilitilia mkazo katika nguzo nne Kati ya 10 za Kilimo Kwanza ambazo ni Nguzo ya 4: Mabadiliko ya mfumo wa kimkakati wa Kilimo Kwanza; Nguzo ya 6: Vivutio kwa ajili ya Kilimo Kwanza; Nguzo ya 7: Viwanda kwa ajili ya Kilimo Kwanza na Nguzo ya 8: Sayansi, Teknolojia na Rasilimali Watu kwa ajili ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Utafiti. Kamati iliishauri Serikali kuviangalia kwa namna ya pekee Vituo vya Utafiti pamoja na watumishi wake. Wizara ilieleza kuwa kwa mwaka 2009/2010, Vituo vya Utafiti viliendelea kuboreshwa kwa kukarabati nyumba 20 za watumishi na kununua samani za ofisi za vituo tisa (9).

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mbegu. Kamati ilielezwa kwamba 70% ya mbegu zinazotumika nchini, zinaagizwa kutoka nje. Kamati iliiagiza Wizara ianze kuzalisha mbegu bora hapahapa nchini ili kupunguza gharama za kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi. Wizara inaimarisha Vituo vya Utafiti ili kuzalisha mbegu bora nchini, kwa kuhusisha makampuni binafsi ya mbegu na kuimarisha uwezo wa wakulima wadogo vijijini kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa *(QDS).*

(d) Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana, katika kuhakikisha Wizara inawawezesha vijana ili washiriki katika kilimo, Wizara ilieleza kuwa imeanza hatua ya awali yaani *pilot phase* kwa kushirikiana na Mikoa ya Lindi na Mtwara na imevipatia vikundi vya vijana mafunzo na seti 20 za mashine za kusindika mhogo.

Kamati inaona kwamba hakuna hatua madhubuti zilizochukuliwa kuwawezesha vijana kujiajiri katika kilimo. Kamati inasisitiza kwamba iandaliwe program maalum ya kuwawezesha vijana kujiajiri katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2010/2011, katika kutekeleza majukumu kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilikumbana na changamoto zifuatazo:-

(a) Mtiririko usioridhisha wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya kutekeleza kazi zilizopangwa;

(b) Ukosefu wa Mawakala wa kutosha, wenye uwezo wa kufikisha pembejeo za kilimo katika maeneo ya vijijini;

(c) Mahitaji makubwa ya wakulima kwa Mfuko wa Pembejeo, wakati bajeti ya Mfuko huo ni ndogo;

(d) Upungufu wa chakula katika baadhi ya maeneo kutokana na mafuriko na ukame;

(e) Idadi ndogo ya Maafisa Ushirika ikilinganishwa na idadi ya Vyama vya Ushirika, hivyo, husababisha kukosekana kwa usimamizi madhubuti wa Vyama hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha na malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ili kutekeleza majukumu yake, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, chini ya Fungu 43 inaomba jumla ya shilingi bilioni 258,350,877,000 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 152,406,152,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 105,944,725,100 ni kwa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida shilingi bilioni 26,758,060,190 na shilingi bilioni 125,648,081,810 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, katika fedha za maendeleo shilingi bilioni 14,260,042,000 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 91,684,683,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazoombwa na Wizara zinakusudia kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Ni kilimo kwanza, Wizara itaendelea kutekeleza azma ya kilimo kwanza kupitia *agricultural sector program* na utekelezaji utakuwa kwa awamu ambao utahusisha nguzo nne kama ilivyokuwa katika mwaka uliotangulia.

(ii) Ni programu kabambe ya mageuzi na *modernization* ya ushirika, Wizara kupitia Fungu 24 itaendelea kutekeleza programu kabambe ya mageuzi na *modernization* ya ushirika kwa kuimarisha sera, mikakati na usimamizi katika Sekta ya Kilimo, kuwezesha na kuimarisha asasi za wananchi katika kilimo na kuimarisha Mfuko wa ukusanyaji uhifadhi, uchambuzi na usambazaji wa takwimu na taarifa za Vyama vya Ushirika.

(iii) Kuongeza uzalishaji wa chakula, katika kuhakikisha nchi inakuwa na chakula cha kutosha, katika mwaka wa fedha 2011/2012, mazao yatakayopewa kipaumbele kuendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji ni mahindi, mpunga, muhogo, mtama, mikunde, mbegu za mafuta, mazao ya bustani na mazao makuu asilia ya biashara. Utekelezaji huu utaliwezesha Taifa kujitosheleza kwa chakula na kuwa na ziada ya kuuza, hivyo kuwezesha kuwa na uhakika na usalama wa chakula na lishe.

(iv) Kuimarisha uongezaji wa thamani kwa mazao ya kilimo na mfumo wa masoko, Wizara imekusudia kuwezesha wakulima kuongeza thamani kwa kuboresha na kusambaza teknolojia ya kuhifadhi mazao ya kilimo na kuhimiza matumizi mbalimbali ya nafaka, kama vile kuchanganya unga wa muhogo na unga wa ngano. Aidha, Wizara imejipanga kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya usindikaji wa muhogo na mtama na kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kuchuna katani yaani *sisal decorticators* na kubagua korosho, *CAMARTEC* na Nyumbu (*TATC*) katika Halmashauri kumi.

(v) Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa ya kilimo, Wizara imekusudia kuhakikisha kuwa masoko ya bidhaa ya kilimo yanapatikana. Ili kufikia lengo hili Wizara imepanga kuboresha huduma za kukagua viwango vya madawa yanayotumika katika mazao na bidhaa za kilimo kwa kuijengea uwezo *TPRI* ili iweze kutoa vyeti vya usafi wa mazao na biashara za kilimo vinavyotambulika Kimataifa. Vile vile Wizara inatarajia kujenga maabara zitakazotambulika Kimataifa, yaani *accredited laboratories*. Aidha, Wizara itaanzisha kilimo cha mkataba kwa wakulima wa pamba, kuendelea kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuungana ili kuongeza nguvu za kukabiliana na mashindano katika biashara ya kuuza mazao nje na kuimarisha usimamizi bora wa mazao kupitia Bodi za Mazao na vituo vya mpakani vya ukaguzi vya mazao ya mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza kuhusu utekelezaji wa maoni ya Kamati, changamoto na maeneo ya utekelezaji kwa mwaka 2010/2011. Naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka 2010/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika bado ni ndogo na hii ni sababu kubwa ya sekta hii kushindwa kuchangia kwa kiasi cha kutosha katika kukua kwa uchumi. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, sekta ya kilimo ilichangia asilimia 26 tu ya pato la Taifa licha ukweli kwamba Watanzania wanaokadiriwa kufikia asilimia 80 wanajishughulisha na kilimo. Ukuaji wa kilimo unashuka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2008/2009, kilimo kilikua kwa asilimia 4.6, mwaka uliofuata mwaka 2010/2011 kilimo kilikua kwa asilimia 4.2 tu wakati huo idadi ya watu inakua kwa asilimia 2.9. Aidha, bajeti inayotengwa kwa kilimo imekuwa ikiongezeka kwa kiasi kidogo sana. Mwaka 2008/2009 ilikuwa ni shilingi bilioni 440 sawa na asilimia 6.4, mwaka uliofuata, 2009/2010 shilingi bilioni 666.9, sawa na asilimia 7.0, mwaka uliopita 2010/2011 shilingi bilioni 903, sawa na asilimia 7.7 na mwaka 2011/2012 shilingi bilioni 926, sawa na asilimia 6.7 ya bajeti yote ya Serikali. Kamati inaishauri Serikali ifanye uamuzi wa makusudi, ifanye uamuzi mgumu wa kuongeza bajeti ya sekta ya kilimo kufikia angalau kiwango kilichokubaliwa na nchi za *SADC* cha asilimia kumi ya bajeti ya Serikali ili sekta ya kilimo iweze kuchangia kikamilifu katika uchumi binafsi na wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kwanza, Kamati inakubaliana na dhana nzima ya kilimo kwanza ambayo ilibuniwa kwa nia ya kuleta mapinduzi ya kijana na kukifanya kilimo chetu kuwa cha kisasa ili nchi iweze kujitosheleza kwa chakula. Hata hivyo, wakati wa kupitia bajeti ya Wizara Kamati imetambua kwamba hakuna mikakati ya dhati ya kutekeleza dhana hiyo. Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Wizara zote zinazohusika na sekta ya kilimo, zipewe fungu la kutosha kutekeleza azma ya kilimo kwanza ili utekelezaji wake uanze mapema na Wizara ziwajibike ifuatavyo kwa matumizi bora ya fungu hilo;

(ii) Serikali itoe elimu kwa wakulima na wananchi kwa ujumla kuhusu maana halisi ya kilimo kwanza ili dhana hii ieleweke kwa mapana zaidi;

(iii) Serikali iendelee kuhusisha sekta binafsi katika utekelezaji wa kilimo kwanza kwa kuhakikisha inawawekea vivutio mahususi ikizingatiwa kwamba sekta binafsi inachangia kwa asilimia kubwa katika kukua kwa uchumi;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utafiti. Ili nchi iweze kuendelea katika sekta ya kilimo ni lazima iwekeze katika utafiti. Kamati inapongeza jitihada zinazofanywa na Serikali za kutenga fedha kwa taasisi mbalimbali ili ziweze kufanya utafiti nchini. Kamati inasisitiza yafuatayo:-

(i) Ni kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu katika taasisi za tafiti zinachelewa sana kuzifikia taasisi hizo. Kamati inashauri kwamba fedha hizo zigawiwe mapema ili taasisi zianze utekelezaji wake bila kuchelewa;

(ii) Matumizi ya teknolojia ya *GMO*, yaani *Genetic Modified Organisms*, bado hayajatiliwa mkazo;

(iii) Serikali itoe elimu kwa umma kuhusu teknolojia hii ili utekelezaji wake uende kwa haraka kwa kuwa una manufaa makubwa;

(iv) Utafiti wa matumizi ya *bio-technology* ufanyike ili kutengeneza mbegu bora zenye vinasaba vyenye uwezo wa kustahimili ukame kwa kuzingatia kwamba *bio-technology* imeendelea kukua kwa kasi ulimwenguni na kuwa nyezo kubwa katika kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo;

(v) Vituo vya Utafiti vitengewe fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vinapatiwa vitendea kazi bora na vya kisasa;

(vi) Serikali ihakikishe matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima kwa wakati

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pembejeo, kwanza, mbolea. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza ruzuku ya pembejeo. Pamoja na pongezi hizo Kamati inasisitiza yafuatayo: Serikali iendelee kuongeza idadi ya wakulima wanaopata ruzuku kwani itasaidia katika kuongeza tija. Aidha, Serikali ihakikishe inafanya utafiti wa kutosha ili kuweza kutambua kwamba misimu inatofautiana katika kila kanda au mikoa, hii itahikikisha mbolea inawafikia wakulima wa mikoa hiyo kwa wakati muafaka. Serikali ijenge

viwanda vya mbolea nchini ikizingatiwa kwamba nchi yetu imebarikiwa kuwa na gesi asilia nyingi na madini ya *phosphate* ambazo ni malighafi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuleta mbolea nchini, ambayo tayari imefungwa katika Mifuko kutoka nje ya nchi ina gharama kubwa. Kamati inashauri mbolea hiyo iletwe nchini *in bulk* ili ifungwe hapa hapa nchini. Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa gharama ya bei kwa wakulima. Vilevile ili wakulima wenye mahitaji ya kiwango tofauti waweze kupata mbolea kulingana na uwezo na mahitaji yao ni vema mbolea zikafungwa katika mifuko yenye ujazo tofauti, mfano kilo tano, kilo kumi, kilo ishirini na tano na kilo hamsini. Hii itasaidia wakulima kujitokeza kununua kulingana na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa vocha za ruzuku ya mbolea ni tatizo kubwa, Serikali ihakikishe inadhibiti na kuwachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kufanya huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mbegu. Mbegu bora ni moja ya misingi ya kuleta tija katika kilimo ili kuwawezesha wakulima kuzalisha chakula cha kutosha na kuhakikisha kunakuwepo usalama wa chakula. Kamati inasisitiza yafuatayo:-

(i) Serikali iache kutegemea kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi, badala yake mbegu za kutosha zizalishwe hapa hapa nchini, hii itapunguza gharama za ununuzi wa mbegu kwa wakulima.

(ii) Vile vile Serikali ihakikishe usimamizi na uratibu wa ubora wa mbegu unafanywa kwa umakini na zile zisizofaa ziondolewe katika soko. Aidha, wakulima wapelekewe mbegu kwa wakati ili kuwadhibiti wafanyabiashara wanaowahadaa kwa kufunga mbegu zisizo na ubora unaostahili kwenye vifungashio vinavyotumika kwa mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, madawa. Kutokana na mazao mengi yakiwemo ya chakula na biashara kushambuliwa na wadudu waharibifu, Kamati inaishauri Serikali iendelee kuongeza bajeti ya madawa ya mazao haya ili kuongeza uzalishaji. Aidha, utafiti wa kutumia viuatilifu vya kimaumbile uendelee ili wakulima wavipate kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji, ili kilimo kikue kwa kiasi kinachotakiwa ni vema basi nchi iweke mazingira mazuri katika kilimo. Kamati inashauri kwamba:-

(i) Serikali iweke vivutio kwa wawekezaji ili washawishike kuja kuwekeza katika mashamba makubwa.

(ii) Serikali ipunguze urasimu ili kuwashawishi wawekezaji wengi zaidi.

(iii) Serikali ihimize ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ili kuongeza thamani yake.

(iv) Serikali iishirikishe sekta binafsi kwani inachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa sekta hii.

(v) Serikali iangalie mikataba inayoingia na wawekezaji ili kuepuka kuingia mikataba ya miaka mingi na hatimaye kupoteza eneo kubwa la ardhi bila tija. Aidha, ushirikishwaji wa wananchi katika kutoa maeneo ya uwekezaji uzingatiwe ili kuepuka migogoro isiyo na lazima kuwepo na mahusiano mazuri kati yao.

(vi) Serikali izingatie matumizi sahihi ya ardhi inayoendana na mkataba unavyotaka ili kuepuka matumizi mengine yanayoonekana kuwanufaisha wawekezaji na kudhoofisha maendeleo ya wananchi.

(vii) Serikali iendeleze kwa kasi zaidi zoezi la kutenga maeneo kwa ajili ya benki ya ardhi ili kuwapatia wawekezaji mara tu wanapojitokeza kuendesha shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uzalishaji wa mazao. Kamati inaendelea kusisitiza uzalishaji wa mazao ya chakula upewe kipaumbele kwa kuongeza ruzuku ya pembejeo kwenye maeneo yanayolima mazao hayo. Aidha, kwa maeneo yenye ukame Serikali isimamie ulimaji wa mazao yanayostahimili ukame kama mtama, uwele na muhogo ili kuepusha baa la njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa mazao mengine, Kamati inasisitiza Serikali ijikite katika kuhimiza uzalishaji wa mazao mengine mapya kama viungo, matunda, mboga na maua ambayo yatasaidia katika kuliongezea Taifa pato na kukuza uchumi wa nchi kwa kuhakikisha inawapatia mitaji na utaalam wakulima. Aidha, Serikali itumie Chuo cha Utafiti cha *KATRIN* katika kupeleka utaalam wa mazao ya viungo kwa wakulima na kwa kutumia taasisi zinazohusika, ifanye utafiti wa mbegu bora za maua na mboga mboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fungu maalum kwa mwaka huu, Kamati inasisitiza mchakato wa kuanzisha Benki ya Kilimo uharakishwe na kukamilishwa ili wakulima waweze kufaidika na mikopo mikubwa na yenye riba nafuu. Aidha, kwa kipindi hiki ambacho benki haijaanza kufanya kazi, Serikali ione umuhimu wa kuweka dirisha hili dogo katika benki zinazowafikia wakulima kwa urahisi Vijijini na Mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua umuhimu wa huduma za ugani katika kuhakikisha kilimo kinakuwa na tija. Kamati inasisitiza huduma za ugani ziboreshwe kwa kuhakikisha kwamba Maafisa Ugani wanapatiwa mafunzo na wanatimiza wajibu wao wa kusimamia wakulima ili kuongeza uzalishaji. Aidha, Maafisa Ugani wasaidiwe makazi bora kwa kujengewa nyumba ili kuwapa motisha katika kutekeleza kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo ni muhimu sana hasa katika kipindi hiki ambacho Benki ya Kilimo bado haijaanza kwani inasaidia kutoa mikopo kwa wakulima. Bajeti ya Mfuko huu kwa mwaka huu 2011/2012 ni shilingi bilioni 3.8 ambayo ni sawa na bajeti ya mwaka 2010/2011 ya shilingi bilioni 3.8 kukiwa hamna ongezeko lolote. Kamati inashauri Serikali iongeze bajeti ya Mfuko ili iweze kuwahudumia wakulima wengi zaidi, kwani maombi ya mikopo ya pembejeo ni mengi zaidi ikilinganishwa na fedha inayotengwa kwa ajili ya Mfuko huu muhimu. Maombi ni wastani wa shilingi bilioni nane kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kulipa madeni ya Vyama vya Ushirika, hatua hii itawapunguzia mzigo wa madeni vyama hivyo na kufufua vile vilivyokuwa vimekufa. Pamoja na hatua hizo Kamati ina ushauri ufuatao:-

Serikali ihakikishe mchakato wa kuanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika, watendaji wa sekta ya ushirika ni wachache, ikilinganishwa na mahitaji na ili kukomesha ubadhirifu unaofanywa na baadhi ya viongozi wa Vyama vya Ushirika, Wizara iongeze Maafisa Ushirika wa kukagua vyama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi za Mazao ni muhimu sana katika kusimamia mazao yetu na kuhakikisha yanazalishwa kwa kiwango kikubwa. Ili Bodi hizi ziweze kusimamia mazao husika vizuri ni lazima ziwezeshwe vya kutosha. Bodi nyingi bado hazitengewi fedha za kutosha hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kamati inashauri Serikali iendelee kuziongezea fungu Bodi hizi kulingana na mahitaji, aidha, Serikali ihakikishe kwamba Bodi hizi zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria ili kuondoa urasimu wa kutoa leseni za biashara za mazao ambao unaathiri ushindani kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuendelea kusaidia Wakala wa Hifadhi ya Chakula nchini, pamoja na pongezi hizi tunashauri yafuatayo, maghala ya kuhifadhia chakula ni machache nchini ukilinganisha na mahitaji halisi, Serikali iongeze maghala haya ili uhifadhi wa chakula uweze kufikia lengo la kuhifadhi na kusambaza chakula cha njaa cha kutosha kwa watu wengi.

Pili, ni kwamba, maghala yaliyopo yamechakaa sana na mengine yanavuja wakati wa mvua. Serikali itenge fedha za kukarabati maghala haya ili chakula kinachohifadhiwa kisiharibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Kutokana na ukame unaojitokeza mara kwa mara pamoja na mabadiliko ya tabianchi, kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi wa uhakika wa upatikanaji wa mazao ya chakula na biashara nchini. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza bajeti, kuainisha na kuyatumia mabonde mengi ya maziwa na mito kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, kuviongezea uwezo wa kiutendaji vituo vya kanda vya umwagiliaji na kuongeza idadi ya wataalam wa umwagiliaji na kuwaajiri katika Halmashauri hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Lakini napenda kuwashukuru na kuwatambua wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa,Mwenyekiti; Mheshimiwa Neema Hamid Mgaya, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mjumbe; Mheshimiwa Abdusalaam S. Ameir, Mjumbe; Mheshimiwa Salim H. Khamis, Mjumbe; Mheshimiwa Namelok E. M. Sokoine, Mjumbe; Mheshimiwa Dr. Christine G. Ishengoma, Mjumbe; Mheshimiwa Seleman Said Jafo, Mjumbe; Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mjumbe; Mheshimiwa Sylevester M. Kasulumbayi, Mjumbe; Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mjumbe; Mheshimiwa Profesa Peter Mahmudu Msolla, Mjumbe; Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mjumbe; Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mjumbe; Mheshimiwa Mansoor Sharif Hiran, Mjumbe; Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mjumbe; Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mjumbe; Mheshimiwa Rose Kamil Sukum, Mjumbe; Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mjumbe; Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mjumbe; Mheshimiwa Seleman Said Bungara, Mjumbe; Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mjumbe na Mheshimiwa Dokta Titus Mlengeya Kamani, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe na Naibu Waziri Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza kwa ushirikiano wao mzuri katika kipindi chote cha kuchambua bajeti yao. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Mohammed Muya na Naibu Makatibu Wakuu Ndugu Sophia Kaduma na Eng. Mbogo Futakamba pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dokta Thomas Kashililah na Katibu wa Kamati hii Ndugu Elieka Saanya kwa kuihudumia vizuri Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kupitia Fungu 43 kwa mwaka 2011/2012 ya jumla ya shilingi 258, 350, 877,100/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji wake na sasa naomba nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hiyo Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa ili aweze kuwasilisha hotuba yake.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hotuba hii kuwa ndefu na kwa sababu ya rasllimali muda kuwa hautoshi, basi napenda hotuba hii kama ilivyowasilishwa kwa Waheshimiwa Wabunge iweze kusomeka katika *Hansard* kama ilivyo. Kwa hiyo, hii niliyonayo hapa ni muhtasari tu wa hotuba nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99 (7) Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na upendo, kwa kunijalia uhai na afya njema hata nikaweza kusimama hapa kutimiza wajibu huu kwa nafasi yangu ya Waziri Kivuli wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kutoa shukrani kwa chama changu cha Demokrasia na Maendeleo – CHADEMA kwa kuniteua kugombea kiti cha Ubunge Jimbo la Meatu na kushinda kwa kishindo. Napenda pia kutoa shukrani za kipekee kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe kwa kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii. Nami natoa ahadi kwake kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu na kwa jinsi Mwenyezi Mungu atakavyonijalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kilimo Tanzania bado haijaleta mafanikio tunayoweza kujivunia. Wakulima wetu bado wanatumia zana zile zile za kizamani tangu tupate uhuru, mbegu wanazopanda

mashambani bado ni zile zile zisizo na ubora unaostahili, wanalima mashamba madogo yasiyotoa mavuno yanayoweza kutoa chakula cha kutosheleza hadi msimu mwingine wa kilimo na bado kilimo chetu ni cha kutegemea mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali kuboresha sekta hii kwa kuweka mikakati na programu mbalimbali kama kutoa vocha za pembejeo za kilimo kwa wakulima, kauli mbiu mbalimbali za kuhamasisha kilimo tangu uhuru na tuliyo nayo sasa ya Kilimo Kwanza zote hazioneshi kuleta mabadiliko chanya katika sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Hali ya Chakula kwa Mwaka 2009/2010 iliyotolewa na Wizara ilionesha Wilaya 61 katika Mikoa kumi ya Singida, Shinyanga, Mara, Manyara, Pwani, Kilimanjaro, Arusha, Dodoma, Mwanza na Dar es Salaam zinakabiliwa na ukosefu mkubwa wa chakula. Taarifa iliyotolewa katika Bunge hili katika Mkutano wa Nne na Waziri wa Wizara hii ilionesha kuwa bado hali ya ukosefu wa chakula inatukabili. Haya yote Kambi ya Upinzani inayaona kuwa ni matatizo yanayotokana na udhaifu wa kiuongozi katika kupanga kwani tuna mito na mabonde ambamo karibu kipindi chote cha mwaka maji hupatikana. Kwa lugha nyingine na rahisi ni kwamba vipaumbele vyetu viko kwenye makaratasi badala ya vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa watendaji hutoa taarifa za kuimarika kwa sekta hii, kwa kunukuu takwimu za tarakimu, ongezeko la tani za mavuno kila mwaka, Kambi ya Upinzani haioni sababu ya kuendelea kujivunia takwimu hizi kama Wilaya zinakabiliwa na njaa mpaka kufikia hatua ya kuomba msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Uhuru zimefanyika tafiti nyingi kuhusu kilimo, chakula na ushirika na matatizo kufahamika. Sera na mipango mizuri imeandaliwa, kuna misaada mingi kutoka kwa taasisi za Kimataifa na nchi washirika wa maendeleo. Nini tena Serikali hii inahitaji kufanya ili sekta hii iwanufaishe Watanzania? La kushangaza ni kwamba baadhi ya viongozi wetu wamekiri hawaelewi kwa nini Tanzania bado ni maskini. Kambi ya Upinzani inaamini kuwa matatizo katika Wizara hii yamefahamika toka zamani, tatizo ni kwamba, Serikali imekuwa ikisuasua kuyakabili kwa makini na upangilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujio wa mwekezaji toka Marekani katika sekta ya kilimo-*agrisol energy*. Kambi ya Upinzani imepata taarifa kuwa Serikali imeingia mkataba wa kumpa mwekezaji toka Marekani ardhi yenye ukubwa wa ekari 327,755, ili afanye uwekezaji katika kilimo cha mazao ya nafaka, miwa pamoja na mazao ya mafuta (*Jiotropha*), pamoja na ufugaji. Pamoja na mambo mengine, Serikali imeamua kumpa mwekezaji ardhi hiyo kwa hoja kuwa mwekezaji huyo ataongeza upatikanaji wa chakula na kutengeneza ajira mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma hiyo, ni vema ikazingatiwa kuwa takriban wakulima wadogo wapatao 162,000, wataondolewa kutoka kwenye maeneo ambayo walikuwa wanalima na kuhamia kusikoeleweka. Kambi ya Upinzani hairidhishwi na hoja za uzalishaji wa chakula na kutengeneza ajira mpya, zinazotumiwa na Serikali ili kuhalilisha mpango wa kuwapokonya wananchi ardhi yao na kumpa mwekezaji huyo. Hoja za kumbeba mwekezaji huyo, hazina ukweli wa kutosha kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza, takwimu zilizopo za hali ya chakula kwa nchi yetu zinaonyesha kuwa Tanzania kama nchi haina tatizo la uzalishaji wa chakula, ila tatizo kubwa lililopo hapa Tanzania ni tatizo la miundombinu mibovu katika maeneo ya uzalishaji mkubwa wa chakula. Tatizo la miundombinu ndilo linalosababisha upungufu wa chakula kwenye maeneo ambayo uzalishaji ni mdogo. Kwa hiyo, hoja ya Serikali ya kutaka kumpa mwekezaji huyo ardhi kwa kisingizio cha kuongeza uzalishaji wa chakula, haina msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasema, kama mwekezaji huyo ni muhimu, basi ingekuwa ni busara akawekeza katika kuimarisha miundombinu mibovu katika Mkoa wa Rukwa ili wakulima na wafanyabiashara waweze kuuza, kununua na kusafirisha mazao yao kwa urahisi na sio wananchi kupokonywa ardhi yao wanayoitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni ya kutaka kumpa ardhi mwekezaji huyo kwa madai ya kuongeza mazao yatokanayo na ufugaji pia inatia shaka. Ni dhahiri kuwa mwekezaji huyo na washirika

wake hawakufanya utafiti wao vizuri, kwani takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania ni nchi ya tatu katika bara letu kwa kuwa na mifugo mingi. Kuna uwiano ulio sawa kati ya idadi ya mifugo na idadi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, hoja kwamba Tanzania kuna upungufu wa uzalishaji wa nyama ni hoja dhaifu isiyokuwa na mashiko. Tatizo tulilonalo si uhaba wa nyama bali ni kutokuwepo kwa viwanda vya nyama na masoko ya uhakika katika sekta nzima ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka wazi nini hasa kilichopo nyuma ya pazia la uwekezaji huu unaotaka kufanyika Mkoani Rukwa? Kambi ya Upinzani haijaona hoja za msingi hata kufanya wananchi wahamishwe kwenye ardhi yao kwa sababu tu ya mwekezaji huyu. Tunaitaka Serikali itupe maelezo ya kina na ya msingi, vinginevyo, hatutakuwa tayari kuona Watanzania wa Mkoa wa Rukwa wakipokonywa ardhi yao kwa manufaa ya mwekezaji huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango na ukuaji wa sekta ya kilimo katika uchumi. Ni kweli kuwa Sekta ya Kilimo ndiyo iliyo na asilimia kubwa (zaidi ya asilimia 70) ya watu wengi katika soko la ajira na sehemu kubwa ya wakulima wako vijijini. Ni wazi kuwa kama kweli wananchi wa nchi hii wangekuwa wananufaika na sekta hii ya kilimo umaskini uliokithiri maeneo ya vijijini usingekuwa kama ulivyo kwa sasa. Tatizo la ukosefu wa chakula katika Wilaya zaidi ya 41 linatokana na miundombinu mibovu na ukosefu wa viwanda vya msingi vya kusindika mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuimarisha sekta hii ya kilimo ambayo inajumuisha viwanda vya kilimo na hivyo kutanua sekta nyingine ya viwanda vya aina nyingine ambayo ni muhimu sana hasa kwa kutoa ajira ya kutosha na kukua kwa uchumi. Aidha, tatizo la ukosefu wa chakula ambalo linazikumba baadhi ya Wilaya zetu litakwisha kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wananchi wengi kujihusisha na sekta hii ya kilimo, bado mchango kwa uchumi wa nchi hii ni mdogo sana na hauonekani kukua. Taarifa ya Hali ya uchumi wa Taifa katika Mwaka wa 2010 inaonesha kuwa mchango wa shughuli za kiuchumi kwa pato la Taifa (% *GDP*) kwa bei ya soko katika mazao ni kama ifuatavyo: Mwaka 2008 ni asilimia 19.0, mwaka 2009 ni asilimia 18.4 na 2010 ni asilimia17.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika uchumi wa nchi hii, Kambi ya Upinzani inapendekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Serikali ni lazima sasa ianzishe utaratibu mzuri na imara wa kusimamia miradi mikubwa ya kilimo inayoanzishwa hasa ile ambayo tumepata msaada mkubwa kutoka Taasisi za Kimataifa. Kwani ni wazi kuwa kumekuwa na udhaifu katika usimamizi wa miradi mikubwa kama ile ya kilimo cha umwagiliaji ambayo ni njia sahihi ya kumaliza tatizo la ukame.

(b) Kuacha kabisa mazoea ya kutenganisha mazao ya biashara na chakula. Tokea tupate uhuru hadi leo, utenganisho huu umewanyima haki wakulima wa mazao ya mahindi, ndizi, mihogo, mtama na kadhalika. Wakulima wanapoyalima mazao haya na kuambiwa kuwa ni mazao ya chakula, wananyimwa haki. Uchumi wa leo si ule wa kijamaa, chochote kinacholimwa na kuuzika ili kumpatia Mtanzania kipato ni biashara. Hivyo, tunaomba tofauti iliyowekwa baina ya mazao ya biashara na chakula ifutike katika akili zetu ili kuwatendea haki wakulima wote.

(c) Serikali ianzishe mafunzo ya kilimo cha oganiki kuanzia kwa shule za sekondari na kwa wakulima wote na kutafuta masoko ya uhakika wa mazao hayo. Kambi ya Upinzani inaamini mazao ya kioganiki yataweza kumudu ushindani wa kibiashara katika Mataifa makubwa kama Marekani, Canada, Ulaya na Mashariki ya Kati na baadhi ya vijana wetu wanaomaliza kidato cha nne wataweza kujihusisha na kilimo hiki.

(d) Serikali sasa ianze kujihusisha moja kwa moja na kutafuta masoko ya mazao ya wakulima na kuviwezesha Vyama vya Ushirika kujihusisha na usindikaji wa mazao. Hii itasaidia wananchi kupata bei nzuri ya mazao yao na itasaidia kuepuka wafanyabiashara kuuza nje ya nchi kwa njia za panya na kuikosesha Serikali mapato.

(e) Kutengeneza au kujenga masoko makubwa ya uhakika ya mazao ili kusaidia kupatikana kiurahisi kwa bei za mazao au nafaka. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki Tanzania ndiyo yenye kuuza mazao mengi kwa nchi jirani lakini mfumo wake wa kimasoko haujafanywa kuwa ni wa faida kwa wakulima wetu.

(f) Serikali iwe makini katika kuingia mikataba ya kilimo na wawekezaji na hasa ile inayowahusisha wakulima na mazao yao. Mara nyingi mikataba hiyo inatumiwa vibaya na makampuni na kuwanyima uhuru wakulima wa kuuza mazao yao eneo lenye bei nzuri.

(g) Serikali ianzishe mamlaka inayojitegemea kwa ajili ya kilimo (*Tanzania Agricultural Authority*). Kazi ya Mamlaka hii itakuwa ni kuwekeza katika kilimo na kuhakikisha kuwa Serikali inasimamia sekta ya kilimo kikamilifu, kama uzalishaji wa mbegu bora na za kisasa za kilimo, usimamiaji na usambazaji wa zana za kilimo na kusimamia utumiaji wa teknolojia na zana za kisasa katika kilimo.

(h) Serikali ikamilishe zoezi la kuwekeza katika kutengeneza barabara zinazounganisha Kata na Kata, Wilaya na Wilaya na Mikoa na Mikoa ili kurahisisha usafirishaji wa mazao kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Hii itasaidia hasa mazao yanayoharibika mapema kufika sokoni mapema kabla ya kuanza kuharibika.

(i) Serikali iwekeze katika kupanua upatikanaji wa nishati ya umeme na maji vijijini ili kuweza kuchochea teknolojia ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hai. Katika nchi zote za Afrika ya Mashariki Tanzania ndiyo nchi yenye Chuo Kikuu cha Kilimo kikubwa na cha kwanza chenye wataalam mahiri. Tatizo tunaloliona hapa ni kuwa wataalam hawa hawatumiwi kikamilifu na hatuna takwimu za wahitimu katika fani mbalimbali za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajua kabisa madhara makubwa yanayosababishwa na matumizi ya muda mrefu ya mbolea ya kemikali kwenye ardhi. Pia inaelewa umuhimu mkubwa uliopo wa kutumia mbolea za mboji kwenye udongo. Kambi ya Upinzani inauliza ni kwa nini Serikali inakataa kuwashauri wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutumia mbolea ya mboji wakati inaelewa kuwa udongo wa maeneo hayo umekwishaharibika na kuwa sumu na haufai kwa kuzalisha na kuvuna kwa tija bila ya kutumia mbolea za chumvi chumvi. Ni jambo la kusikitisha kuwa wakulima hawa tayari wamekwisha kuwa watumwa wa mbolea hizi, na watakapozikosa hawataweza kuzalisha kamwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa mbolea ni eneo lenye siasa nyingi na ni eneo lenye rushwa kubwa. Tunasema hivyo kwa msingi kuwa, tunashindwa kuamini kuwa Waziri aliyepo (pamoja na wataalam wa Kilimo katika Wizara) anaelewa umuhimu wa mboji kwa kilimo chetu lakini anashindwa kuweka mpango mkakati wa matumizi ya mboji kwa wakulima na badala yake anajitahidi kutafuta makampuni ya kuleta mbolea za chumvichumvi nchini au anajitahidi kuona jinsi ya kutoa ruzuku kwa mbolea hizo na kuhakikisha mbolea hizo zinakuwa nyingi kwa wakulima. Kwa nini kiasi cha fedha ya ruzuku isiwekezwe katika uzalishaji wa mbolea za mboji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua jukumu lake la msingi la kutoa ushauri wa matumizi ya aina za mbolea na hasara au faida zake na aina na kiasi cha mbolea inayotakiwa kulingana na aina ya udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya msukumo inaoutoa katika matumizi ya mbolea ya chumvi chumvi ili itoe msukumo kama huo kwa mbolea ya Mboji kwa mikoa ambayo matumizi ya mbolea za chumvi chumvi hayajaanza kuleta madhara kwenye udongo, kwani gharama ya kuihuisha ardhi iliyoharibika ni kubwa mno. Hivyo, kinga ni bora kuliko tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa Wizara haijachelewa kwani kilimo hai bado kina nafasi kubwa ya kukifanya kilimo kishamiri hapa Tanzania na huu ndio muda wa kuangalia jinsi viwanda vikubwa vya mbolea duniani vinavyofanya biashara ya kuendelea kuzifanya nchi zinazoendelea kuwa maskini. Utajiri wetu ni ardhi yenye rutuba; njia pekee ya kuiendeleza ardhi yetu ni kilimo hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usambazaji wa pembejeo za kilimo. Katika nchi hii ambayo haijaweka mazingira mazuri ya kumwezesha mkulima wa kijijini kupata mikopo katika benki zetu kwa masharti nafuu, kwa zaidi ya miaka takriban 50 sasa tangu uhuru. Mpango wa Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo ni muhimu sana katika kuwawezesha wakulima na wafugaji kupata mbegu bora, mbolea na madawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na uzuri wa mpango huu. Kambi rasmi ya Upinzani inasikitishwa na Serikali kushindwa kabisa kusimamia mpango huu. Ushahidi wa wazi wa Serikali hii kushindwa kusimamia mpango huu ni kushamiri kwa mapungufu yafuatayo:-

(a) Kushindwa kuwasimamia mawakala wasambazaji wa pembejeo na kusababisha kufanya udanganyifu kwa kushirikiana na watumishi wa Serikali na kujinufaisha wao binafsi kinyume na taratibu. Kusimamishwa kwa mawakala 168 katika Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Morogoro na Ruvuma na kufunguliwa kwa kesi 22 katika Mikoa ya Rukwa, Manyara, Mwanza, Mara, Morogoro, Manyara, Kilimanjaro, Iringa na Mbeya ni matokeo ya ukosefu wa usimamizi makini kwa Mawakala hao.

(b) Serikali kushindwa kusambaza vocha za ruzuku za kutosha na kwa wakati. Kwa mfano, Mkoa wa Iringa ni mmoja kati ya wazalishaji wakubwa wa chakula nchini ilisambaziwa tani 33,365 tu za pembejeo ikiwa ni pungufu ya tani 56, 445 zilizohitajika.

(c) Upungufu mwingine ni utaratibu mbovu unaofanywa na wakuu wa Mikoa au Wilaya wa kusimamisha zoezi la usambazaji pindi utokeapo ubadhirifu katika usambazaji. Utaratibu huu huathiri wakulima kwa kuwachelewesha kupata pembejeo hizi kwa wakati kwa kuzingatia kuwa maeneo mengi msimu wa kilimo huwa ni mfupi. Usimamishaji wa usambazaji huu umefanywa maeneo mengi ya nchi yetu kwa sababu ya muda natoa mfano wa *DC* wa Wilaya ya Rorya alivyobaini udanganyifu katika Vijiji vya Utegi, Nyandiga, Mang'ore na Osiri mwezi wa pili mwaka huu alisimamisha ugawaji wa vocha na kuwaathiri wakulima wa maeneo hayo wasio na hatia.

(d) Serikali kushindwa kusimamia watumishi wake na kuwapa mwanya wa kufanya uchakachuaji wa vocha za pembejeo, kama vile kuandika majina hewa au ya marehemu kwenye vitabu vya vocha na kugushi saini zao na kwenda kuchukua fedha benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa utaratibu huu wa kugawa vocha ulianza baada ya Serikali kushindwa kusimamia utaratibu uliokuwepo awali wa kutumia makampuni ya wafanyabiashara kusambaza pembejeo hizi. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Waziri atueleze ni lini atamaliza dosari hizi za kuratibu zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bei za zana za kilimo. Lipo tatizo kubwa la uwiano wa bei kati ya zile zinazokopeshwa kupitia Halmashauri za Wilaya na Manispaa na Mawakala wa Serikali kama SUMA JKT na bei za wauzaji binafsi kwenye maduka ya pembejeo. Utofauti huu umejitokeza zaidi hasa katika bei za matrekta na matrekta madogo (*power tillers*). Wauzaji binafsi wanaouza kwa fedha taslimu wanauza zana hizi kwa bei nafuu tofauti na hizi zinazokopeshwa na Serikali kupitia Halmashauri. Wakati wauzaji binafsi wakiuza *Power Tiller* kati ya Sh. 3,000,000/= Halmashauri mbalimbali zinakopesha zana hizi kwa bei ya juu sana kiasi cha kufikia Sh. 9,000,000/=. Kambi ya Rasmi inaona kama Serikali hii badala ya kumsaidia mkulima inazidi kumdidimiza zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo pia la ubora na uimara wa trekta hizi. Wakulima wengi wamelalamika kuharibikiwa na zana hizi kabla hata ya kurudisha mikopo yao. *Power Tiller* katika maeneo mengi zimekopeshwa zikiwa na kiwango cha chini cha ubora. Kwa mfano, *Power Tiller* zilizopelekwa Wilaya ya Kilosa zilibainika kuwa na upungufu hata wa baadhi ya vipuri. Upungufu huu unawaathiri kwa kiwango kikubwa wakulima kwani hulazimika kuendelea kulipia sehemu ya gharama hizo wakati hazitumiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo lingine la wafanyabiashara wa matrekta kutenganisha trekta na vifaa vyake kama majembe kama njia ya kuongeza bei kwa kufanya utenganishi huu. Kwa hiyo, tabia hii humlazimisha mkulima huyu kushindwa kununua jozi nzima ya trekta hii. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa na uhakiki wa bei hizi kwenye maduka ya pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo cha mkataba. Programu ya kilimo cha mkataba inapata upinzani mkubwa kutoka kwa wakulima kwa madai kwamba wanamilikishwa kwa nguvu kwa wakopeshaji wa pembejeo za kilimo na kuwanyima uhuru wa kuuza mazao yao watakavyo chini ya sera za soko huria. Wakulima wengi wamegomea kimyakimya programu hiyo wakidai pia kuwa, ni kinyume kwa mila na jadi ya makabila mengi kwa mtu kumilikishwa na kutumikishwa na mtu mwingine kwa njia ya utumwa wa deni (mkopo) na kwamba, kama wawekezaji hao wanataka kuwakopesha pembejeo za kilimo kwa maendeleo, wafanye hivyo bila masharti yenye kuhatarisha uhuru wa wakulima wa kujiamria jinsi ya kuendesha kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo, wakulima wengi wanakiona Kilimo cha Mkataba kuwa ni aina fulani ya utumwa unaomfanya mkulima mdogo kutumikishwa kwenye ardhi yake na wenye mitaji kwa kivutio cha mikopo ya pembejeo za kilimo wasizopanga bei zake na kwa bei ya pamba inayopangwa na kudhibitiwa na mwenye mtaji mwenyewe. Mfano, unaotolewa ni wa wakulima wa tumbaku walioingizwa kwenye programu kama hiyo miaka michache iliyopita, ambapo wakulima hao walijikuta wanadaiwa zaidi ya Sh. 3,000,000,000/= na makampuni kiasi cha kutishiwa kunyang'anywa ardhi hadi Serikali ilipowakomboa kwa kulipa deni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanunuzi wa pamba nao wanaiona programu ya Kilimo cha Mkataba kuwa inapingana na masharti ya vyombo vya fedha vinavyowakopesha fedha za kununulia pamba. Kwa sababu hiyo, wameitaka *TCB* isitishe programu hiyo ili ifanyiwe maandalizi sahihi ya kutosha, ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wakulima waone ni mpango wao badala ya kuwa mpango uliobuniwa toka juu na kushushwa kwao bila ridhaa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo cha mazao ya biashara. Pamoja na mazao ya biashara kukumbwa na tatizo la soko kwa kukosa bei ya uhakika, licha ya Serikali hii kuwapa matumaini ya maneno matupu kwa kasi zaidi kama kawaida yake, bado wakulima wetu hawajakata tamaa kwani wameendelea kulima mazao haya (kahawa,pamba,tumbaku,chai, korosho na kadhalika).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli ulio wazi kuwa mazao haya yanachangia kwa kiwango kikubwa katika uchumi wetu. Mazao haya yametuingizia fedha nyingi ikilinganishwa na mazao mengine ya biashara. Kwa mfano, mwaka 2008 pamba iliingiza dola za Kimarekani milioni 115, tumbaku dola milioni 108, kahawa dola milioni 80.5, chai dola milioni 40.8 na korosho, dola milioni 40.2. Kushindwa kwa Serikali kuweka usimamizi mzuri katika uzalishaji wa mazao haya licha ya kuwaathiri wakulima wetu na kushuka kwa pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa kuwa kama Serikali hii itaendelea kupiga siasa kwa kuendelea kuongeza kauli mbiu mbalimbali za kilimo huku wakulima wa pamba, korosho, ufuta, miwa, kahawa, alizeti na mazao mengine wakiendelea kuathirika, sekta hii haitabadilika. Kambi ya Upinzani inashauri sasa Serikali ianze kuwa na utaratibu wa kuanza kusimamia kilimo hiki kwa vitendo na kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sekta ya pamba. Kilimo cha pamba, zao ambalo linahusisha zaidi ya asilimia 45 ya Watanzania, linalimwa katika Wilaya 42 za Mikoa 13 kati ya Wilaya 127 za Mikoa 21 nchini. Pamba huchangia asilimia kati ya 20 na 25 ya Pato la Taifa la fedha za kigeni, ikilinganishwa na mazao mengine ya biashara. Kwa mfano, mwaka 2008 pekee, pamba iliingiza dola za Kimarekani milioni 115, ikilinganishwa na dola milioni 108 za Tumbaku, dola milioni 80.5 za kahawa, dola milioni 40.8 za chai na dola milioni 40.2 za korosho. Asilimia 99 ya pamba yote inazalishwa Kanda ya Magharibi ambako Mkoa wa Shinyanga unatoa asilimia 60 ya pamba yote na kufuatiwa na Mkoa wa Mwanza asilimia 20 na asilimia 20 iliyobaki huzalishwa na mikoa 11 iliyobaki, lakini pamoja na hayo wananchi wa mikoa hiyo ni maskini wa kutupwa, ikilinganishwa na wananchi wa mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri sekta ya pamba nchini itakufa na mkulima wa pamba atabaki maskini, kama ufisadi mkubwa ulioivamia sekta hiyo hautadhibitiwa kwa nguvu ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa sana ambalo limekuwa likiwaathiri wakulima wa zao la pamba kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa la kupiga marufuku wakulima kuchanganya pamba na mahindi katika shamba moja. Wakulima wengi wamefungwa na wengine hadi sasa kesi zao zinaendelea, mfano, ni wakulima wa Kata ya Mwanyahina, Meatu. Utumiaji bora wa ardhi ni pamoja na kupanda mazao

mchanganyiko katika eneo moja kama kanuni za kilimo zinavyosema. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza wananchi wa mikoa inayolima pamba, wataendelea kufanyiwa uonevu huu hadi lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba (*CDTF)*. Wanachama ambao ndio wachangiaji wa Mfuko huo wanahoji matumizi ya Sh. 52,000,000,000/= zilizochangwa msimu uliopita na msimu huu zinatarajiwa kufikia sh. 60,000,000,000/=. Hii ni baada ya kupandisha mchango wa *CDTF* kutoka Sh. 30 kwa kilo msimu uliopita hadi Sh. 200 msimu huu. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu matumizi ya fedha hizi za wananchi ambazo miaka yote hazimnufaishi mkulima wa pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko kwa mazao ya chakula kwa wakulima. Bado mkulima wa Tanzania anaendelea kukabiliwa na soko la kuuza mazao yake kwa bei ya kumwezesha kurudisha gharama zake alizotumia na kupata faida kidogo. Wakulima wamekuwa wanauza mazao yao kwa bei karibu na bure na hulazimika kuuza mazao yake ili apate fedha ya kutatua matatizo yanayomkabili au kwa kuogopa mazao yasimharibikie kwa kuyachelewesha na sio kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ushahidi wa wazi hata wakulima wanaolima maeneo yanayopitika kwa barabara nzuri bado hata wao wanakabiliwa na ukosefu wa soko la mazao yao. Kwa mfano wakulima wa viazi vitamu maeneo ya Gairo na Mtyangimbole-Songea, vitunguu maeneo ya Ruaha Mbuyuni na nyanya maeneo ya Ilula na maeneo mengine yaliyoko barabarani. Pamoja na kuwepo barabarani bado wanaozewa na mazao yao au kuyauza kwa bei sawa na bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya zaidi kwa wakulima walioko maeneo yasiyofikika kwa barabara kwa urahisi. Ukitembelea maeneo ya Matombo na Mgeta huko Morogoro matunda yanaozea mashambani, yakifikishwa soko la Mawenzi Morogoro mjini au hata soko kuu la Kariakoo hali ni hiyo hiyo ya kuharibikiwa na matunda na mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefikia hatua sasa waliokuwa wakulima wakubwa wenye mitaji mikubwa hawalimi tena wamegeuka wafanyabiashara wakubwa. Wanachofanya kwa sasa ni kununua mazao ya wakulima pindi tu mazao yanapovunwa na kuyahifadhi katika maghala makubwa waliyojenga kusubiri kuyauza kwa bei ya juu zaidi wakati mazao yanapoanza kupungua kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha hali ya masoko kwa wakulima wetu, Kambi ya Upinzani inapenda kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko makubwa yanayojengwa ya mazao ya wakulima yaende sambamba na ujenzi wa viwanda vya usindikaji. Kwa mfano, hakuna sababu ya wafanyabiashara wa soko kubwa la mahindi la Kibaigwa kusafirisha mahindi badala ya kusafirisha unga. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kwa kupitia wawekezaji ufanyike mkakati wa kujenga viwanda maeneo yote ya masoko kulingana na mazao yanayozalishwa kwa wingi katika Wilaya hiyo. Kila mmoja anajua faida ya hili, nafaka kwenda nchi za nje kama Kenya, Malawi, Zambia na kwingineko basi wasafirishe unga badala ya nafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu kwa miaka 50 baada ya uhuru matunda kuozea Kariakoo, Tandale na masoko mengine na tunashindwa kuyasindika matunda yetu na kutoa juisi inayoweza kukaa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya chakula kwa mwaka 2010/2011. Taarifa ya hali ya chakula tunayoendelea kupokea kutoka Serikalini mwaka hadi mwaka inaonesha kuwepo kwa upungufu wa chakula katika baadhi ya Wilaya na Mikoa yetu. Sababu kubwa ya kuwepo kwa upungufu huo tunaambiwa ni kupungua kwa uzalishaji unaotokana hasa na ukame unatokana na mabadiko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoelekea kuazimisha miaka 50 sasa ya uhuru wetu bado hatujaweza kuyatumia maji yanayosababisha mafuriko katika nchi yetu kwa kuyahifadhi katika mabwawa makubwa na baadaye kuyatumia katika kilimo cha umwagiliaji. Miradi mbalimbali ya kilimo na tafiti zake zilizofanyika miaka yote ya nyuma imeshindwa kutatua tatizo la ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado lipo tatizo katika utaratibu wa kutambua maeneo mbalimbali yanayokabiliwa na njaa katika nchi yetu. Wakati mwingine maeneo yanayokabiliwa na njaa hayatajwi na

wahusika kwa kuogopa kuonekana wazembe katika kusimamia maendeleo ya kiuchumi na kilimo katika Wilaya zao na hivyo kuwa na hofu ya kuondolewa kazini. Kambi ya Upinzani inataka kujua nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inatoa rai kuwa sababu nyingine zinazosababisha upungufu wa chakula licha ya ukame ni:-

(a) Ni uuzaji wa chakula kwa wingi wakati wa mavuno kunakofanywa na wakulima na kwa kuwa kilimo ni cha msimu katika maeneo mengi ya nchi yetu, tabia ya uuzaji mavuno kwa wingi hupelekea kukosekana kwa chakula kipindi cha kusubiri mavuno mengine.

(b) Mazao huharibika wakati wa kuyahifadhi, kunakotokana na ukosefu wa utaalam wa kuyahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikichukua hatua za kupiga marufuku uuzaji wa mahindi unaofanywa na wafanyabiashara hasa wakati wa mavuno kama njia ya kuthibiti upungufu wa chakula nchini. Pamoja na nia hii nzuri ya serikali, uamuzi huu wa upigaji marufuku uuzaji wa chakula nje ya nchi, huathiri sana wakulima kwani husabisha bei ya mazao kuwa chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili lilipitisha Sheria ya Uanzishwaji wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko kwa lengo kuu la kuwa Bodi itakuwa inatoa bei dira katika soko huria. Bodi hii ihakikishe kuwepo kwa ushindani katika soko la mazao ya kilimo ili mkulima anufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwasaidia wakulima kuuza mazao yao kwa bei ya chini Kambi ya Upinzani inatoa ushauri ufuatao:-

(a) Wakala wa Hifadhi ya Chakula Taifa aongezewe uwezo wa kununua mazao kwa bei inayolingana na ya wafanyabiashara au ya juu kidogo. Hii itasaidia wakulima kuendelea kuwa na soko la ndani la uhakika kwa mazao yao. Mbali na kuwasaidia wakulima hii itasaidia pia kuwa na hifadhi ya kutosha kwenye maghala ya *NFRA*. Kwa mfano, taarifa ya Wizara inaeleza *NFRA* kushindwa kufikia lengo la kununua tani 200,000 za mahindi katika kipindi cha mwaka uliopita kwa kununua tani 181,091 tu. Kiasi cha kuhifadhi kimekuwa kidogo sana hata kwa mazao mengine. Matokeo yake tumekuwa tunashuhudia kaya zilizoathirika zikigawiwa kiasi kidogo sana. Kwa mfano, kila kaya kuwapa kilo za unga mbili, tano au kumi, sio msaada sana kwa wananchi wetu walioathirika na njaa.

(b) Uanzishwe utaratibu wa kuwawezesha wakulima kupata mikopo isiyo na riba kubwa hasa kupitia vyama vyao vya wakulima. Utaratibu huu utasaidia wakulima kutouza mazao yao kwa bei nafuu wakati wa mavuno na wataweza kuwakwepa wafanyabiashara matapeli wanaotumia msimu wa mavuno kununua mazao kwa bei nafuu.

(c) Kambi ya Upinzani inashauri pia Serikali kuongeza wigo wa kutoa elimu ya usindikaji mazao kama njia nyingine ya kuwezesha kuendelea kuwepo kwa chakula mpaka msimu mwingine wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji. Limezuka tatizo kubwa linalowakumba wakulima katika maeneo mengi ya nchi hii ya mashamba ya mazao kuvamiwa na mifugo. Hii imesababisha kuibuka kwa migogoro mikubwa kati ya wakulima na wafugaji na kusababisha mauaji kati ya makundi haya muhimu kwa maendeleo ya nchi hii. Wapo watoto wameachwa yatima, akinamama wamekuwa wajane, watu wamepotelewa na jamaa wa karibu. Taarifa za maeneo yaliyotokea mapigano ni mengi na Watanzania wote wanafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makundi haya ya wakulima na wafugaji yote ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu na yanategemeana. Wakulima wanahitaji nyama, wanahitaji kunywa maziwa, wanahitaji kutumia mbolea. Hata wafugaji wanahitaji kununua mazao ya wakulima kwa ajili ya chakula. Uwekezaji katika sekta ya ardhi usioangalia uwiano wa makundi ya watumiaji wa ardhi ndilo tatizo kubwa linalosababisha mtafaruku huu unaojitokeza katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka kujua hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kutekeleza mapendekezo ya Tume kama hatua za kukomesha mauaji. Sio busara kutumia pesa ya walipa kodi kwa kuunda Tume halafu wananchi waendelee kukaa kimya wasipoona Serikali wakitekeleza ushauri wa Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wakulima. Kama kweli tunataka kuwakomboa Watanzania kuondokana na kilimo kisichokuwa na tija kwa Taifa hili ni lazima Benki ya Wakulima ianzishwe na imenadiwa sana katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kama njia ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo (*ASDP*) na Kauli mbiu ya Kilimo Kwanza. Kambi ya Upinzani inataka kujua Kama Benki hii itaanzishwa hivi karibuni au miaka hii mitano ni ya mchakato ya uanzishaji wake. Benki hii imeelezwa itatoa mikopo kwa wakulima wakubwa na wadogo kwa masharti nafuu. Ingekuwa vema Serikali ikaweka sawa mipango ya uanzishwaji wa benki hii ili ianzishwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji. Wote tunajua kuwa kilimo cha umwagiliaji ndiyo njia ya pekee itakayoweza kuinua uchumi wa Tanzania. Nchi nyingi zilizofanikiwa katika kilimo zinatumia kilimo cha umwagiliaji. Mazao ya wakulima wetu huathirika sana kwa ukame na wakati mwingine baadhi ya maeneo hupata mavuno machache au kukosa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasikitishwa na taarifa kuwa ni wakulima 85 tu waliopata mafunzo katika teknolojia mbalimbali za umwagiliaji na matumizi bora ya maji ya umwagiliaji kati ya zaidi ya asilimia 70 ya wakulima wa nchi hii. Taarifa inaendelea kubainisha mafanikio mengine kuwa wamejenga mabwawa mawili tu katika Kijiji cha Maliwanda Musoma Vijijini na Kijiji cha Nhalanga, Nzega. Ni aibu Serikali kuwaarifu Watanzania waliosambaa katika zaidi ya vijiji 12,176 kuwa Serikali imejenga mabwawa mawili tu. Kambi ya Upinzani inataka kujua ni mabwawa mangapi yanahitajika Tanzania nzima na ni lini yatakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti katika kilimo. Ni ukweli kabisa kuwa hapa nchini kwetu tunavyo vituo vya utafiti katika maeneo mengi. Hii ni kwa sababu ya kutambua umuhimu wa kufanya utafiti. Tafiti zinazofanyika katika kilimo hazina budi kujielekeza zaidi katika kubuni teknolojia bora za uzalishaji wa mazao na hatimaye kumwezesha mkulima kupata mavuno mengi na kujiongezea kipato. Baadhi ya tafiti zilizofanyika ni za kutafuta aina za mbegu zinazofaa kwa kilimo kulingana na hali ya hewa ya mahali husika. Hii imepelekea kuwa na aina nyingi sana za mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa aina nyingi za mbegu za mazao kumewafanya hata baadhi ya wakulima kushindwa kuelewa ni aina gani ya mbegu watumie kulingana na hali ya hewa ya eneo husika. Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kutumia wataalam wake hasa Maafisa Ugani kuwapa elimu ya kutosha wakulima badala ya mwananchi kumsikiliza muuzaji wa mbegu ambaye hulazimika kutoa mbegu kulingana na bidhaa aliyo nayo. Hii imesababisha mbegu inayohitaji mvua nyingi kupandwa sehemu yenye mvua kidogo na matokeo yake ni kupatikana kwa mavuno kidogo au mvua kukatika kabla mazao hayajaanza kukomaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kubwa linalowakumba wakulima hasa wale wadogo ni ukosefu wa fedha za kuweza kumudu gharama za kununua mbegu hizi. Wakati wa msimu wa kilimo ni kipindi ambacho wakulima wengi hukabiliwa na upungufu wa chakula kwa matumizi yao, hii hupelekea wao kushindwa kununua mbegu hizi na kulazimika kupanda mbegu walizohifadhi wenyewe baada ya mavuno ambazo hazina uhakika wa ubora. Kambi ya Upinzani inashauri Serikali kufanya mabadiliko ya upatikanaji wa mbegu hizi kwani bila kufanya hivyo wakulima wanaweza kukopeshwa mbegu hizi kwa riba kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo lingine la mbegu kuchelewa kuwafikia wakulima wakati wa msimu wa kilimo. Hii hupelekea mbegu nzuri zilizofanyiwa utafiti kushindikana kupandwa na wakulima kwani huwa tayari wameshapanda mbegu zao za kienyeji au kupanda mbegu za kisasa katikati ya kipindi cha mvua na matokeo yake ni mavuno kidogo au kukosa kabisa. Ushauri kwa Serikali ni kuwa ihakikishe mbegu hizi zinamfikia mkulima kwa wakati kwa kuwachukulia hatua za kisheria watakaohusika na ucheleweshaji huu, mathalan kuwanyang'anya vibali Mawakala wa usambazaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya ushirika nchini. Uzoefu katika nchi mbalimbali umeonesha kuwa Mataifa mengi yaliyofanikiwa katika kilimo kutokana na kuwepo kwa vyombo imara vya wakulima vikiwemo Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi maskini kama Tanzania ambayo sehemu kubwa ya wakulima hawana elimu wala mafunzo yoyote ya ujasiriamali, ushirika ndio njia pekee inayoweza kuwaunganisha wakulima na kuwapa elimu kwa urahisi. Ushirika ndio unaweza kuwaunganisha wakulima na wafugaji wenye uwezo mdogo kupata pembejeo, mikopo, mitaji, teknolojia bora, masoko ya mazao yao na taarifa mbalimbali za kuwasaidia katika uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa Vyama vya Ushirika, ufanisi wake bado sio wa kujivunia pamoja na kuongezeka kwa vyama hivyo tunakoelezwa na Serikali. Bado kuna madudu makubwa yanafanywa na viongozi wake hasa ubadhirifu wa fedha. Kuna upungufu katika kujituma na hakuna uadilifu. Hii imevunja moyo wa makundi mengi ya wakulima na wafugaji na hivyo hawajiungi na hii imepunguza Vyama Vingi kukosa nguvu hasa za kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyama Vingi viko maeneo ya mijini kuliko kwa walengwa wenyewe walioko vijijini. Wakulima wametelekezwa vijijini wakiuza mazao yao kwa wafanyabiashara walaghai na matapeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba Vyama vingi vya Ushirika, badala ya kuwa mkombozi wa wakulima, vimekuwa ndio matapeli wa wakulima na kupelekea kushindwa hata kulipa madeni yao. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu ya maswali yafuatayo:-

(a) Serikali ililazimika kufuta baadhi ya madeni ya vilivyokuwa Vyama vya Ushirika. Pamoja na nia hiyo njema, Kambi ya Upinzani inataka kujua ni viongozi wangapi wamechukuliwa hatua kwa kusababisha hasara katika vyama hivyo?

(b) Serikali ililazimika kuwalipa wakulima waliokuwa wanadai Vyama vya Ushirika vilivyofilisika. Ni wakulima wangapi wameshalipwa na ni shilingi ngapi na ni wangapi wanasubiri malipo yao na ni kiasi gani na ni lini watalipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ianze kufikiria namna ya kuwasaidia wakulima wa matunda na mbogamboga wa maeneo mbalimbali hapa nchini, mathalan, Matombo, Mgeta, Lushoto, Muheza na kadhalika. Wakulima hawa wanapata hasara sana kwa sababu wanauza matunda kwa bei ndogo sana na mengi huharibika. Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kupitia Vyama vya Ushirika na kwa kushirikiana na *SIDO*, kujenga viwanda vya usindikaji vijijini ili badala ya kuuza matunda wakulima wauze juisi. Aidha, Vyama vya Kuweka na Kukopa kwa masharti nafuu viwepo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya bajeti ya Wizara. Katika Wizara zilizotengewa fedha nyingi Wizara hii ni ya 12, ikiwa imetengewa jumla ya Sh. Bilioni 258.35 sawa na asilimia 1.91 ya jumla ya bajeti yetu ya takriban Sh. trilioni 13.5. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ni sh. bilioni 105.94 sawa na asilimia 41 ya fedha zote zilizotengwa. Katika fedha zote hizi za maendeleo asilimia 86.5 tunategemea kutoka kwa wahisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana na bajeti ndogo iliyotengwa kwa Wizara hii muhimu katika uchumi wetu, Wizara ambayo inaongoza kwa kuajiri watu wengi (zaidi ya asilima 70), sekta tunayotegemea kuinua sekta nyingine kama viwanda. Kinachosikitisha zaidi, kiasi cha fedha za maendeleo ni kidogo ukilinganisha na kile cha matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inasikitika zaidi kuwa bajeti ya maendeleo inategemea zaidi fedha za nje kwa sababu katika kila sh.100 itakayotumika kwa maendeleo fedha yetu ya ndani ni sh. 3.50 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka maendeleo katika nchi hii hasa kwa kuinua sekta hii hatuwezi kukwepa kufanya mabadiliko makubwa kwa kuiongezea fedha Wizara hii. Bila kufanya hivyo tutegemee tatizo la upungufu wa chakula kuzidi kuongezeka zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu mbadala iliyosomwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa wizara ya Fedha inaainisha mgawanyo mzuri wa fedha kwa mwaka ujao wa fedha. Na kwa kuwa serikali hii imeanza kuyakubali yale tunayowashauri. Kambi ya Upinzani inashauri sasa kama ilivyo kwenye bajeti mbadala fedha iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ibaki kama ilivyo na fedha ya maendeleo iongezwe kutoka sh. bilioni 105.99 mpaka sh. bilioni 363.59 . Ili fedha hii itakayoongezeka isaidie kuongeza ufanisi katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, tunaamini kuwa Serikali hii sikivu ya Chama Cha Mapinduzi kama inavyojiita, itayachukua maoni haya ya Kambi ya Upinzani ili kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, nakushukuru sana Mheshimiwa Meshack Opolukwa kwa kuwasilisha hotuba hiyo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge nadhani sasa tutaanza mchango wetu wa jumla na labda tu ningewapa taarifa kidogo. Orodha yetu inaanza na wachangiaji watano (5) ambao hawajawahi kuchangia kabisa na baada ya hapo tuna orodha ya wachangiaji kama ishirini na nane (28) walioomba kuchangia ambao wamekwishachangia mara moja na itafuata orodha ya wachangiaji karibu ishirini na nne (24), walioomba kuchangia ambao wamekwishachangia mara mbili na pia tuna orodha ya walioomba kuchangia, lakini wamekwishachangia mara tatu ambayo ina mtu mmoja tu ambaye ni Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa. Orodha ya mwisho ni ya wale waliochangia mara nne ndani ya Bunge ambayo pia ina mchangiaji mmoja tu ambaye ni Mheshimiwa Tundu Lissu.

Tutawapa kipaumbele kwanza hawa watano ambao hawajawahi kuchangia halafu tutaendelea na hiyo orodha nyingine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje ataanza na Mheshimiwa Selemani Bungara atafuatia, bado tuna Mheshimiwa Donald Max, Mheshimiwa Anna Abdallah na Mheshimiwa Shaffin Sumar. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Kama ulivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mara yangu ya kwanza kabisa kusimama katika Bunge lako Tukufu na kutoa hotuba katika Bunge hili la Kumi (10).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze kwanza kuwashukuru sana Wapiga kura wangu wa Jimbo la Chilonwa kwa kunirudisha hapa Bungeni mara nne mfululizo. Napenda niwashukuru sana kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni na vile vile naomba niwahakikishie kwamba, nitakuwa mtumishi mwaminifu kwao na niendelee kuomba ushirikiano wao ili kwa pamoja tuweze kujiletea maendeleo yetu katika Jimbo la Chilonwa. Wao ni mashahidi wa nini tumekifanya na wana mategemeo makubwa zaidi ya kufanya pamoja nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza na Watendaji wote wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Mohamed Muya, Manaibu Katibu Wakuu, Mama Kaduma na Ndugu yangu Mbogo Mfutakamba kwa kazi nzuri wanayoifanya pale Wizarani na kwa hotuba nzuri ambayo imewasilishwa leo hii asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mdau katika Wizara hii kwa sababu kabla ya kujiunga na siasa hapo mwaka 1995 nilikuwa ni Mtumishi wa Wizara hii, nikitumikia sekta ya Ushirika, sekta ambayo nimeitumikia katika maisha yangu yote ya utumishi wa umma. Sasa kutokana na hali hiyo pamoja na hotuba nzuri iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri hapa leo asubuhi nataka nitangulie kusema kwamba naiunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo niipongeze Wizara kwa hotuba yake leo asubuhi kwa kuelezea azma ya kuanzisha Tume kuu mbili ambazo kwa kusema kweli, naipongeza sana Wizara; Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Hizi ni sekta mbili kuu sana ambazo kwa maoni yangu nadhani zikisimamiwa vizuri zitatufikisha mbali na zitatukomboa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikianzia kwenye shughuli za Ushirika kwa mfano, kazi za Ushirika sasa hivi zinakwenda lakini nasikitika kusema kwamba haziendi kwa jinsi inavyotakiwa ziende. Shughuli moja kubwa sana ya Wizara inayosimamia Ushirika ni kufanya ukaguzi wa Vyama vya Ushirika ili viweze kujiendesha ipasavyo, lakini kwa sasa hivi kwa bahati mbaya kazi hiyo haifanyiki vilivyo. Zamani kulikuwa na kile kitengo cha *Corporative Inspection* na sasa hivi nadhani watu wamesahau kabisa kwamba kulikuwa na watu wanaitwa *Corporative Inspectors*, hawa ndiyo watu ambao walikuwa wanasimamia ukaguzi wa mara kwa mara wa Vyama vya Ushirika na hatimaye vyama hivyo vilikuwa vinakwenda vizuri. Sasa hivi pamoja na ongezeko la vyama hivyo ambavyo vimetolewa taarifa kwenye hotuba hii, lakini hotuba yenyewe imekiri kwamba uwiano wa idadi ya Wakaguzi na Vyama hauendi sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme kwamba, maadam sasa Tume hii inakusudiwa kuanza na nashukuru, kusema kweli imeanza kwa sababu nimeona hata *Vote* imekwishaandaliwa, *Vote* 24. Niipongeze sana Wizara katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nisisitize tu kwamba, Tume ifanye kazi vizuri kwa yafuatayo:-

Kwanza, muundo wa utendaji katika Idara ya Ushirika. Watumishi hawa wa Idara ya Ushirika kazi yao kubwa sana ni hiyo ya ukaguzi, lakini sasa wakishakuwa ni Wakaguzi na huku tena wako *attached* kwa Mkurugenzi, kule wanatumika kwa kazi za aina nyingi tu, anaweza akatumwa kazi ya kukusanya maduhuli na kuandika vitabu vya Halmashauri, kwa hiyo hata kama kuna vyama havikaguliwi kazi zake zile ambazo zimewekwa kwa mujibu wa sheria hazifanyiki. Kwa hiyo, niombe kwamba Tume itakapokuwa imeanza ijipange vizuri ihakikishe watumishi hawa wanafanya kazi kwa uhuru, wawe *independent.* Kwa sababu kimsingi ni Wakaguzi, Mkaguzi anatakiwa awe huru. Kwa sasa uhuru wake unabanwa sana kwani anakuwa anapewa maagizo na kazi nyingine. Kwa hiyo, ningeomba sana Tume ijipange vizuri ihakikishe kwamba ina *independent inspectors* na wasimamie kazi hii vizuri. Lakini hivyo hivyo, waongeze watumishi wa kutosha, watakapokuwa wameongezwa wakapelekwa Wilayani hivi hivi bila mpangilio, bila ya kuwa wanawajibika kwa Mrajisi, bado nitakuwa na mashaka kwamba kazi hazitafanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme sijui Mheshimiwa Waziri anafanyaje kazi. Ninazo taarifa kwamba pale Idara ya Ushirika ambapo Mkuu wake wa Idara ni Mrajisi na huyu anatajwa kwa mujibu wa sheria kwamba ndio *custodian* wa sheria. Lakini Idarani pale nina taarifa kwamba mwaka mmoja na nusu sasa hana Mrajisi na huyu ndiye msimamizi na mshauri wake mkuu. Sasa atafanyaje kazi kwa utaratibu huo na huyu anatajwa kwa mujibu wa sheria. Sasa sioni sababu kwa nini mpaka sasa hivi Mrajisi hajateuliwa na kazi zake anazifanyaje, kwa sababu akiwa anakaimu na wote mnajua maana ya kaimu anafanya kazi kwa mashaka mashaka, kwa hiyo aidha, anathibitishwa mtu au anateuliwa mtu *substantive registrar* ndio kazi zinaweza kwenda vizuri. Kwa hiyo, niombe sana kwamba, kazi za Idara ya Ushirika ili ziweze kufanyika vizuri ateuliwe Mrajisi wa Vyama vya Ushirika ambaye atamshauri kwa karibu sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pengine nigusie na lingine moja la Idara hii kuhamahama, leo iko Dodoma kesho Dar es Salaam, hivi watafanyaje kazi. Nilikuwa mtumishi wa Idara ile, wakati mwingine huwa sijui faili langu liliishia wapi ama lilibaki Dodoma ama lilikwenda Dar es Salaam, maana yake kila siku Idara hii iko barabarani. Kwa hiyo, niombe kabisa Tume itakapoanza hebu iwe na msimamo kwa sababu hapa Dodoma ndio Makao Makuu basi hiyo Tume *substantively* ikae Dodoma na watumishi wajue hivyo kila siku wawe wanafanyia kazi zao Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nimesema utendaji wa kazi za Idara hii ya Ushirika unakuwa wa mashaka mashaka hata kazi zile za kisheria ambazo zinatakiwa zitekelezwe baadhi ya vyama havifanyi kazi vizuri. Nina mfano mmoja, hapa kwetu na Mheshimiwa Waziri umetaja tunalo shamba kubwa sana la zabibu ambalo shamba lile linaendeshwa kwa utaratibu wa bega kwa bega na Vyama vya Ushirika vimeandikishwa pale. Kiko cha *AMCOS* kwa maana ya Chabuma na kiko kimoja cha *SACCOS*, lakini vyama hivyo toka vimeandikishwa pale viko kwa jina tu hakujafanyika ukaguzi. Sasa huu ni mfano mzuri wa shamba lile pale, tungetegemea iwe *modal* ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Idara ya Ushirika haijakanyaga pale na tunaposema haijakanyaga yupo kijana mmoja pale Wilayani ambaye nae utekelezaji wake ni wa mashaka mashaka. Nilishapeleka tatizo hili mpaka kwenye Idara ya Ushirika kwenyewe, lakini bado kuna kigugumizi, kuna nini juu ya hili. Hebu tusaidieni Mheshimiwa Waziri kuhakikisha kwamba hapo ukaguzi unafanyika na vile vile tunahakikisha kwamba uchaguzi unafanyika. Maana pale wamepewa fedha nyingi sana na *CRDB*. Wanachama

waliokopeshwa hawajui wao wenyewe walichochangia hawajui, tunafanyaje kazi. Mheshimiwa Waziri, kwa hili ningeomba sana tusaidie ili tuweze kufanya kazi zetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la umwagiliaji. Nimefurahi sana kusikia kwamba itaanzishwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Kilimo chetu Mkoa wa Dodoma hapa ni cha wasiwasi sana kwa sababu ni ukame, hakuna maji na Waziri amesema kwamba pembejeo namba moja katika kilimo ni maji, bila maji hakuna kilimo. Sisi Mkoa wetu wa Dodoma ni mkame, nilitegemea sana kwamba Tume hii ya Taifa ya Umwagiliaji itakapokuwa imeanza kufanya kazi zake itajikita katika maeneo kame kama Dodoma, ilete mipango yake thabiti kabisa kuhakikisha kwamba matunda yanapatikana. Maana yake sisi udongo wetu hapa Dodoma ni mzuri sana, unamea karibu kila kitu, kama maji yanapatikana. Maana udongo wetu unaota mazao ya nafaka, matunda, miti na kila kitu na Mheshimiwa Waziri anajua. Lakini kutokana na kwamba tumekosa maji, mambo hayaendi vizuri, hebu mpango huu wa umwagiliaji ujielekeze katika Mkoa wa Dodoma kwa nguvu zote kuhakikisha kwamba na sisi tunaingia katika watu wanaozalisha mazao ya kilimo bila wasi wasi na bila mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba sasa hivi ziko *scheme* chache ambazo zimetajwa hata kwenye hotuba nimeziona na sisi kwa upande wa Chilonwa tunashukuru sana. Hapo kwenye shamba la zabibu Chinangali nadhani sasa hivi tumekuwa ni mfano wa umwagiliaji wa matone, lakini pale Chalinze kuna bwawa kubwa kabisa ambalo lilianzishwa kipindi kile cha ile Idara ya zamani iliyokuwa inajulikana kama *WD and ID.* Hata pale wananchi wa eneo lile walikuwa wanapaita *Debrid* kwa maana ya *WD and ID.* Bwawa lile Mheshimiwa Naibu Waziri analifahamu vizuri sana, ningeomba nguvu zote sasa zielekezwe katika hizi *scheme* kuhakikisha kwamba zinazaa matunda na zionyeshe mfano na sisi Wanadodoma wanapozungumzia habari ya uzalishaji wa kilimo angalau tuwe na uhakika wa kilimo ambacho kinatuvusha, hatupati njaa za mara kwa mara, hatupati upungufu wa mazao ya biashara. Hapa Dodoma ukisikia majina hata ya watoto mengi yanaashiria njaa njaa hivi, kwa sababu hatuna mazao ambayo yanazalishwa kwa uhakika. Mkimkuta mtoto wa kiume anaitwa *Malogo* huyo ni njaa na wa kike *Ilogo* ni njaa. Unawakuta namna hiyo, kwa sababu njaa ni kitu cha kila mara na si kwamba hatuwezi kulima lakini udongo wetu unahitaji maji na maji hatupati na kwa hiyo, tunakuwa na janga hili. Tuondokane na janga hili kwa kutuletea kilimo cha umwagiliaji kuhakikisha kwamba tunaondokana na janga hilo la njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nizungumzie zao la biashara Dodoma. Waziri amezungumza habari ya mazao ya biashara. Mkoa wa Dodoma sisi hapa hatuna zao la biashara la kudumu na sababu kubwa ni hiyo hiyo tu ya kwamba eneo letu ni kame. Lakini bahati nzuri kwetu zao la zabibu limekubali kumea. Siku za nyuma kidogo wakulima walichangamkia lakini Kiwanda cha Zabibu cha *DOWICO* kikafilisika na zao lenyewe likadorora kidogo. Lakini sasa hivi tuna bahati kwamba kuna Kiwanda kikubwa cha Mvinyo kule Hombolo pamoja na wazalishaji wengine wadogo wadogo wamefufua hali mpya ya soko la zabibu hapa Dodoma na sasa hivi watu wameshaanza kulima mashamba ya zabibu kule kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, hebu mkitazame kilimo hiki cha zabibu hapa Dodoma. Tunacho Kiwanda cha Utafiti hapa Makotopora, ningeomba kiwanda kile kipanuliwe na kipewe nyenzo kuweza kufanya utafiti wa zao la zabibu na wananchi wa Dodoma waweze kupata ahueni angalau ya kupata zao la kudumu la biashara ili nasi angalau tuwe tunazungumza kama watu wengine wanavyozungumzia habari ya kahawa, niache hawa akina Nkumba wanaozungumza habari ya tumbaku, lakini na sisi tupate zao la biashara ambalo linaweza likatukomboa katika Mkoa wetu wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kugongewa kengele ya pili, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara, , niwatakie kila la kheri na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana Mheshimiwa Chibulunje na leo umeonesha uwezo wako kwenye eneo hilo la Ushirika. Waheshimiwa Wabunge anayefuata sasa ni Mheshimiwa Selemani Bungara, atafuatiwa na Mheshimiwa Donald Max.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa kunipa nafasi hii leo na hii ni mara yangu ya kwanza. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata ushindi katika Jimbo langu la Kilwa Kusini. Chama cha Wananchi (*CUF*) pia nikishukuru kwa kunisimamisha kuwa mgombea na nimeshinda. Nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuzungumza kidogo kuhusu kilimo katika nchi yetu ya Tanzania. Natambua tulipopata uhuru mwaka 1961, maadui wetu walikuwa watatu, umaskini, ujinga na maradhi. Lakini kwa miaka 50 ya uongozi wetu wa Serikali yetu Tukufu maadui hawa watatu bado hatujawatoa hata robo yake. Waheshimiwa Wabunge pia Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alituambia ili tuendelee tunahitaji vitu vinne kwanza ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. Tunashukuru sana ardhi tunayo, watu wapo na mpaka sasa hivi tunapanga mpango wa uzazi wa mpango ili watu wapungue kwa kuwa watu wako wengi sana. Tatu, Siasa safi, siasa yetu tunaiona tangu mwaka 1961 ni Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini miaka 50 ya uhuru nchi yetu ya Tanzania hatujaweza kujitegemea, kama hatuwezi kujitegemea kama alivyosema Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mtu asiyeweza kujitegemea hayupo huru, kwa hiyo, sisi tunaishukuru Serikali ya CCM kwa kuendelea kuwa ombaomba kwa miaka 50 ya uhuru. Jambo la nne, anasema uongozi safi. Tunaishukuru Serikali ya CCM uongozi wao ni safi na mzuri imefikia hatua leo CCM asilimia 87 ya bajeti ya Serikali ya kilimo tunategemea wafadhili, tunawashukuru sana Serikali ya CCM. Tunaamini kabisa kwa uongozi wa miaka 50 ya CCM siasa hapa mlitotufikisha *Alhamdullilah*, tunashukuru sana. Naamini tukiwapa tena miaka 50 mingine basi watatufikisha maahali pabaya kuliko hapa tulipofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno hayo, leo nazungumzia sana habari ya zao la ufuta katika Wilaya ya Kilwa, ndio mada yangu leo. Kabla sijaanza napenda kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Lindi Mheshimiwa Sadiki kwa kuwazuia wakulima wa Mkoa wa Lindi wasiuze ufuta katika masoko yenye bei zaidi namshukuru sana. Nampongeza Mkuu wa Wilaya kwa kuzuia watu wa Wilaya ya Kilwa wasiuze ufuta kwenye bei nzuri ili wauze kwa bei ya shilingi 1,000/=. Nampongeza sana Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, nampongeza mno na Mungu amzidishie kwa sababu yeye anapozuia watu wasiuze ufuta katika bei nzuri basi Chama cha Mapinduzi kinateketea katika Mkoa wa Lindi, Namshukuru sana kwa kutuongezea nguvu Upinzani katika Mkoa wa Lindi, namshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Lindi na Mkuu wa Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni siku yangu ya kwanza kusema, nasema sisi watu wa Wilaya ya Kilwa tunaonewa sana. Wakulima wa Kilwa wanalima ufuta wenyewe, wanapanda, wanapalilia, Serikali hawaioni kuwasaidia hata sehemu moja, lakini wanapoanza kuvuna tu Serikali inakaribia. Wakianza kuvuna wanaanza kuwaambia wakulima wa Kilwa si ruhusa kuuza ufuta sehemu nyingine yoyote isipokuwa muuze katika Vyama vya Msingi. Vyama vya Msingi ambavyo vinanunua ufuta kwa shilingi 1,000/= wakati kuna watu wengine wananunua ufuta shilingi 1,500/=, wanawazuia, hayo ndiyo matunda ya Serikali ya CCM. Naomba kwa heshima na taadhima, nimeandika barua kwa Mkuu wa Mkoa, Waziri Mkuu na Waziri wa Kilimo kuwaambia wakulima wa Kilwa wanaonewa, lakini majibu hata mtu mmoja hajatupa katika mambo hayo matatu. Hata jibu moja sijapata, wanamlinda Mkuu wa Mkoa wa Lindi. Hili wanamlinda Mkuu wa Mkoa wa Lindi na chama cha Ilulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahakikisha kabisa kwamba chama cha Ilulu kinawanyonya wakulima wa Mkoa wa Lindi. Naamini hivyo na ni kweli kabisa wanawanyonya wakulima wa Mkoa wa Lindi na hii Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema, nchi yenye utajiri ukiona wananchi wao si matajiri basi kuna mlango umefungwa. Kuna mlango umefungwa, kuna kikundi kidogo cha watu kinawanyonya watu na hiyo inadhihirika katika Mkoa wa Lindi kwamba kuna kikundi cha watu wachache kikiongozwa na Mkuu wa Mkoa kuwanyonya wakulima wa ufuta wa Mkoa wa Lindi. Ni mpango rasmi, haiwezekani Chama cha Msingi kinanunua ufuta shilingi 1,000/= na kuna wafanyabiashara wananunua ufuta shilingi 1,500/= unawazuia. Huu ni mpango rasmi na ukimwambia Waziri Mkuu anamwogopa Mkuu wa Mkoa, ukimwambia Waziri wa Kilimo anamwogopa Mkuu wa Mkoa, twende wapi sisi wakulima wa Mkoa wa Lindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaambia wakulima wa Mkoa wa Lindi tuungane tupambane na Serikali ambayo inawadhulumu wakulima wa Mkoa wa Lindi. Tunasema wafanyakazi mnaandamana, walimu wanaandamana, Madaktari wanaandamana, mkulima ataandamana wapi? Akiandamana mazao yao yanaliwa na wanyama, wakigoma watakufa na njaa. Wakulima watagoma nini wakiwa wanaonewa katika nchi hii? Mkulima hawezi kugoma, akigoma anakufa, hawezi kuandamana atapata wapi umoja wa kuandamana. Lakini nawaambia Serikali kama mtaendelea kutukandamiza watu wa Mkoa wa Lindi, basi *Inshallah* tutaandamana angalau maandamano hamyataki. Serikali ya CCM inasema sikivu, lakini nawaambia Serikali ya CCM sio sikivu kwa ushahidi na dharura kwa Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa

Mkoa, Waziri Mkuu, Waziri wa Kilimo awajibu, nawaomba wakulima wa Mkoa wa Lindi sisi hatuwezi kuandamana lakini siku yao ipo 2015, tutaandamana katika visanduku vya kura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wanapata tabu sana. Mkulima wa Kilwa leo akilima akienda katika Wizara ya Kilimo au Wizara ya Maliasili tunaomba wanyama waharibifu katika mazao yetu wanasema silaha hakuna, risasi hakuna, ma-*game* hakuna. Lakini siku akilima akivuna anaambiwa lazima uuze ufuta katika Chama cha Msingi na kama hukuuza bunduki mkononi wanataka kufa na bunduki kwa sababu ya ufuta wao. Nimesimama kwa ajili ya ufuta tu, naiomba Serikali leo Waziri wa Kilimo atoe tamko ili wakulima wa Wilaya ya Kilwa wawe huru katika zao lao la ufuta, atoe tamko waendelee kuuza ufuta katika chama chochote au kwa mtu yoyote na Chama cha Msingi wauze cha mtu binafsi wauze. Kama si hivyo nitatoa shilingi angalau najua shilingi hiyo itakuwa haipiti kwa sababu CCM kazi yao kusema ndio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tamko rasmi leo, Bunge hili ili Waziri aseme kwamba mkulima wa ufuta ataruhusiwa kuuza ufuta sehemu yake yoyote au haruhusiwi. Kama ataruhusiwa *inshallah,* kama haruhusiwi natoa shilingi na kama nikishindwa kutoa shilingi nakwenda kuandamana usiku na mchana angalau maandamano hamyataki. Namwomba Waziri wa Kilimo aje kujibu swali langu hili, je, ni ruhusa watu wote kuja kununua ufuta Kilwa au si ruhusa. Kama si ruhusa nitatoa shilingi na najua nitashindwa kwa sababu mko wengi, lakini nitakwenda kuandamana usiku na mchana mpaka Kilwa ipate uhuru katika hili. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina zaidi, naseme siungi mkono. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina zaidi langu moja tu nataka wakulima wa Mkoa wa Lindi wawe huru katika mazao yao. Wanalima wenyewe, wanapanda wenyewe, wanavuna wenyewe na wauze wenyewe sehemu wanayoitaka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo hawapewi, ukulima wao wa kizamani, leo Nabii Adam akifufuka Kilwa ataona kama alivyokuwa analima yeye na ndivyo wanavyolima watu wa Kilwa kwa jembe la mkono. Nataka Waziri wa Kilimo aje kutoa jibu leo hadharani watu wa Kilwa wasikie, wakulima wa ufuta wako huru au wanakandamizwa na jinamizi la Mkuu wa Mkoa? Bila kutoa jibu natoa shilingi. *(Makofi/Kicheko)*

Najua shilingi sitafanikiwa lakini tutaandama japo maandamano hamtaki lakini ninachojua Serikali ya CCM kama hamkuandamana hampati haki zenu, kama hawakuua, hawapati haki zao. Ninachoomba Watanzania tuungane, tupambane na madhalimu ili tupate haki zetu. Siungi mkono hoja na nitatoa shilingi mpaka jibu la wakulima wa ufuta wapate uhuru katika Wilaya ya Kilwa. Bila ya hivyo siungi mkono hoja kwa sababu Mkuu wa Mkoa nimemwandikia barua, Waziri wa Kilimo nimemwandikia barua, Waziri Mkuu nimemwandikia barua wote hawakunijibu. *(Kicheko)*

Mkuu wa Mkoa mwenyewe yupo chugwa chugwa, mara Dar es Salaam mara Lindi, sina lingine nataka Waziri wa Kilimo akifika aje kujibu hoja hii tu watu wa Kilwa wajue habari zao. Mwisho nasema chama legelege huzaa Serikali legelege. Ahsante sana. *(Kicheko/ Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli naomba nishukuru leo tumepata nafasi kwa mara ya kwanza kumsikia Mheshimiwa Selemani Bungara, kwa mara ya kwanza amechangia katika Bunge letu. Baada ya Mheshimiwa Bungara sasa nimwite Mheshimiwa Donald Max. *(Makofi)*

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Awali ya yote naomba nichukue nafasi ya kwanza kuwashukuru wananchi wangu wa Geita kwa kuniamini na kunipa dhamana hii ya kuwawakilisha hapa Bungeni. Niwape shukrani nyingi sana Jimbo lote la Geita, hususan wanachama wa CCM ambao waliona mimi ni kioo chao cha kuweza kusaidia Jimbo la Geita kwa ujumla. Shukrani za pili naomba nipeleke wa familia yangu ambayo muda mrefu sipo nayo, mke wangu mpendwa na watoto pamoja na ndugu, jamaa na marafiki ambao wamenipa mimi msukumo wa kuweza kuja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naomba nipongeze viongozi wetu wa Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, wewe pamoja na Spika wa Bunge letu Mama Anne

Makinda, Mawaziri wote na Naibu Mawaziri pamoja na Wabunge wenzangu wote ambao tuko pamoja humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo nafikiri nimefanya nayo kazi kwa muda mrefu. Wizara ya Kilimo kidogo ni tatizo na haya matatizo ni malimbikizo ambayo baadae yanatusumbua. Kilimo cha pamba wakati na *Victoria Federation* kabla ya Uhuru hakukuwa na pamba iliyokuwa inathaminika kama pamba iliyokuwa inatoka Ziwa Victoria na wakati ule ilikuwa inaitwa dhahabu nyeupe. Leo pamba tunayozalisha sisi ipo na unjano njano sana, sio dhahabu nyeupe tena. Ndiyo sababu unakuta kwamba zao letu sisi haliendi na kutokwenda kwake kwa sababu ya ukiritimba umezidi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 1995 wakati tumeona kwamba zao linasuasua mwaka 1998 tulipigwa na *El Nino* mbaya sana ambayo kidogo ipoteze zao letu hili. Sasa kwa sababu vyama vyetu vya ushirika vilikuwa vimelegalega sisi wadau wa pamba tukaona tujiunge pamoja tuanzishe chama, tukakusanyana na wakulima na wao wakaanzisha chama, tukaunganika na Bodi ya Pamba upande wa Serikali na Wizara ipo kulinusuru zao hili tulianzisha mifuko, tukaanzisha vilevile taratibu zetu wenyewe. Tulikuwa tunakaa vikao vyetu, tukianzisha taratibu tulikuwa tunafuata hizo taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 1999, 2000 na mwaka 2001 ndiyo tukaanza kunusurika kutoka kwenye zao. Lakini cha ajabu ni kwamba Chama cha Wadau wa Pamba *(TCA)* na *Tanzania Cotton Board*, tulikuwa tunafanya kazi pamoja lakini tunapoleta masuala yetu Wizarani kule kidogo kuna matatizo. Huwezi kufanya kazi ya *field* ukiwa kwenye *desk*, hata siku moja. Kwa sababu sisi tunaozunguka vijijini ndiyo tunaelewa taratibu, tunajua wakulima tuwasaidiaje, njia gani tupite kwa sababu miundombinu ni mibaya. Ukiangalia hali ya wakulima wanaoishi kule ni tete sana na ni ngumu. Sasa kama sisi tunashindwa kuwasaidia ina maana tunapoomba msaada wa Serikali inakuwa haipo. Sasa sisi wakulima tulikaa nao chini tukawapa mambo mawili cha kwanza tuwe tunawasaidia mbegu lakini na wao wawe wanachangia kahela kadogo ili ule mfuko tuutunishe wawe wanapata pembejeo na wawe wanapata mbegu kwa wakati. Tukaanza vizuri, baadae tukawa tunaishawishi Serikali ina yenyewe katika hizi asilimia tunazokusanya iwe inarejesha kuutunisha ule mfuko. Mfuko huo umeshindikana kupanda na mimi nimekaa kwenye zao la pamba kama mkulima na mwendeshaji wa zao hili kwa muda wa miaka kumi na tumepambana sana. Kaka yangu Shibuda yuko hapa, bahati mbaya Mheshimiwa Richard Ndassa hayupo, lakini tulikuwa kila leo tunakwenda *Tanzania Cotton Board* kuwauliza na kuwaomba waweze kutupenyeza *at list* Serikali hata mwaka mmoja ingeweze kutoa mchango mkubwa sana ili kusudi tuweze kupata pembejeo pamoja na dawa tukaweza kulirudisha zao hili kwa haraka zaidi. Lakini mpaka leo hali imekuwa mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi kinachonishangaza zaidi ni kwamba kila tunapokaa kwenye haya makabrasha Wizara mara nyingi inatuambia kwamba tuna miradi, tunaunda aina fulani ya kumboresha mkulima. Wakati wewe unajaribu kuleta miradi wadau wapo kule huwahusishi, hiyo miradi itakwendaje. Kwa sababu pale Nzera, kule Geita kwa sababu nilikuwa natembelea sana tuliambiwa kwamba kuna mradi wa *irrigation*, *pump* na *motors* kila kitu hakuna walishang'oa wakaondoka lakini hakuna anayeguswa pale. Unapokuja kwa huyu Afisa Ushirika mimi nina takwimu sahihi za Jimbo la Nyang'hwale, Busanda na Geita tuseme Wilaya nzima najua kila kijiji gani kinalima heka ngapi.

Lakini nikiingia kwenye ofisi ya kilimo hawana takwimu, wanataka mimi ndiyo niwape. Sasa ndiyo nasema hatuwezi kuendeleza hili zao bila takwimu na kingine ni kwamba kwa nini hawa wakulima hawasajiliwi kwenye vijiji vyao. Kwa sababu kama wale wakulima wanasajiliwa mle sisi tunaweza kujua kwamba Wilaya nzima ya Geita inahitaji mbolea kiasi fulani na dawa kiasi fulani. Sasa hapa inakuwa tu wakulima wa pamba, wakulima wa pamba ukiuliza takwimu hazipo, maendeleo ya kilimo hayataweza kutokea hata siku moja, tunapokuja kwenye suala hili la pesa za maendeleo zinatumika vibaya kwa sababu yale maendeleo hayapo. Huwezi kuniwekea mimi Afisa Ushirika kwenye Wilaya moja ambayo ni kubwa kuliko Mkoa wa Lindi, kubwa kuliko Zanzibar unaniwekea Afisa Ushirika mmoja hana pikipiki, hana usafiri. Hivi hiyo kazi tutaifanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi namwomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu tulikutana naye mwezi wa nne nafikiri tulikueleza. Mmetuletea vocha kitu ambacho ni hatari sana, pesa iliyoliwa ni kubwa na nyingine imefichwa, hata ya Geita imefichwa. Lakini tutaipekua tuipate tu. Kwa sababu sisi *TCA* na *TCB* zilianzisha kitabu kama *passport* ya kusafiria. Kile kitabu kinakuwa mali ya mkulima, kina *page* kama tano. Kwa hiyo, kila anapouza pamba unasaini pale kuwa amekuuzia pamba ili kusudi unapoleta mbegu

anapata na unapoleta dawa nazo anapata, lakini hiyo imeshindikana. Kwa hiyo, wachakachuaji wakaona labda vocha zile ndiyo zitasaidia, sasa hiyo imetuumiza. Hivi vyama vya ushirika kuvifufua ni vigumu kwa sababu tumeshaomba mara nyingi, hivi vyama zamani vilikuwa na watu wenye nidhamu.

Sasa hivi ukitizama wale wazee tuliowaacha mle ndani wengi wao hata zile tarakimu hawawezi kusoma. Vijana wetu wanaomaliza *form four* vijijini wapo wengi, vijana wanaomaliza kidato cha sita wapo wengi na vyuo. Wangeweza kurudisha hivi Vyama vya Ushirika kwenye barabara. Sasa mimi naomba kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kurudisha hivi vyama vya ushirika wakati wa Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin Mkapa nafikiri alimrudisha mtu ambaye ni mzoefu zaidi katika masuala ya ushirika *Sir* George Kahama aliandika namna ya kufufua Vyama vya Ushirika mwaka 1995. Sasa leo tupo mwaka 2011 hakuna kinachoendelea kwa hiyo, inamaana hata kile kitabu hakijafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ombi langu, kuna Wabunge wenzangu wameuliza na mimi nimeangalia hii *volume two sub-vote* kuanzia ya 1001 mpaka 5001 ukiziangalia hizi *sub-vote* hizi *traveling expenses* ni kubwa sana. Sasa kama *traveling expenses* ni kubwa hivi kama Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje alisema kila siku ni hizi *trip* za Dodoma - Dar es Salaam, wakati mwingine ni Dar es Salaam - Mwanza. Hizi *traveling expenses* wakati unakuta huku kwenye *research* vilevile zinatumika pesa nyingi lakini ukiangalia ile *production* yenyewe haipo. Mbegu ya pamba kila baada ya miaka mitano lazima utoe mpya, lakini hapa unasikia unatumia UK 77, unatumia UK 99 sasa mimi sidhani kama tutaweza kuendelea namna hii. Kwa hiyo, sasa badala ya hizi pesa kukaa tunazivuruga ni mara kumi kuajiri mabwana shamba mtu una tarafa mbili unakuwa na mabwana shamba hata wanne wanagawana zile kata kuweza kuelimisha hawa wananchi.

Mimi kwenye Wilaya nzima ya Geita ukichukua Jimbo la Busanda, uende Jimbo la Nyang'hwale uende Jimbo la Geita mimi sijawahi kuwaona mabwana shamba. Maafisa Tarafa wenyewe wapo, kwa nini wao wasihusishwe kwenye hizi *task force* za mbegu na pembejeo na mnapoleta hizi pembejeo sijaelewa ni kwa nini wale wahusika hawahusishwi? Madiwani mnawatenga kwa nini? Unaleta *task force* ile *task force* unakuta kwamba inaongozwa na kiongozi wa Serikali. Kiongozi wa Serikali anawapa zile vocha viongozi wa Serikali wanaingia benki wanachakachua halafu ile hela wanakula wenyewe. Sasa kwa nini Madiwani mnawakwepa wakati wao ndiyo wenye watu kule kwenye mashamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri naomba hii *task force* ya Wilaya, sisi Wabunge tupo, Madiwani wapo na watendaji wa vijiji wapo. Hii *task force* hawawezi kuongozwa na watu ambao hawaelewi yale mashamba yako wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi pesa za hiki kilimo cha kuchanganya pamba na mahindi. Naomba tuelewe kwamba kilimo cha mkulima ni kigumu sana. Anavyofanya vile yale mazao mawili huyavuni pamoja yanavunwa tofauti. Sasa kama mtu hana uwezo ana heka yake moja unataka aanzishe hekari ya pili, ule uwezo hana na hatumsaidii chochote. Sasa mimi nafikiri kwamba kwa sababu zipo taratibu, kanuni za kilimo zipo kama mkulima haelimishwi mtakuwa mnamwonea. Mimi naomba hizi ofisi za kilimo zitumie hawa Madiwani na Watendaji wa Vijiji. Kwa sababu haiwezekani wewe Wizara ukapeleka kila kitu kwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa vinaishia pale, wale wahusika wenyewe hawapati kitu chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho naomba kusema kwamba unapobuni miradi naomba tuwe waangalifu kidogo. Hizi *power tillers* aliyebuni simuelewi. *Power tillers* zote zipo vijijini kule, kule vijijini watu hawazitumii kwenye mashamba kwa sababu haiwezekani kuitumia ile *power tiller* shambani. Geita nililima hekari 1000, nilikuwa nina *farm track*, trekta za India tano, nimelima pale miaka mitatu, nikaunguza vidole hekari 1000 nikaacha. Hizi *power tillers* umeleta, *power tillers* unaweza kutumia kwenye mashamba ya Arusha ambayo hayana kisiki, hayana mawe ni *plain land,* unaweza kuyatumia Morogoro na unaweza kutumia kwenye mbuga za Shinyanga. Geita unaweza ukaleta *power tillers* kwenye mashamba na kulazimisha, wamenifuata wengi wenye *SACCOS,* kila wakiangalia wanaonunua wanafunga toroli kule nyuma wanaanza kusombea mawe na tofali. Tunafanyaje hapo? Ndiyo sababu nasema *research* hii sijui inafanyikaje? Wahusika wapo kule, lazima tuifanye ile kazi baada ya kuwauliza wenyewe. Lakini mtu anayebuni miradi hata sisi zile *farm track* zilituunguzia vidole. Mtu analeta *farm track* anazi-*dump* pale watu wanakuja wanakuzunguka zunguka, mkubali kuyanunua na ndicho tunachofanya hapa. *Power tillers* haziwezi kufaa maeneo ya visiki na mkulima hayupo tayari kuanza kung'oa visiki ni kazi ngumu. Mimi ilinipata nilipoteza dola laki mbili. Kwa hiyo, mimi nafikiri vitu vingine kwanza tuwaulize wenyewe wale wahusika ambao wanashughulika na hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru lakini la mwisho nitaomba Mheshimiwa Waziri hili suala la bei ya pamba kama inawezekana tupate jibu katika siku hizi mbili. Sasa mkulima hatoi pamba yake kwa sababu wanunuzi wanataka walipwe shilingi 700/=.

Mimi naomba Serikali iwalipe wanunuzi shilingi 1100/= lakini Serikali ibebe mzigo huu. Serikali inaweza kununua *bonds* na wanunuzi wote wamekopa benki, Serikali icheki kwa sababu pale una saini mkataba. Serikali inunue *bonds* ili iweze kuzi-*retain* hizi robota, wakulima walipwe, wakikaa na ile pamba itaharibika. Pamba haitakiwi kukaa sana kwenye maghala. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kununua hizi *bonds,* bei itakapo-*improve* Serikali itamalizana na wanunuzi ili yule mkulima aondokane na hii dhana ya kusema kwamba soko la dunia, wao hawaelewo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kwamba mchangiaji aliyemaliza sasa hivi ametaja Zanzibar na akaifananisha kama Wilaya. Tunachomwambia kwamba Zanzibar ni nchi, ina Serikali yake, ina Rais wake, ina Katiba yake na ina bendera yake. Kuna Wilaya zaidi ya 100 Tanzania Bara, asiichukue Zanzibar akaifananisha na Wilaya, tunataka hili suala likome. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba ukae chini, kwanza muda umeshatuishia lakini pamoja na hayo hiyo taarifa yako itazingatiwa tu kwa maana ya mchangiaji kuisema Zanzibar kama nchi. Hayo maneno mengine yote sidhani kama kuna msingi katika hilo. Taarifa hiyo itazingatiwa kwenye *Hansard,* Zanzibar ni nchi hakuna kingine cha ziada. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naona shughuli zetu zilizokuwa hapa zimetuishia naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, tumebakiza wachangiaji watatu ambao hawajachangia hata mara moja humu Bungeni. Nitamwita Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Shaffin Sumar.

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu. Siyo kawaida yangu mimi kutokuunga mkono hoja ya Serikali, siyo kawaida wala sijawahi kufanya jambo la namna hiyo. Lakini naomba kusema kwa hii hoja iliyo mbele yetu siiungi mkono mpaka nipate maelezo kwa hoja tisa nitakazozitoa na mpaka nitakapopata maelezo, mimi sitaki kusema zaidi ya kwamba siiungi mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza ya kutokuunga mkono hoja ni kuwa mwaka 2006 tulifanya mabadiliko ya Sheria ya *Finance Bill*, katika sehemu ya 10(a) ya sheria wakati huo ya Bodi ya Korosho. Ile sheria ilitaka kuwatoza watu wote wanaosafirisha Korosho ghafi nje *(FOB Value)* asilimia 10 ya mauzo. Katika hiyo asilimia 10, asilimia 6.5 zinakwenda kwa Halmashauri zinazozalisha korosho, asilimia 3.5 zinakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Hiyo ni sheria ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu ni kwamba tangu tulipopitisha na hii inathibitishwa pia na taarifa ya *review* ya *finance* na *performance review* ya mwaka 2009 inayoonyesha kwamba kwa mwaka 2007/2008 Bodi haikupokea hata senti moja ya *Export Levy*, mwaka 2008/2009 Bodi haikupata hata senti

moja, inaonyesha sifuri sifuri kwenye ile ripoti ya *Export Levy*, mwaka 2009/2010 imepata sifuri, sifuri, sifuri fedha ya *Export Levy*. Lakini fedha hizi zinakusanywa na *TRA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri asije akasema mbona tulipitisha Sheria ya Korosho ya mwaka 2009, naijua tulipitisha hapa hapa na tukapitisha na *Finance Bill* ya mwaka 2010. Lakini *Finance Bill* ya mwaka 2010 haikufuta, hata kama imefuta ile *Finance Bill* ya mwaka 2006, fedha zilizokusanywa tangu mwaka ule 2006 mpaka tunapitisha hii *Finance Bill* mpya, fedha hizo ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninayo taarifa kwamba *POAC* ilipokutana mwezi Mei, iliwaita wahusika wa Bodi ya Korosho kuwauliza juu ya mfuko huu. Hawakutoa majibu ya kuridhisha, *POAC* ikaagiza kwamba hizi fedha zikaguliwe na *CAG.* Mimi ninataka sababu yangu ya kwanza hiyo, *CAG* akague kwanza hizi fedha tujue ziko wapi, ametumia nani, nani anayetunza fedha kabla hata ya sheria hii mpya haijaanza kazi, fedha zile hazipo na nitaeleza mengine huko mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyosema, hakuna pembejeo za zao la korosho, katika mikoa yote imeadimika. Tangu kulikuwa na zile kidogo ambazo sisi wenyewe wakulima tulichangia fedha tukapewa kidogo, dukani hakuna *sulfur*. Leo Masasi mfuko wa *sulfur* ni shilingi 50,000/= kwa mfuko mmoja wa kilo 25. Kwa shamba langu mimi nahitaji angalau kwa mpulizo mmoja mifuko 25. Nikinunua kwa shilingi 50,000/=, hiyo korosho itauzwa kwa shilingi ngapi kwa kilo mpaka mimi nipate *break even?* Vema mimi na hao wakulima wengine je, na hiyo *sulfur* inayopatikana ni kwa magendo, hakuna *sulfur* madukani? Sijui mikoa ya watu wengine, lakini kwa Mtwara ninao uhakika huo, hakuna *sulfur*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu yangu nyingine kama nilivyosema kwamba Bunge limepitisha Sheria ya *Cashewnuts Industry Act* ya mwaka 2009 na tukafanya mabadiliko ya *Finance Act* Na. 15, 2010. Lakini kabla ya huko nyuma, hela hizi zimeenda wapi? Kabla ya hii *Finance Act* ya mwaka 2010?

Lakini hata hiyo *Finance Act* ya mwaka 2010, naomba ninukuu; "Inafanya marekebisho na kwa kuwa hii ilifuta ile ya mwaka 2006 kwa kifungu cha 17(a)," nikaenda kutafuta Sheria ya *Cashewnuts Industry*. Kifungu cha 17 hakizungumzii *Export Levy*. Kifungu cha 17, kinazungumzia, ngoja nisome kinazungumzia, *"cancellation or suspension of licences,"* Kifungu cha 17. Sasa *Finance Bill* inazungumzia kifungu hicho, lakini huku ni *cancellation*, na tumekwenda tangu asubuhi, ndiyo maana nikaomba nichangie jioni, natafuta kama tumefanya *amendment* ya hii sheria, siioni. Hakuna mahali popote tulipoiona na sheria hii inasema itaanza kutumika siku Waziri atakapotangaza kwenye *Official Gazzete*. Nataka kujua umeitangaza lini mpaka sheria hii inaanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *amendment* inasema tutashirikiana na wadau na Wizara kuweka utaratibu wa hizo fedha. Leo nimeshangaa kupata maelezo kwamba eti wadau hao wapo, walikutana sijui wapi! Hivi inawezekana Wabunge wote wanaolima korosho hawajui juu ya wadau, anayejua Waziri wa Kilimo tu peke yake? Wadau hao umewaokota wapi? Ni kikao gani cha wadau hata cha *RCC* kilichochagua mdau kila Mkoa, kila Mkoa waende kwenye hicho kikao cha wadau ambacho ninyi mmewahalalisha, mmewaandikisha *RITA* na Mfuko mmeandikisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa ambayo nimeipata kutoka huko huko kwenye Wizara, mwaka huu, fedha za *Export Levy* zilizopatikana ni shilingi bilioni 15. Ngoja nisome, nisije nikakosea, mkasema aah hukusema sawa sawa. Zimepatikana shilingi 15,747,429,683.40. Eti kwa sababu Mfuko umesajiliwa, mwezi Juni, 2011 mmewapa hao wadau ambao sisi hatuwajui, tunauliza kwenye *RCC* hatupati majibu hela zimekwenda wapi, mmewapa shilingi bilioni 1.4. Tunataka kujua hizi pesa nyingine ziko wapi? Mmezipeleka wapi? Hivi ni zao gani katika nchi hii, kahawa, tumbaku, pamba, inafanywa hivi? Ila mnafanya kwa korosho peke yake kwa nini? Serikali inachukua hela za wakulima wa korosho, mnaunda watu, mnaita watu wachache, mnasema mmeunda timu ya wadau, halafu wadau hawa wameandikishwa, hela zimeingia kwenye mfuko, wamefungua na akaunti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumekuwa katika *RCC* Mtwara, tunaulizia hizi, Wabunge wote wa Mtwara, wote 11 hawajui, hata *RCC* haijui. Sasa mtuambie, hicho kikao cha wadau ni nani aliwateua hao wadau? Maana si Halmashauri za Wilaya zinazolima korosho, si *RCC*, si Mikoa, hata Wabunge ambao ndiyo tumepitisha ile sheria kwa kuamini kwamba sisi ndiyo tutashiriki katika kuunda hao wadau tuwajue, hatujui! Mmepata wapi *mandate* ya kutumia hela za wakulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hakuna *sulfur*, hela mmekalia. Wakati huu tungekuwa tunapuliza kwa mara ya pili au ya tatu kwenye korosho, hatujapuliza, wengine hawajapuliza kabisa. Mimi nimepuliza mara moja. Hasara itakayotokea mwaka huu nani atalipa? Sababu nyingine ya kutokukubaliana kabisa na hii hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema katika kitabu chako hiki cha hotuba, ukurasa wa 104, Ibara ya 105 eti unajirabu hapa unasema kwa ajili ya stakabadhi ghalani, watu tumepata hela zaidi mwaka jana. Hii ni *fact*, ni kweli. Halafu unasema mwaka huu tutazidisha korosho. Korosho mtazidisha kwa nini? Leo *sulfur* hakuna, dawa hakuna, tutazidishaje? Hatujapuliza, muda unapita! Kwa hiyo, hii ni *statement* ambayo kama walikupa hawajakuambia ukweli. Hiyo ni sababu mojawapo ambayo sitaki kabisa kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine nimekwishakuisema kwamba mmekusanya shilingi bilioni 15 na milioni 700, hao wadau kwenye Mfuko huo, huo *Trust Fund* mmepeleka shilingi bilioni 1.4, nyingine zipo wapi? Usiponijibu hela hizo ziko wapi, mimi kabisa na ninachelea, siwezi kusema natoa shilingi kwa sababu sijakusikia majibu yako, inawezekana unayo majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu, katika hiyo *amendment* ya mwaka 2010, ilikuwa utengeneze *regulation* ya namna ya kugawanya hizo fedha kati ya hao wadau na wadau wote nafikiri na wadau hapa ni Halmashauri zinazolima korosho ndio wanaochacharika kusaidia namna ya kuongeza zao la korosho hapa. Halmshauri hawa wanapata kiasi gani? Na hiyo *regulation* ipo umeandika? Na kama *regulation* bado inakuwaje unaanza kutekeleza sheria kabla hujaweka *regulation*? *Regulation* iliyoko katika sheria hii ni ile ilikuwa tu ni nyongeza kwa ajili ya kuunda Bodi ya Zao la Korosho, lakini hii nyingine bado. Kama umekwishaiandika, utatuambia kwa nini umetekeleza sheria kabla ya kuweka *regulation* ya namna ya kugawanya hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine Bodi ya Korosho iliyokuwepo kabla ya Sheria hii ya mwaka 2009 ya *Cashewnuts Industry Act,* imekwisha muda wake tangu mwaka 2009. Leo Bodi haina Mwenyekiti, haina Wajumbe wa Bodi. Huyu anayeendesha mambo haya ya korosho ni nani? Huu ndiyo utawala bora! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu hapo ndiyo mmeunda, mkaitisha kikao cha wadau ninyi wenyewe. Huyo mliyempa kazi ya kuendesha Bodi, Bodi ambayo haipo, hakuna *Board of Directors*, hakuna, mmeitisha kikao cha wadau, hatuna taarifa, mmefanya kila kitu na mpaka hela zinakwenda huko! Mimi nasema hili wala siyo utawala bora. Hiki ni kinyume kabisa cha utawala bora. Mimi ninashangaa, hivi ni Serikali hii hii ya kwangu ya CCM inafanya mambo kama hayo? Inashangaza kabisa! Ni nani mmemuachia madaraka ya maamuzi ya Sera ya Bodi ya Korosho, nani mmemuachia? Meneja Mkuu ndiye mliyempa madaraka ya kuendesha kila kitu? Mimi sijui, lakini nimeambiwa vile vile eti mnasema hivi, kama kuna jambo linatakiwa la Bodi, ita Bodi ya zamani ili ipitishe. Mmepata kuyasikia hayo? Kwa sheria ipi iliyokupa wewe *mandate* kufanya hivyo? Na baadhi ya wajumbe wamekataa kwenda kwenye Bodi kwa sababu ni kinyume cha sheria. Kwa hiyo, mimi siungi mkono hoja hii. Ninazo sababu nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, pia unijibu ni *RCC* gani iliyoshiriki katika kuunda hicho kikao cha wadau na mlikutania wapi na ni akina nani? Sisi hatukatai, tumepitisha sheria hiyo sisi. Lakini wadau wa korosho bila Halmashauri zinazolima korosho, bila mikoa inayolima korosho, bila hata Wabunge tuliopitisha sheria hatujui, hiyo kwa kweli ni kinyume kabisa, kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wakulima wa korosho mnawaonea. Kwanza, mmepitisha sheria kwa kufuata kifungu cha 17(a), kifungu cha 17(a) hakisemi chochote juu ya hili jambo. Kwa hiyo, mimi kwa mawazo yangu na makubaliano yangu naona kwamba sheria ya sasa hivi iliyopo, kwanza nadai mtuambie, hela za mwaka 2006/2007, 2007/2008, 2008/2009 na 2009/2010. Hizi nyingine zipo mahali, shilingi bilioni 15, shilingi bilioni 1.4 mmeishatoa, lakini huko nyuma ziko wapi fedha? Mmezitumiaje na kwa sheria ipi iliyowapeni ninyi *mandate* Kilimo kufanya hayo?

Sasa mimi ninasema hivi, mimi namwamini sana Waziri Mkuu, tena sana. Mengine mnayafanya hata Serikali yenyewe haijui na mimi nitashangaa. Nakuomba Waziri uyajibu haya yote karibu pointi nane/tisa hizi, uzijibu vizuri, niridhike ili niunge mkono hoja. Vinginevyo mimi natoa *notice* kwamba hapa

hapatoshi, hela hizo za wakulima wa korosho lazima tuzijue, Halmashauri zinazochacharika kuhimiza kilimo cha korosho lazima zijue.

Mimi najua kuna Bodi mmetangaza hiyo Bodi ya wadau, mmechagua na wawakilishi wapo. Hivi kweli Mkoa wa Mtwara, Lindi, Ruvuma, mnachukua mwakilishi mmoja sawa na wengine wote wanao-*produce!* Sisi ndiyo *giant* wa korosho! Lakini waliteuliwa wapi, mbona hatujui? Hivi kwa nini mnafanya siri kwa hela za korosho? Mnafanya hivi kwa kahawa? Mnafanya hivi kwa pamba? Mnafanya hivi kwa tumbaku? Kwa nini korosho peke yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kusema mengi. Naomba kusema kabisa siungi mkono hoja hii na ninasikitika kweli kweli kwamba kwa mara ya kwanza naipinga Serikali yangu, lakini nasema…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa!

**MHE. ANNA M. ABDLALLAH:** Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia mawili, matatu na kwa kuwa ni mara ya kwanza mimi kuchangia Bajeti, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya njema na kuniwezesha kushinda katika Uchaguzi Mkuu uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nikishukuru chama changu cha CCM kwa kuniteua kuwa mgombea. Naomba nitumie fursa hii kumshukuru mke wangu Reshma Sumar, watoto wangu wawili Sarah na Kush Sumar kwa kunivumilia na kunipa moyo kila wakati. Naomba niwashukuru kwa kipekee sana wananchi wangu wa Jimbo la Tabora Kaskazini kwa kunichagua kwa kishindo. Nimeweza kushinda kwa asilimia 85 jambo ambalo halijawahi kutokea katika historia ya Jimbo la Tabora Kaskazini. Nataka niwahakikishie kwamba sitowaangusha na nitahakikisha nawafanyia kazi kwa nguvu zangu zote, *Inshallah! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na zao la tumbaku. Sasa kwa kuwa mimi ni mvutaji wa sigara, sijui ni-*declare interest* hapa! *(Makofi)*

Naomba niseme kwamba tumbaku inayozalishwa Tanzania ni takriban tani 130,000 na zaidi ya asilimia 50 ya tumbaku hii inayozalishwa Mkoa wa Tabora, tuseme ni asilimia 50. Lakini wakazi wa Tabora ambao ni takriban asilimia 70 wanalima zao la tumbaku. Lakini jambo la kusikitisha sana hapa ni kwamba soko la zao la tumbaku la mwaka huu bado linasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba soko limechelewa sana kuanzishwa, lakini bado haiendi, haifanani na manunuzi yanavyotakiwa yafanyike kwa mwaka huu kwa sababu wanunuzi wananunua mara moja kwa mwezi, jambo ambalo hata Serikali yetu imekosa kauli kwa ajili ya kushinikiza ununuzi uende haraka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wetu kwa kweli wana matatizo sana. Kwa mfano zao la tumbaku limewekewa daraja 65, lakini ukiangalia vizuri ule mche wa tumbaku unakuwa na majani kati ya kumi na mbili mpaka kumi na sita, sasa nashindwa kuelewa kama mche unakuwa na majani hayo machache, ardhi ni ile ile, eneo ni lile lile, mbolea ni ile ile inakuwaje tuwe na *65 grades.* Hali hii inawakandamiza zaidi wakulima wetu, lakini bado wanaendelea kunyanyasika kwa sababu wakulima wanapofunga tumbaku yao, ile tumbaku inapoenda inakuwa na magunia ya wakulima ambayo wamenunua wenyewe. Yale magunia yakishatumika yakirudi tunayaita Majafafa yanarudishwa tena sokoni na mkulima anatakiwa tena anunue ili aweze kufunga tumbaku yake. Hali hii hairidhishi na gharama ambayo siyo ya lazima kwa wakulima wetu wa tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali itusaidie, ihimize haya masoko ili yaweze kununuliwa angalau mara mbili kwa mwezi kwa sababu mwaka huu sisi wote tunafahamu ni mwaka wa njaa. Wakulima hawana fedha kwa sasa hivi wanategemea kwamba wakiuza tumbaku yao watapata fedha kwa ajili ya kununua chakula ili waweze kukabiliana na njaa inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi soko linavyochelewa wananchi na wakulima hawalipwi, hali ambayo inasababisha chakula kuendelea kupanda bei siku hadi siku, hasara hii inayotokea ni nani ataifidia. Lakini tayari mkulima huyu bado anadaiwa fedha benki ambazo anatakiwa alipe ndani ya mwezi wa nane nan asipolipa atatakiwa kulipia riba ya mwaka unaofuata. Hivi inakuwaje mkulima huyu amelima msimu mmoja lakini atatakiwa alipe riba ya miaka miwili ndani ya msimu mmoja, haiwezekani!

Lakini mkulima huyu bado tunamtegemea kwamba aweze kuchangia miradi ya maendeleo, mkulima huyu bado atatakiwa achangie ujenzi wa shule, ujenzi wa zahanati, ada ya watoto na kadhalika. Wahenga walisema mzigo mzito mpe Mnyamwezi, lakini katika hili naomba niseme sisi Wanyamwezi wa karne hii hatuko tayari kubebeshwa mzigo mzito usiokuwa na maana. Hatutakubali, mzigo huu tutautua chini na Serikali ije itusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumbaku ni zao ambalo tunalitegemea na ni zao ambalo linatuletea maendeleo, kama Serikali mwaka huu isipotusaidia katika msimu huu, hakika tutakosa imani na Serikali yetu. Lakini naamini kabisa Serikali yetu ni sikivu na itatusaidia kuanzia leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika unatusaidia sana na Rais amejitahidi sana kulipa madeni ya ushirika na kuyafufua upya, lakini bado Maafisa Ushirika hasa wa Wilaya hawajapewa uwezo mzuri wa kuweza kusafiri kwenda kukagua maeneo yao ya Vyama vya Ushirika hali ambayo inazorotesha sana utendaji mzuri wa vyama vyetu. Lakini pia kuna maafisa wachache wa ushirika ambao wanasababisha kabisa kwa maksudi kuhakikisha kwamba vyama vya ushirika vinakufa, naomba Serikali yetu isiruhusu hali kama hii, na pindi mtakaposikia sisi Wabunge tunalalamika kuhusu Afisa fulani basi tupewe ushirikiano mzuri ili vyama vyetu vya ushirika visije vikafa, masuala ya kulindana tunasema sasa basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji ni mkombozi pekee kwa Watanzania na mimi pia naamini kabisa Serikali tukijikita zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji hali ya uchumi itabadilika. Lakini naomba nishauri kwamba tuende hatua moja zaidi na tuweze kuanzisha kilimo cha umwagiliaji wa matone. Tukianzisha itatusaidia sana kuona kwamba wananchi wetu wanatumia maji machache lakini wanazalisha zaidi, kilimo hiki kitawasaidia wananchi wetu waweze kulima miezi yote 12 na kilimo hiki kitatutoa katika utegemezi wa mvua ya vocha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya leo sikuona mahali ambapo mradi huu wa kilimo cha umwagiliaji unaanzishwa au unafanyiwa kazi Jimbo la Tabora Kaskazini katika hili naomba niseme kwamba nitatoa shilingi kama sikupewa majibu ya uhakika kwa sababu tangu dunia ianze Jimbo langu la Tabora Kaskazini halijawahi kupewa mradi wa kilimo cha umwagiliaji, naomba nielezwe ni sababu zipi zinafanya Serikali yetu isione Jimbo la Tabora Kaskazini kama linaweza kunufaishwa na kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho naomba niseme kwamba *power tillers* hizi tunazoletewa kwa kweli hazitusaidiii, tunachohitaji ni Serikali itusaidie tupate trekta ili ziweze kufanyakazi zenye tija zaidi. Vilevile nitapenda kuiuliza Serikali kwamba kuna msaada wa matrekta tuliletewa kutoka India ambayo nasikia yapo SUMA JKT yamekaa, ni kwa nini Serikali haiwezi ikaona kwamba iwasaidie wananchi ili wakulima wetu waweze kujikwamua kimaendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo yangu ni hayo machache lakini narudia kwamba nitatoa shilingi mpaka nipate majibu ya uhakika na hapo ndipo nitakapounga mkono Bajeti hii, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango wangu mfupi katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwanza napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Naibu Waziri wake Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza, Katibu Mkuu na timu yao yote kwa uwasilishi mzuri wa hotuba ya Bajeti ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kama uti wa mgongo ukichangia zaidi ya nusu ya Pato la Taifa na kuchangia zaidi ya robo tatu ya mauzo ya nje na zaidi ya asilimia 70 hadi asilimia 80 ya ajira katika nchi yetu, hapana shaka ni Wizara muhimu sana kwa maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa changamoto kubwa ambayo inaikabili nchi yetu ni umaskini bado tunahitaji mikakati madhubuti na mizuri sana ya kutekeleza kilimo ili tukabiliane na umaskini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukiangalia kwenye takwimu za Dira ya Taifa ya 2025 bado tunaona kwamba kilimo bado kiko mbali sana katika kufikia malengo hayo. Kwa mfano, takwimu zinasema kwamba katika hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo bado ni asilimia 23.1 tu ambayo imelimwa na katika hekta milioni 29 ni asilimia moja tu ambayo inafaa kwa *irrigation* ambayo imekwishatumika, kwa hiyo tukiangalia kwa mapana kabisa bado kilimo chetu kiko mbali sana na Dira ya Taifa ya 2025, kwa hiyo ni changamoto ambayo Wizara inabidi iangalie kwa upana ili tuweze kufanikiwa katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichangia kidogo kuhusu kilimo na idadi ya watu na changamoto kubwa ya ardhi finyu, umuhimu na uhitaji wa rasilimali ardhi unazidi kuongezeka siku hadi siku, tunaambiwa kwamba kesi nyingi zilizoko mahakamani sasa hivi hasa mkoani kwetu Manyara nyingi ni kesi za migogoro ya ardhi, baina ya wakulima kwa wakulima, wakulima kwa wafugaji na wananchi wenyewe. Nadhani hii ni changamoto kwa sababu ardhi ni mali na watu wanaongezeka ardhi inabaki ile ile na kwa hiyo Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Ardhi hii ni changamoto ambayo siyo ya kupuuza kwa sababu tukitizama asilimia 75 ya ardhi ya nchi yetu, haina wakazi, haifikiki, ni miamba na miteremko, hailimiki, kuna mbung’o, mvua haitabiriki na kadhalika. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri badala ya kuangalia tu wawekezaji wanaokuja katika nchi yetu kuweka viwanda na uzalishaji wa kupata mapato, ni vizuri pia tukaangalia ni namna gani tunaweza sasa tukakomboa kidogo kidogo hiyo asilimia 75 ya ardhi yetu ambayo haifai kwa kilimo. Ongezeko hili la watu ni vizuri tukafikiria kwa mapana kwamba tutaongezaje sehemu ya ardhi yetu ambayo inaweza ikalimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo moja ambalo linasikitisha zaidi, jambo hili ni la wakulima na wafugaji, migogoro baina ya wakulima na wafugaji ni suala ambalo limechukua sura na limekaa muda mrefu hapa nchini kwetu, lakini halijaweza kufikiwa na kupewa ufumbuzi wa kudumu. Kwa mfano mkulima anapolima anaacha shamba lake linakuwa ni alama, mbaya zaidi ardhi yetu sasa hivi inamilikishwa kwa hiyo mkulima akikaa kwa muda fulani anaweza akamilikishwa hiyo ardhi ambayo mwanzoni pengine ilikuwa ardhi ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wenzetu wanahamahama, wanakwenda mbali pengine wanatoka Arusha wanakwenda mpaka Mkoa wa Lindi na huko wanafukuzwa wanaporudi kwenye ardhi yao wanakuta imemilikishwa. Hili linasikitisha, nadhani ni vizuri Serikali ikaanza kufikiria kwa upana badala ya kufikiri tu kwa wepesi kuona kwamba hawa ni wafugaji wanahamahama, lakini huko tunakoenda ardhi yetu inazidi kuwa ndogo, wafugaji hawatakuwa na kwao, wao hawatakuwa na ardhi hata ya kusema kwamba watamilikishwa ardhi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo migogoro hii ya wakulima na wafugaji ninaomba Wizara husika ziweze kuangalia kwa macho ya huruma na kuona kwamba wafugaji nao hiyo ardhi ni yao, nchi ni yao na kwa hivyo waone ni namna gani wataweka mikakati ya kuwamilikisha ardhi ili nao baadaye wataacha kufuga, maana nadhani ufugaji kadri nchi yetu inavyotoka kwenye mfumo wa kutegemea kilimo kwenda kwenye viwanda na wafugaji hali kadhalika watapata mfumo wao wa kutoka kwenye ufugaji na kuweka uchumi wao kwenye viwanda vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu pembejeo za kilimo, hili ni eneo ambalo limekuwa kama wimbo. Mimi tangu niingie hapa Bungeni tangu waanze kutoa ruzuku na vocha za pembejeo, Wabunge wanalalamika, Kamati asubuhi imelalamika, Kambi ya Upinzani inalalamika, mimi naona kama ni wimbo sasa maana yake sioni kama Serikali inachukua jukumu ama kuweka mkakati mzuri wa namna gani wakulima watapewa utaratibu mzuri wa kutumia pembejeo za kilimo, dawa, mbolea na mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, unapoleta mbegu wakati mkulima tayari amekwishapanda, sielewi zile vocha sasa zinakwenda kufanya nini, ama unapoleta mbolea ya kupandia wakati mkulima anakaribia kufanya palizi, inakuwa ni hasara na haieleweki sasa zile vocha zinakwenda kufanya nini. Unapoleta mbolea ya kukuzia *(NPK)* kwa mfano, mkulima anahitaji *sulphute ammonium* anakuwa hawezi kutumia kwa msimu huo, sasa naona kama hili ni tatizo ambalo linawapata wakulima wengi sana nadhani ni nchi nzima lakini sioni kama linapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Waziri wakati atakapokuwa ana *wind up* atatueleza ni utaratibu gani sasa ambao tutaacha kuzungumzia hili suala la vocha tuende katika hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni mazao ya mafuta katika nchi yetu. Kuna matatizo mengi ya kiafya ambayo yanazuka ambayo yanatokana na matatizo ya kutumia mafuta kutoka nje ambapo tunalima mazao yao katika nchi yetu. Tumekuwa tukiendelea kuagiza mafuta lakini mafuta yenyewe tunayoletewa kutoka nje ya nchi yanaathiri afya zetu. Lakini kumbe ndani ya nchi yetu tunalima mazao mazuri sana ambayo mafuta yake ni mazuri kwa afya, hayana *cholesterol* lakini tunaishia kuuza nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa wito kwamba mazao haya ya mafuta ya kula ya alizeti, ufuta na mafuta yanayotokana na pamba ifike wakati sasa na sisi tuweze ku-*produce* kwa *internal consumption* ya Watanzania badala ya kufikiria kuuza tukiendelea kutumia mafuta ambayo yanatoka nje na hayafai kwa maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii mimi niliona nina mchango mdogo naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, lakini kabla sijachangia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na uhai wa kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbali nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa jinsi alivyotukumbuka Wanadodoma hata alipokuwa safarini. Ni wiki iliyopita tu Rais alikuwa Afrika Kusini na akakutana na wakulima wakubwa wa zao la zabibu na akawahamasisha na kuwaomba waje Dodoma kushirikiana na wananchi wa Dodoma kulima zabibu. Napenda kumhakikishia kwamba sisi Wanadodoma tutashirikiana kwa asilimia mia moja pamoja na wawekezaji hao watakaokuja kulima zao la zabibu katika mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Waziri Mkuu kwa somo zuri tulilopata siku ya Jumamosi alipotembelea kitongoji cha Nyerere na kuhamasisha wakulima watakaotumia maji katika ukulima wa umwagiliaji na pia ufugaji wa nyuki. Tulipata somo zuri sana tuliokuwepo pale kwamba kweli mazao yanayotokana na ufugaji wa nyuki kwa mfano asali lita moja ni shilingi 8,000 na hakuna zao ambalo linauzwa shilingi 8,000 kwa lita au kwa kilo. Kwa hiyo, nakushukuru sana Waziri Mkuu kwa kutuhamasisha kufuga nyuki na pia kilimo cha umwagiliaji na matumizi mazuri ya maji ya visima ambayo tunapata kutokana na wafadhili wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilete kilio cha Wanadodoma katika Bunge lako Tukufu kwamba mwaka huu hatukupata mvua ya kutosha kwa hiyo, Mkoa wa Dodoma tuna njaa ya kutisha. Kutokana na taarifa za wana hali ya hewa na Maafisa Kilimo ni kwamba mwezi Novemba tulipata mvua kwa siku tatu tu, lakini mwezi Disemba tukapata mvua kwa siku nane, Januari tulipata mvua kwa siku 12 na mwezi wa pili tulipata mvua kwa siku kumi na mwezi wa tatu tulipata mvua kwa siku saba, mwezi wa Aprili tulipata mvua kwa siku mbili. Ukiangalia hali ilivyokuwa kwa mtawanyiko wa mvua ni kwamba hatuwezi kuvuna kitu, kwa hiyo, Mkoa wa Dodoma una njaa na hasa Wilaya ya Dodoma Mjini ambayo ina Kata 37 na wakazi wengi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika takwimu ambazo tunazo hadi Juni, tulikuwa tumevuna tani 52,508 mazao ya chakula kwa asilimia 40 na tani 30,472 mazao ya biashara. Kwa hiyo, ukiangalia hali halisi utaona kwamba kwa vyovyote hatutakuwa na chakula cha kutosha kwa mwaka huu kwa wananchi wetu, hivyo Serikali ituangalie kwa jicho la huruma, siyo kwamba tuna njaa kwa sababu hatukulima, tuna njaa kwa sababu hatukupata mvua za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoanza kutekeleza azma ya Kilimo Kwanza, ni vizuri sasa tukatafakari tumepiga hatua kiasi gani. Tukiangalia matumizi ya zana bora za kilimo, nikinukuu Hotuba ya Waziri wa Chakula, Kilimo na Ushirika, mwaka 2005 ni asilimia 10 tu ya Watanzania waliweza kutumia trekta. Lakini mwaka 2010 ni Watanzania asilimia 12 tu ambao walitumia trekta kwa ajili ya kilimo. Ndani ya miaka mitano kuna ongezeko la asilimia mbili tu. Lakini pia mwaka 2005 asilimia 20 ya Watanzania walikuwa wanatumia majembe ya wanyamakazi.

Lakini mwaka Watanzania asilimia 24 tu ndio wanaotumia majembe ya wanyamakazi yaani ongezeko la asilimia 4 tu. Mwaka 2005 asilimia 70 ya Watanzania walikuwa wanatumia majembe ya

mkono, lakini mwaka 2010 asilimia 64 ya Watanzania wanatumia jembe la mkono. Kwa hiyo, utaona jinsi ambavyo kilimo chetu kilivyo duni na jinsi Watanzania walio wengi bado wanatumia vifaa duni. Nikisema hivyo ina maana kwamba hatuwezi kusema kilimo chetu kinakua. Kilimo hakiwezi kukua kama Watanzania asilimia 64 bado wanatumia jembe alilotumia babu yangu na bibi miaka 50, 60 iliyopita. Ni vizuri sasa tufike wakati Wizara hii iangalie namna ya Watanzania wengi watakavyoweza kutumia vifaa vya kisasa au pembejeo za kisasa katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka utumiaji wa vifaa duni ndio pia unaleta upungufu wa chakula katika nchi yetu. Kundi kubwa pia la vijana katika nchi yetu hawajahamasika kulima, ndio maana wengi wao wako mjini kutafuta kazi kwa sababu kilimo wanacholima katika vijiji vyetu havilipi. Kule vijijini hawana zana za kilimo, pembejeo hazitoshelezi. Wanatumia mbegu kama mahindi ambazo ni mbegu za kumaliza miezi sita ndiyo wavune, kama ni karanga hakuna pembejeo. Mimi nadhani ifike wakati vijana watumike katika kilimo. Lakini hawawezi kutumika kama hawatawezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la pili ni la wanawake. Wanawake wanalima na watoto migongoni kwa jembe la mkono. Wanalima tangu asubuhi na watoto migongoni kwa jembe la mkono na mtoto wake wa kike pembeni. Miaka nenda rudi Watanzania hawa wanahangaika kulima kwa majembe ya mikono. Hatuwezi kufika mbali kwa kutumia majembe ya mikono. Ifike wakati Serikali ione umuhimu wa kwamba vikundi vianzishwe katika vijiji vyetu na katika Halmashauri zetu, wananchi wakopeshwe zana bora za kilimo pamoja na mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeona katika maonyesho mbalimbali, wanawake sasa hivi wanajitahidi kusindika matunda, mboga mboga na mazao mbalimbali, wengine wanauza asali, lakini soko la uhakika hawana. Wanategemea soko la humu ndani na soko la humu ndani pia siyo la uhakika. Hawana masoko ya kuuzia mazao. Siku kwa siku wanajikuta wanaendelea kuwa masikini pamoja na kutumia jembe la mkono pamoja na kuumia sana kwa kazi ngumu za tangu asubuhi, lakini bado hawana masoko ya uhakika, bado hawana vifungashio kwa wale ambao wanajitahidi kutengeneza au kusindika mazao bado hawana vifungashio. Lakini hata vifungashio vinavyopatikana, bado ni vya ghali. Ninaomba Serikali yetu Tukufu iangalie namna ya kuwasaidia wanawake hawa pamoja na vikundi vya vijana vitakavyoundwa, kwa sababu vijana ndio nguvu kazi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposoma hotuba ya Waziri, pia nimeona jinsi Serikali inavyoagiza asilimia 70 ya mbegu bora kutoka nje wakati tuna Vyuo vya Utafiti na ndio sababu mbegu zinauzwa ghali sana katika maduka ya pembejeo. Serikali ione namna ya kuwasaidia wananchi. Katika Hotuba ya Waziri kati ya tani 20,826.4 za mbegu ambazo ziligawanywa kwa wakulima tani 12,717 ziliagizwa kutoka nje. Hii inawapa taabu sana wakulima kununua mbegu. Hebu fikiria mwaka huu hatukuvuna, lakini itakapofika mwezi Novemba au Desemba kipindi cha kilimo, na kupanda, mkulima anatakiwa kununua mbegu kwa Sh. 3,500/= hadi Sh. 4000/=. Hizo fedha anatoa wapi? Kwanza chakula hana, na pili, anatakiwa kununua pembejeo na fedha hana. Mimi nadhani ufike wakati Serikali itumie vyuo vyetu vya utafiti kuzalisha mbegu bora kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wana Dodoma tunalima karanga, mahindi, ufuta, alizeti na mazao mengine. Lakini katika Hotuba ya Waziri anasema tani 356 ya mbegu za mtama zilisambazwa katika Mikoa sita, wastani wa tani 59 kwa kila Mkoa. Huku siyo kuipa umuhimu Kilimo Kwanza? Tani 59 ni mbegu kidogo sana kwa Mkoa mzima hasa wa Dodoma. Kama Serikali ina nia ya kuwasaidia wananchi wake mbegu bora, nadhani utafiti ufanyike na ijulikane kwamba wananchi wanataka tani ngapi na Serikali itoe hizo tani kama ruzuku kwa wananchi wake. Tani sita tu ya mbegu za alizeti kwa kila Mkoa kwa Mikoa inayolima alizeti hamkututendea haki hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ufike wakati wa kuweka kilimo katika dhana ambayo tunaitarajia sisi Watanzania. Dhana ya Kilimo Kwanza pia mimi ninavyoiona haijaeleweka kwa Watanzania. Azma ilikuwa ni kuleta kichocheo kwa kuongeza uzalishaji kwa wananchi, lakini hebu tuangalie wananchi, uzalishaji umeongezeka kiasi gani? Kama Watanzania bado wanatumia jembe la mkono, uzalishaji umeongezeka? Mimi sioni kama uzalishaji umeongezeka. Kama kweli azma ni kuongeza uzalishaji, kuongeza usindikaji wa mazao tunapopita katika maeneo mengine tunakuta machungwa yameoza, nyanya zimeoza, matunda mengi, mananazi yameoza mkulima anapata kitu gani? Mkulima anafaidi kitu gani kama lengo letu ni kuwawezesha wakulima wafaidi kila wanachokifanya ili kufaidi jasho lao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna shida ya miundombinu katika maeneo ya mashamba ya vijijini. Maeneo mengi hayapitiki kipindi cha mavuno. Kuna haja ya kutengeneza miundombinu katika maeneo ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri pia tukafanya tathmini kwamba Nane Nane imetusaidia nini sisi Watanzania? Sherehe za Nane Nane: Je, wakulima wa kule vijijini wamefaidika nini katika shughuli za Nane Nane? Kama hawajafaidika kitu au ni *percent* ndogo sana iliyofaidika, basi Serikali iangalie namna ya kufanya tena kwa ajili ya kuwafikia wakulima wale ambao hawawezi kufika katika shughuli za Nane Nane kitaifa au Kimkoa. Lakini pia kuna haja ya kuwasaidia wananchi. Maafisa Ugani pamoja na kwamba hawatoshelezi, lakini pia wawafundishe wananchi juu ya tabia nchi, kila siku kuna mabadiliko. Sisi hapa Dodoma ilikuwa mwezi wa tatu tunavuna, lakini mwaka huu mwezi Machi, bado hatujapalilia. Ni vizuri Maafisa Ugani wakatufundisha juu ya tabia nchi tukaelewa nchi inabadilikaje kila mwaka au kila msimu unapokaribia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu tuliomba fedha kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo ya Chinangali, *Mvumi Mission*, Mvumi Makulu, Mpwayungu, Chalinze na maeneo mengine. Ninashukuru kwamba Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kilimo hiki cha umwagiliaji, lakini hizi fedha ziwahi. Siku zote fedha za maendeleo zinachelewa. Mwaka huu basi fedha ziwahi jamani. Zikija wakati mvua zimekwisha hazitatusaidia. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kama ni pembejeo, kama ni mbolea kama ni miradi ya umwagiliaji, basi fedha zije kwa wakati. Zinakuja kidogo, lakini pamoja na uchache wake, basi ziwahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma pia kwamba kuna baadhi ya Halmashauri inasema imetenga fedha kwa ajili ya *power tiller* mbili, trekta moja au trekta tatu. Hatuwezi kufikia malengo yetu ya kilimo kwanza kama Halmashauri inaweza kununua *power tiller* moja au mbili kwa mwaka. Halmashauri zetu ziangalie kama Serikali Kuu itawasaidia, basi wanunue *power tiller* nyingi wananchi wakopeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAID JUMA NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini vile vile niseme kwamba mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Maji na Mafugo, kwa hiyo, mambo mengi ambayo yameletwa hapa na Mheshimiwa Waziri, leo yamepitishwa kwenye Kamati ambayo na mimi ni mshiriki. Kwa hiyo, nina michango michache hapa ya kuboresha, naomba sana Serikali izingatie na wakati itakapokuwa inafanya majumuisho, basi ipate fursa vile vile ya kunijibu yale ambayo nitakayokuwa nimeyaelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni kubwa ni na kwa ukubwa wake na matarajio makubwa ya Watanzania, napenda nichukue fursa hii kwanza kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watalaam wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinakuwa endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la kwanza ambalo nataka kulichangia hapa ni suala la wataalam kwa maana ya Maafisa Ugani katika maeneo ya vijijini. Kilimo cha kisasa ambacho mwamko wake ni kutoa tija kwa wakulima ama mapinduzi ya kijana ambayo tunayahubiri kila wakati hayawezi yakafanikiwa kama hatuna watalaam kule vijijini. Naangalia takwimu hapa za watalaam wanaoandikwa katika karatasi kila mwaka kwamba kuna watalaam hawa wanapelekwa vijijini. Lakini ukienda vijijini hawapo. *(Makofi)*

Mimi leo nilikuwa naulizana hapa na Maafisa wangu pale Sikonge wale ambao niliwaleta mwaka jana, mwaka juzi wengine wameshaolewa, wameshaondoka, wanahamia mijini. Naomba sana Serikali iangalie sasa, maana inawezekana kabisa hata hawa vijana ambao tunawaandaa kwa ajili ya kuwapeleka katika hivi vyuo, hatuna maandalizi na hatuwajui. Wengine wanaamua kupitia tu anasema nataka nipite Uyole nisome halafu baada ya hapo nikishapata *Diploma* nitaendelea na msafara wangu mwingine. Chuo cha Kilimo kinakuwa ni njia tu ya kupitia. Nilikuwa naomba sana Serikali katika jambo hili iangalie sana. Naomba sana Wizara ihakikishe ajira ambazo kwa kweli zinafanyika mwelekeo wake mkubwa iwe kuwasambaza vijana hawa vijijini.

Lakini vile vile tujitahidi sana kuwawezesha watumishi hawa wanapokwenda maana wengine wanakimbia kwa sababu ya mazingira magumu, hakuna nyumba huko wanakokwenda. Kwa walimu tumefanya ingawa hatujafanya vizuri sana, lakini angalau tumefanya kitu. Tuwajengee vile vile watalaam wetu kwa kweli kwa maana ya kilimo, vile vile maandalizi mazuri ya kuishi, tuwape na vitendea kazi. Unampa Kata Bwana Shamba au Bibi Shamba unampa baiskeli kutoka eneo moja kwenda eneo lingine kilometa 20, hawezi kufanya kazi yake vizuri. Kwa hiyo, nilikuwa naiomba sana Serikali katika jambo hili izingatie kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ljingine naomba nizungumzie suala la mpango wa mbolea ya ruzuku. Mimi nasema wale wanaobeza mpango huu hawana la kusema. Mpango huu umetusaidia sana, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeandaa utaratibu mzuri wa kuwasaidia wakulima ambao hawana kipato kikubwa waweze kushiriki katika shughuli za kilimo kwa kutumia kanuni bora za kilimo ambazo zinaambatana na mbolea, mbegu bora pamoja na madawa.

Kwa hiyo, mpango huu kwa kweli haupaswi kupuuzwa na watu ambao kwa kweli hawakitakii mema Chama cha Mapinduzi. Nilikuwa nataka niendelee kusema kwamba mpango huu uendelee kuwa endelevu pamoja na kwamba mwaka huu tutakuwa na uwigo mdogo kidogo kuliko mwaka uliopita. Lakini naiomba Serikali iendeleze mpango huu kwa sababu mbadala wa mpango huu ni Serikali kuamua kuwa na viwanda vya kutosha hapa nchini. Kama hakuna viwanda vya kutosha hapa nchini mpango huu ndiyo mpango mbadala wa kumsaidia mkulima aweze kupata pembejeo hizi kwa gharama nafuu. Hata Mataifa mengine makubwa yanatoa ruzuku kwa wakulima wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto katika mpango huu, kwa mfano mawakala na watendaji wasiokuwa waaminifu. Mambo haya yanaweza yakapewa kipaumbele kusimamiwa vizuri sana na Serikali katika ngazi zinazohusika. Sasa isiwe sababu ya kuwa na tatizo kutoka sehemu moja halafu jambo hili sasa linarudi kwa wakulima kwamba tunasimamisha utaratibu kwa muda, wakulima wanakosa pembejeo katika wakati muafaka. Nilikuwa naomba sana jambo hili lizingatiwe, tuhakikishe kwamba wakulima wetu wanalindwa katika kupata pembejeo zao, lakini kwa namna moja ama nyingine wale wanaohusika na matatizo mbalimbali juu ya pembejeo hizi za ruzuku wachukuliwe hatua ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba wale ambao kwa kweli wanaona hawajafanya vizuri sana katika maeneo yao, wajitahidi kwenda kuiga katika maeneo mengine waweze kujifunza na kwenda kufanya vizuri zaidi katika suala la kuendesha Mfuko huu wa Pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba nizungumze kidogo, ni suala la Benki ya Wakulima. Nashukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kuhakikisha kwamba chombo hiki kinaendelea hatua kwa hatua kupata fedha kwa ajili ya dirisha ambalo linaanzishwa ili ya kuwasaidia wakulima kupata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na maombi yafuatayo, kwamba wakati Benki hii ya wakulima haijaanza rasmi, basi uwepo mfumo kupitia *TIB* utakaounganisha *TIB* na Benki zilizopo vijijini ambazo zipo karibu zaidi na wananchi ili madirisha haya yaweze kuwasaidia wananchi/wakulima walioko katika maeneo ya vijijini. Nani anayetoka Mole, Tututua Usoke, Isongea atakwenda *TIB* Dar es Salaam? Tunataka mambo haya yaende kwa wakulima huko. Naendelea kusisitiza kwamba Benki ya Wakulima iwanufaishe wakulima wadogo wadogo walioko vijijini. Hapa watazuka watu hawalimi, lakini wanalima kwa kutumia karatasi, anakwenda kukopa fedha nyingi, anakwenda anafanyia shughuli zake nyingine, anarejesha. Tunahitaji Benki hii ya wakulima itakapokuwa inaanza hata kuanzia sasa iwanufaishe wakulima waliopo katika maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba vile vile kwamba mchakato huu wa uanzishwaji wa Benki hii uanze haraka. Benki ya akina mama imekwenda *speed,* haraka haraka imeanza, kwa hiyo, Serikali katika jambo hili la Benki ya Wakulima, wakulima ambao wanasaidia uchumi mkubwa sana wa Taifa isizembee. Tujitahidi sana tujiweke vizuri tuanze jitihada za kuhakikisha kwamba utaratibu wa Benki hii unaanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, nimesema nitataja mambo manne yatawatosheni. Napenda kuchambua mchango mkubwa wa mazao ya biashara. Nikisimama hapa nisipotaja mazao ya biashara

sitaeleweka sana huko ninakotoka. Kwanza, nawapongeza wakulima wetu wa mazao makuu yakiwemo pamba, korosho, kahawa, chai lakini bila kusahau tumbaku.

Nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukuza uchumi na hasa kwa kukusanya kipato kikubwa sana cha fedha za kigeni nchini. Lakini yako matatizo, kwa mfano mwaka huu tunashuhudia matatizo ya kushuka kwa bei kwenye mazao makuu hasa mawili ambayo ni pamba na tumbaku. Bei imeshuka. Lakini mazao haya ukiunganisha na korosho na mazao mengine chai na kadhalika ni mazao ambayo yanasaidia sana kukuza Pato la Taifa mwaka hadi mwaka. Sasa Serikali inasema nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ambapo wakulima hawa wanaendelea kupata fedha zao vizuri katika miaka mingine, mimi sina maneno. Lakini Serikali kwa nini isiandae utaratibu wa kuhakikisha inatoa fidia au inatengeneza utaratibu kama Bima? Sasa tuna Bima za ajali za magari, lakini kwa wakulima wetu hawa tunawaacha tu, wakipata ajali, bei imeanguka, tunakaa na sisi tunaangalia. Hapana, lazima Serikali sasa ithubutu kuhakikisha kwamba inaunda angalau mfuko wa kusaidia mazao haya ya wakulima pale ambapo mazao haya yanapopata muanguko wa bei. Hili ndilo jambo litakalowasaidia wakulima kuiona Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi kwamba iko pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba mwisho kabisa siyo kwa umuhimu, nimwombe Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na wataalamu wake, masoko yanayoendelea kama alivyosema Mheshimiwa Suma hapa na tunauliza maswali mengi hapa, masoko ya tumbaku nchini hayawezi yakaendelea kwa tija kama utaratibu wa kununua soko moja mara moja kwa mwezi utaendelea. Naomba sana, Serikali tuna tatizo la kushuka kwa bei, tusiongeze matatizo mengine tena ya wakulima wetu kununuliwa kwa muda wa mwezi mmoja, mwezi mmoja soko, halafu mtu anaendelea kukaa na tumbaku kwa muda wa mwezi mwingine tena asubiri soko. Tutaendelea kuwaumiza wakulima wetu bila sababu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali kupitia Mawaziri niliowataja hapa, hebu chukueni hatua za makusudi kupunguza huu muda ili wananchi wetu kwa kweli waweze kupatiwa fedha zao kwa kupitia masoko haya angalau mara mbili kwa mwezi, yatawasaidia sana kukidhi mahitaji yao ya chakula. Lakini masomo kwa ajili ya watoto wao na wengine wana maandalizi ya ujenzi wa nyumba. Naomba sana michango vile vile ya maendeleo katika maeneo yetu. Maendeleo yanahitajika kupitia michango mbalimbali ambayo wakulima wetu watapata kutokana na fedha ambazo wanazipata kwa tumbaku. Lakini uchumi vile vile wa maeneo yetu ambao unagusa vile vile wafanyabiashara, unaweza ukaendelea kukua kama tumbaku sasa itaingizwa sokoni na kuuzwa kwa haraka na wakulima wakaanza kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maombi haya, naiomba tena Serikali ijitahidi sana kuzingatia jambo hili la msingi na hiki ni kilio cha Wabunge wote kwa kweli wanaotoka katika maeneo ambayo tumbaku inalimwa, kwamba masoko sasa yapunguzwe, ratiba isiwe ya mara moja kwa mwezi. Tukiwa na ratiba ya mara mbili kwa mwezi, tutawasaidia wakulima wetu waweze kupata fedha zao, lakini wawe na maandalizi mazuri sana ya kilimo katika msimu unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, sitaki kengele inigongee. Nachukua fursa hii kwa mara nyingine tena kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Kwanza nianze kwa kusema kwamba katika taarifa ya hali ya uchumi tuliambiwa kwamba moja ya sababu zilizopelekea kuwepo kwa mfumuko wa bei, ilikuwa ni uhaba wa chakula nchini.

Sasa nikishukuru Chama changu kwa Ilani yake kwamba tunao mpango sasa wa kukabiliana na tatizo hilo na kuwa na chakula cha kutosha, lakini naomba tu nitoe ushauri katika maeneo yafutayo: kwanza ni Serikali kuimarisha mfuko wa pembejeo, lengo la mfuko wa pembejeo ilikuwa ni kuwasaidia wakulima kuweza kupata mikopo yenye masharti nafuu, lakini pia kuzalisha chakula kwa ajili ya chakula pia na ziada kwa maana ya biashara. Lakini kwa taarifa tunazozipata ni kwamba mfuko huu umekuwa ukipata fedha kidogo sana. Maombi kwa mwaka ni karibu Shilingi bilioni 12, lakini Serikali imekuwa ikiwapa ruzuku Shilinig bilioni 3.8, maana yake nini? Maana yake ni kwamba, uwiano wake ni kama katika watu

kumi watapata watatu, katika watu elfu moja watapata watu 300. Uwiano huu ni mdogo sana na mfuko huu ukiwezeshwa fedha, mathalan mwaka huu wameomba Shilingi bilioni 12.2 na bado za mwaka jana hawajapata. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Serikali iwape fedha mfuko huu wa pembejeo ili wananchi, wakulima wadogowadogo waweze kukopa, kama alivyosema Mbunge aliyepita sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu aliyekuweko Mvomero mpaka afike *TIB,* wapi na wapi? Ni vigumu sana. Lakini mfuko huu wa pembejeo ukipewa fedha, unao uwezo wa kuwafikia watu waliopo vijijini huko Mvomero, Sikonge, Nalima, Litisha, Songea, Peramiho au kwa Mheshimiwa Prof. Maghembe kule Mchalilongwe, mwananchi wa kawaida anaweza akapata mkopo kupitia Mfuko huu wa Pembejeo. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kusisitiza kwamba mfuko huu utengewe fedha na wapewe kwa wakati. Mfuko huu unapewa fedha kidogo kidogo sana. Naomba wapewe fedha kwa mkupuo ili waweze kutoa mikopo kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, naipongeza Serikali kwa kilimo cha umwagiliaji maji, kwamba tunayo matarajio kwa kilimo cha umwagiliaji, kimetengwa kwamba hekta milioni moja, kama kweli Serikali itatekeleza mpango huu, kwa kweli Tanzania tutakuwa na uwezo mkubwa sana wa kuwa na chakula cha kutosha. Nami nashukuru kwamba Jimbo la Mvomero maeneo kama Mkindo, Lukenge, Msufini, Wami, Luhindo yote yametengewa fedha. Namshukuru sana Waziri, lakini tunaomba utekelezaji wa fedha hizo ziwafikie walengwa kwa wakati. Lakini wamesahau eneo lingine la Tarafa ya Mugeta kule kuna mito, kilimo cha umwagiliaji kipo kule, lakini watu nao wakumbukwe maana mmeweka eneo moja tu na nilikuwa naomba pia Tarafa ya Mugeta nao wafikiriwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni kwamba kama tumeamua kilimo cha umwagiliaji: Je, wataalamu tunao wa kutosha? Maana siyo kila Afisa Kilimo basi anajua, ana utaalamu wa umwagiliaji, hapana. Kwa hiyo, hawa wataalamu wapo? Lakini wataalamu hawa pia wawepo, lakini pia wawezeshwe maana wapo wataalamu, lakini unawasikia kwamba yuko Wilayani, hana gari la kwenda huko mpaka aazime, aombe, huyu anaitwa afisa Kilimo. Afisa Ugani atamfikia wapi mwananchi huko kijijini? Kwa hiyo, wawezeshwe kwa maana ya usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ni mbolea ya ruzuku. Nami niungane na wenzangu kwamba mpango wa Serikali wa kutoa mbolea ya ruzuku ulikuwa na lengo zuri la kumsaidia na kumwinua mkulima. *(Makofi)*

Hili ni jambo jema, naomba liendelee, lakini kinachotakiwa sasa ni kudhibiti hawa Mawakala ambao ni matapeli, hawana nia njema. Ni kwamba kwa kila Wilaya, Kamati ile inayowapa *tender* hawa Mawakala ijiridhishe na Wakala ambao wanataka kumpa hiyo kazi ili wawe waaminifu na hatimaye wakulima wafaidike kutokana na hiyo nia nzuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ambalo ndiyo kubwa kwangu, ni kiwanda cha sukari Mtibwa. Tangu nimeingia hapa, nimeshaongea mara nne kuhusu kiwanda cha Mtibwa, nilichangia hotuba ya Rais, nikauliza swali, nimechangia hotuba ya Waziri ya Mkuu, nimeuliza swali tena hivi majuzi, lakini matatizo kiwanda cha Mtibwa bado yanaendelea na yameanza muda mrefu toka kiwanda hiki kibinafsishwe mwaka 1997. Mimi sitachoka kuongelea suala la Mtibwa. Sitachoka, najua kwamba nikiongea suala la Mtibwa kwa wananchi wangu watafurahia, lakini kuna watu wachache litawaudhi sana. Lakini kwa kuwa mimi nimechaguliwa na wananchi, nasema mpaka kieleweke, matatizo ya Mtibwa yatatuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kiwanda cha Mtibwa, kuna matatizo pale ya wakulima. Wakulimwa wanalipwa bei ndogo ya miwa. Mkulima wa Mtibwa anatumia Sh. 43,000/= lakini anauza kwa Sh. 42,000/=, hii ni biashara gani? Sh. 43,000 ndiyo gharama halafu wewe unauza kwa Sh. 42,000/=, na nasikia sasa hivi ameongeza ni Sh. 42,500/=. Lakini wenzetu wa Kilombero wanauza miwa kwa Sh. 56,000/=. Hivi karibuni niliuliza swali juu ya kuwepo kiwanda mbadala nikaambiwa kwamba kuna sheria kwamba kiwanda kingine kijengwe kilomita 80. Sasa hii sheria kwani ni torati? Hakuna ushindani hapa. Kwa hiyo, wananchi hao wataendelea tu kunyanyasika eti kwa sheria kwamba kiwanda kingine kijengwe kilomita 80. Nilikuwa naomba sana Serikali iangalie upya, hii sheria ni ya ukandamizaji. Wananchi hawa watakwenda wapi? Kwa hiyo, mnunuzi ni mmoja anapanga bei mwenyewe, kama ukikataa utamuuzia nani miwa yako? Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana suala hili Serikali iliangalie.

Lakini pia, hata uvunaji wa miwa ya nje umepungua. Umetoka tani laki 246 mpaka mwaka jana tani 179. Kwa hiyo, hata upungufu wa sukari ambao umeelezwa katika hotuba ya Waziri, amesema sababu ni ukame. Sisi Mtibwa hakukuwa na ukame, sababu ni kwamba uzalishaji umekuwa mdogo, lakini pia na wananchi wanakatishwa tamaa kulima miwa. Kwa hiyo, suala hili lazima liangaliwe vizuri sana. Lakini pia lipo suala la kuchelewesha malipo kwa wakulima. Mkataba unasema ukimuuzia mwenye kiwanda miwa akulipe ndani ya siku 40, lakini analipa baada ya miezi mitatu, minne, watu wamekopa hela kwenye *SACCOS,* matokeo yake *SACCOS* yenyewe inadaiwa na mtu mwenyewe huyo anadaiwa. Hii siyo kumjenga mkulima kiuchumi, bali ni kumfanya kuwa masikini zaidi. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iliangalie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia liko tatizo la wafanyakazi. Wafanyakazi wanadai mafao toka kiwanda kile kibinafsishwe mwaka 1997 mpaka leo hawajalipwa. Nimeuliza hapa, lakini bado sijapata majibu. Naomba wakati anahitimisha Waziri anijibu kwamba watumishi wale wanaokidai kiwanda cha Mtibwa watalipwa lini? Lakini pia kumekuwepo na tabia ya kuchelewesha mishahara, mishahara unapata tarehe 30 ya mwezi mwingine, hilo nalo ni tatizo sana.

Lakini lingine ni kwamba naambiwa kwamba hivi sasa wafanyakazi karibu 2000 ambao walikuwa wameajiriwa kwa msimu sasa wanakuwa vibarua. Watakuwa wanalipwa kwa wiki tatu, tatu badala ya msimu ambao walikuwa wanaweza kufaidika na *NSSF*. Lakini hii sasa hata ubinafsishaji wenyewe ukimuuliza mtu Mtibwa kule ukamwambia kuna manufaa gani ya ubinafsishaji, anasema afadhali ya Shirika la Umma *(SU)* kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Waziri, niliwahi kukuandikia barua, nikakueleza juu ya suala hili, na nilikupa maazimio 12, siyo ya Makalla, ni ya wakulima, ukaniahidi utakwenda Mtibwa, hujakwenda. Ukarudia tena kwamba utakuwa na safari, hujakwenda, kinakusibu nini kwenda Mtibwa? *(Makofi)*

Nilikuandikia maazimio na naomba niyasome na yaingie katika *record*, kwamba moja ya matatizo ya kiwanda cha Mtibwa, la kwanza ni ucheleweshaji wa malipo kwa wakulima wa miwa umekuwa kero kwa muda mrefu. Serikali iingilie kati mwekezaji aheshimu mkataba, alipe malipo ndani ya siku 40. La pili, ilikuwa kiwanda kiboreshe maslahi ya wafanyakazi, ku-*sign* mkataba wa hiari na kuhakikisha kuwalipa madai wastaafu wote. Tatu, Serikali itunge sheria elekezi ya bei ya miwa kama ilivyokuwa kwa mazao mengine kwa lengo la kumlinda mkulima wa miwa. Nne, Serikali itazame upya endapo mwekezaji wa viwanda bado ana vigezo vya kuendelea kumiliki kiwanda, kwani kwa jinsi ilivyo sasa mitambo ya kiwanda imechakaa na uzalishaji umepungua.

Tano, Serikali isimamie Bodi ya Sukari na kuipa nguvu kusimamia sheria ya sukari. Sita, Serikali imbane mwekezaji atoe kibali cha hesabu zake kukaguliwa ili kubaini gharama za uendeshaji. Saba, Serikali itengeneze mazingira mazuri kwa wawekezaji wa ndani na nje kuja kuwekeza, kuwa na kiwanda kingine mbadala. Nane, Serikali itoe tamko zile hisa 25 alizouziwa, aliuziwa nani na ni lini kwani wananchi walikuwa wako tayari kununua hizo hisa asilimia 25.

Tisa, kuhusu bei ndogo ya miwa, Serikali inaombwa kuangalia upya suala la kumbana mwekezaji kutoa bei nzuri ya miwa. Kumi, Serikali imbane mwekezaji kupunguza ajira nyingi kwa wageni. Kumi na moja, Serikali inaombwa kuanzia sasa iwe karibu kushughulikia kero za kiwanda cha Mtibwa na kumi na mbili, Waziri mhusika anaombwa kufika na kutembelea kiwanda cha Mtibwa na kuongea na wafanyakazi na wadau wa miwa. Nikakukabidhi barua hii, utekelezaji haujafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine kinachonisikitisha ni kwamba Rais alipokuja kule aliagiza kwamba nataka kuanzia sasa nisisikie matatizo ya *Mtibwa Sugar.* Sasa kama Rais anaagiza na mimi nimeshaleta haya maazimio ya hawa wadau wa miwa, sasa wananchi wangu wakimbilie wapi? Eh! Wakimbilie wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekit, tatizo hili ni la muda mrefu. Kwa hiyo, naomba sana, mimi sitaunga mkono hoja hii, nataka maelezo ni lini matatizo yatakwisha Mtibwa, tushughulike na matatizo mengine. Lakini inaonekana hata Bodi ya sukari, nakushukuru ulifanya jitihada ukamwandikia Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari, ukamwambia kwa nini alikudanganya kwamba eti Mtibwa hakuna tatizo na barua yake ni hii hapa.

Kwa hiyo, inawezekana zipo taarifa za uwongo zinazopatikana huku chini, inaonekana kama Mtibwa hakuna tatizo. Jamani tatizo lipo kubwa sana. Naomba sana Serikali na hasa Waziri wakati anahitimisha, atoe majibu yatakayotoa matumaini mapya kwa watu wa Mtibwa kuhusu kiwanda cha sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kama nilivyosema, siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Lakini kwanza kabisa, niseme kwamba tangu nichaguliwe mpaka leo, sijaweza kupata neno ambalo linaweza likawakilisha shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini ambao walinichagua kwa kura nyingi sana. Nawashukuru sana na nitawatumikia vyema. Naamini kabisa Waziri wa Kilimo anavyo vitabu hivi ambavyo nimevishika. Kwanza Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pili anacho kitabu chake cha hotuba ambayo ameisoma hapa leo. Kwa hiyo, binafsi uchangiaji wa hoja uta-*base* zaidi katika vitabu hivyo viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niungane kabisa na Mheshimiwa Anna Abdallah, lakini nitaungana pia na Mheshimiwa Nkumba kuhusiana na suala la pembejeo. Nimesoma kwenye hii bajeti hapa, Mfuko wa Pembejeo umepewa Shilingi bilioni 6.7, mahitajio halisi ni Shilingi bilioni 14. Kama kweli tunadhamiria kumwinua na kumsaidia mkulima, kwa nini hawa watu hawapewi pesa za kutosha ziweze kuwainua wakulima? Kwa kuwa hili nilikuwa naliungia hoja, niende kwenye mambo ya msingi kabisa ambayo yanahusiana na Jimbo la Kilwa Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema naungana na Mama Anna Abdallah kwamba Wizara ya Kilimo, Ushirika na Chakula inabidi warejee upya wakati wanatoa matamko yao au maelekezo yao. Kwa sababu ziko sheria ambazo zinatungwa na Bunge hili lakini wao wanazikiuka kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasema hivyo kwamba Wizara ya Kilimo, Ushirika na Chakula sijui mfumo huo umetolewa wapi? Lakini ukiangalia *Finance Bill* ya mwaka 2006 imeelekeza kwamba asilimia 10 ya *Export Levy* ya korosho igawanywe katika mfumo wa asilimia 6.5 kwa Halmashauri husika zinazolima korosho na asilimia 3.5 ziingie katika mfuko. Pesa hizi hakuna Halmashauri hata moja inayolima korosho mpaka hii leo imewahi kupata hizi pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 58 wamesema kwamba korosho zitaendelea kuboreshwa kwa kupewa pembejeo za kutosha. Leo hii maua ya korosho yameshatoka, hakuna dawa ya korosho iliyokwenda kwenye Mikoa inayolima korosho. Kweli mna nia ya kutaka kuongeza korosho au tunapigwa blaa blaa. Wakati anajumuisha hilo, nitaomba nipate majibu, kwa sababu taarifa nilizonazo, Kampuni zilizoomba ni 18. Lakini mpaka leo hazijapewa ruhusa ya kuuza madawa kwa wakulima. Sijui tunaitakia kheri gani Mikoa hii ambayo uchumi wake unategemea mikorosho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza hapa kwamba nitatumia Katiba. Ibara ya 23 (a) (1) na (2) imetoa ruhusa, naomba niinukuu ili nisikosee. Katika kipengele ambacho kinasema haki ya kufanya kazi: (1) “Kila mtu bila ya kuwapo ubaguzi wa aina yoyote anayo haki ya kupata ajira inayolingana na kazi yake na watu wote wanafanya kazi kulingana na uwezo wao, watapata malipo kulingana na kiasi na sifa za kazi wanazofanya.” (2) inasema: “Kila mtu anayefanya kazi, anastahili kupata malipo ya haki.”

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge rekebisha kidogo pale kwa sababu unanukuu Katiba. Ni ujira, siyo ajira.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Ujira. Sawa, napokea hilo Mheshimiwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kumaanisha hapo ni kwamba wananchi wa Kilwa pamoja na wananchi wa Mkoa mzima wa Lindi wanapangiwa masharti magumu kwenye mazao wanayolima, wanalazimishwa kuuza mazao kwa masharti ambayo wanapewa na ndiyo maana nilisema kwamba mimi nimeipitia vizuri sana Sheria ya Stakabadhi ghalani. Mwanzo mpaka mwisho wake, hakuna sehemu yoyote katika Sheria hii ambayo imetungwa na Bunge hili ambayo imesema kwamba Sheria hii ni lazima mtu kufuata. Ni jambo la hiari. Sasa kwa nini wananchi wa Wilaya ya Kilwa pamoja na Mkoa nzima wa

Lindi wanalazimishwa kufuata mfumo wa Stakabadhi Ghalani ambayo ni jambo la hiari? Hili ni jambo ambalo nitaomba nipate ufafanuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunakwenda pia katika mazao ya asili. Wilaya ya Kilwa ni moja kati ya maeneo ambayo yameendelea tangu enzi ya ukoloni au kabla ya ukoloni na chachu ya ukombozi wa nchi hii kwa taarifa ya Bunge hili na wale ambao hawafahamu, vita ya kwanza kupigana katika Ukanda mzima wa Sahara Kusini ni Vita ya Maji Maji. Tumepigana sisi watu wa Kilwa tukishirikiana na ndugu zetu wa Songea na maeneo mengine ili tuweze kujitawala na kujiendesha na mambo ambayo tunataka sisi wenyewe. Sasa leo hii tunalazimika kulipa ushuru kwenye mazao ya asili ambayo hatujachangiwa kuyalima, pembejeo wala kitu kingine chochote. Sasa ulazima huu unatokana na nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili mimi nitasema kwamba itabidi nipate ufafanuzi. Leo asubuhi hii nilitamani niwe karibu na Waziri wa Maliasili na Utalii. Wananchi wa Kilwa hasa Kaskazini wanyanyaswa na wanyama waharibifu. Wanajitahidi kulima, lakini hawapati nafasi ya kuvuna mazao yao yote na tunapoleta malalamiko yetu Serikalini inaweza ikachukua miezi mitatu bado hujajibiwa.

Kwa mfano, mwaka huu, watu walilima na walikuwa wanategemea kupata mazao makubwa sana. Lakini wanyama waharibifu wakiwemo panya wanasumbua, wanakula mbegu. Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa iliomba ipewe *at least* kwa makadirio ya chini tani moja na nusu ya sumu, wamepewa kilo 45. Sasa sisi hatuna haja ya kupita kuomba vyakula. Tunajitolea wenyewe kulima, lakini tunaomba msaada, basi mtuletee. Chakula hatuwezi kupata, tupeni basi sumu tuuwe hivi viumbe. Tembo wanavamia mazao, wanyama wengine wote wanavamia mazao na hata panya nao, sisi hatuli panya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo jambo lingine katika kuboresha kilimo. Ukirudi kwenye kitabu cha hotuba hii, ukurasa wa 60 na kwa aya ya 112 kuna suala ambalo limezungumzwa hapa. Suala hili linasema kwamba kama nitanukuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa ruhusa yako kwamba Wizara ilishiriki katika kuandaa mpango wa kukuza kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa *Tanzania Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania.* Hii inatokana na mkataba ambao ulisainiwa Davos tarehe 28 Januari, 2011. Hii Davos iko Switzerland kwa wale ambao hawafahamu. Lakini unawezaje kutamka Mikoa ya Kusini bila kutaja Lindi na Mtwara? Unawezaje kutamka Mkoa *Southern, Southern* kila mtu aliyekuwemo humu ndani ya Bunge, na Tanzania nzima hata asiyejua kusoma, ukisema Kusini lazima Lindi na Mtwara iwemo. Katika mpango huu mwanzoni nilivyousoma Mikoa kwa mfano, kama Mkoa wa Dar es Salaam unaingizwa kwenye mpango wa kilimo, wanalima wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni Mkoa wa Ruvuma haukuwekwa na Zanzibar haikuwepo, lakini kwenye kitabu hiki cha hotuba Mikoa hii tayari imeshaingizwa. Sasa na sisi tunataka tuambiwe sababu za kutokuingizwa katika mpango huu ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia suala la uboreshaji kwenye kilimo. Mheshimiwa Makalla ni *interest* yake kwamba watu wa Mtibwa wapate sukari ya kutosha, lakini mimi nashangaa mpaka leo kwa nini Tanzania hatujaingia kwenye kilimo cha sitivia. Ni kilimo ambacho kinaweza kikastahimili ukame lakini sukari hiyo sitivia utamu wake ni mara 300 zaidi ya sukari ya kawaida. Kila siku tunapata matatizo ya sukari, lakini tunaweza tukaingia kwenye teknolojia nyingine tukaweza kulimaliza tatizo la sukari. Katika hili pia nitaomba Mheshimiwa Waziri aweze kunijibu kwa sababu kwenye kitabu chake aya 162 ya hotuba amezungumzia suala la sukari na inaonyesha kwamba ina matatizo na upungufu mkubwa mpaka tunakwenda kuchukua mbegu nyingine katika nchi za *Mauritius, Seychelles* na *South Africa*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la mfumuko wa bei ya chakula. Kama nitakumbuka vizuri, mwaka huu kulikuwa na upungufu mkubwa, lakini bei ya chakula ilipelekea kuwa na mfumko wa hali ya juu. Serikali iliamua kuwauzia wafanyabiashara binafsi ili waweze kuzalisha unga na mazao mengine kama mchele, kuwauzia wananchi kwa bei nafuu. Mpaka leo hii kwa nini bei ya chakula haijashuka? Kama Wizara, wanatueleza nini na wanawaambia nini Watanzania? Tumetoa chakula kwenye ghala yetu ya Taifa, lakini bei ya chakula haishuki. Ukiangalia wastani wa bei iliyouzwa kuanzia Januari mpaka hivi leo inazidi kuongezeka. Sasa hili ni jambo ambalo inabidi tupatiwe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba nitakuwa na mengi ya kuzungumzia, lakini binafsi, lazima nikiri kwamba siko katika hali nzuri, naumwa kidogo. Lakini nasema kwamba kama majibu ya haya hayatapatikana kwa wakati muafaka, sitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Lusinde. Mheshimiwa Lusinde, tafuta *microphone* inayosikika.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba na wenzetu kila *microphone* zinaposumbua, watengeneze basi! Sasa yatakuwa haya haya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata fursa hii ya kuzungumzia mchango wangu juu ya suala kilimo. Kwanza kabisa, kwa masikitiko makubwa kabisa nitoe taarifa kwenye Bunge hili Tukufu kwamba ule uti wa mgongo tuliokuwa tunausema sasa umevunjika, pengine Serikali haina taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari ya kusema tena kilimo ni uti wa mgongo tutakuwa tunawadanganya watu. Mgongo ulishavunjika, watu wako hoi, wanasubiria kuzikwa. Huwezi ukawa unasema kila kukicha kwamba katika Taifa hili kilimo ni uti wa mgongo. Huyu mtu nyama zinaongezeka, uzito unakuwa mkubwa na uti wenyewe unazidi kukonda, mtu wa namna hiyo hawezi kuishi. Kama tunasema kilimo ni uti wa mgongo, basi lazima vitendo viendane na kauli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la kilimo, nataka niseme adui mkubwa wa Chama cha Mapinduzi siyo Wapinzani, wala siyo CHADEMA. Adui mkubwa wa CCM ni Watendaji wetu hawa ndiyo watatuua. Mipango wanayotuletea kila siku haitekelezeki, haina maendeleo makubwa, tunafika mahali kila siku tunawakuza tu watu, wenyewe hawana kitu chochote hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la kilimo kwa Mkoa wa Dodoma, nataka nizungumze kwa uchungu sana. Mkoa wa Dodoma ni Mkoa mkame kila siku, na wataalam wanasema ni mahali pakame. Lakini Mungu ametuonyesha zao mbadala, ameleta zabibu zinazostawi hapa. Mnatusaidiaje? Kila tukileta hoja, yanakuja maneno, ooh, sasa hivi hatuna mpango wa kuuza Bodi. Mpo tayari kuunda Bodi ya Tumbaku inayoua watu, kuliko Bodi ya Zabibu. Imekuwaje nyinyi watu! Haya mambo hayakubaliki hata kidogo. Tukizungumzia masoko, Dodoma hakuna. Hakuna soko linaloweza kukidhi hata mahitaji ya watu wa hapa. *Stand* ya ma-*bus* hakuna. Nyinyi mnataka kutuua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la kilimo, lazima tuzungumze hoja ambazo zinafanikiwa. Hebu ngoja niwaambieni kitu kimoja, wataalam walikuwa wanapiga hesabu kwa kutumia peni, wakaona taabu, wakagundua *calculator,* sasa hivi kuna kompyuta, yote hiyo ni kurahisha. Lakini kilimo bado jembe ni lile lile. Mbona hamfanyi mabadiliko kwenye sekta hii? Bahati nzuri Waziri ni Profesa, basi leteni mambo hapa tuone! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafika mahali Watanzania watachoka na haya maneno tunayosema, kwa sababu njaa haina adabu. Bahati nzuri sisi Wagogo tukishikwa na njaa tuko tayari kwenda jalalani, lakini sasa tutabadilika, tutakuja Bungeni. Ndiyo! Kwa sababu haiwezekani kila siku tunazungumzia kilimo, mabadiliko hayako. Tunazungumzia pembejeo kila siku vitu vinavyozungumzwa havitekelezeki. Tunawaomba, safari hii hatutaki kusikia porojo tena, tunataka kuona vitendo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ndiyo nchi pekee duniani ambayo inamshangaza hata Mungu. Mvua ikinyesha sana janga, isiponyesha janga. Sasa Mungu atufanyie nini? Maana inafika mahali inashindikana, huwelewi hawa watu wanataka nini. Ikinyesha sana mvua utasikia dini zote wakisema tukusanyike kuombea janga la mafuriko. Isiponyesha, tukusanyike kuombea janga la mvua. Nyinyi mnataka nini sasa? Wasomi wetu wanafika mahali wanashindwa hata kuiga tu. Nchi za wenzetu zimeendeleaje? Maana huwezi kusema kuna jambo la utafiti, mimi hilo sikubaliani nalo. Kuna nchi ambazo zimetoka kwenye umaskini wa chakula, kwa nini tusiige tu? Hata kuiga nako ni shida!

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Rais alikuwa Malaysia. Unaona vitu vya ajabu hata kwenye *TV*! Ameongozana na wataalam, lakini Rais ndio anayeomba *business cards* za watu ili waje

wawekeze huku. Wao wenyewe wapo, tumeona mpaka kwenye TV! Mambo ya aibu kabisa! Sasa hawa wataalam wanafuatana na Rais kwenda kufanya nini? Kumbe hata vitu vizuri hawavioni mpaka Rais tunamwona anaomba *business card,* anawaambia, "nitakutafuta," wakati wataalam wapo kwenye msafara. Msiende! Aende Rais peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji. Katika Jimbo la Mtera, kwanza Mkoa mzima wa Dodoma, sisi maji hapa hayakai, yanapita kwa kasi. Kwa hiyo, inabidi tuwe na mabwawa ya kutosha ili tuvune maji halafu tumwagilie. Mwalimu Nyerere alijenga mabwawa mengi sana wakati wa utawala wake. Sasa hivi yamejaa tope, hata kuyafukua tunashindwa. Sasa hivi tuna mradi wa umwagiliaji, Mheshimiwa Waziri amekwenda Mgangalenga pale Tarafa ya Mpwayungu, mradi una miaka mitatu. Leo nimekwenda pale, Halmashauri inaniambia kwamba Wizara watazileta hela mwezi Novemba. Yaani, mwezi Novemba ndiyo waanze kujenga, watapishana na kilimo. Kwa hiyo, ina maana hata mwakani tena huo mradi hautafanya kazi pesa zisipowahi.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri badala kuleta mwezi Novemba, wawahishe, kwa sababu ukizileta mwezi Novemba mpaka Desemba mvua inanyesha, ujenzi utakaokuwa unaendelea utasimama maana maji yanapita kwa kasi. Kwa hiyo, hali inazidi kuwa mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahali mtusaidie, tukishiba, watu watawaza namna ya kufanya. Hata hao vijana ambao tunasema, ooh, vijana warudi nyumbani wakalime. Hebu tuanzishe shamba la Bunge twende tukalime kwa mikono kama tutaweza! Maana tusiwe tunasemea watu tu wakati sisi wenyewe hatufanyi. Kama tunataka kujua uchungu na ugumu wa kilimo tuanzishe shamba la Bunge. Halafu sisi Wabunge twende tulime, mwone shughuli yake kama hatujaghairi na kuliacha hilo shamba. Shughuli ya kilimo siyo mchezo! Hakuna kijana anayeweza kwenda kulima kilimo kisichokuwa na tija na halafu asomeshe ndugu zake, asomeshe watoto, auze mazao hayo hayo, halafu anunue nguo. Hawezi kufanya biashara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao yanapatikana kwa taabu. Sasa hivi nimesoma hapa Mfuko wa Taifa wa Pembejeo, wanataka Shilingi bilioni 14 tu ili waweze kufanya maajabu. Lakini sisi hapa tunawapangia, tunapeleka Shilingi bilioni moja. Unapeleka, mara milioni 300, hawawezi kutoka watu kwenye umasikini kama hatujakuwa *serious.* Wizara nyingine tunazochangia kwa uchungu kama Wizara ya Nishati na Madini, inaonekana kama vile Wabunge tuna hasira, kwa sababu kwenye friji zetu nyama zinaoza. Lakini Wizara inayotakiwa tuchangie kwa hasira ni hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Wizara nyingine inaonekana ni ubinafsi wa Wabunge. Nyama zitaoza, ndiyo maana wanakuwa wakali kwenye umeme. Kwenye kilimo ndiyo inatakiwa tutoe macho na hapa, ndipo inatakiwa tuone kwamba kweli tuko *serious* kwa suala hili. Maana tunasema asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima. Tunawatoaje kwenye lindi la umasikini kwa maneno haya tunayozungumza? Kila mwaka matunda yanaozea pale Tanga, wenzetu wote wanasema hilo hilo. Hivi ninyi tunaposema mnasikiliza au mnaona kama viburudisho? Au mnaonaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi tukakaa hapa kila Bunge, tunaona Wabunge wanazungumzia vitu hivyo hivyo, ukipita viko hivyo hivyo. Sasa tunakuwa kama tumelogwa! Ni vitu ambavyo haviwezekani! Tunataka kuona mabadiliko katika awamu hii. Vinginevyo tutakataa zisipite Wizara zote, potelea mbali hata turudi kwenye uchaguzi tena. Itakuwa biashara gani? Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka tunakakaa, tunazungumza, Wabunge waliopita tumeona wanazungumzia kwamba matunda yanaoza Tanga, sasa hivi bado nyanaoza, hata viwanda vidogo vya kusindika jamani! Inakuwaje? Halafu tunaambiwa kuna mtaalam, hawa wataalam wamesoma wapi? Mbona hawafanyi vitu vikaonekana? Vinginevyo, watolewe waje wengine. Kuna Watanzania wana hamu ya kufanya kazi. Kwa hiyo, ndugu zangu tusiweke watu ambao wanatufanya tukosane na wananchi kwa kuleta mipango isiyotekelezeka. Haiwezekani! Tuokoe matunda ya wakulima wetu, tuokoe mazao yale yanayoweza kutuletea tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia zabibu hapa, Rais kaenda kule, kasema zitakuja hapa. Lakini namna sisi tutakavyopokea, ndiyo itakuwa tatizo, kwa sababu tumefika mahali sisi kila tukiletewa kitu kizuri nacho tunakiharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia mbolea kweli? Kwenye uchaguzi ma-*box* ya kura tunafikisha kila kijiji, lakini peleka mbolea, inaishia Makao Makuu ya Wilaya, haiwezekani. Hatuwezi kuendesha nchi hivyo. Lazima tufike mahali tuangalie vitu vya msingi vinavyogusa wenzetu na vinavyotugusa sisi wenyewe tulioingia humu. Tusisahau kwamba miongoni mwetu sisi ni maskini wa kutupwa na tumeishi kwa mlo mmoja mpaka tunafikia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwa uchungu mkubwa sana, wala sitaki kukutisha kwamba sijui siungi mkono hoja, hoja hii naiunga mkono. Lakini tunataka mabadiliko. Awamu ijayo ukituletea mambo ya namna hii, tutapinga na tutatoa kabisa hiyo bajeti na hatutaki kuiona hapa. Ahsante sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. JITU V. SONI:** Ahsante sana Mwenyekiti. Kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu na wananchi wote wa Jimbo la Babati Vijijini na ninaomba nitamke kwamba mimi nina *interest.* Mimi ni mkulima na ni Mjumbe wa Baraza la *SUA* ambayo mmenichagua katika Bunge hili Tukufu. Mimi kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika historia, Tanzania hatujawahi kupata viongozi ambao wanaipenda na wanajali kilimo kama viongozi ambao tunao sasa hivi. Mipango yote ambayo imewekwa ni mipango mizuri, isipokuwa huku chini basi utekelezaji unakuwa mgumu.

Mipango inaweza kuwa mizuri, lakini utekelezaji ukawa haupo. Huko nyuma tulikuwa na hadithi nyingi tu, lakini hatujawahi kuletewa pembejeo mpaka ikamfikia mkulima. Tatizo ni huku chini pia kuna vidudumtu, vinatafuna haya mambo yote mazuri ambayo tunaletewa. Pia ninawapa pole Waziri, pamoja na Wizara ambayo inafanya kazi katika mazingira magumu. Hii ni Wizara ambayo inahitaji bajeti kubwa kabisa, lakini kila mwaka inaendelea kupungua. Ukilinganisha bajeti ya mwaka jana na mwaka huu na ukilinganisha na fedha ya dola mwaka huu bajeti imepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie Sekta ya Umwagiliaji. Hii ni Sekta ambayo inaweza kutondoa katika umaskini. Umwagiliaji umeondolewa katika Wizara ya Maji umeletwa Kilimo, lakini fedha zote ambazo ilitakiwa ihame nazo, zimebaki kule, imekuja tu umwagiliaji katika Wizara ya Kilimo. Fedha hizi hazitoshi katika mambo ya umwagiliaji. Pia ninaomba katika Miradi hii yote ambayo imeandikwa kwamba wataanzisha umwagiliaji katika Bonde la Kati, Wilayani kwangu Babati Vijijini, ni eneo pekee ambalo lina maji ya mtiririko. Sijaona mahali ambapo umewekwa Mradi hata mmoja wa umwagiliaji. Tunaanzisha Miradi mipya mingi, lakini ile ya zamani ambayo inahitaji ukarabati sijaiona. Kwa mfano, ile ya Masware, Kisangaji, Shaurimoyo na visima 15, ambayo imeshafanyiwa upembuzi na wataalamu wameshapima, sijaona mahali ambapo imetamkwa kwamba itafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Bwawa hili la Girababiek, ambalo liko jirani na kwetu, pia lingefanyiwa kazi. Leo ni mwaka wa tatu linafuatiliwa lakini bado halijapatiwa fedha yoyote. Pia katika Wilaya ya Simanjiro na maeneo mengine, Wilaya yetu ndiyo inazalisha asilimia 80 ya mbegu inayozalishwa Kanda ya Kaskazini, lakini hatuoni umuhimu wowote ambao eneo hilo linapewa katika uzalishaji huo. Pia katika masuala ya mazao mengine, kuna mazao mengi tunaweza kupanda; kwa mfano, matunda mbalimbali, mojawapo ikiwa ni haya ya zabibu, *apple, peaches,* ambayo tunaagiza kutoka Afrika Kusini.

Kwa nini hiyo miche isiagizwe tukapanda hapa na tukazalisha sisi Tanzania na tukasambaza katika soko la ndani na pia katika soko la nje?

Ninaomba suala la kuzalisha hizi mbegu kwa njia ya *tissue culture,* ifanyike haraka, lakini mahali ambapo itafanyika ninasisitiza isiwe Dar es Salaam. Kama ni zabibu ifanyike Dodoma, kama ni mazao ya migomba ipelekwe katika maeneo ambayo yanazalisha migomba na zao lingine lolote lipelekwe huko. Dar es Salaam tupahame jamani, kila kitu ni Dar es Salaam; hivi tunalima huko kwenye maghorofa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Wizara ya Kilimo, iwe mstari wa mbele kuwatetea Wakulima. Mfano, katika Kitabu cha Hotuba leo, ukurasa wa 62 na 114, mahali ambapo kwenye *Finance Bill* tulipitisha kuwa ongezeko la *VAT,* yaani itaondolewa kwenye spea za trekta; hapa imekosewa; ya kwanza imesema kusamehe kodi, ongezeko la *VAT;* kwenye mashine za kupura, kukaushia, kukoboa mpunga na *power tillers,* wakati kule tulikubaliana pamoja na matrekta yapo. Mimi ningeomba hii kitu irekebishwe na Wizara iwe mstari wa mbele kutetea Wakulima. Pia Wizara ifanye kazi kwa karibu na Vyama vya Wakulima, hasa *ACT* ambayo ndiyo inawawakilisha Wakulima wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaomba nizungumzie Mfuko wa Pembejeo na *TIB* kama ambavyo wenzangu wote wamezungumzia. Mifuko hiyo ingepewa pesa ya kutosha na pesa hiyo ipelekwe kwa wakati. Isipopelekwa kwa wakati, hakuna kitu ambacho wao wanaweza kufanya, hawawezi kufanya miujiza. Mfuko huu wa Pembejeo, bilioni moja wala haiwezi kusaidia nusu ya Wilaya moja ndani ya nchi hii. Ingepelekwa pesa ya kutosha. Pia *TIB* iangalie ile mikopo ipelekwe kwa Wananchi wadogo wadogo kwenye Vikundi vya *SACCOS.* Itengwe kabisa asilimia kubwa ya ile pesa iende kwenye *SACCOS* na siyo ziishie kwa wajanja na baadhi ya makampuni ambayo pia yanatoka nje ambayo ni ya wawekezaji, kwa sababu kama ni muwekezaji, aje na pesa zake, hizi za ndani zibaki kwa ajili ya Wakulima wadogo na hizi *SACCOS* zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ruzuku ambalo ni mbegu na mbolea linawagusa Watanzania wote. Mimi ninaomba Serikali iangalie upya suala hili. Kwenye mbolea, ninaomba Serikali ichukue jukumu la kufikisha mbolea moja kwa moja mpaka kwa Mkulima. Wanaonufaika na hii mbolea ni hao Mawakala na watu wa ngazi ya Wilaya, Mkulima hapati hii mbolea. Hili ni suala ambalo linatakiwa liangaliwe. Ruzuku ambayo Serikali inatoa kwenye mbegu, inasaidia makampuni ya nje, asilimia ya mbegu ambayo inaletwa nchini tunayozalisha ni kumi tu katika mbegu ambayo ipo inatumika, nyingine yote inatoka nje. Hiyo mbegu ya nje ndiyo inayopewa ruzuku kwa sababu hakuna *hybreed* inayozalishwa hapa Tanzania. *Hybreed* karibu yote, asilimia 80 ya *hybreed* inayopewa ruzuku, ina maana ruzuku ya mbegu ya Mtanzania inakwenda kwa nchi za jirani; Kenya, Malawi, Zambia na Zimbabwe. Kwa hiyo, tuangalie mbegu za hapa za *hybreed* zingetolewa ili hiyo ruzuku ibaki hapahapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala la mbolea, tuna viwanda ambavyo vinazalisha mbolea, wangepewa jukumu basi wao moja kwa moja waifikishe hadi kwa mkulima. Katika hiyo hiyo mbegu, bei ya mbegu hakuna haja ya kuwa na mfumo wa vocha. Bei ya mbegu ipunguzwe, Serikali itoe ruzuku kwa wanaozalisha mbegu. Ikishatoa kwa wanaozalisha mbegu, *automatically* bei itapungua. Leo hii shilingi 220 ni ushuru wa mazao tu kwenye hiyo kilo. Kwenye shilingi 1,500; shilingi 220 ni ushuru wa mazao tu, ukiondoa na zile kodi za *ASA* na *TOSKI* ambayo wanatoza wazalishaji, bei ingeweza kuwa shilingi 1,000. Serikali ikiongezea ruzuku yake pale, wala hakuna haja ya kutoa hizi vocha ambazo wananufaika watu wachache. Ina maana bei ya mbegu ikiwa chini wote tutanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala ambalo ni muhimu kuliko yote; tuna Chuo Kikuu kimoja tu cha Kilimo ambacho ni *SUA,* lakini mazingira ya pale ya kufundishia, vifaa ambavyo wanafundishia, ni sawa na hizi sekondari zetu ambazo wanafunzi wanasoma sayansi, lakini hawana maabara. Pale Chuo Kikuu, wanafundishwa mambo ya *drip irrigation,* lakini ni kwa nadharia tu, hakuna mahali ambapo wanaweza wakafanya *practical,* kwa sababu hawana vifaa. *Laboratory* ya pale wanaosoma *Ph.D.,* mimi ninasema Mungu amesaidia wapo 15 tu; hivi wangekuwa 50, hao 15 wanafanya kwa zamu kutumia ile *laboratory* ambayo pia tumefadhiliwa na watu wa nje, pesa ya ndani hakuna iliyopelekwa pale. Mimi ninaomba hili jukumu isiachiwe Wizara ya Elimu peke yake, Wizara ya Kilimo ikiangalie hicho Chuo na Wizara zote ambazo zinahusika pale zisaidie ili wataalamu wetu wabobee. Mtu asifikie hatua ya kupata *PhD* yake lakini hajawahi kufanya *practicals;* ni muhimu Chuo hicho mambo yote ambayo tunataka hata upande wa *mechanisation,* kuna trekta moja tena la miaka mingi ambalo liko pale! Hawana *power tiller,* hawana mambo yote, wakati sisi tunasema tunakwenda na mambo ya kisasa, mambo ya kwenda na *mechanisation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho Chuo kiangaliwe upya na bajeti ambayo inapelekwa pale ifikishwe kwa wakati. Pesa zinazofika pale, zifike kwa wakati. Tulipokuwa kwenye Baraza juzi, tulisikia kwamba, pesa ambayo ilitakiwa kuingia mwezi wa tatu imeingia mwezi wa sita; hivi kweli huyo mwanafunzi muda wake wa kusoma pia anaongezewa? Suala lingine ni mambo ya *research,* fedha zipelekwe za kutosha, lakini pia wapewe pesa ili ile *information* yoyote ambayo wanaifanyia *research* waweze kuifikisha kwa Wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba suala la *power tiller* liangaliwe upya. *Power tiller* nyingi hazina *quality* ambayo inahitajika. Leo hii wengi watashindwa kulipa yale madeni na *power tiller* zinatakiwa katika maeneo ya tifutifu ya kulimia mpunga. Maeneo ambayo hayafai kwa *power tiller,* wangepelekewa matrekta mengine ili yaweze kuwasaidia Wananchi. Wafanyiwe utafiti kwanza, maeneo ya kwangu ya mpunga ni sahihi, lakini kuna maeneo ambayo hayafai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la bei ya mazao. Mimi ninaomba Serikali iangalie sana, kwa sababu mwaka ambao ni wa njaa ndiyo Mkulima anaona kidogo afadhali mazao yake yanapata bei; lakini hapo hapo Serikali inatoa mahindi ya msaada, mkulima anakandamizwa. Wafanyakazi wakihitaji mshahara wakigoma wanapandishiwa. Hivi Mkulima anaweza kugoma? Hivi wakijifunza na wakiweza kugoma; siku mbili tu wasipopeleka mazao sokoni; nchi hii kweli itaendesheka? Mimi ninaomba wao pia waangaliwe. Wao pia zile siku ambazo wanafanya kazi, waangaliwe kama Wafanyakazi wengine ili bei ya mazao na kitu wanacholima pia wapate tija. Siyo mtu anafanya kazi kwa kusaidia hii *Middle Class* na *Upper Class;* wao pia wanahitaji kuwa na maisha bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhimu kuliko yote ni miundombinu, iendelee kuboreshwa kule vijijini kwa sababu hakuna miundombinu. Tunapozungumzia umwagiliaji, mabwawa makubwa, barabara, umeme, upelekwe vijijini, ndiyo tutaweza kuwa na unafuu katika masuala ya kilimo. Pia suala la Wataalamu; ninaona wangekuwa wanalipwa *minimum salary* halafu kama kuna uzalishaji, basi ndiyo waendelee kuongezewa hapo kama *bonus.* Kwa sababu wengi wamekaa tu kule hakuna tija. Mtu yuko pale miaka 15. lakini hakuna kitu ambacho ameweza kubadilisha katika eneo ambalo analifanyia kazi kwa miaka yote hiyo. Wawe wanalipwa kutokana na kazi ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara iuangalie Mkoa wa Manyara, hakuna zao ambalo linazalishwa Tanzania ambalo halizalishwi ndani ya Mkoa wa Manyara. Sasa hivi kuna Miradi mingi ambayo inaletwa, hii ya *Southern Agricultural Development Program,* kuna mipango mingine, lakini hakuna hata mmoja ambao unalenga Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Ziwa. Hivi katika maeneo haya ni lini sisi tutafanikiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna-*import* asilimia kubwa ya mafuta ya *palm oil* kutoka Malaysia na sehemu nyingine; eneo la Kigoma linaweza kuzalisha mafuta hayo; kwa nini tusiwawezeshe watu wale wakazalisha badala ya kupeleka pesa zetu nje? Tanzania inaweza kuzalisha mazao mengi sana tukawa sisi tuna-*export* badala ya ku-*import.* Pia ni ajabu kuona nchi kama ya kwetu ambayo ni ya asali na maziwa, bado tuna njaa kila mwaka. Mimi ninaona tujitahidi kabisa bajeti ya Wizara hii iwe inaongezwa na pia iangaliwe katika kona zote, wenzetu wanalalamika wa Lindi na Mtwara, maeneo ya Kigoma na maeneo ya Kanda ya Ziwa, yote yanatakiwa yapatiwe. Sisi tunaweza kuzalisha mazao; tuna *climatic zones* tatu, yaani Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kati na Kanda ya Pwani, mazao yote yanaweza kuota katika maeneo mbalimbali tukawa na matunda, mbogamboga, kila wakati ndani ya nchi yetu badala ya kutegemea mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaunga mkono hoja hii, lakini Serikali iangalie namna ya kuongeza Bajeti. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi hii. Nitoe pongezi za hali ya juu kwa Rais wetu, Kiongozi mahiri, pamoja na Waziri, katika juhudi zote za kuendeleza utekelezaji wa Kilimo Kwanza. Jambo ambalo siyo la kujificha ni jinsi ambavyo mtiririko wa Bajeti ya Kilimo umeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Nimejaribu kuangalia tangu mwaka 2005 mpaka bajeti hii tunayoizungumzia ni takriban mara tano; ni ongezeko zuri kutoka bilioni 200 mwaka 2005 mpaka leo hii bilioni 926. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo inajitokeza katika kilimo ni suala zima la ardhi. Hivi tunavyozungumza ni kwamba, asilimia 75 mpaka 80 ya Watanzania wanategemea kilimo, lakini kilimo hiki klinachangia katika pato la nchi kama asilimia 24 hivi! Haiwezekani, ni sawa na unakuwa na askari 100 halafu unawaambia nendeni mkapigane na askari mmoja; hiyo vita itakuwa ni ngumu na itakuwa ni *wastage* ya *resource.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nitangaze dharura na ninaomba Serikali iipokee hali ya njaa iliyoko katika Wilaya ya Serengeti. Imekuwa ni mazowea tunakwenda kufanya vigezo vile ambavyo havi-*apply* kwa leo hii. Hali ya hewa jinsi ambavyo inabadilika, kwendana na tabia ya nchi, Serengeti ya leo siyo ya jana; Wilaya ya Serengeti ni kweli katika miaka iliyopita katika Mkoa wa Mara wangeweza kukaa hata bila kulima kwa miaka minne kwa sababu uzalishaji ulikuwa ni mzuri. Leo mabadiliko ya tabia nchi yamechangia hali ya ukame, uzalishaji umepungua. Wanyama, kama tunavyofahamu Wilaya ya Serengeti asilimia 94 ni eneo la hifadhi, kwa hiyo, jinsi eneo hili lilivyo kubwa, ndivyo jinsi wanyama wa porini

walivyo wengi. Jinsi ambavyo vyakula vinashambuliwa na tembo na wanyama wengine, ni tatizo kubwa katika Wilaya ya Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapenda dharura hii ieleweke hivyo ,kwa sababu kilimo hiki cha kujikimu, ndicho ambacho Wananchi wanauza mahindi hayo hayo ili wapate fedha kwa ajili ya karo, matibabu na kwa ajili ya matatizo mengine ya kifamilia. Sasa leo hii upungufu huu ambao ukijaribu kuangalia katika kiambatanisho namba mbili, ukurasa wa 117, kwenye kitabu cha Waziri, zimeorodheshwa Wilaya pale, lakini Wilaya ya Serengeti katika Mkoa wa Mara, haimo. Ninapenda hii ichukuliwe kuwa ni dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tumekaa katika Kikao cha Ushauri cha Mkoa tarehe, 8 Machi, 2011 kulikuwa na wastani wa kama shilingi 8,000 kwa debe katika Mkoa wa Mara. Hiyo ni wastani; lakini leo hii tunapozungumza ni shilingi 10,000 mpaka shilingi 12,000 Wilaya ya Serengeti ikiwemo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu Wilaya ya Serengeti bila kujenga mazingira ya kusaidia chakula, wale Wananchi tuwaonee huruma jamani! Wanyama hawa ambao tunajivunia tunao, *Serengeti shall never die,* hawa Wananchi wa Serengeti ndiyo wamewalinda wanyama hawa mpaka leo hii wapo. Hivi sasa tuwaache walale barabarani au waingie porini wakavune basi wale wanyama angalau wajikimu. Ninasema hivyo kwa sababu hata hali ya hewa inavyobadilika na hali ya kilimo imebadilika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ambayo inachangia kutokuwepo kwa chakula katika Wilaya ya Serengeti ni suala la hamasa nzuri ambayo Wananchi wameipata; siku hizi wanalima tumbaku na pamba, jambo ambalo halikuwepo katika miaka ya huko nyuma. Sasa kutokana na mazingira hayo, unakuta katika kulima tumbaku bei ndiyo hiyo inagomba, lakini Mwananchi anategemea alime tumbaku auze, apate pesa na nyingine anunue chakula, hilo halifanyiki. Pamba vivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba suala zima la ku-*survey* nchi, ukienda Mataifa mengine kila kipande cha ardhi unachogusa kiko-*surveyed.* Nchi ndogo kama ya Swaziland, ambayo wanazalisha mazao mengi sana yakiwemo mananasi kwenda South Africa, asilimia 85 ya *imports* za mazao ya kilimo inatoka Swaziland. Sisi leo hii kilimo cha kumwagilia, hizi hekta ambazo tunasema tunazo milioni 44, asilimia 20 ndiyo zinalimwa. Kama ingewezekana suala la umwagiliaji likaimarishwa, mbona fursa ziko nyingi; hizi hekta milioni 29 ambazo tunasema tunazo, ni asilimia moja tu ambayo kuna kilimo cha kumwagilia. Kwa kweli unaweza ukawa na macho lakini usione; katika Kanda ya Ziwa, nimepitia kitabu hiki cha Waziri, hakuna Mradi hata mmoja wa masuala ya umwagiliaji. Maji haya ambayo Mwenyezi Mungu ameumba dunia akatupatia Kanda ya Ziwa, ni vipi yanakwenda Sudan wanafanya kilimo kikubwa sana, kama kule *Swan Dam,* wanamwagilia; Misri vivyo hivyo wanamwagilia maji haya ambayo yanatoka hapa nyumbani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kuna kosa gani katika Kanda ya Ziwa hauwekwi Mradi mkubwa wa umwagiliaji? Vivyo hivyo katika Mkoa wa Mara; katika historia, mwaka 1976, kwa mfano, kulikuwa na *survey* kwa Mkoa mzima wa Mara; wakaainisha maeneo ikiwemo Bugwema, Ihemo, Kiaramo, Butiama, Bonde la Mto Mara na maeneo ya Ikongo; ilipofika mwaka 1978 Vita ya Nduli Idd Amin, kwa kusaidiana na Wayugoslavia ambao walifanya ile *survey,* mchezo ukaishia pale; Bonde la Ikongo hatulisikii! Wizara ya Kilimo wana taarifa hizi. Sasa ile *project* imekwenda wapi? Maana maeneo yale, wahamiaji holela wanaingia na kutoka Mikoa ya jirani na kutoka Wilaya za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni fursa ambayo tunaipoteza. Nimesikia kuna Mradi ambao unakuja pale kutoka Mkoa wa Mara, hatuna habari kwamba, wanataka kufanya kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mto Mara, bila ya ushauri, bila kushirikiana hata na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ninaomba nipate majibu. Waziri atuambie hivi vikao ambavyo anachomolewa mtu mmoja mmoja kutoka Idara ya Kilimo Wilayani, anachomolewa Mtendaji wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kijiji pale Borega, wanapelekwa kule Narok – Kenya, kinyemela; Mradi huu utapokelewa vipi? Mimi mwenyewe Mbunge sina habari; hivi wale wananchi watakubali uwekezaji uwepo pale? Ninaomba nipate majibu katika kuhitimisha. Ninatangaza kwamba, nitaunga mkono hoja kwa masharti ya kupata majibu ya uhakika na ya ukweli. *(Makofi)*

Tukijaribu kuangalia suala zima la maandalizi ya kilimo katika nchi yetu ni lazima tukubali siyo zuri; hivi hawa wakulima tulikaa nao tukauliza hasa wanataka nini au ni maandiko mazuri ya mezani halafu tukayapeleka kule chini? Tungekubaliana na hawa wakulima kwamba, tunataka pembejeo, pembejeo hizi zisingekuwa zinahujumiwa kiasi hiki, kwa sababu kama walishiriki wakashirikishwa na wakaelewa umuhimu wake; kwa nini pembejeo zipotee? Tumekaa Kikao cha *RCC* mwezi wa tatu, nimepiga hesabu nikaona tulikuwa kama na bilioni tano ambazo zilikuwa Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Sasa nikaona bilioni tano hizi, ingekuwa ni matrekta haya tumeuziwa ya bei mbaya, bilioni zaidi ya 50, tungepata matrekta kama 100 ndani ya Mkoa wa Mara. Hata hivyo, nusu ya fedha hizo zingenunua trekta, tungeweza kupata matrekta hata 50, ile asilimia 50 ya hizo bilioni tano ingeweza kusaidia kwenye pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la msingi ni bei ya matrekta; hivi SUMA matrekta haya yameletwa kama *window shopping* au kwa ajili ya nini? Mwaka jana yameingia matrekta 600, mwaka huu yameingia 1260, jumla matrekta 1860. Hivi matrekta haya ya SUMA kuna mkono gani; kuna jinamizi gani?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninajua bajeti hii siyo yako lakini Waziri Mkuu, mtoto wa mkulima, kweli suala hili la kilimo umeliona, umelifanyia kazi; kwa nini asitafutwe huyu mchawi ambaye anahujumu kuuziwa matrekta ya SUMA JKT. (*Makofi*)

Mimi nilikuwa njiani nakwenda kumwona Waziri, bahati nzuri nikakutana naye Waziri wa Kilimo nikiwa na Waraka wangu kumwonyesha jinsi bei za matrekta zilivyo, hata uki-*visit* kwenye *internet,* matrekta kutoka China milioni 15, milioni 18. Sasa haya ya SUMA leo tunaambiwa milioni 57; hivi hapa kuna nini; kuna mkono wa mtu au kuna mchawi? Hawa ambao wanaingiza matrekta ambayo ni *practice* nzuri ya *public private practice* lakini kuna hujuma; haiwezekani matrekta yawe yameingia nchini halafu yanaota kutu. Hivi yameletwa mpaka hapa Dodoma kwa nini msiyasogeze basi hata Kanda ya Ziwa?

Wilaya ya Serengeti yapo maeneo kadhaa ambayo kuna tatizo kubwa, kama nilivyosema, eneo hilo la Bonde ya Mto Mara liendelezwe; ni sehemu ambayo ipo katika *plan* ya nchi zetu. Urasimu huu wa kumpa matrekta tunaomba upunguzwe, kwa sababu inasikitisha, mwaka jana peke yake, Wilaya ya Serengeti imeweza kukopa trekta moja na kwa sababu watu wengine hawana uhakika, kuna miongozo mizuri, yule Mwananchi amekwenda kulikodisha katika shamba la ngano kule Karatu. Sasa ukija kuangalia matrekta ambayo yako Wilaya ya Serengeti, matrekta 13 na haya yamo machakavu na mengine yanajikongoja. Ninaomba vikundi vyangu 12 ambavyo vipo tayari, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo anihakikishie kwamba, nitakapokuja na maombi yao tutapata matreketa haya 12; hii ndiyo itakayotunasua. Mbona mmejaribu kulima kidogo tu, japokuwa unapolima sehemu kubwa unategemea *output* nayo itakuwa kubwa, mbali na ukame na changamoto zingine ambazo ziko, ni kwamba unaweza ukapata ile ambayo inasema jembe halimtupi mkulima. Nimelima kidogo lakini Wananchi kwa sababu ya hali ya njaa na ilivyo, wamevuna shambani, nimechelewa kwenda kuchukua. Juzi ninaambiwa Wananchi wamechukia kutokana na njaa ilivyo kali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hii asilimia ambayo tunayo, karibu asilimia 60 ya nguvu kazi, miaka 15 mpaka 35 hawana ajira; nayo kwa nchi zingine ukimwambia mtu una eneo la kulima halafu una watu hawana kazi, kwa utaratibu wa *unemployment* hiyo siyo *define. Unemployment* ambapo unakuwa na watu *surplus* halafu huna sehemu ya ku-*engage*, haiwezekani sisi tuna sehemu ya ku-*engage* Watanzania asilimia 80 halafu tunawaambia kwamba, hakuna kazi; hiyo haiwezekani. Cha msingi, hii nguvu kazi ambayo ipo ninaomba sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba masoko ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa masharti. *(Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila, nitakuwa sina shukrani kama sitamshukuru sana Waziri wa Kilimo na Naibu wake, kwa habari njema aliyotutangazia sisi Watu wa Vunjo na Mkoa wa Kilimanjaro, tunaolima kahawa. Wakati wenzetu wa pamba wanalalamika bei ya pamba imeshuka kwenye Soko la Dunia, bei ya tumbuku imeshuka kwenye Soko la Dunia, lakini bei ya kahawa na hii ninaomba Wakulima wa Kahawa wa Vunjo waliangalie sana suala hili ili tuweze kunufaika. Kahawa ya maganda ni kati ya shilingi 5000 mpaka 6000 kwa kilo moja.

Ninakumbuka juzi nilikuwa ninaongea na Waziri, Mheshimiwa Profesa Maghembe kwamba, kwenye mnada wa kahawa ile kahawa *AA* kilo moja ni shilingi 8000. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni furaha, kwa sababu Wakulima wa Kahawa tumeteseka sana kwa muda mrefu. Watu wametelekeza ile kahawa, gharama ya kuitunza imekuwa kazi kubwa, madawa ni ghali na kinachozalishwa hakiwezi kutimiza mahitaji ya wakulima. Kwa hiyo; ni kama tumetelekeza.

Kuanzia leo ninaona tutahamia kwenye ulimaji wa kahawa na kitu nilichokipenda kwenye Wizara hii ni kazi wanayofanya ya *research*. *Tanzania Coffee Reasearch Institute* (*TACRI)* ya Lyamungo, chini ya Profesa James Terry, wamefanya kazi nzuri tu kwa sababu kahawa ile ilikuwa inatutesa. Sasa wamekuja na kahawa mpya, ambayo tija yake ni hali ya juu; haina magonjwa sugu kama yale yaliyokuwa yanasumbua kahawa ya zamani, hakuna haja ya mrututu au dawa ya kimatira na gharama ya uzalishaji imepungua sana na ni kahawa ambayo unaweza ukazalisha ndani ya miaka miwili, miwili na nusu unavuna. Sasa nilitaka niwaambie Wakulima wa Kahawa wa Mkoa wa Kilimanjaro, kwa kuwa utafiti huu ni mzuri na kahawa imeshapatikana nzuri, inayopambana na magonjwa sugu na inayozalisha kahawa nyingi kuliko ile ya zamani na huyu Profesa James Terry tayari amekwishaanzisha vitalu 29 kule Vunjo, kahawa kama miche 350000 na ninahitaji msaada wa Wizara ya Kilimo ili aweze kupata miche 650000 na mashine ya kukoboa, tuna viwanda vitatu vyenye mashine ya kukoboa ya kisasa anavyo, lakini bado viwanda viwili.

Sasa ninachotaka kuwaambia Wakulima wa Kahawa ni kwamba, bei ya kahawa imepanda kwa sababu watu wengi duniani wanakunywa kahawa, hasa baada ya wale waliokuwa wanalima kule Columbia kahawa yao kuungua; kufa kufaana, kwa hiyo, mahitaji ya kahawa ni makubwa duniani na Mheshimiwa Profesa Maghembe, alikuwa anasema bei ya kahawa itaendelea kupanda kwa miaka 20 ijayo. Kwa hiyo, ina maana Serikali sasa tuwekeze kwenye zao hili ambalo tayari bei yake inajulikana. Tuwekeze tuisaidie *Lyamungo Reaserch Institute* ya kahawa, tumsaidie yule Profesa aweze kuendelea kuzalisha hii kahawa ya kisasa, ambayo inapambana na magonjwa sugu, haina tena gharama za kupiga dawa sijui za mrututu au kimatira. Ningeomba msaada, siyo wa Serikali kwa sababu sisi hatuna fedha za kigeni na tayari bei ya kahawa imepanda, kwa nini tusichukue hela nyingi mahali zilipo tukapeleka Vunjo, tukapeleka Kilimanjaro, tukasaidia hili Zao la Kahawa tukauza tukapata bei nzuri duniani, tukainua uchumi wa nchi hii.

Kwa hiyo, kwanza, nilikuwa ninaomba hilo. Pili, ninaishukuru sana Serikali, kwa sababu Wananchi pamoja na lawama zinazoweza kutolewa kwenye Wizara ya Kilimo, lakini fikiria kahawa ya Kilimanjaro ambayo tayari ilishakufa, magonjwa sugu, dawa ilikuwa haipatikani ya kuweza kutibu tena magonjwa yale. Sasa wanafanya utafiti mpaka wanakuja na kahawa chotara, ambayo haiwezi kushambuliwa tena na magonjwa, haihitaji madawa ghali ambayo yalikuwa yanaumiza wakulima na inazaa baada ya miaka miwili, miwili na nusu. Kwa nini tusikubali kwamba kuna kazi inafanyika kwenye maeneo fulani haiwezi kufanikiwa kote.

Yapo maeneo fulani lazima tutambue uwepo wao na kazi wanayofanya, la sivyo, tukiwakatisha tamaa watasalimu amri wataona hatuna shukrani, hakuna sababu, kuna watu wazuri, kuna watu wema, kuna wasomi wazuri, ambao wana-*dedicate* maisha yao katika kuwasaidia wakulima.

Eneo moja ambalo ninasema ni lazima niwapongeze na kuwashukuru sana ni ule utafiti wa kahawa mpya inayotoka Kituo cha Utafiti wa Kahawa Lyamungo. Kwa hiyo, ninaomba wapatiwe msaada wasaidiwe. Sasa hivi hata afisa ugani nimemwona kule Vunjo, ni mama mmoja tu anaitwa Vailet sijui nani, hana hata pikipiki; yuko peke yake. Sasa niliomba msaada hao maafisa ugani waendelee kusaidiwa na hivi vitalu mashamba mama yapatikane mengi. Sasa kama kule kuna Kata 15, mashamba mama 29 tu hayatoshi na tunataka hili zao hii bei mpya iweze kutusaidia. *(Makofi)*

La pili, ambalo ni lazima niwashukuru ni kuhusu umwagiliaji; ninaona mmejitahidi sana kule kwangu, kwa mfano, Kata ya Kahe Mashariki na Kongama, mmepeleka fedha lakini ninachosema fedha zile mnazopeleka mara nyingine ni kidogo, mnapeleka kidogo kidogo na ile mifereji inatakiwa kusakafiwa; pelekeni fedha nyingi kama mnavyopeleka kwenye ujenzi wa barabara za lami. Utaona hizi hela mnazopeleka kidogo kidogo, kwa mfano, Mfereji wa Ugama kule Mawala, 2007/2008 mmepeleka 600,000 hazitoshi, hazikufanya kazi inayotosheleza. 2009/2010 mmepeleka milioni 210 na 2010/2011 mmepeleka milioni 250. Sasa ningeomba pia Waziri utume watu wako wafike pale, kwa sababu huo mfereji unajengwa kwa miaka yote haumaliziki; je, yale malengo mliyokubaliana yatakuwa yamefikiwa?

Kwa hiyo, ninachoomba mumsaidie sana huyu Juma Omari, afisa wa pale ambaye anahangaika na umwagiliaji. Kuna Mfereji wa Kimangamao, 2007/2008 wamepeleka milioni 60, 2008/2009 wamepeleka milioni 150, 2010/2011 milioni 250 na mwaka huu 2011/2012 milioni 250; ni fedha nzuri kidogo lakini kwa kuwa zinakwenda kidogo kidogo haumaliziki. Ningeomba zipelekwe fedha za kutosha mmalize ule Mradi *once for all*. Hata kule Kochakindo; 2008 nimepeleka milioni 155, 2010/2011 milioni 200; na 2011/2012 milioni 250; mnajitahidi, lakini bado kazi haijamalizika. Kule mnakokwenda bado kuna njaa, huwezi kujua ni kazi gani ilifanyika. Kwenye soko pale 2007/2008, nimepeleka milioni 32, 2009/2010 milioni 250, sasa 2011/2012 mmepeleka milioni kumi, kule Kiomu mwaka huu wa 2011/2012 mmpeleka milioni 250.

Sasa ninachosema, fedha haipo, lakini fedha zile kwa kuwa zinakuja, ile kazi haikamiliki na mngeshafanikiwa kumwagilia kule Kahe, ina maana njaa kule Vunjo itakuwa imemalizika na kama wenzangu walivyosema kwamba, mwaka huu hakuna chakula cha kutosha; ni kweli hata kule kwangu Vunjo kuna matatizo makubwa ya chakula na niliwaombeni katika kipindi fulani nilisema kwenye Bunge mmepeleka chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu njaa; nilimweleza Waziri kwamba, mahindi yanakwenda Kenya na kweli yanakwenda pamoja na kuweka askari barabarani; ninachotaka kukwambia, yale mahindi bado yanakwenda Kenya. Hali ya chakula kule Vunjo siyo nzuri, nikaomba tuwe na soko pale Himo; Watu wa Sudan na wana fedha za kigeni, Watu wa Somalia wana njaa, Watu wa Kenya wana njaa, kwa nini tuwapelekee mahindi kupitia vichochoroni? Kwa nini tusifanye soko kubwa pale Himo na tayari umekwishatenga milioni 93 kwa ajili ya kujenga soko kubwa pale Njiapanda? Kwa nini tusiwe na soko la Kimataifa pale Himo? Kwa nini msiitangazie dunia nzima kwamba kama unataka mahindi ya Tanzania tena kwa fedha za kigeni njooni Himo; tatizo ni nini?

Badala ya kuweka polisi barabarani, kwanza, ninataka kusema kwamba, hakuna kazi inayofanyika kuzuia chakula tunajidanganya, uliza mtu yeyote. Chakula kinakwenda, kama hatuwezi kukizuia ni afadhali wawe huru wakauze kuliko kuweka vizuizi vya uwongo njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba, Waziri atafungua soko pale. Ahsante sana.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Vilevile ninawashukuru Wananchi wa Jimbo la Kwela, kwa imani yao kwangu. Ninawashukuru sana tena zaidi ya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niseme machache ambayo ninadhani Serikali imefanya vizuri pamoja na changamoto ambazo zipo. Ninaipongeza Serikali kwa kubuni mfumo wa pembejeo. Mfumo huu kwa kiasi fulani umesaidia japokuwa una changamoto na matatizo mengi lakini yanaweza yakarekebishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninaweza kuipongeza Serikali ni ongezeko la Maafisa Ugani. Lazima nikiri, kwenye eneo langu, maafisa ugani wameongezeka kuliko ilivyokuwa pale mwanzo kutokana na ongezeko hilo na utoaji wa pembejeo. Ongezeko la uzalishaji wa mazao limeongezeka. Pamoja na ongezeko la uzalishaji kuongezeka, lakini wakulima wetu bado ni maskini tena maskini wa kutupwa. Sababu kubwa ya watu hawa kuwa maskini ni kuuza mazao yao kwa bei ndogo na kutokuwa na uhakika na soko la kuuza mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kitu kinachompa raha mkulima kama kufahamu bei ya mazao na uhakika wa soko. Vitu hivyo vinamhamasisha mkulima karibu kwa asilimia 75, mengine yote ni ziada tu; soko na bei nzuri ya mazao. Vitu hivyo vinamhamasisha mkulima, mengine yanakuwa ni ziada tu hata

kama ungepeleka pembejeo, upeleke kitu gani, kama bei ni mbaya ni mbaya na hakuna uhakika wa soko, mkulima anadhoofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, majuzi tu Serikali imezuia Wananchi kuuza mazao nje tangu tangazo lilipotoka. Huu ndiyo mwanzo wa mateso ya Wananchi ya Mikoa inayozalisha kwa wingi na hasa Mkoa wa Rukwa. Pia ni mateso makubwa hata kwa wafanyabiashara, ambao walikuwa wananunua, maana bei ilikuwa imekwishafika mpaka gunia lilikuwa linauzwa kwa shilingi 40,000, walikuwa wanapeleka nje na wao, lakini kwa sasa wamesimama, wakulima hawana mahali pa kuuza na ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali ilitizame hilo; kitendo cha kuzuia Wananchi wasiuze mazao nje wakati haijajipanga kukidhi ununuzi wa mazao hayo ni mateso makubwa kwa Wakulima. Hilo lazima mlifahamu; mnatengeneza chuki kwa Wananchi. Serikali inatengeneza chuki bila sababu na mnatoa ufahari hata kwa watu wengine; hivi mnataka siku moja mwone Wakulima wanagoma au wanafanya maandamano ndiyo mjue kwamba kitendo hiki kinawaudhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa Mikoa inayozalisha vizuri sana na hakuna zao lingine la biashara wanategemea mahindi. Wamezalisha mahindi, lakini kwa sasa chombo cha kununua mazao hakipo na hata kikiwepo hakiwezi kukidhi uzalishaji uliopo kwa sasa. Mazao ni mengi, nitakupa mfano, labda nitoe mfano kwa takwimu; msimu wa mwaka 2006/2007, Mkoa wa Rukwa ulizalisha karibu tani 314,379, shirika la ununuzi wa mazao lilinunua tani 32 tu, karibu asilimia kumi, mazao yote yalikuwa yananunuliwa na wafanyabiashara kwa bei wanayotaka. Msimu wa mwaka 2007/2008, Mkoa wa Rukwa ulizalisha tani 37,044, lakini Serikali ilinunua tani 26,951, sawa na asilimia saba. Mwaka 2008/2009, Mkoa wa Rukwa ulizalisha tani 3,065,538, lakini Serikali ilinunua tani 39,689, sawa na asilimia kumi. Msimu wa mwaka 2009/2010, Mkoa wa Rukwa ulizalisha tani 5,080321, lakini Serikali ilinunua tani 56,000 tu, sawa na asilimia tisa. Kwa hiyo, karibu asilimia themanini na zaidi zinabaki zina-*hang,* hakuna mtu wa kununua, jambo ambalo ni mateso makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu nilizonazo za uzalishaji wa mwaka huu na ziada ya chakula iliyopo Mkoa wa Rukwa ni tani 8,030,590. Ninaomba Waziri aniambie amejiandaa kiasi gani kununua hayo mazao maana wamezuia Wananchi wasiuze nje ya nchi na kwa sasa ni mateso makubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba Shirika la Ununuzi wa Mazao, linawasaidia Wakulima wote, ni Wakulima wachache tu kwa sababu kwanza eneo linalozalisha mazao ni mbali, Wakulima hawana vyombo vya usafiri; barabara ni mbaya, fedha zenyewe ni kidogo, kunakuwa na msongamano; ni kama ugomvi nani auze na asiuze. Katika dunia ya leo kumtesa mkulima kiasi hicho; Serikali inategemea nini ndugu zangu? Tunaomba Serikali ijaribu kufungua mipaka ili Wakulima wauze, kama Serikali ina hofu ya uchache wa chakula si ikanunue ihifadhi? Kwa nini isiende kununua? Mimi ninashangaa, kama mwaka ambao chakula ni kidogo nchini Serikali inasuasua kununua; je, mwaka ambao Mikoa yote itakuja kulima si itakuwa tabu sana? Kwa hiyo, ninaishawishi Serikali kama ina dhamira ya kuendelea kuzuia Wananchi wasiuze mazao nje, basi ianze kununua tena sasa.

Ninasikitika kusema kwamba, siku ile Spika alisema wanafunga mipaka miezi sita; miezi sita kuanzia sasa mkulima ataanza kuuza mazao mwezi wa ngapi? Miezi sita, karibu tunakwenda mwezi Januari, katikati ya kilimo, sasa huko ni kumtesa mkulima, kama mnataka kununua anzeni kununua sasa tena kwa bei nzuri. Kama wafanyabiashara wananunua kwa shilingi 40,000, Serikali inunue zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni tatizo kubwa sana kwa Wananchi wa Mkoa wa Rukwa na sisi Wabunge wa Mkoa wa Rukwa, tumeambiwa tunapokwenda twende na majibu kwamba, tunakwenda na fedha zinakwenda za kununulia mazao; vinginevyo, Wananchi wanasema hapatatosha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Serikali itambue kwamba, hilo ni tatizo.

Ninaishukuru Serikali kuwa na ubunifu wa mfumo wa pembejeo, lakini pembejeo zinachelewa kufika, wakati mwingine zinafika wakulima wameshaanza kupanda halafu bei ni kubwa. Ninaomba Serikali ijaribu kutoa ruzuku ya kupunguza bei ya pembejeo, bei ya pembejeo iko juu, mazao yananunuliwa kwa bei ndogo. Mkulima anauza mazao kwa bei ya hasara.

Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuzungumza alisema hivi; Wabunge wote tungeandaliwa mashamba ya kulima ndipo tungejua ugumu wa kilimo ulivyo. Inawezekana tunazungumza, tumesoma kwenye madaftari, hatujakwenda kwa vitendo halisi; hakuna kazi ngumu kama kilimo, ni kazi ngumu mno inahitaji tuwafariji Wakulima kwa kuwekea bei nzuri na kununua kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu umwagiliaji. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, katika eneo ambalo limejaliwa kuwa na maeneo mazuri ya umwagiliaji ni pamoja na Mkoa wa Rukwa, Jimbo la Kwera. Jimbo la Kwera, Ukanda wa Ziwa Rukwa, lina mito mingi sana, yaani unapotembea kilomita tano au nane lazima ukute mto tena usiokauka. Tuna mito mingi na mabonde mazuri ambayo muda wote unaweza kulima kama miundombinu itatengenezwa vizuri ni kilimo cha mwaka mzima, yaani mzunguko. Pamoja na mito mingi, Serikali imegusia mto mmoja katika Kijiji cha Sakarilo.

Ninashukuru kwani mafanikio ni mazuri na tunakwenda vizuri, lakini ningeishawishi Serikali itumie ile mito ambayo imebaki katika kuzalisha. Tumesikia wenzetu wanalalamika njaa, lakini mimi mtu akisema njaa kwenye Mkoa wangu ninamwonea huruma, kwa sababu vyakula vinaoza na hata ukienda kwenye maghala ya Mkoa wa Rukwa, hakuna hata pa kuweka kwani mazao yako chini na mengine yanaoza na hatujui hata mwaka huu Serikali ikitaka kununua itanunua itaweka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaishauri Serikali ijaribu kuchukua uzito wa kutosha katika kununua mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile nizungumzie suala la Ushirika. Waheshimiwa Wabunge, waliotangulia wamezungumzia mambo ya Ushirika na udhaifu wake. Lazima tukubali udhaifu ule ni mwanzo wa kujifunza, unapoona udhaifu ulitokea cha msingi ni kuweka misingi ya kujifunza ili kuuondoa kwa sababu hakuna namna wala hakuna chombo ambacho kinaweza kikatumika katika kumsemea mkulima ni Ushirika tu. Hata tungefanya nini Ushirika ndiyo chombo ambacho kinaweza kikatumika katika kumsemea Mkulima.

Hata tungefanya nini Ushirika ndiyo chombo kinachoweza kuwasaidia Wananchi, lakini cha msingi tuwe wakweli kuchukua hatua pale ambapo kuna ubadhirifu. Tatizo Serikali nayo inakuwa na kigugumizi cha kuchukua hatua hata kwenye ukweli ambao imeona hapa kuna tatizo; sijui ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika ni nyenzo muhimu sana na hata ile Mikoa ambayo bado upo mpaka hivi sasa, hiyo Mikoa imepiga hatua na Wakulima wake wameneemeka. Kwa hiyo, chombo kinachoweza kuwasaidia Wakulima ni ushirika; cha msingi tusimamie, tupeleke Wataalamu waende mpaka kwenye ngazi ya Tarafa na Kata ili waweze kutoa elimu kwa Wanaushirika kutambua mali yao na namna ya kuchukua hatua na Serikali tuwasaidie pale ambapo watahitaji msaada.

Tatizo Wanachama wanaweza wakalalamika kwamba, watu fulani wamekula fedha kama Mbunge mmoja alivyosema, wale waliokula fedha hizo wanashirikiana na Afisa Ushirika, majibu ya ukaguzi hayatolewi yanatolewa kwa maneno na wala hakuna usimamizi. Hiyo ndiyo inayovunja imani kwa Wananchi. Wananchi wanataka kuona jambo linafanyika kadiri alivyoliona bila mzunguko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaishauri Serikali ijitahidi kufuatilia ule upungufu unaoonekana katika ushirika na vilevile iongeze ajira kwa Maafisa Ushirika kutoka ngazi ya Wilaya, Tarafa mpaka Kata ili waweze kusaidia Wakulima wetu.

Ninaomba kuzungumzia kuhusu upungufu wa Wataalamu wa Umwagiliaji. Umwagiliaji una Wataalamu wachache sana, katika Halmashauri yangu ya Wilaya tunao Wataalamu kama wawili ambao kwa namna moja ama nyingine, wanapata shida sana namna ya kuzunguka kuangalia wanaweza kuwasaidia vipi wakulima wetu. Kwa hiyo, ninatoa wito kwa Serikali; kama ina nia kweli ya kukuza umwagiliaji basi ijitahidi hata kutafuta Wahandishi wa kutusaidia kuinua kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninasema kwamba, ninaomba Waziri wa Kilimo anithibitishie namna gani atayaondoa yale mazao ambayo yamejaa kwenye maghala; na namna gani atanunua mazao ya Wananchi wa Mkoa wa Rukwa; maana msimu wa kuanza maandalizi ya kilimo tayari umeshasogea lakini mazao bado yamejaa kwenye maghala?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa mashaka, lakini baadaye ninaweza nikachukua shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nimwite Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nina yangu machache tu, kwa kuanzia, ninamwomba Waziri wa Kilimo, akaifute hii picha, inamdhalilisha Rais Kikwete kwa kupanda *power tillers* ambazo hazifai katika kilimo katika nchi hii. Hii *power tiller* umeiweka hapa kama nembo kwenye Kitabu chako cha Bajeti, umemdhalilisha Mheshimiwa Rais wetu kwani tumekataa *power tillers* katika Mkoa wa Rukwa na Mikoa mingi wamezikataa kwani hazifai. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Waziri amehakikisha katika Kitabu chake kwamba, atanunua mazao katika Mkoa wa Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma, tani 200,000 na wakati huo huo amefunga mipaka. Wananchi walianza kununua mahindi Rukwa lakini leo Wananchi wa Nkansi wananihangaisha, kila siku wananipigia simu wanasema kwamba, mahindi yalikuwa yananunuliwa kwa shilingi 30,000 mpaka 35,000, lakini leo yananunuliwa kwa shilingi 24,000 mpaka shilingi 20,000 na hawana mahali pa kuuzia.

Kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja amezungumza kwamba, waweke soko Tarakea; Tarakea hawalimi mahindi kwa nini unataka kuweka soko Tarakea? Mwananchi yeyote anunue mahindi apeleke anakokujua kwa sababu kufa kufaana, huu ni mwaka wa neema kwa wakulima wa mahindi. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri afute kauli yake ya kwamba, mahindi yahifadhiwe mpaka mwezi Januari ili watu wafungue mipaka; Januari ni msimu wa kulima na njia hazipitiki.

Ukifungua vituo vya kuuza mazao ya Wakulima katika Mkoa wa Rukwa, Nkansi kuna vituo vitatu; yaani Namanyere, Taramila na Mtenga. Wilaya ni kubwa na kuna Kata kama ya Mkwamba na Itingi. Kutoka Itingi mpaka Namanyere ni kilomita 90; huyo Mkulima wa kupeleka mahindi mpaka huko utamsaidia usafiri?

Leo Wakulima wa Itingi wanauza gunia la mahindi kwa shilingi 12,0000 mpaka shilingi 15,000 wakati walikuwa wanauza kwa shilingi 30,000, wewe unazuia tu mpaka mahindi yameteremka bei; una uchungu wa wakulima? Huna uchungu na Wakulima kabisa.

Kusema kweli sisi tukienda watatupiga mawe na hatukubali kupigwa mawe ndugu yangu. Tunakuhakikishia kwamba, sisi hatukubali kupigwa mawe, Serikali ya CCM inasema kwamba, Kasi Mpya; Kasi Mpya itakuwa Kasi Mpya namna hii? Hii ni Kasi Mpya ndugu zangu? Hii ni Kasi Mpya au Kasi Bora? Hili ni balaa tupu! Baadhi ya wafanyakazi wako wa vituo vya kununulia mazao ndiyo wameanza kununua mahindi, ukifika wakati wa kufungua mazao ndiyo wa kwanza kupeleka mahindi kuuza, wananchi hawapati nafasi wanakaa vituoni kwa siku 14, hawana pa kula, wanatoka vijijini na wala hawauzi mahindi, wanadhalilishwa. Waonee huruma Profesa, waonee uchungu. *(Makofi/Kicheko)*

Hizi Vocha ni balaa; hii ni *EPA* nyingine. Kuna wizi mkubwa katika Vocha, kuna mtandao mpaka wa wakubwa labda wanahusika na hizi Vocha. Tumeshazungumza kuwa hizi Vocha hazifai, lakini ninyi mmekazania tu. Mkamtosa *DC* wa Sumbawanga peke yake wakati wameiba mabilioni ya pesa, mkamtundika kwenye Msalaba *DC* peke yake wakati wezi ni wengi.

Nimetoa huo mfano wa Mpembe kule kwetu, hakuna hata mfuko mmoja wa mbolea, lakini wameandika mpaka maiti na hakuna hatua iliyochukuliwa.

Wametuuzia *power tiller* mpaka Katibu wa Chama wa sehemu fulani anakwenda kuuza *power tiller* Sumbawanga Mjini kwa bei anayaoijua yeye kwenye *briefcase*, anachukua kwenye mkoba Katibu wa Chama, mwuza chai anakwenda kuuza *power tiller* kwa bei anayotaka yeye. Tunasema tuchukuliane hatua; mbona hamchukui hatua yoyote? Hii Kampuni ya *Power Tiller* ni ya nani mpaka mnamuweka Rais kwenye kitabu akiwa kwenye *Power Tiller* ili kuvutia watu wakati ni mbovu? *(Makofi)*

Nimelalamika mpaka barua nimeandika kuhusu Bonde la Kirando, kuna wakulima wanahangaika, mto unapitisha maji mwaka mzima, kuna wakulima zaidi ya 4,000, lakini Serikali haiwasaidii hata kuziba ule

Mto wa Lwanfi, wanahangaika wakulima wanaziba mto wenyewe wanashindwa, maji yanakuja yanabomoa.

Bonde liko pale wanahangaika kulima ekari 3,000, lakini hamuwasaidii. Nkenge kule mlipeleka shilingi milioni 15 zimeliwa, hakuna cha mfereji lakini Wakulima wa Kata ya Kabwe wanahangaika; hii Serikali tunakwenda wapi?

Mimi siungi mkono hoja kwa sababu mahindi yanawaozea wakulima na ninyi mmekaa hapa mnafunga mipaka kwa kutaka wakulima wasiuze mnasema Kilimo Kwanza. Hiki siyo Kilimo Kwanza, hatuwezi kufanikisha Kilimo Kwanza kwa mtindo wa kufunga mipaka, hiki ni Kilimo Mwisho. Ninataka kuanzia sasa Mheshimiwa Waziri anihakikishie kwamba, atanunua mahindi yote ya Mkoa wa Rukwa lakini asiponunua atalipa fidia kwa Wakulima kama mlivyolipa fidia Wafugaji wa Ng'ombe?

Mazao yakioza wewe ulipe fidia, Wakulima wanahangaika hawana sehemu ya kuhifadhi mahindi. Mkulima anavuna magunia mpaka 1,500, lakini hakuna nyumba; ataweka wapi mahindi yake?

Mkulima gani ana hifadhi ya mahindi ya magunia 1,000; ana nyumba ya kukaa ambayo ina sehemu ya kuweka magunia 30 au 40 tu? Wewe unamlazimisha aweke mahindi gunia 1,000 mpaka mwezi Januari, Januari utatengeneza Barabara za Rukwa? Unaweza kupitisha gari Rukwa? *(Kicheko)*

Ninakwambia siungi mkono hoja na sitoi shilingi maana mtanishinda kwa kura, lakini mimi siungi mkono hoja mpaka mwisho wa dakika. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri akanunue mazao ya Rukwa yote, asiponunua awalipe fidia Wananchi wa Rukwa na leo atangaze bei ya kununua mahindi na ahakikishe ananunua mahindi yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge ...

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanya, nikishasimama hakuna tena hoja nyingine, hoja sasa inabaki kwa Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu waliotakiwa kuchangia leo kama nilivyokuwa nimetoa maelekezo, wamefikia hapo ambapo tumehitimisha na Mheshimiwa Keissy. Kesho tumebakiwa na mchangiaji mmoja, ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu, ambaye hajawahi kuchangia hata mara moja. Baada ya Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Khamis na wengine wataendelea kadiri ya Mwongozaji wa Kiti atakayekuwa katika Meza kuongoza ratiba ya kesho.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru sana kwa michango yenu ya leo na baada ya kusema hayo, ninaahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.35 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 26 Julai, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*